

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Sita - Tarehe 14 Februari, 2006

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Viwango Tanzania kwa mwaka ulioishia Tarehe 30 Juni, 2003 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Bureau of Standards (TBS) for the Year ended 30th June, 2003*).

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2005 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Communications Regulatory Authority for the Year ended 30th June, 2005*).

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita muuliza swali wa kwanza kwa siku ya leo, naomba niwatakie heri wale wote ambao wanaitambua siku ya wapendanao. Kipekee nawatachia heri wale wote ambao wanapenda lakini hawapendwi na wale wote ambao hali ya mapenzi imelegalega. (*Kicheko/Makofi*)

Na. 59

Kituo Kikuu cha Mabasi Ubungo

MHE. HALIMA J. MDEE aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo Kikuu cha Mabasi yaendayo Mikoani kipo katika Jimbo la Ubungo, na kwa kuwa Kituo hicho kinatoza aina mbalimbali za ushuru:-

Je, wakazi wa Jimbo la Ubungo wanafaidika vipi na mapato yanayopatikana kutoka katika Kituo hicho?

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Kituo Kikuu cha Mabasi yaendayo Mikoani kipo katika Jimbo la Ubungo. Kituo hicho kilianza Desemba, 1999 na kilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam mwaka 2000. Aidha, kazi za Kituo hiki ni kutoza ushuru mbalimbali hususan ushuru wa kulaza mabasi, kutumia kituo, wasindikizaji, kodi ya pango, kodi ya mabango, kodi ya vioski na kadhalika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na kodi zinazotozwa, wakazi wa Ubungo wanaendelea kufaidika na mapato ya kituo hicho katika nyanja mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upannde wa usafi, Jiji la Dar es Salaam linatoa huduma za usafi kwa Manispaa zote tatu likiwamo Jimbo la Ubungo na Halmashauri ya Jiji inatoa mitambo na magari kuhudumia maeneo ya Tandale Sokoni, kizimba kilichopo barabara ya Sam Nujoma na Mburahati kwa Jongo.

Mheshimiwa Spika, elimu, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imesaidia kugharamia ujenzi wa Maabara ya Shule ya Sekondari Kiluvya na imenunua madawati kwa ajili sekondari hiyo.

Mbeshimiwa Spika, kwa upande wa biashara na uchumi, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imechangia na kuboresha kituo cha uchongaji wa vinyago kilichoko Mwenge ambapo kimelipa umeme jumla ya shilingi milioni 3.5. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ajira, kama tunavyoelewa kwamba Kituo cha Mabasi cha Ubungo kinafunguliwa saa 10.30 alfajiri na kinafungwa saa 4.00 usiku. Kutokana na kuwepo kwake ndani ya Jimbo la Ubungo, kituo hicho kimetoa ajira kwa wakazi zaidi ya 1,000 na zaidi ya nusu ya waajiriwa hao ni wakazi wa Jimbo la Ubungo.

Pia eneo hilo kwa sasa hivi lina thamani kubwa sana kwa sababu hoteli za kisasa zimejengwa kama vile *Landmark, Royal Kibadamo* na *Ubungo Plaza*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miundombinu, Halmashauri ya Jiji imejenga daraja la Kiluvya ili kuwarahisishia wakazi wa Kiluvya kwenda maeneo mengine bila kupata adha yoyote. (*Makofî*)

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalî dogo la nyongeza. Kwa kuwa Kituo hiki kinasaidia na kinahudumia wasafiri wote wa nchi nzima, lakini kwa pia kuna wapigadebe ambao Serikali imesema wasiwepo na wanakera na wanasababisha wizi.

Je, Serikali inatamka nini kuhusu kuwepo kwa wapigadebe ambao wanasabaisha matatizo kwa wasafiri kutoka Mikoa ya Bara?

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, tatizo la wapigadebe linafahamika katika vituo vyote vya mabasi katika nchi nzima. Serikali inaweka utaratibu kwa hao wapigadebe ili wafahamike ni watu gani ambao wanaweza kufanya kazi hiyo ya usindikizaji. Kwa hiyo, zinatafutwa sheria ili kuwalinda hao wapigadebe kuhakikisha kwamba hao wasafiri hawapati adha kutokana na wapigadebe hao. (*Makofî*)

Na. 60

Udhibiti wa Takataka

MHE. SUSAN A. J. LYIMO aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo mengi ya Mjini yamekithiri kwa uchafu unaotupwa na wananchi wenyewe, mfano mifuko ya plastiki maarufu kama *rambo*:-

(a) Je, Serikali ina mkakati au mpango gani wa kudhibiti takataka hizo hasa zile za mifuko ya plastiki?

(b) Je, Serikali itafanya nini kuhakikisha kila mwananchi anaweka eneo lake safi?

(c) Je, Serikali itafanya nini kuhakikisha kuwa madampo yanayojaa uchafu yanasaafishwa kwa wakati ili kuondoa kero ya harufu mbaya inayotokana na uoza wa taka wa muda mrefu?

WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA aliujibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalî la Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hatua ya kwanza iliyochukuliwa na Serikali kudhibiti tatizo la mifuko ya plastiki ni kuweka ushuru kwenye mifuko hiyo kwa madhumuni ya kupunguza utumiaji wake.

Hatua ya pili ni kuwezesha uingizaji, utengenezaji na matumizi ya mifuko mbadala. Matarajio ni kwamba watumiaji wakuu na wananchi kwa ujumla wataanza kuona gharama kutumia mifuko ya plastiki na hivyo kutumia vifaa mbadala.

Mheshimiwa Spika, hatua zingine zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ni pamoja na kuhamasisha viwanda vinavyozalisha bidhaa za plastiki vijihusishe zaidi na kurejeleza taka za aina hiyo, kuhamasisha Asasi na vikundi mbalimbali visivyo vya Kiserikali katika kurejeleza bidhaa zitokanazo na plastiki ili kutengeneza vifaa mbalimbali kama vile madawati ya shule, meza na mabomba ya maji na yale ya kupitisha nyaya za umeme, kuhimiza mifumo madhubuti katika Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji ya kukusanya, kutenganisha na kurejeleza taka ikiwa ni pamoja na kuweka vyombo maalum vya kukusanya taka za plastiki na kuanzisha vituo na maghala ya kukusanya taka za mifuko ya plastiki na nyinginezo za plastiki zikisubiri kurejelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatua ya kuweka ushuru wa asilimia 15 kwenye mifuko ya plastiki inayoingizwa nchini imepunguza kiasi uingizaji wa aina hii ya palastiki kwa asilimia 50.

(b) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, sheria Na. 20 ya mwaka 2004 katika kifungu cha 122 inataka kila mmiliki au mkazi wa eneo lolote kuweka mazingira yake safi na kwa wakati wote. Akishindwa kufanya hivyo anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria. Mtu ye yote atakayetupa takataka hovyo hovyo au kushindwa kusafisha mazingira yake au kuweka eneo lake katika hali ya usafi, chini ya kifungu 190 cha sheria hiyo atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni moja.

(c) Sheria ya Serikali za Mitaa Na.7 na Sheria ya Serikali za Mitaa Na.8 zote za mwaka 1982 zinazipa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji jukumu la kukusanya na kuondoa takataka katika maeneo ya umma, maeneo yanayomilikiwa na watu binafsi, taasisi, viwanda na biashara.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa kwanza wa kutunza mazingira ni wa mwananchi anayeishi katika mazingira hayo. Serikali kwa upande wake kupitia Serikali za Mitaa itaendelea na juhudhi za kuboresha ukusanyaji wa taka ngumu na taka za maji maji. Aidha, Serikali itaendelea na jukumu la kukuza weledi na kujenga hamasa ili jamii ya Kitanzania ikabiliane na tatizo la takataka zinazotupwa hovyo zenye athari kwa mazingira, mandhari na afya kwa binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi ya kumjibu Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo Mbunge wa Viti Maalum, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na wananchi na wengine kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. Nawashukuru kwa dhati kabisa wananchi wa Rungwe Mashariki kwa kunichagua tena bila kupingwa kuwa Mbunge wao. Imani hiyo ni kubwa na ni deni kwangu linaloweza kulipwa kwa utumishi kwao na kwa Watanzania wote. (*Makofii*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini nina swali moja dogo la nyongeza.

Pamoja na kwamba Waziri amesema kwamba mifuko ya plastiki imewekewa ushuru ili kupunguza matumizi, lakini bado amesema ni asilimia 50 tu katika punguzo hilo. Je, haoni kwamba kuna umuhimu wa Wizara yake kuleta Muswada Bungeni ambao utahakikisha kwamba mifuko ya plastiki inazuiliwa?

WAZIRI NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:
Mheshimiwa Spika, tunaangalia hatua mbalimbali nyingizo za kuchukua kama Serikali ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la mifuko ya plastiki. Pamoja na hiyo tutaangalia uwezekano wa kuzuia uingizaji wa aina ya plastiki mbalimbali. Lakini hili lazima tulifanyie kazi kwa sababu linaweza kuathiri biashara. Tuangalie makubaliano na nchi nyingine. Lakini tutachukua hatua ambazo haihitaji kuzitangaza hapa kwa sababu tuna mamlaka ya kufuta uingizaji. (*Makofi*)

MHE. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kuhusiana na takataka, kwa sasa hivi kwanza tunapongeza juhudzi za Serikali kwa kuwahusisha watu binafsi na vikundi vya watu kufanya biashara ya kubeba taka. Lakini kutokana na hali ya usalama barabarani na magari ambayo yanatumika kwa uwezo wao mdogo.

Je, Mheshimiwa Waziri asingeona ni wakati mzuri wa kupata hata kama *grants* kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara hao ili waweze kupata magari mazuri ya kuwawezesha kubeba takataka na walipe polepole?

WAZIRI NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:
Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nichukue fursa hii kwa niaba ya Serikali kuvipongeza vikundi mbalimbali vya kijamii, visivyo vya Kiserikali pamoja na makampuni ambayo yanaendesha shughuli za kuondoa uchafu katika miji yetu na katika vijiji vyetu. Kwa mfano, Dar es Salaam kuna vikundi vya wananchi 23, mashirika yasiyo ya Kiserikali 23 na makampuni binafsi 23 yakihuksika katika kuondoa takakata ngumu na takataka nyingine. Kwa hiyo, nawashukuru sana na kuwapongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupata mikopo, suala hili ni zuri kwa sababu inaonyesha kwamba mazingira vile vile yanaweza kuwa biashara. Lililopo ni kuwaomba wenye vikundi au wafanyabiashara kuandika maombi kwa mabenki wakionyesha jinsi gani wanaweza wakafanya biashara hiyo ili waweze kurejesha mikopo. Serikali tutakuwa tayari kusaidia pale inapowezekana. (*Makofi*)

MHE. PASCHAL C. DEGERA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imefanya matengenezo makubwa kwenye barabara kuanzia Kondoa hadi Dalai ambayo ni sehemu ya barabara ya Kondoa hadi Olboloti na kwa kuwa sehemu ya barabara iliyobaki kuanzia Dalai hadi Olboloti ni mbaya sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo makubwa sehemu hiyo ya barabara iliyobaki ya kutoka Dalai hadi Olboloti?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara ya Dalai hadi Olboloti yeny urefu wa kilometra 47.6 iko katika barabara ya Mkoa inayotoka Olboloti - Dalai - Kolo inayohudumiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali imezifanya matengenezo makubwa ya kiwango cha changarawe barabara za Mkoa wa Kondoa - Bicha - Dalai yeny urefu wa kilometra 28.7 na sehemu ya Dalai - Kolo yeny urefu wa kilometra 71.2 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.645. Barabara hizi mbili za Mkoa zinaungana na barabara ya Dalai hadi Olboloti katika kijiji cha Dalai.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuifanyia matengenezo sehemu ya barabara ya Dalai hadi Olboloti kutokana na umuhimu wake kiuchumi na kijamii na ndiyo maana katika mpango wa matengenezo ya barabara wa mwaka 2005/2006, sehemu hii ya barabara itafanyiwa matengenezo ya kawaida na ya sehemu korofii katika jumla ya ufefu wa kilometra 31 kwa gharama ya shilingi milioni 27.84 ili iweze kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba sehemu ya barabara ya Dalai hadi Olboloti inapata matengenezo makubwa kama yalivyofanyika katika barabara zilizokamilika chini ya mradi wa *HIPC*. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha za matengenezo kwa barabara hii kila mwaka wa fedha ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal la nyongeza. Aidha, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba atatenga ama Serikali itatenga pesa za kutosha kufanya sehemu hiyo ya barabara matengenezo makubwa. Je, ni lini ama katika Bajeti ipi hizo pesa zitatengwa?

(b) Kwa kuwa eneo la barabara kati ya kijiji cha Songolo na Chandama hasa wakati wa Masika haipitiki kabisa, je, atachukua hatua gani ya dhalura kunusuru eneo hili la barabara ili usafiri na usafirishaji uweze kufanyika hasa wakati wa masika?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Paschal Degera, kwa namna ambavyo anafuatilia barabara kwenye Jimbo lake na kwa kweli ufuatiliaji wake ndiyo umefanya wananchi wa Jimbo la Kondo Kusini waweze kumrudisha Bungeni kama na ambavyo wananchi wa Ukonga walivyofanya kwangu mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali ni lini Bajeti itawekwa kwa ajili ya barabara hii. Nimeeleza kwamba kazi hii imeanza kwa kilometra 31. Barabara hii ina urefu wa kilometra 47.6, kilometra 31 inatengenezwa. Nimesema katika kila Bajeti ya mwaka tutaendelea kuweka fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara hii. Ina maana kwamba katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 inayoanza Julai, fedha zitatengwa tena kwa ajili ya barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu hiyo korofii anayozungumzia, kwa sababu matengenezo sasa hivi yanaendelea kuangalia sehemu korofii, nitamshauri awasiliane na Meneja wa *TANRODS* Mkoa wa Dodoma ili kuangalia matengenezo hayo yanapofanyika, wajaribu kuangalia sehemu hii anayosema ni korofii ili hatua za dhalura ziweze kuchukuliwa.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Olboloti inafanana sana na barabara ya Rombo mpaka Kamwanga; ni lini Serikali itamalizia sehemu iliyobaki kutoka Kamwanga kwenda Ngaranairobi mpaka Sanyajuu?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naona swali hili kwa sababu linagusia barabara nyingine kabisa iliyo Mkoa mwingine, basi sitaliruhusu. (*Kicheko*)

Na. 62

Janga la UKIMWI Nchini

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inazo takwimu sahihi zinazoonyesha Wilaya ambazo zimeathirika sana kwa ugonjwa wa UKIMWI nchini:-

Je, ni hatua gani ambazo Serikali imezichukua au inatarajia kuzichukua kuzipa Wilaya zilizoathirika sana kama Kyela kipaumbele katika kupelekewa vifaa vyaa upimaji,

dawa za kurefusha maisha, madaktari na wauguzi wa kutosha pamoja na misaada ya hali na mali kwa wajane wanaotokana na ugonjwa huo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, naomba nitoe taarifa fupi kuhusu suala la utoaji wa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2003, Baraza la Mawaziri lilipitisha Mpango wa Taifa wa Huduma ya Tiba ya UKIMWI . Mpango huu umelenga kuwapatia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI wagonjwa wapatao 500,000 ifikapo mwaka 2008. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 20 ya wanaoishi na virusi vya UKIMWI nchini kwa takwimu za UKIMWI za mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, mpango huu una maeneo matatu ya utekelezaji ambayo kwanza ni:-

Kuimarisha vituo vya kutolea huduma kwa kuvipatia vituo vifaa vya upimaji na utambuzi wa ugonjwa. Vifaa hivi vimepelekwa vituo vyote 98 vinavyotoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, zikiwepo Hospitali za Rufaa Maalum, Mikoa na za Taasisi zisizo za Serikali ambazo zipo kwenye mpango huu, pia Wilaya kumi za pembezoni ambazo zina mazingira magumu kufikika, zimepewa mashine za kupima wagonjwa wa UKIMWI. Mpango utapeleka vifaa vya kupima damu na *biochemistry* Wilaya zote nchini. Hadi sasa vifaa hivi vimekwisha pelekwa katika Wilaya 10, katika mwaka huu wa fedha kwa kupitia Bajeti ya Serikali na wafadhili. Tutaendelea kuagiza vifaa hivi kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, pili, kuimarisha ujuzi wa watoa huduma kwa wagonjwa, mpango huu una kadiriwa kuhitaji watumishi 10,000 wakiwemo madaktari, wafamasia, wauguzi na watumishi wa maabara. Utekelezaji wake utahitaji fedha nyingi kwa ajira hii. Ili kupunguza gharama, Serikali inawafundisha na kuwatumia watumishi waliopo katika vituo vyetu vya tiba kwa sasa. Wizara inawasiliana na Mfuko wa Pamoja wa Dunia (*Global Fund*) kuomba fedha za kugharimia ajira ya watumishi hawa ili tuweze kutoa huduma kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, tatu, huduma ya dawa ambayo inalenga kupata dawa za kutosha kupunguza makali ya UKIMWI kwa wanaostahili wakati wote kupitia fedha za Serikali, wafadhili na Mfuko wa Pamoja wa Dunia (*Global Fund*). Huduma hizi za kutoa dawa za kurefusha maisha utekelezaji wake unaenda sambamba na uwezo wa Serikali, nia na malengo ya Serikali ni kufikia kila mwananchi anayehitaji huduma hii nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 Serikali ilichagua hospitali 96 kutekeleza zoezi hili. Hospitali hizo ni za Serikali ikijumuisha pia hospitali ya Wilaya ya Kyela na hospitali binafsi za mashirika ya dini. Uchaguzi wa hospitali hizo ulitokana na uwezo wa

hospitali kutoa huduma na pia baadhi ya hospitali tayari zilikuwa zimeshaanza kutoa huduma hiyo ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inazipa kipaumbele Wilaya zilizoathirika zaidi na ugonjwa UKIMWI na inahakikisha kwamba malengo yake ya usambazaji wa huduma na tiba katika mikoa, Wilaya hadi vijijini na pia kutathmini hospitali zinazotoa huduma kwa kuziandalia mipango ya uimarishaji ikiwa ni pamoja na kutoa dawa bora na vifaa bora vya upimaji virusi vya UKIMWI, pia mafunzo kwa wafanyakazi ili kuhakikisha kwamba huduma bora zinatolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesambaza huduma, kinga na tiba kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI Wilayani Kyela. Pia huduma za kinga na tiba kwa magonjwa ya ngono na magonjwa mengine zinapatikana katika vituo vyote vya kutolea huduma vya Serikali na binafsi vya mashirika ya dini vilivyoko katika mpango huu. Aidha, wataalam wake wamepewa mafunzo na wanaendelea kuwahamasisha wananchi wanaohitaji huduma hizo kuzitumia ipasavyo.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa utafiti katika jamii uliofanyika mwaka 2001 na 2003, umedhihirisha wazi kwamba Wilaya ya Kyela ni ya pili Kitaifa kuathirika kwa ugonjwa huo, lakini utoaji wa dawa za kurefusha maisha (*ARVs*) unatolewa kwenye hospitali moja tu ile ya Wilaya na vile vile kupata *CD4 Count* ya mgonjwa inabidi tusafiri mpaka Mbeya Mjini ambako kuna mashine moja tu kwa mkoaa mzima! Je, Serikali haioni udharura wa Kyela kupewa kipaumbele kwa kuongezewa vituo vya kutoa hizo dawa za *ARVs* na vile vile kusogezewa huduma ya *CD4 Count* ili kuokoa na kurefusha maisha ya wapiga kura wangu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya Kyela imeathirika kwa kiasi kikubwa na kwamba kuna uchache wa *ARVs* ambazo zinapatikana kule; na ni ukweli kwamba ile mashine ya *CD4 Count* kule Kyela haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, lakini ni kwamba si Kyela tu au katika Mkoa wa Mbeya ambaa hii Mashine ya *CD4 Count* haipatikani. Tatizo la UKIMWI liko katika Tanzania nzima na Mikoa mingi bado haijapata hiyo mashine. Lakini tunazingatia uwezo wa Serikali yetu na pindi itakapokuwa tayari, Wizara yangu itahakikisha kwamba kipimo hiki kinapatikana. (*Makofii*)

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanayohusu msaada wa hali na mali. Nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa hali ya chakula nchini kwenye baadhi ya maeneo kuna njaa ya kutisha na waathirika wa UKIMWI katika nchi yetu wametapaka nchi nzima. Je, Serikali na Wizara yako Mheshimiwa Waziri imeweka Mkakati gani wa kugawa chakula kwa wanotumia *ARVs* ili wasije wakaathirika zaidi kwa sababu tiunajua *ARVs* zinanguvu sana na wanahitaji chakula cha kutosha? (*Makofit*)

SPIKA: Nasikitika hili nalo ni swali jipya kwa sababu linaulizia juu ya kuwapa vyakula waathirika. Swali la msingi linahusu Hospitali ya Kyela kwa kuhudumia wagonjwa wa UKIMWI. Kwa hiyo, siliruhusu.

Na. 63

Vifo Vya Akina Mama Wajawazito

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR aliuliza:-

Kwa kuwa akina mama wengi wajawazito hufariki dunia kutokana na kutokwa na damu.

(a) Je, ni sababu gani zinazosababisha wazazi kutokwa na damu nyingi?

(b) Je, ni ushauri gani unaofaa kwa akinaamama wanaopata matatizo kama haya ili yasitokezee tena?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baadhi ya sababu zinazofanya akinamama wajawazito kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua ni kama zifuatazo:-

- Mama mwenye uzao zaidi ya mara tano;
- Mama kukaa kwenye uchungu zaidi ya saa kumi na nane;
- Kuchelewa kutoka kondo la nyuma baada ya mama kujifungua;
- Kuchelewa kuachia mapema kwa kondo la nyuma baada ya mama kujifungua (*Retained Placenta*);
- Mama mwenye shinikizo la damu;
- Kama mama ana matatizo ya kutoka damu nyingi wakati wa kujifungua katika historia yake ya uzazi; na

- Kama mama amechanika kwenye viungo vya uzazi kwa mfano shingo ya uzazi au mama alikuwa na upungufu wa damu wakati wa ujauzito akitoka damu kidogo tu wakati wa kujifungua anaweza kupoteza maisha.

(b) Mheshimiwa Spika, ushauri kwa mama mwenye matatizo haya ni kama ifuatavyo:-

(i) Mara mama anapojihisi kuwa mjamzito anashauriwa kuhudhuria *clinic* ya afya ya uzazi ili kupimwa na kuchunguzwa afya yake.

(ii) Mama mjamzito ahakikishe pia anahudhuria *clinic* kama anavyopangiwa na wakati wowote anapopata matatizo basi aende haraka sana kwenye *clinic*.

(iii) Mama mjamzito ashauriwe kula chakula bora ili aweze kuwa na damu ya kutosha wakati wa kujifungua.

(iv) Mama mjamzito anashauriwa kutotumia dawa za kienyeji wakati wa kipindi chote cha ujauzito na pia wanashauriwa wajifungulie kwenye vituo vya tiba vyenye huduma na wahudumu wenyewe ujuzi.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu lilielezea wazazi baada ya kujifungua pale wanapotokwa na damu nyingi na kwa kutokwa na damu nyingi kabla ya kujifungua.

(a) Kuna wazazi ambao hufariki dunia, je, tatizo hili pia linasababishwa na nini?

(b) Kwa kuwa wazazi wengi wanaoishi vijijini ndiyo zaidi wanaoathirika na tatizo hili kwa sababu ni maeneo ya mbali sana na hakuna usafiri. Je, Serikali inalionaje tatizo hili la wazazi wanaokaa vijijini kuwapelekea usafiri wa haraka?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza amesema kwamba kuna akinamama wanatokwa na damu nyingi kabla ya kujifungua na anauliza tatizo lake ni nini?

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa inayomfanya mama atokwe na damu kabla ya kujifungua anapokuwa na mimba inawezekana ni kwa sababu kondo la nyuma linatangulia, kwa lugha ya kitaalam inaitwa *ant partum hemorrhage. (Makofî)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, anaulizia kuhusu akinamama wanaokaa vijijini na kuwa na matatizo ya usafiri. Ushauri ninaoweza kutoa ni kwamba Halmashauri nazishauri ziweze kutafuta uwezekano wa kujenga majengo karibu na hospitali kama *waiting homes* ili akinamama wale wenyewe vidokezo vya hatari waweze kukaa pale kabla ya kujifungua ili pindi uchungu utakapoanza, matatizo hayo yakajitokeza waweze

kupata huduma hii kwa urahisi badala ya kuwa na matatizo ya usafiri. Nashukuru.
(*Makofî*)

Na. 64

Ulipaji wa Mishahara ya Watumishi wa Serikali

MHE. MGANA I. MSINDAI aliuliza: -

Kwa kuwa ni jukumu la mwajiri kumlipa mwajiriwa mshahara kwenye eneo analofanya kazi; na kwa kuwa hivi karibuni Serikali iliamua mishahara ya walimu na watumishi wengine wa Serikali ipitie benki, utaratibu unaomfanya mtumishi kutumia gharama kubwa ya nauli toka eneo lake la kazi kwenye Wilaya na usumbufu mkubwa na madhara kwa watumishi kwa kutokuwa na uhakika na tarehe za mishahara kwenye benki ambazo huduma hizo zinazorota: -

(a) Je, Serikali haioni kwamba utaratibu huo ni mbaya na unasababisha unyanyasaji kwa walimu na watumishi wengine kwa hiyo ufutwe mara moja na iwe jukumu la Serikali kupeleka mishahara katika maeneo ya kazi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutowarudishia watumishi fedha wanazotumia kama nauli, malazi, chakula na kadhalika ni ukiukwaji wa haki za binadamu kwa kumfanya mtumishi atumie mshahara wake aliotakiwa apelekewe kituoni kwake?

(c) Je, Serikali inapokataa kuwapelekea watumishi mishahara vituoni kwao kwa kisingizio cha kutokuwa na usalama wa fedha haioni kwamba, ni kukwepa majukumu yake kwa vile vyombo vya usalama viko chini yake na ni jukumu lake kuvitumia kwa faida ya watumishi wake na wananchi wote?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali bado inaona kimsingi utaratibu huu unafaa na inachofanya ni kuboresha huduma ya mishahara ili kukabiliana na mapungufu yaliyojitekeza. Kwa maana hii, Mkataba kati ya Serikali na *NMB* utaangaliwa kwa makini kuona kama unaweza kuboreshwa na pia itaangalia uwezekano wa kutoa zabuni kwa benki zaidi ya moja ili hata benki za wananchi ambazo zipo karibu zaidi na wananchi ziweze kulipa mishahara ya watumishi wa Serikali. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Wilaya, Serikali itatafiti uwezekano wa kufikisha mishahara karibu zaidi na vituo vya kazi vya watumishi wake.

(b) Mheshimiwa Spika, kutowarudishia fedha za nauli watumishi wanaofuata mishahara siyo ukiukwaji wa haki za binadamu ila ni kwa mujibu wa kanuni za utendaji katika sekta ya umma. Aidha, kwa kuwa hatua zinachukuliwa kurekebisha hali hii, haitegemewi kuwa tatizo hili litaendelea kwa muda mrefu.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inawajali sana watumishi wake ila hajawa na uwezo wa kumpelekea kila mtumishi mshahara wake katika kila kituo cha kazi kwa kutumia vyombo vya usalama kusindikiza fedha za mishahara katika vituo vyote vya kazi nchi nzima na hivyo haitawezekana kwa sasa kwani gharama yake itakuwa kubwa mno. Hatua nilizozieleza katika jibu langu la sehemu (a) ya swali zitasaidia kupunguza tatizo hili.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Je, kwa kipindi hiki ambacho bado hatua hazijachukuliwa, walimu na watumishi wengine watarudishiwa fedha zao za nauli, kulala na chakula wanapofuata mshahara?

(b) Kwa sababu *pay day* inajulikana ni tarehe 23 kwa Serikali, lakini sasa watumishi wa Serikali wakiwemo walimu na wengine wanalipwa zaidi ya tarehe 5 mishahara yao. Serikali inasemaje juu ya hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB): Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema haitawezekana kuwarudishia nauli wafanyakazi wakifuata mishahara, ila juhudzi zitafanywa kurekebisha hali iliyopo hivi sasa ili hapo baadaye matatizo haya yasiwepo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sawli la pili kwamba mpaka leo bado wafanyakazi au walimu wanalipwa zaidi ya tarehe 5, Mheshimiwa Mgana Msindai, tunakushukuru.

Kwa muda wa miaka 10 yote uliyopo Bungeni umekuwa ukigombania haki za wafanyakazi na wewe unajua hatua iliyochukuliwa na Serikali toka hapo walipokuwa wanapata mshahara tarehe 25 ya mwezi unaofuata mpaka sasa angalau ni sehemu chache ambazo wanapata mshahara tarehe 5. Kwa hiyo, juhudzi za Serikali bado zitaendelea kuhakikisha kwamba watu wanapata mshahara siku ambayo imewekwa wapate mshahara. (*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kati ya watumishi wanaofuata mishahara mbali ni pamoja na walimu na kwa kuwa walimu wanapofuata mishahara mbali wanafunzi pia hukosa vipindi kila mwisho wa mwezi. Je, Serikali inasema VIP namna ya kufidia vipindi hivyo ili wanafunzi wasije wakapoteza vipindi ambavyo wanastahili kuvipata kwa kila mwaka? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB): Mheshimiwa Spika, bila shaka walimu ni wajuzi na wanajua namna ya kupanga ratiba

zao, anajua kama leo nimekosa kipindi changu au siku fulani, ni vipi ninaweza kukirejea kipindi hiki ili kuwapa haki yao wanafunzi wasikose. (*Makofii*)

Na. 65

Maeneo Wazi (*Open Areas*)

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH aliuliza: -

Kwa kuwa kuna sheria inayosimamia maeneo yaliyoachwa wazi kwenye miji yatumike kwa malengo yaliyokusudiwa, lakini idara zetu za ardhi zimekuwa zinayagawa maeneo hayo kwa kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kusimamia maeneo hayo: -

(a) Je, ni sheria ipi mojawapo inayowapa madaraka ya kuyagawa maeneo hayo kinyume na makusudi yaliyowekwa?

(b) Kama sheria hairuhusu kufanya hivyo, je, kwa nini Serikali isiyarudishe maeneo hayo kama yalivyokusudiwa katika sheria?

(c) Kama yapo maeneo ya aina hiyo ambayo hayajaendelezwa, je, Serikali itakuwa tayari kutoa tamko sasa kwa maeneo haya yarudishwe Serikalini kama yalivyoainishwa kwenye mipango miji ya mikoa husika?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna sheria yoyote inayotoa madaraka ya Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya au Mamlaka nydingine yoyote kugawa au kuyamiliki maeneo ya wazi kwa mtu au Taasisi yoyote. Endapo itabidi kufanya hivyo, hapana budi halmashauri husika kuwasilisha mabadiliko ya matumizi ya ardhi kwa Waziri wa Ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji na Vijiji, sura namba 378 ya mwaka 1956 ili aidhinishe maeneo ya wazi kutumika kwa shughuli nydingine. Vinginevyo, maeneo ya wazi hayatakiwi kuvamiwa na yanatakiwa yatumike kwa malengo yanayokusudiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa maeneo yanayovamiwa au kutolewa kinyemela, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya tutahakikisha kuwa wavamizi wanaondolewa kwa mujibu wa sheria za ardhi ili maeneo ya wazi yatumike kadri inavyokusudiwa.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ya wazi ambayo hayajaendelezwa ni dhahiri kuwa yako mikononi mwa Serikali. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya zimekwishachukua hatua za kukagua, kutambua na

kutangaza baadhi ya maeneo ya wazi kwenye gazeti la Serikali ili yalindwe kisheria. Kwa mfano, baadhi ya maeneo ya wazi yametambuliwa katika Miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Njombe, Mbeya, Musoma, Morogoro, Mbarali, Moshi na miji mingine. Pia, Wizara imeagiza Halmashauri zingine kuendelea kuyatambua maeneo ya wazi na kuwasilisha taarifa Wizarani ili yatangazwe kwenye Gazeti la Serikali na kutambuliwa kisheria.

(d) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kutoa elimu kwa umma ili utambue kuwa maeneo ya wazi hayamaanishi kuwa hayana wenyewe, bali ni ya wanajamii wote wanaoyazunguka na wanaotoka nje ya Halmashauri husika.

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nashukuru kwamba Serikali imekiri kwamba yapo maeneo ambayo yamevamiwa na sheria hairuhusu jambo kama hilo.

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri utakubali ushauri wangu, sisi Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yetu kama tunabaini yapo maeneo hayo tukuorodheshee ili uyafanyie kazi kwa uhakika zaidi?

(b) Serikali kwa maana ya Wizara ya Ardhi inaweza ikatupa *time frame*, ni muda gani itatuletea taarifa hapa Bungeni kutupa uhakika ni maeneo mangapi ambayo ni ya wazi yamekwisharudishwa na iko mikononi mwa mipango miji ya maeneo hayo ili tuweze kupata taarifa sahihi? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: (a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana sana na ushauri wa Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge wote mtusaidie kubaini maeneo ya wazi yaliyovamiwa na vile vile kama mtayaona mtusaidie pia kuwashauri na kutoa elimu kwa wananchi kuwa maeneo hayo yamepangwa kwa shughuli maalum.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili napenda kusema kuwa kutoa muda kamili kwamba tutakupa jibu kwa muda fulani, hiyo haitakuwa rahisi. Lakini naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali imeshatambua wananchi wamekiuka mipaka, wamevamia maeneo mengi na wanapofuatwa wanakuwa wakali sana. Sasa Serikali itakuwa kali mara mbili. Nawatangazia wote waliojiandaa au wako kwenye maeneo ya wazi waanze kuondoka maana tunayabaini na kazi inaanza mara moja. (*Makofî*)

SPIKA: Kabla sijamuita Mheshimiwa anayeuliza swali linalofuata, nimepewa taarifa na vyombo vya habari, wanaorekodi picha na mazungumzo yetu kwamba kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaacha vinasa sauti (*microphone*) wazi hata kama hawachangii chochote. Kwa taarifa yenu ni kwamba wale ambao wamefanya hivyo baadhi ya mazungumzo hayo ambayo mengine siyo rasmi na wala hayawezি kutangazwa

vijana wameyanasa na haipendezi, wanajisikia vibaya kusikiliza maneno ya Waheshimiwa Wabunge ambayo mengine si rasmi. (*Kicheko*)

Na. 66

Shirika la Nyumba la Taifa

MHE. JANET B. KAHAMA: Honourable Speaker, I wish you happy Valentine's day, you and your wife and your family and I wish Members of Parliament also happy Valentine's day. (*Makofi*)

(a) Je, ni lini Shirika la Nyumba la Taifa (*National Housing Corporation*) litaweka utaratibu rasmi wa kujenga nyumba za kuishi na kuwauzia wananchi wa Tanzania wa rika zote?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni jambo la busara kuunganisha shughuli za Shirika la Nyumba la Taifa na zile za Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*NHBRA*) ulioko chini ya Wizara ya Miundombinu kusudi utsalamu wa kujenga nyumba uwe chini ya kiangozi mmoja na hivyo kuweza kuwa na michoro ya kisasa na inayopendeza kama ilivyo kwa nyumba zilizojengwa na *NSSF* na kadhalika?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria namba 2 ya mwaka 1990 iliyounda upya Shirika la Nyumba la Taifa na kufanyiwa marekebisho mwaka 2005, Shirika la Nyumba la Taifa linajiedhesa kibashara.

Majukumu yake ya msingi ni kujenga nyumba au majengo nchini kote kwa madhumuni ya kupangisha na kuuza kwa watu binafsi, Taasisi za Umma na binafsi na kusimamia miliki ya majengo ya Shirika (*Estate Management*) ikiwa ni pamoja na matengenezo na utunzaji wa nyumba au majengo hayo. Shirika hili limekuwa halipati ruzuku Serikalini hivyo linaendesha shughuli zake kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kutekeleza jukumu la kujenga nyumba za kuishi nchini kwa kutumia mtaji uliopo, Shirika limekuwa likijenga nyumba za kuuza kwa kulenga miji ambayo lipo soko la uhakika. Kwa kiasi kikubwa Shirika limekuwa linawahudumia wateja wenye kipato cha juu na cha kat. Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, Shirika limejenga nyumba katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha kama ifuatavyo: -

Dar es Salaam nyumba 69, Tabata nyumba 21 na maduka 21Keko, nyumba 8 Ilala, nyumba 191 Boko na nyumba 24 *Mbezi beach*. Mwanza Shirika limejenga nyumba 3 *Capri Point* na nyumba 8 Isamilo. Arusha zilijengwa nyumba 7 eneo la Kijenge. Kwa

sasa Serikali inaandaa mfumo utakaowezesha wananchi katika makundi yote kupata mikopo kwa ajili ya kununua au kujenga nyumba. Pia, mfumo huu utawezesha shughuli za Shirika kupanuka na kuwafikia wananchi walio wengi. *(Makofî)*

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuunganisha shughuli za *National Housing Cooperation* na Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vyta Ujenzi (*National Housing Building Research Agency*) kwa kuwa kila chombo kimeundwa kwa malengo na madhumuni maalum kama ilivyofafanuliwa na sheria zilizoanzisha vyombo hivyo.

Shirika la Nyumba la Taifa liliundwa chini ya sheria namba 2 ya mwaka 1990 na Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vyta Ujenzi (*National Housing and Building Research Agency*) ulianzishwa kwa sheria ya Wakala wa Serikali namba 30 ya mwaka 1997.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, bado nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria hiyo ni ya miaka mingi iliyopita, hivi haiwezi ikaangaliwa? Kwa sababu ukiangalia nyumba ambazo ziko *Area D* za ghorofa ambazo Waheshimiwa Wabunge wengine wanaishi, kwanza zilijengwa chini ya *National Provident Fund*, halafu zikaja zikawa chini ya *NSSF* halafu sasa Ujenzi. Halafu zimejengwa tena nyumba chini ya Wakala wa Serikali ambazo ziko eneo la Kisasa, je, Serikali haioni kwa kuunganisha nyumba hizi zote kutakuwa na ubora mzuri sana wa majengo ambao unaendana na *century* hii ya 21? *(Makofî)*

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba swali lako liliandikwa kwa makosa, nadhani unaongelea *National Building Agency* iliyo chini ya ujenzi na swali limeonyesha umeongelea juu ya Kitengo cha Utafiti kilichopo chini ya Wizara yetu. Pamoja na hayo, mawazo yako ni mazuri na tutayatazama kama Serikali na kukupa majibu husika. *(Makofî)*

Na. 67

Mapato Yatokanayo na Dhahabu

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikipata mapato ya nje moja kwa moja yatokanayo na dhahabu:-

(a) Je, ni kiasi gani kilichopatikana kuanzia mwaka 2000 - 2005 kila mwaka kutokana na ubia na mrabaha?

(b) Je, ni nini maoni ya Serikali katika kuongeza mapato yatokanayo na dhahabu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu: -

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imekuwa ikipata mapato ya moja kwa moja kutokana na mauzo ya dhahabu ikiwemo mrabaha. Mrabaha huo hulipwa kwa Serikali kutokana na Serikali kupoteza au kuruhusu sehemu ya maliasili yake (madini) kutumika. Kwa mujibu wa kifungu namba 86 cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998, mrabaha hulipwa kwa kuzingatia *netback value* ambayo ni thamani halisi ya madini husika baada ya kuondoa gharama za usafirishaji na usafishaji (*insurance - freight and refining costs*). Aidha, viwango vya malipo hutofautiana kati ya aina moja ya madini na nyingine. Madini ya vito yasiyokatwa na almasi hutozwa asilimia 5 na madini mengine yote ikiwemo dhahabu hutozwa asilimia 3.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2004, Serikali ilipata jumla ya Dola za Marekani 54,765,462 kama mrabaha utokanao na mauzo ya madini ya dhahabu yanayochimbwa na makampuni makubwa tu. Mwaka 2000 Dola za Marekani 3,256,249.4, mwaka 2001 Dola za Marekani 6,162,385.5, mwaka 2002 Dola za Marekani 10,213,267.9, mwaka 2003 Dola za Marekani 15,304,667.7, mwaka 2004 Dola za Marekani 19,828,891.1. Jumla ikiwa Dola za Marekani 54,765,462. Aidha, katika kipindi hicho hicho, jumla ya Dola za Marekani 158,601,141.68 zilizokusanywa kutokana na kodi mbalimbali ikiwemo kodi ya zuio, *payroll levy*, *Veta levy* na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Spika, maoni ya Serikali juu ya namna ya kuongeza mapato yatokanayo na dhahabu ni kutunga na kutekeleza mikakati ya kuongeza uzalishaji wa madini ya dhahabu. Hii inawezekana kwa kuendelea kuainisha maeneo mapya ya dhahabu, jambo ambalo kwa sasa linafanyika kupitia Taasisi zake za *Geological Survey of Tanzania* na Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*).

Mheshimiwa Spika, njia nyingine ni kwa kupanua wigo wa kodi ili kuwa na vyanzo vingi vya kodi. Kwa mfano, kuwa na migodi mingi au kuongeza *linkages* kwa kutoa huduma mbalimbali zinazohitajika migodini (*service supply*). Vile vile mkakati mwingine ni kuongeza usimamizi katika ukusanyaji wa kodi. Jambo hili limeshaanza kufanyiwa kazi ambapo mnamo Juni, 2003 Serikali iliteua Kampuni ya *Alex Stewart (Assayers) GBC* kutoka Marekani kufanya kazi ya ukaguzi wa uzalishaji na usafirishaji wa dhahabu na ukaguzi wa gharama za uwekezaji na uendeshaji katika migodi mikubwa ya dhahabu. Ukaguzi huu utasaidia kujua thamani halisi ya dhahabu inayozalishwa na pia gharama halisi za uwekezaji na uendeshaji wa mgodi kwa lengo la mgodi kulipa kodi zinazostahili kwa Serikali. (*Makof*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika swali langu la kwanza niliulizia ubia na mrabaha. Nimejibowi sehemu ya mrabaha, lakini sehemu ya ubia sikujibowi kabisa kwa sababu Serikali inao ubia katika baadhi ya makampuni hata kama ni asilimia ndogo. Je, kwa nini Serikali haikunijibu hilo?

Pili, kwa kuwa Serikali iliunda Tume kuchunguza mapato yanayotokana na dhahabu baada ya Wabunge katika Bunge lako Tukufu kupiga kelele sana, je, Serikali kwa nini imeshindwa kutoa taarifa hiyo hadi leo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ubia, kwa hivi sasa Serikali ina ubia na Kampuni moja tu ambayo inachimba madini ya dhahabu hapa nchini Tanzania. Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ina ubia wa asilimia 50 na Kampuni ya *TRIENNE* ya Afrika Kusini katika Kampuni ya MEREMETA inayoenadesha mgodi wa Buhemba. Katika makubaliano ya Mkataba wa ubia, faida yote inayopatikana kutohana na mapato ya dhahabu inayochimbwa Buhemba ni kwa ajili ya kuimarisha Jeshi la Ulinzi. Mgodi wa Buhemba umeanza uzalishaji mwaka 2003 ambapo umezalisha dhahabu na fedha kama ifuatavyo:-

Mwaka 2003 dhahabu *Troy ounces* 75,543 yenye thamani ya *US Dollar* 27,999,226. Fedha *Troy ounces* 7,114 yenye thamani ya *US Dollar* 36,651,000 na mwaka 2004 dhahabu *Troy ounces* 82,869 yenye thamani ya *US Dollar* 33,985,150 na fedha 61,204,000.

Serikali iliwahi kuwa na ubia katika Kampuni ya *Kahama Mining Cooperation* iliyokuwa inamili kiwa na Bulyanhulu, lakini asilimia 5 ambayo ilikuwa inamili kiwa na Serikali ilinunuliwa na Kampuni ya *Barrick* mwaka 1999. (*Makofit*)

SPIKA: Swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa. Ama arudie?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Naomba arudie swali la pili.

SPIKA: Tafadhali Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, namsamehe. (*Kicheko*)

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa mapato yote ya fedha ya mrabaha ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyataja ambayo yametolewa tangu mwaka 2000 mpaka 2005 yamekwenda kwenye Serikali Kuu, lakini kwa kuwa machimbo haya ya dhahabu yako chini ya ardhi ambayo ni ya Halmashauri ya Wilaya na kwa kuwa machimbo haya au migodi hii hailipi kodi au ushuru wowote kwenye Halmashauri.

Je, Serikali iko tayari kutoa angalau *percent* fulani ya huo mrabaha kwa ajili ya Halmashauri au kuanzisha kodi kiasi fulani kwa ajili ya kulipia ardhi ambayo inatumia na wachimbaji wa migodi hii? (*Makofit*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, suala la mapato yatokanayo na madini limekuwa na mjadala hadi kufikia Serikali kuunda Kamati ambayo aliiteua Waziri Mkuu mwaka juzi. Taarifa imetolewa na Serikali imejiandaa kuifanyia kazi taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, ni kwamba kila nchi ina utaratibu wake. Hapa sisi suala la mapato na ukusanyaji wa mapato ni suala ambalo linaendana na mfumo wa Serikali tuliokuwa nalo kwamba tunapeleka mapato katika chungu kikuu cha Taifa Hazina na Hazina inagawa mapato hayo kila sehemu inayohusika katika nchi yetu. Sisi hatuna sera ya Majimbo hapa nchini ambayo kutokana na sera hiyo katika maeneo mengine duniani mapato ya madini huwa yanagawiwa kwanza katika maeneo yale yanayotoka madini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Rais amekwishawahi kusema sisi hapa hatuna sera ya Majimbo na ni sera ambayo ina athari zake. Sasa hii haina maana kwamba hatuwezi kufanya kazi nzuri zaidi katika kujihakikishia mapato kutokana na madini na ndiyo maana Serikali imechukua hatua ya kuunda tume kutafakari taarifa hii na baadaye tuone namna gani tunaweza kuongeza mapato kwenye sekta ya madini na kazi hiyo tutaifanya. (*Makofî*)

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba Mpanda ni mionganoni mwa maeneo ambayo yana dhahabu. Sasa ili kuongeza mapato ya Serikali, Serikali itawasaidia vipi vijana kuweza kutupatia ajira ya kujajiri kwa kuapelekeea vifaa wachimbaji wadogo wadogo kule Mpanda? (*Makofî*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, kama ifuatavyo:-

Kwanza, maeneo mengi nchini yana madini na labda tutakachofanya Wizarani kwa kuwa Bunge hili ni jipya ni kuchapisha upya vitabu vile vinavyoonyesha madini karibuni katika kila Wilaya na kuvigawa kwa Waheshimiwa Wabunge wote. (*Makofî*)

Lakini la pili, suala la ajira na kuongeza ufanisi wa wachimbaji wadogo wadogo. Kama nilivyosema awali wakati nawahutubia Waheshimiwa Wabunge kutoa mada pale *Ubungo Plaza* ni kwamba ni jambo ambalo tunalifanyia kazi hivi sasa, katika sura mpya kabisa ili tuhakikishe kwamba katika zile ajira ambazo Chama chetu cha Mapinduzi kimeahidi katika Ilani yake ya uchaguzi, je, sekta ya madini itatoa kiasi gani. Nilisema pale *Ubungo Plaza* kwamba tunaifanyia na tayari tume maalum tumeiunda ikiwa chini ya *STAMICO* kuhakikisha kwamba wanatoa kipaumbele katika kuongeza ajira kwa vijana, taarifa ya awali imeshatolewa na itatolewa taarifa kamili kabla Bunge la mwezi Aprili na kazi hiyo tunaifanya hivi sasa. (*Makofî*)

MHE. GRACE S. KIWELU aliuliza:-

Kwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne, katika kampeni zake za kuwania nafasi hiyo, alionyesha azma yake ya kutoa ajira kwa vijana na wananchi:-

Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge hatua na mikakati iliyokusudiwa na uongozi wa Awamu hiyo ya Nne katika kutimiza azma na ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwapatia vijana na wananchi ajira?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imekusudia kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na suala la upatikanaji wa ajira kwa vijana na wananchi, mikakati ifuatavyo inaandaliwa na Serikali.

(a) Kwa kutambua kuwa suala la ajira ni suala mtambuka (*cross cutting*), Wizara yangu imekwisha bainisha maeneo ambayo yatazalisha ajira kwa wingi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika sekta rasmi na isiyo rasmi. Maeneo hayo ni pamoja na kilimo, uvuvi, madini, utalii, ujenzi, biashara na utumishi wa umma.

(b) Kwa upande wa kilimo Serikali itahakikisha:-

(i) Upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa bei nafuu unasimamiwa vizuri.

(ii) Aidha, unaandaliwa utaratibu wa upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa vijana na wananchi ili waweze kujajiri wao wenyewe. (*Makofî*)

(iii) Zaidi ya hayo, Selikali itahakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa mazao ghafi na yasiyosindikwa yanapatikana kwa urahisi.

(iv) Zaidi ya hayo kusaidia kuimarishwa kwa Vyama vya Ushirika pamoja na vyama vya kuweka na kukopa *SACCOS*. Tunaamini kuwepo kwa mazingira hayo, tunaamini yatavutia vijana na wananchi wengi kujishughulisha na kilimo na biashara na hivyo kujihakikishia ajira. (*Makofî*)

(c) Kwa upande wa sekta ya madini, Serikali itawahamasisha wananchi kuijundia vyama vya kuweka na kukopa ili kuwasaidia kupata mitaji ya kuchimba, kuyasafisha na kuyakata madini ili hatimaye yawefe kupata bei nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la ajira litakuwa katika miradi mingi ya uwekezaji ambayo tunazidi kuivutia kuja Tanzania. Mwaka 2005 nchi yetu ilivutia wawekezaji wengi kuliko nchi zote za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Serikali ya Awamu ya Nne itajenga juu ya msingi huu mzuri kuvutia wawekezaji wengi zaidi. Vitega uchumi katika eneo hili vinakadiriwa kuwa chanzo cha ajira mpya laki mbili na nusu kwa mwaka 2006 - 2010. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na mikakati ya kuimarisha na kutoa mafunzo ya ustadi za kazi mbalimbali kama vile useremala, uashi, ufundi magari, ufundi wa umeme, upishi, huduma za mahoteli na ushonaji ili wahitimu wamalizapo mafunzo hayo waweze kuajiriwa katika sekta za umma, sekta za binafsi au waweze kujiajiri wenyewe wao. Aidha, Serikali inalenga kuwawezesha wataalamu wasio na kazi kuanzisha miradi ya kujiajiri katika fani zao.

Mheshimiwa Spika, mwisho pamoja na mikakati yote hii, Wizara yangu itaendelea kuimarisha na kuboresha kituo cha ajira kilichopo Dar es Salaam ili kiendelee kutoa huduma kwa wananchi wengi zaidi na pia itapanua huduma hizo kwa kufungua vituo mbalimbali Mikoani, tukianzia na Mkoa wa Mwanza kwa mwaka ujao wa fedha 2006/2007. (*Makofî*)

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa makampuni mengi yamebinafsishwa na mengi yamechukuliwa na wageni kutoka nje na wageni hao wameajiri wafanyakazi wengi kutoka nje. Je, Serikali itafanya nini ili kuhakikisha wazawa wanapata ajira katika makampuni hayo? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO): Mheshimiwa Spika, maeneo na mashirika mengi yaliyobinafsishwa mengine yamesaidia kutoa ajira zaidi kwa vijana wetu. Yale maeneo ambayo yanamilikiwa na wageni Wizara yetu kama nilivyosema ni Wizara mtambuka tutaendelea kufanya kila linalowezekana kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanapata ajira katika maeneo rasmi na yasiyokuwa rasmi. (*Makofî*)

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majambazi sasa wanatumia silaha kali katika kufanya ujambazi na kwa kuwa vijana wengi wa Kimasai wameingia katika Miji Mikuu kwa ajili ya ulinzi na wanatumia silaha za jadi katika kulinda. Je, Serikali haiioni kwamba hizi jitihada zake za kuongeza ajira ya vijana sasa itaathirika kwa sababu majambazi hayo yanatumia silaha kali na wananchi wetu hawa vijana wanatumia rungu na sime katika ulinzi?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO): Mheshimiwa Spika, suala la majambazi kutumia silaha za kisasa ni tatizo la muda kwa sababu majambazi hayawezi kuwa badala ya vyombo vyaa ulinzi na usalama. Nasema ni tatizo la muda na dawa yake iko jikoni, baada ya muda si mrefu haya majambazi yatapata salama zake. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. CHACHA Z. WANGWE: Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo ya Naibu Waziri, kwamba Serikali ina mpango wa kuongeza ajira ya vijana na pia ametaja kwamba ajira hiyo itaongezwa katika sekta ya madini vile vile.

Sasa ningependa kuuliza kwamba Serikali ina mpango wa kuwarudishia vijana wa Tarime waliokuwa wanajihuisha na uchimbaji wa madini hadi hapo maeneo waliyokuwa wakiyatumiya yalipochukuliwa kinyume cha sheria na Waziri wa Madini aliyejekuwepo mwaka 1999 na kupewa Kampuni kubwa ya machimbo huku sheria ya madini inaeleza bayana ya kwamba uchimbaji mkubwa wa madini utakwenda sambamba na uchimbaji mdogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwarudia eneo hilo ili waendelee kujajiri wachimbaji wadogo wadogo? (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge na hata Mheshimiwa Mbunge nadhani atafurahi apate majibu kamili, kama swali hili lingeelekezwa kwenye Wizara ya Nishati na Madini kwa maandishi. Kwa hiyo, una nafasi ya kufanya hivyo Mheshimiwa Mbunge. (*Makofii*)

Na. 69

Askari Kupatiwa Vifaa vya Kujikinga

MHE. MHONGA S. RUHWANYA aliuliza:-

Kwa kuwa askari ni watu muhimu sana kwenye jamii yoyote hasa katika kupambana na maovu; na kwa kuwa askari wawapo katika majukumu yao kikazi hawapatiwi vifaa vya kujikinga na risasi za moto. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia askari hao vifaa vya kujikinga na risasi (*bullet proof*) pindi wanapokuwa kwenye harakati za kuwasaka majambazi au katika operation inayohatarisha maisha yao?

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA alijibu:

Kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kunateua kuwa Mbunge, pia kunateua kuwa Naibu Waziri na leo kuweza kusimama hapa. Aidha, nitoe pongozi zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuweza kufanikiwa kuwemo katika Bunge hili Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba askari wetu wanapokuwa katika operesheni za kuwasaka majambazi maisha yao yanakuwa hatarini.

Kutokana na umuhimu wa vifaa hivyo vya kujikinga, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inatarajia kununua vifaa hivyo, *bullet proof vests* na *bullet proof helmets* katika mwaka wa fedha 2006/2007. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Jeshi la Polisi linaendelea kutoa mafunzo maalum ya kupambana na uhalifu kupitia vyuo vyake vya hapa nchini na baadhi ya askari wamepata mafunzo nje ya nchi ili kujifunza mbinu za kisasa za kupambana na uhalifu na ugaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutokuwepo kwa vifaa vya kutosha Jeshi la Polisi litaendelea kupambana na majambazi kwa nguvu zetu zote. (*Makofi*)

MHE. MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na ametupa muda kamili kwamba lini wataanza kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuboresha mazingira yao ya kazi na kuwapa vifaa vya kazi, je, Serikali haioni umuhimu pia wa kuboresha makazi yao kwani wao ndiyo wanaolinda raia na mali zetu? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu sana wa kuboresha makazi ya polisi hapa nchini na sasa hivi kazi hii inafanywa kwa kishindo kikubwa sana. (*Makofi*)

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri kasema kwamba vifaa hivyo ataagiza katika mwaka huu wa fedha. Kwa muda huu tunaosubiri kwani hawezি kushirikiana na Jeshi la Wananchi wakapata vifaa hivyo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari fedha zimetengwa kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya kununua vifaa hivyo naomba Mheshimiwa Mbunge asubiri na kazi hiyo itafanya vizuri. (*Makofi*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa kuhusiana na vijana wetu wa Jeshi la Polisi. Katika majibu yake ameellezea habari ya mafunzo mazuri ambayo vijana wetu wa Jeshi la Polisi wanapata katika vyuo mbalimbali. Swali langu linahusiana na masharti ya vijana wanaojunga na vyuo kwa ajiri ya mafunzo, sharti mojawapo linahusiana na urefu wa kijana anayeruhusiwa kujiunga na Jeshi hili. Je, Serikali haioni kwamba sharti hili linabagua baadhi ya Wilaya zenye watu wafupi? (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, swali la msingi lilihusu namna ya kuwahami vijana wetu askari dhidi ya silaha mbalimbali ambazo zinazoweza kupenya miili yao, hili swali kuhusu ufupi au urefu kwa askari watarajiwa naona ni jipya na litengewe siku maalum labda liulizwe. (*Makofi/Kicheko*)

Malalamiko ya Askari Polisi Zanzibar

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR aliuliza:-

Kwa kuwa yapo malalamiko ya Askari Polisi Zanzibar juu ya kucheleweshwa na hata wakati mwingine kukosa kabisa fedha za posho zao za kusimamia ulinzi katika Taasisi nyingine kama vile Tume ya Taifa ya Uchaguzi na usimamiaji wa usambazaji mitihani vituoni:-

(a) Je, Serikali inayo taarifa kuhusu jambo hilo?

(b) Kama Serikali inayo taarifa juu ya tatizo hilo, je, imechukua hatua gani dhidi ya Taasisi husika au Ofisi yoyote inayohusika na malipo hayo?

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Jeshi la Polisi ni kusimamia usalama wa raia na mali zao na kuhakikisha shughuli za Serikalii na zile za kijamii zinafanyika katika mazingira ya amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwalipa posho askari wanaosimamia ulinzi katika Taasisi nyingine kama vile Tume ya Taifa ya Uchaguzi na usimamiaji wa usambazaji wa mitihani ni utaratibu ambao unatawaliwa na Taasisi husika kulingana na makubaliano/mikataba iliyopo, hivyo posho za askari hulipwa na Taasisi husika kulingana na makubaliano au mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina taarifa rasmi juu ya malalamiko ya askari polisi walioko Zanzibar juu ya kutolipwa au kucheleweshwa fedha za posho zao za kusimamia ulinzi katika baadhi ya Taasisi zikiwemo Taasisi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara yangu haikuwa na taarifa rasmi ya tatizo hilo huko Zanzibar kama nilivyojibu katika swali (a) hivyo Wizara haikuchukua hatua dhidi ya taasisi husika. Lakini inawezekana kuwa kuna baadhi ya Taasisi hazikulipa au zimechelewesha malipo bila ya Wizara kuwa na taarifa rasmi hivyo napenda kutoa wito kama wapo askari waliokuwa hawajalipwa posho zao na Taasisi husika, wawasilishe majina yao kwa viongozi wao na hatimaye yaweze kuwasilishwa kwa Inspekte Jenerali wa Polisi kwa ufuatiliaji ili Askari wapate malipo yao.

Mheshimiwa Spika, iwapo itabainika kuwepo kwa mapungufu katika makubaliano na mikataba hiyo basi Wizara, itachukua hatua mahususi ili askari wetu wasipate usumbufu wa kucheleweshewa malipo yao. Aidha, kama zitakuwepo Taasisi ambazo hazijafanya malipo tutazifua tilia kufanya malipo hayo mara moja ili kuondoa usumbufu kwa askari wetu. (*Makofi*)

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, kutokana majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hizi Taasisi nilizozitaja zimefanya tendo hilo katika Mkoa wetu wa Kaskazini hazijalipa na taasisi au mtu yejote ambaye anakiuka mikataba au anakwenda kinyume na masharti waliyokubaliana anaadhibiwa.

(a) Je, taasisi kama hizi kama hazijalipa wanapata adhabu gani za kutowalipa hawa Askari wetu?

(b) Kuna posho za kisheria ambazo askari wetu hawajalipwa kama posho za uhamisho, upandishwaji wa vyeo na hili Mheshimiwa Naibu Waziri, je, analifahamu na kama halifahamu wanalifuatilaje? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kwa sababu hatuna taarifa rasmi za watu hawa za kulipa na kutolipa na kama nilivyosema kwamba ikiwa wapo ambao hawajalipa Wizara itachukua hatua kuhakikisha kwamba malipo hayo yanafanyika. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira ili tufuutilie kwa ukaribu zaidi kuhakikisha kwamba askari wetu wanapata malipo yao. (*Makofi*)

Kuhusu posho na malimbikizo mengine ninazo taarifa hizi na si kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja peke yake bali ni kwa Tanzania nzima na hatua zinachukuliwa kurekebisha hilo. Hivi sasa askari wanadai zaidi ya shilingi bilioni 8 kwa ajili ya posho na uhamisho na shughuli zingine. Kwa hiyo, naomba tuwe na subira ili kuhakikisha kwamba hatua kwa hatua tunamaliza tatizo hili. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali sasa yamekwisha. Naomba mnivumilie kwa matangazo yafuatayo ambayo ni muhimu.

Kwanza kabisa tutakuwa na Semina ya Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Parliamentary Association*) kuanzia Jumatatu tarehe 20 hadi Jumatano tarehe 22 Februari, 2006. Hii ina maana Wabunge waliojipangia kuondoka mwisho wa wiki pengine wazingatie hili kwa sababu semina hii ni muhimu inajumuisha kwanza wataalam kutoka nchi mbalimbali.

Baadhi ya watoa mada ni Mheshimiwa Denis Masher, Katibu Mkuu wa *Commonwealth Parliamentary Association* kutoka London, *Miss Deborah Della* kutoka Ontario, Bunge la Canada na Mheshimiwa Neil Jimson Mkurungezi wa Mipango ya Maendeleo Makao Makuu ya CPA.

Pia tutakuwa na wageni kutoka Mabunge rafiki ya Zambia na Kenya. Mada zenyewe kwa kawaida semina hii inaitwa *Post Election Seminar* yaani tunagawana, tunachangia uzoefu na wenzetu kutoka Mabunge mbalimbali nini hatma ya mambo baada ya Uchaguzi Mkuu. Kwa hiyo, nasihi sana Waheshimiwa Wabunge, muiweke kwenye mipango yenu. Gharama zote za malipo zinafahamika na zitashughulikiwa kama kawaida. (*Makofii*)

Kuna Mikutano ya Kamati kama ifuatavyo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ikutane chumba namba namba 219 baada ya kipindi cha Maswali na Majibu, Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira ikutane chumba namba 432 saa 5.00 asubuhi, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ikutane chumba namba 133 saa 5.00 asubuhi, Kamati ya Fedha na Uchumi ikutane chumba namba 231 saa 5.00 asubuhi. Wabunge wote wa CCM kutoka Zanzibar kutakuwa na Mkutano saa 7.00 mchana chumba namba 432, Kamati ya Kilimo na Ushirika wakutane chumba namba 428 saa 7.00 mchana na *The Tanzania Parliamentary Association of Population and Development* wakutane ukumbi wa Bunge watabaki hapa saa 7.00 mchana.

Sasa pamoja na matangazo haya nilikuwa nataka kuwataarifa Waheshimiwa Wabunge kwamba utaratibu wa kujibu hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa muda huu uliobaki utahusisha Waheshimiwa Wabunge walio upande wa Serikali. Sasa wakati huo huo Wenyeviti wameita Kamati nyingi lakini kipindi hiki cha saa 4.30 asubuhi hadi saa 7.00 mchana majibu mengi ya hoja ambazo mmezitoa Waheshimiwa Wabunge, ndiyo yatatolewa. Kwa hiyo, ningekuwa nimetafakari vizuri zaidi mapema na Wenyeviti ningewaomba Kamati zikutane baada ya saa 7.00 mchana. Lakini sasa ninawaachia wao kwa sababu ni uhuru wao. Majibu yatakuwa yanatolewa wakati Waheshimiwa Wabunge wengi hawamo ndani ya ukumbi.

Kwa mpangilio ili Waheshimiwa Mawaziri wafahamu tu nimepewa orodha hapa, Waziri wa Usalama wa Raia ataanza saa 4.30 asubuhi, Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ataanza saa 4.45 asubuhi, anatafutiwa na Waziri wa Kilimo, Chakula na Masoko, Waziri wa Maji, Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundsi, Waziri wa Miundombinu na saa 6.15 mchana ninavyokisia itakuwa ni Waziri wa Fedha. Baadaye tutamsikia mtoe hoja saa 11.00 Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

KAULI ZA MAWAZIRI

Hali ya Uzalishaji na Usambazaji Umeme Nchini

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Februari, 2006 nilitoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge hapa Dodoma juu ya hali ya uzalishaji na usambazaji umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, hali ya ukame imepelekea kuwepo na upungufu mkubwa wa maji katika mabwawa yanayotumiwa na *TANESCO* kuzalisha umeme. Bwawa la Mtera

lina uwezo wa kuzalisha asilimia 80 au lina uwezo wa kutunza maji ya kuzalisha umeme kwa asilimia 80 hapa nchini, hivi sasa ni maji ya akiba tu, *dead storage* ndiyo yanayotumika kuzalisha umeme baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuidhinisha maji ya akiba yatumike hadi kina kitakapofikia mita za ujazo 687 juu ya usawa wa bahari.

Mheshimiwa Spika, ili kunusuru mfumo wa usafirishaji na usambazaji umeme wa *TANESCO* usisambaratike, Serikali iliidhinisha kuanza kwa mgao mdogo wa umeme, tarehe 4 Februari, 2006. Madhumuni ya mgao wa umeme ni kutumia maji kidogo kidogo yaliyobakia katika Bwawa la Mtera, ili tuweze kufika katika msimu wa Mvua za masika unaotegemewa kuanza katikati ya mwezi Machi, 2006.

Mheshimiwa Spika, mgao ulianza tarehe 4 Februari, 2006 ulikusudiwa kupunguza matumizi ya umeme kwa *MW 60* na ulihusisha mgao wa saa 17 kila siku yaani saa mbili na nusu wakati wa asubuhi na saa nane na nusu wakati wa jioni. *TANESCO* pia iliendelea kununua umeme wote unaozalishwa na *Songas* yaani *MW 190* na *IPTL MW 100*. Hata hivyo kutokana na wateja kuhamisha matumizi wakati umeme unapokuwepo, *TANESCO* ilishindwa kufikia lengo la kupunguza *MW 60* na badala yake iliweza kupunguza wastani wa *MW 40*. Wakati huo huo uzalishaji wa umeme Mtera, umepungua kwa kiwango kikubwa kutokana pia na sababu za kiufundi za jinsi bwawa lilivyojengwa (*Technical Design Limitations*) kwa mfano uzalishaji umepungua kutoka wastani wa *MW 33* mwanzoni mwa mwezi Februari, 2006 hadi kufikia *MW 17* hivi sasa. Aidha, tathimini inaonyesha kwamba mitambo ya Mtera inaweza kusimamia wakati wowote kutokana na ukosefu wa maji kama hatua za ziada za kupunguza matumizi ya maji hazitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, leo Bwawa la Mtera lina mita 687.35 za maji juu ya usawa wa bahari. Ili kunusuru mfumo wa uzalishaji na usambazaji umeme usisambaratike kabisa Serikali imeidhinisha mpango wa *TANESCO* wa kuongeza mgao wa umeme kama ifuatavyo:-

Kwanza lengo ni kupunguza wastani wa *MW 120* katika gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, pili, wateja wa majumbani, biashara na ofisi zilizopo katika maeneo ya kuishi zitakatiwa umeme kwa muda saa 12 kwa siku toka saa 1.00 asubuhi hadi saa 1.00 jioni kila siku isipokuwa siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili ambapo umeme utazimwa kuanzia saa nane mchana hadi saa moja jioni.

Hatua hii imechukuliwa ili kuwawezesha waumini wanaokusanyika kwa wingi katika misikiti na makanisa siku hizo za ibada kufanya ibada zao kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, sehemu za viwanda na biashara kubwa, maeneo nyeti, vyombo vya Ulinzi na Usalama, Hospitali za Rufaa, Benki na *TRA* hazitahusishwa katika mgao wa umeme. Lengo ni kunusuru uzalishaji usiporomoke nchini na hivyo tukakosa umeme kwa upande mmoja na pia tukakosa mapato.

Mheshimiwa Spika, migodi mikubwa ya madini ya Kahama, Mwadui na *Resolute* haitahusika na mgao huo. Migodi mingine mikubwa kama Geita inajitegemea katika

uzalishaji umeme wao. Viwanda na ofisi zinazopata mgao mdogo katikati ya Jiji la Dar es Salaam kutokana na kuharibika kwa *transformer* za Ilala wataendelea na hali hiyo mpaka hapo *transformer* mpya zitakapoanza kazi. *Transformer* hiyo, ambayo inakuja kuchukua nafasi ya *transformer* zilizoharibika iliyonunuliwa kutoka India tayari imewasili nchini na kazi ya kuifunga imeanza. Tunatarajia itakabidhiwa kwa *TANESCO* yaani kuwa *commissioned* na kuanza kazi katikati ya Machi, 2006.

Mheshimiwa Spika, kila mkoa umeagizwa kupunguza matumizi yake ya umeme kwa asilimia 50. Nako huko pia viwanda na biashara zinazoingiza mapato makubwa kwa Serikali hazitahusishwa na mgao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu imekuwa ikikumbwa na matatizo ya uzalishaji umeme mara kwa mara na ili kuondokana na hali hii kabisa siku za usoni Serikali imeamua kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kununua mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya kati ya megawati 60 hadi 100 itakayokuwa mali ya *TANESCO* na kuifunga pale Ubungo na Ilala haraka iwezekanavyo badala ya kuikodisha mitambo hiyo kama ilivyokuwa awali. (*Makofi*)

Pili, kununua na kufunga mitambo ya dharura ya megawati 40 inayotumia mafuta na kuifunga huko Arusha, Mwanza na Moshi kwa ajili ya kuboresha umeme katika maeneo husika yaani *Voltage Stabilization*. (*Makofi*)

Tatu, kuendelea na mpango wa *TANESCO* wa kufunga mtambo wa megawati 45 hapo Tegeta kwa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi kwa kufumia fedha za msaada wa Serikali ya Uhlanzi na fedha za ndani. Kituo kinatarajiwaa kukamilika mwezi Desemba, 2006.

Nne, kufanya maandalizi ya ujenzi wa kituo cha umeme wa gesi hapo Kinyerezi cha ukubwa wa megawati 300 kwa kushirikisha Taasisi za umma za ndani za hapa nchini. Kituo hiki kinawenza kukamilika katika miezi kati ya 12 hadi 18 ijayo.

Tano, kukamilisha majadiliano na mgodi wa Kiwira ambaa utawezesha kuzalisha megawati 200 kwa hatua. Kwanza megawati 50 karibu na mwisho wa mwaka huu, megawati 150 katikati ya mwakani na kufikia kiwango cha megawati 200 ifikapo mwishoni mwa mwakani.

Sita, kuanza sasa kushughulikia miradi mikubwa ya kuzalisha umeme wa Mchuchuma, Ruhuji na *Stiegler's Gorge*, ambayo itakidhi mahitaji ya nchi pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kuuza umeme kwa nchi jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua adha wananchi watakayoipata kutokana na mgao wa umeme. Tahadhari kubwa imechukuliwa ili kupunguza makali ya mgao huu wa umeme na *TANESCO* wameagizwa kuwa waadilifu katika kutekeleza mgao na uongozi wa Shirika hilo umeahidi kwamba utatekeleza kikamilifu zoezi la mgao kwa

makini, ufanisi na uwazi kwa faida ya nchi yetu. Mgao huu utafuati liwa siku hadi siku na kwa kadri itakavyowezekana makali yake yatapunguzwa.

Mheshimiwa Spika, mgao huu mkubwa unatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia kesho Jumatano, tarehe 15 Februari, 2006 hadi hali ya uzalishaji wa umeme itakapoanza kubadilika.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wawaeleze wananchi tatizo la umeme na hatua za dhati ambazo Serikali yao inazichukua sasa kuondokana kabisa na kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

HOJA ZA SERIKALI

Hoja ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Bungeni Tarehe 30 Desemba, 2005

(*Majadiliano yanaendelea*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwanza suala la utunzaji wa mazingira ya bahari, Mtwara-Lindi. Mazingira haya yalikuwa tulivu kwa kipindi cha miaka 1999- 2004 baada ya kufanya kwa *operation* uvuvi haramu mwaka 1999, ambapo wavuvi haramu 300 walijisalimisha na mabomu tani 150 na vifaa vingine *detonators* na kadhalka. Samaki wakaanza kuzaliana na kuwa wengi na watu wakawa wanakula samaki wasio na sumu ya mabomu, maana kabla ya *operation* hiyo, wananchi wa Mtwara na Lindi walikuwa wanakula samaki wenyewe sumu waliovuliwa na mabomu. Lakini sasa tena wavuvi nao wa kutumia mabomu kwa kuwavua samaki wamerudi tena kutumia mabomu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaiomba Serikali iweke angalau katika Mikoa hiyo boti (*speed boat*) itakayozunguka Lindi na Mtwara kufanya *patrol* vinginevyo wananchi hawa, watakuwa wanakula tena samaki wenyewe sumu.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la afya, upande wa wakunga wa jadi. Akinamama wengi hukimbilia kuzalia watoto wao kwa wakunga wa jadi. Hawa wanazalisha vizuri hawadharau mzazi, bei yao ni nafuu labda upande wa kaniki tu na huo karibu na wazazi.

Kwa hiyo, ombi langu ni kuiomba Serikali iweke fungu kwa ajili ya kuwapa semina wakunga wa jadi ya jinsi ya kutumia vyombo ya kisasa na vile vle kutumia kwa uangalifu hivyo vyombo bila kuleta uambukizo. wakunga wa jadi (*TBA*) ni wafanyakazi wazuri ila hawana vyombo. Wasaidiwe asilimia arobaini ya wazazi huzalia kwa wakunga wa jadi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni huo tu. Ahsante sana.

MHE. HEMED MOHAMED HEMED: Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni juu ya hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wakati akizindua Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku ya tarehe 30 Desemba, 2005.

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo na hatimaye kutupa nguvu kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Aidha, niwashukuru wafuatao:-

Moja, wapiga kura wa Jimbo langu kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na kwa hili naahidi kuwatumikia kipindi changu chote.

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu ni kwako wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, fursa ambayo ni ya kihistoria kwangu kwani hii ni mara yangu ya kwanza kuchangia hoja katika Bunge lako Tukufu.

Tatu, ni vema nikatoa shukrani kwa watumishi wa Ofisi ya Bunge walioko Dar es Salaam na hapa Dodoma kwa maelezo na msaada wao ambao kwa kiasi kikubwa umenifanya kupata huduma ambazo kwa kiasi kikubwa kuweza kuhimili maisha ya hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani na pongezi hizo naomba sasa uniruhusu nieleze mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yetu na niende moja kwa moja katika ukurasa wa kumi na nane wa hotuba ya Mheshimiwa Rais katika kuzungumzia Umoja wa Kitaifa amesema kwamba naomba kumnuuu: “Nachukua uongozi wa Taifa letu nikiwa nasononeshwa sana na mpasuko wa kisiasa kati ya Unguja na Pemba na pengine kati ya Pemba na sehemu nyingine za Jamhuri yetu, matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 yanetukumbusha tena mpasuko huo ambao naamini chanzo chake ni cha kihistoria.” Mwisho wa kumnuuu.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Rais Kikwete kusema kweli inatoa mwanya wa matumaini kwani Rais aliyeondoka madarakani Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alisema hivyo hivyo aliposhika uongozi wa miaka kumi iliyopita lakini badala ya kushughulikia matatizo ya Zanzibar alijali zaidi yale ya Burundi, Rwanda na *DRC* hata walipoulizwa watu zaidi ya 50 Kisiwani Pemba mwezi Januari, 2001, Rais Mkapa hakukatisha safari zake za nje na hatimaye aliendelea na safari hiyo kama vile mauaji hayo yalikuwa ya kawaida tu au askari wake waliua kuku au vinyama vilivyokosa thamani.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Rais huyo mstaafu katika kusaini muafaka wa Zanzibar yeye alisema kuwa tatizo la Zanzibar linamyima usingizi lakini kumbe Watanzania walimshuhudia akilala fofofu na kukoroma katika kushughulikia tatizo hilo matokeo yake likaongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo kuhusiana na suala hilo mimi binafsi napata matatizo yafuatayo:-

Kwanza, viongozi wetu wakuu mara nyingi hupenda kusema maneno badala ya kutenda matendo. Kitu ambacho ufanisi wa jambo lolote hukosekana. Kwa mantiki hiyo baada ya kutibu tatizo hupelekeea kutuongezea matatizo kwa hili ni vema viongozi wetu wakabadilika na kuona kuwa kula uhondo kwataka matendo na asie matendo hula uvundo. Kwa hali hiyo tatizo la Zanzibar linahitaji kutatuliwa haraka tena kwa matendo na sio kwa kuchapa maneno kama vile walivyofanya Marais waliotangulia.

Pili, madai ya Rais Jakaya Kikwete kuwa tatizo la Zanzibar ni la kihistoria. Nadhani kauli hii inaweza kupotosha ukweli halisi wa kadhaa hii kwani tatizo la Zanzibar ni la kisiasa linahusiana na chafuzi za chaguzi kuanzia mwaka 1995 - 2005 lililotayarisha na CCM, SMZ, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri kwa kupiga teke maamuzi ya Wazanzibar walio wengi kwa kuwaweka madarakani wagombea kuanzia mwaka 1995 hadi hii leo. Ni dhahiri kuwa Wazanzibar walio wengi kwa kuwaweka madarakani wagombea wa CCM katika chaguzi zetu tatu za Vyama Vingi kuanzia 1995 hadi hii leo.

Ni dhahiri kuwa Wazanzibar chini ya kivuli cha Muungano na demokrasia changa si rahisi kuleta mabadiliko kuitia masanduku ya kura kama mawazo yangu ni kweli basi ni vema tukaziba ufa badala ya kusubiri kujenga ukuta. Busara, hekima, umoja na huruma ya Mheshimiwa Rais ni vema zikatumika haraka iwezekanavyo ili kuinuszur Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika falsafa ile ile ya watani wangu CCM ya ari, nguvu na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nashukuru sana na ahsante.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu sana katika historia ya Bunge lako Tukufu katika nchi yetu. Ikiwa ni mara yangu ya kwanza kabisa katika historia ya maisha yangu kusimama katika Bunge lako napenda kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mikumi na kwa niaba yangu binafsi nachukua fursa hii kuwapongeza viongozi wafuataao, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wake Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa na bila kukusahau Spika, Mheshimiwa Samuel Sitta na Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kwao wote kwa kura nyingi zilizowafanya kushika nyadhifa walizonazo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana pia wananchi wote wa Jimbo la Mikumi kwa kunipa ushindi mnono kuwa Mbunge wao dhidi ya kushindana na wagombea wa Vyama vingine vitano vya *CUF, TLP, CHADEMA, UDP* na *CHAUSTA*. Naahidi kuwa Mbunge endelelevu na makini katika kuwatetea kwa dhati ili sisi sote tufanikiwe kutekeleza mambo na majukumu ya kuinua uchumi wa nchi yetu, kipato cha kila

Mtanzania na kupunguza umaskini, kadri ya maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005.

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii kabla yangu na kuiunga mkono hoja iliyo mbele yetu. Kwanza sina budi kutamka kuwa Mheshimiwa Rais ametoa hotuba yake kwa wananchi na Bunge lako Tukufu kwa ustadi mkubwa sana, ametumia lugha nyepesi, fasaha na yenye mvuto fulani wa aina yake ambao unamfanya yejote aliyemsikiliza, anayeisoma hotuba ya Rais, inamvuta ajione kana kwamba yuko karibu sana na Mheshimiwa Rais kindugu au kirafiki.

Mheshimiwa Spika, kwa njia hii Mheshimiwa Rais amejionyesha kabisa yeye ni kiongozi anayewapenda sana watu na maendeleo yao, amejinyenyekesha kwa watu wote ili awe karibu nao katika kuwatumikia. Mheshimiwa Rais Kikwete ana mvuto wa pekee kwa kila mwananchi na hata watu wasio Watanzania. Kama ni kiongozi basi kweli tumempata.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hoja hii unalenga moja kwa moja katika masuala yafuatayo, hifadhi endelevu ya mazingira ambalo Mheshimiwa Rais amelilia mkazo sana kwa kifupi naiomba Serikali iunde kikundi cha wataalam cha kudumu kutoka Wizara za Maji, Misitu, Nishati, Mifugo, Kilimo, Serikali za Mitaa na Mazingira ili kipewe madaraka ya kupanga utekelezaji, kuratibu na kuunganisha juhudzi za kudhibiti vyanzo vyote vya maji nchini. Vyanzo vyote viwekewe mipaka ambako mtu yejote asivuke huko kwa shughuli yoyote. Umuhimu wa kuwajumuisha wataalam wa Wizara zote hizi ni kwa sababu uharibifu wa vyanzo vya maji na matukio yanayogusa majukumu ya Wizara nyingine zilizotajwa.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai kwa hiyo, naiomba Serikali ipange utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitao kwa Jimbo la Mikumi wakati wa kampeni ili kutatua haraka tatizo la maji. Nitakuwa mstari wa mbele kulifuatilia suala hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kadri ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 ukurasa wa 54 aliaahidi wananchi wa Jimbo la Mikumi ujenzi wa barabara ya lami kati ya Mikumi hadi Kilosa kuelekea Korogwe. Wananchi wanaomba sana ahadi hii itimizwe kwani wamejiandaa vivilyo kukuza uchumi wa kilimo cha mahindi kwa bidii zaidi kwa kuwa silo la bidhaa hiyo na nyingine litakuwa na kuwaongezea kipato katika jamii.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa wananchi wa Jimbo la Mikumi unawenza kufanikiwa haraka kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya kama maeneo ya mashamba makubwa yaliyokuwa na mkonge miaka ya nyuma, yaliyokuwa yanamilikiwa na wafanyakishara binafsi na ambayo yameachwa kuwa mapori yasiyoendelezwa kwa miaka mingi yangepewa wananchi walime. Wananchi hao ndio waliokuwa waajiriwa kama manamba miaka hiyo. Yalipokufa mashamba hayo, walibaki katika maeneo hayo, wamezaliana, hivyo hawana pengine pa kulima isipokuwa katika maeneo hayo. Vijiji husika ni Kwalukwambe, Kilangali, Masanze, Zombo, Mhenda na Ulaya. Naiomba

Serikali ilitazame jambo hili kwa makini ili wananchi waruhusiwe kupewa miliki ya maeneo hayo kwa kilimo cha mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, suala la wachungaji kuhamahama na mifugo yao ameliwekea mkazo sana Mheshimiwa Rais wetu. Ili kulitatu jambo au tatizo hili haraka mimi napendekeza hatua zifuatazo zifikiriwe kutayarishwa na kutekelezwa na Serikali:-

(a) Wachungaji waliopo na wanaomiliki mifugo wote nchini wasajiliwe mara moja katika kila Wilaya au Kata na wazuiwe kuondoka kwenda sehemu nyingine hadi taratibu kamili za kuwatengea maeneo ya malisho zikamilike ikibidi wapewe maeneo ya malisho ya muda wakati maandalizi ya maeneo maalum ya malisho.

(b) Serikali ichukue uamuzi haraka kujenga mabwawa katika kila Kata katika maeneo ya malisho yaliyotengwa. Kisha mpige marufuku kuhamisha kwa mifugo toka sehemu moja hadi nyingine.

(c) Wachungaji wanaomiliki mifugo hawatakubali kubadilika ghafla kuwa wafugaji kwa sababu ya hulka ya binadamu yoyote kukataa mabadiliko kwa tabia aliyoizoea. Kwa hiyo, naishauri Serikali ipange utaratibu wa kuwasafirisha makundi ya wachungaji kwa awamu kutoa maeneo mbalimbali nchini na kuwapeleka *study tour* katika nchi za Afrika ambako ufugaji unatekelezwa kwa mafanikio ili kuwa-*convince* kwa kuona kwa macho yao kuwa ufugaji wanaoshauriwa wautekeleze unawezekana.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kuhusu kuiomba Serikali kufanikisha usambazaji umeme katika maeneo ambayo juhudzi za awali ziliishia katikati kwa kusimika nguzo halafu zikaachwa hivyo kwa zaidi ya miaka mitatu katika Kata ya Mabwerebwere jirani na Kilosa, Kata ya Kilangali (eneo Kivungu).

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kisanga kuna wafadhili - Wataliano (shule ya Msolwa) ambao wako tayari kuungana na Serikali kugharamia ujenzi wa kuunganishwa umeme toka Kilosa au Mikumi hadi Kisanga. Vivyo hivyo Kijiji cha Zombo na Ulaya yapata kilomita thelathini toka Kilosa viko tayari kuunganishwa umeme kwa kuwa wanalima mahindi kwa wingi sana na kuvuna mara mbili na nyakati nyingine hadi mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kuniwezesha kutoa mchango wangu kwa hoja hii ambayo ni chachu ya mawazo na mipango ya kuchochera maendeleo ya nchi yetu. Naiunga mkono hoja hii kwa nguvu zote. Ahsante sana.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuipongeza hotuba nzuri ya Rais iliyolenga sehemu zote muhimu za nchi yetu. Ningependa nichangie sehemu ya hotuba katika kilimo, kama hotuba ya Rais ilivyosema kilimo ni mhimili wa nchi yetu na Mtanzania hatoweza kujikomboa na kupiga hatua kwa kutumia jembe la mkono. Naipongeza nchi yetu kwa kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa kuanzisha Mfuko wa Pembejeo kwa ajili ya kuwakopesha wakulima.

Lakini ukiangalia kwa umakini sana utagundua kuna matatizo ndani ya ukopeshaji kutoka Mfuko huo.

Kwa mfano, mkulima anayelengwa kukopeshwa wengi wao wanaishi Vijijini lakini cha kushangaza benki ambayo imepewa dhamana na Serikali ni *Exim Bank* ambayo ina matawi sita tu nchini na yote yako Miji Mikuu ya nchi yetu. Kila mwananchi anayetaka mkopo huo inabidi atafute kwa shida mahali ilipo benki hiyo kwa vile haifahamiki na wananchi wengi wa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu naiomba Serikali kwa kupitia Wizara ya Kilimo kuangalia upya mpango wake wa kutumia benki moja katika Mfuko huo na sasa itumie mabenki ambayo yapo mpaka Wilayani kwa ajili ya kuwasogezza wananchi wa Vijijini huduma hiyo karibu ya kukopa pembejeo na ukiangalia kwa undani zaidi utagundua wengi wanaokopa si walengwa na tusipokuwa makini na masuala yanayohusu kilimo nchi hii tutakuwa tunapiga kelele za kilimo zisizo na maana bila utekelezaji. Naamini kabisa kama tutaipa ushirikiano Serikali yetu kwa uongozi wa Awamu ya Nne, kuna uhakika wa kufanikiwa katika kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa ujumla kwa wewe, Naibu Spika, Waziri Mkuu na Mawaziri na Manaibu Waziri wote kwa kuchaguliwa na kuteuliwa wa wadhifa zao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliyoitao alipofunga rasmi Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa hotuba nzuri ya mwelekeo mzuri aliouonyesha kwenye hotuba yake. Pia nimpongeze kwa matamshi yake, uchaguzi umekwisha tuungane, tuwe kitu kimoja, tujenge na kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni jambo lisilofichika kwamba kuna baadhi ya viongozi wa Serikali ambao kama Mheshimiwa Rais alivyotamka kwenye hotuba yeke, bado hawajakubali mfumo wa demokrasia ya vyama vingi na hivyo kufanya mambo yanayobagua wananchi kwa maoni yao ya kisiasa au itikadi zao ambayo ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Tanzania (1977) ilivyoainishwa katika kifungu 3(1). Katika hotuba yake alizungumzia suala la rushwa. Ni jambo lililo wazi kwamba Tanzania katika kipindi cha miaka kumi iliyopita tumegubikwa na ulaji rushwa wa kutosha. Tatizo kubwa lilipo kama Mheshimiwa Rais alivyobainisha ni kwamba rushwa imeingia karibu kila mahali na hata kwenye masuala ya uchaguzi ambao Mheshimiwa Rais anadai suala hili linamsumbuua.

Mheshimiwa Spika, ni kweli watu wengi na hasa wafanyabiashara wakubwa wanatoa michago mikubwa kwa ajili ya uchaguzi na kama alivyosema Mheshimiwa Rais tusipokuwa waangalifu, nchi yetu inaweza kuwekwa rehani na watu wenye pesa. Mimi

nashauri kwamba watu wote wenye kuchanga mamilioni ya pesa wachunguzwe na Taasisi ya Kuzuia Rushwa kama inavyofanyika katika Mataifa mengine. Mtu hawesi kuchangia zaidi ya shilingi milioni kumi hivi hivi kama hana lake jambo.

Mheshimiwa Spika, ili vita hii ya rushwa iweze kufanikiwa nashauri mambo yafuatayo:-

Kwanza, nashauri Sheria ya Taasisi ya Rushwa iangaliwe upya ili Taasisi ya Kuzuia Rushwa iwe Taasisi huru zaidi na ipewe uwezo wa kumchunguza mtu yeoyote mwenye wadhifa wowote bila kibali kutoka Ofisi ya Rais.

Pili, nashauri Mheshimiwa Rais awashinikize viongozi wote wanaohusishwa kujihusisha na rushwa wajiuZulu nyadhifa zao kama ilivyo katika nchi nyingine za Jumuiya ya Madola. Mfano, majuzi nchini Kenya tumesoma kwenye vyombo vyahabari kuwa Waziri wa Fedha amejiuzulu kwa kashfa ya Mikataba mibovu.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania tuna Mikataba mingi mibovu kama wa *IPTL* ambapo Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake ameahidi kuangalia upya. Hii Mikataba itaangaliwaje upya wakati walio saini bado wapo madarakani? Suala hili ili liweze kuangaliwa upya na lifanikiwe, nashauri wale wote waliohusika wajiuZulu ili uchunguzi ufaniyiwe kwa uhuru zaidi.

Tatu, nashauri pia Serikali ipitie kwa undani ripoti ya Jaji Joseph Warioba juu ya mianya ya rushwa na namna ya kukabiliana nayo.

Nne na mwisho kabisa, nashauri ili kutokomeza rushwa Tanzania inabidi jamii yote ikiwa ni pamoja na uongozi katika ngazi zote zihusishwe katika haya mapambano. Silaha mojawapo kubwa ni elimu kwa Watanzania kujua haki zao Kikatiba. Ni vizuri basi elimu hii ikaanza katika kaya na hata shule za awali zikiwemo zile na shule za Jumapili kwa watoto wadogo (*Sunday schools*). Mkakati kama huu unaweza kuwakuza watoto katika maadili mazuri kiroho na kimwili na hatimaye kuelewa rushwa ni adui wa haki katika jamii.

Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo. Naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Rais. Ni hotuba nzuri yenye mwelekeo na dira ya nchi. Nawapongeza Mheshimiwa Rais kwa ushindi mkubwa na wote waliochaguliwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuendelea na zoezi la urasimishaji ardhi na nyumba chini ya mpango wa MKUKUTA kwa nia ya kuwawezesha wananchi kutumia hati wakatazopata kuweka dhamana katika vyombo vinavyotoa mikopo ili waweze kutumia fursa hiyo ya mikopo kujiendeza kiuchumi sambamba na kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Spika, tunakabiliwa na tatizo kubwa la uhalifu nchini, nashauri Jeshi la Wananchi wa Tanzania litumike katika mapambano ya sasa na majambazi. Hili si jambo geni kwani huko nyuma limefanyika kwa kupiga vita uvuvi haramu (mabomu) na kufanikiwa sana. Ni vema tukatumia tena utaratibu kama huo na hakika tutashinda vita hii.

Katika eneo la uvuvi eneo ambalo hatujalitumia vizuri rasilimali zilizopo baharini/maziwani na kwenye mito, wakati umefika sasa wa kuanza kutumia rasilimali hii kwa kujenga viwanda vya kusindika samaki kwa lengo la kuuza nje na ndani zao la samaki. Hii itasaidia sana kupata uhakika wa soko kwa wavuvi wetu na vile vile kutoa nafasi za ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, suala la mpasuko wa amani na utulivu huko Zanzibar kutokana na kutokuwa na maadili na uzalendo wa nchi, viongozi wa Vyama vya Upinzani huko Zanzibar ni suala linalosikitisha sana na linahitaji hatua madhubuti zichukuliwe za kisiasa na ulinzi wa nchi. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa ahadi yake ya kulishughulikia hili.

Mheshimiwa Spika, ni vema kero za Muungano zikazungumzwa na Bunge kwa kushirikisha waasisi wa Muungano na wanasiasa mashuhuri. Nashauri pia washirikishwe wote waliotumikia Wizara inayoshughulika na mambo Muungano tangu enzi hizo mpaka sasa. Mazungumzo haya yawe ya faragha, bila kushirikisha vyombo vya habari.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia kuwa na afya njema katika Bunge jipya lenye matumaini mapya kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe binafsi, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa na Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda, kwa nyadhifa nzito mlizopewa, ni imani yangu kuwa mtenda haki kwa wenge haki.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchache wa fadhila kama sikuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati kabisa wananchi a Jimbo langu la Mtambile kwa kunichagua kwa kura nyingi sana, ninawaahidi kupitia Bunge hili Tukufu nitawatumikia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais Jakaya Kikwete ilikuwa nzuri yenyewe kujaa matumaini, lakini tatizo ni utekelezaji. Mheshimiwa Rais alisema Wapinzani wasiwe wepesi kutafuta mchawi kila wanaposhindwa uchaguzi. Lakini jibu ni kwamba Wapinzani kushindwa kwao kunatokana na mazingira mabaya katika ujumla wa mapungufu makubwa katika Katiba yenyewe kama sheria mama.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya mwaka 1977 ya mfumo wa Chama kimoja inayofanyiwa marekebisho bado haikidhi hoja na matakwa ya demokrasia katika mfumo wa vyama vingi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba Katiba ni lazima iandikwe upya ambapo yafanyike yafuatayo, kwanza, kuwepo na mjadala wa Kitaifa unaohusisha wadau mbalimbali kama vile wataalam wa Katiba, Vyama veya Siasa, madhehebu mbalimbali ya dini, wakulima, wafanyakazi, Taasisi zisizokuwa za Kiserikali, wanafunzi, makambi ya jamii kama walemavu, vyama veya wanawake, wazee na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali zote mbili yaani Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hazitakubali kuanzishwa mjadala huo na kuundwa (kuandikwa) kwa Katiba mpya wao watakuwa wanadhihirisha kuendeleza uchawi kwa Vyama veya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, Rais amegusia mpasuko wa kisiasa kati ya Unguja na Pemba na akasema chanzo chake ni historia. Mpasuko huo si wa kihistoria ila ni utashi wa kisiasa wa upande mmoja wa visiwa kuwafanya Wapemba hawana haki ya kuongoza Serikali kwa kisingizio kwamba wao ndio waliopindua na ni lazima waendelee kutawala wao peke yao na kushika nafasi za juu zote za uongozi.

Mheshimiwa Spika, wanaotumia rasilimali na kuwekeza sehemu zote za Jamhuri sio Wapemba peke yao ila taswira inayojonesha ni kwamba Wapemba kuchagua Upinzani ndani ya mfumo wa demokrasia ya Vyama Vingi haikutoa picha nzuri kwa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya CCM.

Mheshimiwa Spika, Wapemba kuchagua Upinzani sio kujitenga kwa mintarafu ya Uchaguzi wa mwaka 2005 bali ni maamuzi ya demokrasia kwani maeneo ndani ya Tanzania Bara ambapo wamechagua Upinzani wao hawakujitenga pamoja na kutumia rasilimali kama wanavyotumia Wapemba, kauli hiyo si sahihi katika azma ya kuwaunganisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iongeze ulinzi katika maeneo mbalimbali kwani majambazi wamewafanya Watanzania wasiamini tena kama nchi hii ni kisiwa cha amani. Naishauri Serikali kuhakiki upya utendaji na ufanisi ndani ya jeshi lenyewe, kuongeza ulinzi mipakani na ushirikishwaji wa wananchi mipakani uongezwe ili kutoa taarifa za uingiaji haramu wa watu, vifaa au zana za doria (magari na kadhalika) ziongezwe na viongozi wa mitaa, watendaji waitwe, waulizwe watu wanaowatilia shaka ndani ya mitaa yao na wakabidhiwe wapelelezi wa Usalama wa Taifa na watoa taarifa kwa majambazi walindwe kwa namna ya siri, kwani wengine hujikuta wakiteswa au kuuawa pale wanapotoa taarifa kwa polisi, wanajiuliza raia wema kulikoni polisi?

Mheshimiwa Spika, pia boti za doria kwenye maziwa ziongezewe zana za kukabiliana na ujambazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwenye kilimo. Kama tunavyojuwa kilimo ndio uti wa mgongo na wananchi wa Tanzania walio wengi wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kwamba nguvu kubwa ipelekwe kwa wakulima kule vijiji ni kwani vijiji ndani kuna wakulima wengi ambao walio wengi hawawezi kulima kwa matrekta bado wana kilimo cha jembe la mkono na wakulima hawa wengi ni wanawake. Wakati umefika sasa wa kuwakomboa wakulima wadogo wadogo kwa kuwapatia mikopo na kuwafikishia mbolea kwa wakati na wataalam wawafikie ili waweze kulima kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye majambazi kwani umekuwa ni mtindo endelevu kwenye nchi yetu. Jeshi la Polisi liwezeshe na liwe Jeshi la kisasa ambalo linaweza kupambana zaidi na majambazi kwani majambazi wanaonekana kujiandaa na uhalifu, Jeshi hili ni jeshi tegemeo kwa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, Jeshi hili liwezeshe kwa mishahara na posho, mafunzo ya kuweza kupambana na majambazi na wapewe vitendea kazi vya kisasa na waweze kukabiliana na hali yoyote inayojitokeza. Jeshi la Polisi kwa kuwa ni jeshi la kulinda raia na mali zao kwa nini kwenye taasisi ya fedha kama benki ambazo raia wanaweka mali zao wasilinde Jeshi hili? Naiomba Serikali iliangular upya tatizo hili na naomba Serikali ilazimishe taasisi hizo ziweze kulindwa na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, wanawake wafanyabiashara wadogo wadogo wanadhalilika sana na baadhi ya taasisi zinazotoa mikopo inakua na riba kubwa, hivyo mfanyabiashara huyu akimaliza kulipa anajikuta hana kitu umaskini umezidi, naomba Serikali kuitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, iweze kutenga fungu kubwa la kuweza kuwakopesha wanawake walio wengi kwani mwanamke ndio nguvu kazi ya familia na pia ifanye mazungumzo na hizo taasisi zinazotoa riba kubwa wakapunguza riba ili wanawake wengi waweze kujikwamua na umaskini.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kutoa hongera kwa Mheshimiwa Rais, wewe mwenyewe Spika, Waziri Mkuu na Mawaziri na Naibu Mawaziri, Wabunge pamoja na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali.

Napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri iliyojali maslahi ya wananchi wote. Pia inatoa moyo kwa wananchi wote hasa vijana waliokata tamaa na kuwa na lengo la kuhamia ughaibuni kuosha vyombo na kutunza wazee hawataendelea na kuosha vyombo na kutunza wazee, hawataendelea na azma hiyo na walioko huko nadhani watarudi.

Mheshimiwa Spika, vile vile naiangalia hotuba hii kama changamoto kwa watendaji wote wa Serikali katika kutimiza aliyoahidi. Yote ni mazuri na yanalenga kuleta maisha mazuri kwa kila Mtanzania.

Nitaanza kuchangia hotuba hii na suala la utawala bora, nchi yetu imekuwa na tatizo la utawala bora kwani maeneo mengi ya kazi haki haitendeki kuanzia Serikalini hadi sekta binafsi, rushwa imekuwa ni tatizo la kutekeleza utwala bora kwani bila kutoa ni kikwazo. Ili kuondoa hayo naiomba Serikali ikisimamiwa na Mheshimiwa Rais kuhakikisha nchi yetu inakuwa na utawala bora. Watendaji wote wa Serikali wafuate maadili ya kazi zao na wajibu wao kwa wananchi na urasimu wa kesho kesho umepitwa na wakati tunawajibika kulinusuru Taifa letu na ili kuepuka rushwa katika nchi yetu. Rais katika hotuba yake anasema namnukuu ukurasa wa 23: "Tutaimarisha uwezo wa kifedha na kiutendaji wa taasisi zilizo mstari wa mbele kwenye vita dhidi ya rushwa katika Jeshi la Polisi na Mahakama."

Mheshimiwa Spika, naomba jambo hili litekelezwe na wahusika kama ilivyoagizwa na vile vile mishahara iongezwe na maslahi ya watumishi wa umma ili kupunguza vishawishi vya rushwa, mfano, askari, madaktari na walimu.

Mheshimiwa Spika, bila kusahau suala la elimu, pamoja na Serikali kuwa na mipango mizuri ya kuboresha elimu yetu, lakini bado elimu yetu iko katika kiwango cha chini mno na haikidhi mahitaji ya Watanzania. Naomba wahusika waboreshe taaluma ili kuongeza viwango vya kufaulu katika ngazi zote na juhudzi za makusudi zifanyike kama au kwa mpango wa dharura watoto wote (wanafunzi) wapate nafasi za kuendelea na masomo kuliko mpango wa sasa wa asilimia hamsini tu. Ili kufanikisha hilo, shule za sekondari zijengwe nchi nzima na ziwe na sifa ya kuitwa sekondari, ziwe na maabara na maktaba.

Mheshimiwa Spika, vile vile maisha ya walimu yaboreshwe kwa kuwapa mishahara mizuri, nyumba za kuishi na bila kusahau kuboresha taaluma yao kwa kuwapa elimu zaidi, hivyo itakuwa rahisi kwao kufanya kazi yao kwa moyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu ujenzi wa barabara, vivuko na madaraja (miundombinu). Ili nchi yoyote iendelee kiuchumi inabidi kuhakikisha kuwa miundombinu inakuwa bora kwani nchi inakuwa imeunganishwa. Nchi yetu bado ina tatizo la barabara hasa Mikoa ya Magharibi ikiwemo Kigoma na Rukwa, hivyo umaskini unazidi kukithiri katika Mikoa hiyo wakati ina maliasili nyingi na ni wazalishaji wakuu katika sekta ya kilimo na uvuvi. Kwa kukosa barabara wanashindwa kusafirisha mazao yao ndani ya Mikoa yao na nje ya Mikoa yao, hivyo inakuwa ngumu kwa wao kujikomboa katika lindi la umaskini. Naishauri Serikali ya Awamu ya Nne ihakikishe kabla ya mwaka 2010 tatizo hilo liwe limetatuliwa kwani barabara zitakuwa zimejengwa na umaskini utapungua kwa wananchi na usafiri wa kawaida utakuwa rahisi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nina mengi ya kuchangia lakini naiomba na kusisitiza Serikali itekeleze yote yaliyoahidiwa na Mheshimiwa Rais kwani nchi yetu itakuwa imepiga hatua katika maendeleo na Serikali isisahau kuangalia upya mikataba yote yenye utata ya wawekezaji wa nje na ndani ya nchi kwa ajili ya maslahi ya Watanzania.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda niwashukuru wananchi wa Misungwi walioniwezesha kwa kura zao nyingi kufika hapa Bungeni. Nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi alioupata na kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Edward Lowassa kuwa Waziri Mkuu na kwa kuthibitishwa na Bunge kwa kura nyingi. Pongezi zingine ni Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, si vema kutokukupongeza wewe na Naibu Spika, naahidi kutoa ushirikiano kwenu na Mungu awajali vizuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita zaidi katika tatizo la njaa. Njaa waliyonayo wananchi ni kubwa na kwa sasa imesababisha wananchi wasifanye kazi za maendeleo hasa kilimo ili wapate chakula kwa msimu ujao. Hakuna mtu ambaye anaweza kwenda shambani kama ana njaa. Kutokana na hali hii ningeshauri Serikali iongeze kasi ya kutoa misaada ya chakula kwa wananchi ili wakipate kwa wingi zaidi. Wakati Serikali inafanya hivyo na kuhakikisha kuwa hawafî na njaa kama alivyosema Mheshimiwa Rais, ni vema wananchi wakahimizwa kutumia mvua zinazonyesha baadhi ya maeneo kulima mazao yanayostahimili ukame kama vile muhogo, uwele, mtama na pia mazao yanayoiva kwa muda mfupi kama viazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hali ya njaa Wilayani Misungwi inatisha. Tumepokea tani 329 mgawo wa kwanza, kaya zenye hali mbaya ndani ya vijiji 44 zilipatiwa chakula hicho kwa bei ya shilingi 50 kwa kilo, kati ya kaya 28 za Wilaya nzima. Serikali kwa awamu ya pili imegawa tani 436, kaya zisizo na uwezo ndani ya vijiji ni 34 na vijiji hivyo ni vyenye idadi kubwa ya watu kama vile Maluki, Misasi, Usagara, Misungwi. Chakula hiki ni wastani wa kila kaya kati ya kaya hizo kupata kilo nane. Hii ni hatari, naiomba sana Serikali iendelee kutoa chakula na itoe kwa aina nne ya migawo:-

- (a) Chakula cha bure kabisa kwa wasiojiweza;
- (b) Chakula cha bei nafuu shilingi 50 kwa kilo kaya zisizo na uwezo mkubwa;
- (c) Chakula cha kazi (watu wafanye kazi za maendeleo wapewe chakula); na
- (d) Chakula toka wafanyabiashara, bei ipungue Serikali itoe ruzuku kwa hao wafanyabiashara, bei iwe shilingi 200 siyo 300.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kama hayo yatafanyika mapema hakuna mtu atakufa kwa njaa.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwa mishahara kulipwa kwa wafanyakazi hili nalo ni tatizo linalowafanya watumishi wasiwe na moyo wa kufanya kazi. Nilifurahishwa na agizo la Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundis aliposema kuwa

mishahara ya walimu ilipwe tarehe 25 ya kila mwezi, nilifurahi sana, hili tatizo au huu ufumbuzi ufanyike kwa watumishi wote.

Mheshimiwa Spika, nauliza juu ya malipo yaliyotolewa ahadi na Waziri wa Ushirika mwezi Septemba na Oktoba, 2005 katika Mikutano Mikuu ya *SHIRECU, Nyanza, KDCU, KANU*. Waziri alisema angelipa mishahara yaani malimbikizo na madai ya wakulima, takwimu wanazo watumishi wa Wizara hiyo. Tatizo ni nini? Naomba sana walipwe ili wajikimu na suala zito la njaa na kupeleka watoto shule.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la ulinzi na usalama. Hali ya ujambazi inazidi kuwa mbaya zaidi, uvamizi unafanyika mchana, majambazi yanatumia silaha za moto na za hali ya juu. Serikali ijipange vizuri, ni aibu kubwa kwa nchi yetu ambayo ni kisiwa cha amani wakati watu wake wanauawa ovyo. Kijiji ninachotoka tarehe 20 Januari, 2006 saa 2.00 za usiku mapema wamevamia majambazi na kuua mfanyakishara Ntingi Peter, msaada wa polisi ulichelewa ni kwa sababu ya vitendea kazi, Wilaya ya Misungwi nayo gari moja tu. Mwaka jana Serikali ilinunua gari la pili na kulipeleka Mwanza hadi leo haijafika Misungwi ni sababu zipi gari hiyo haijafika?

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mambo ya Ndani mwaka 2005 aliahidi kulishughulikia suala hilo hadi leo ufumbuzi bado. Naomba Serikali itoe jibu ili haki ya wana Misungwi wapate gari yao.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie fidia kwa watu walioguswa na mradi wa maji kwenda Kahama kutoka Victoria vijiji vya Nyang'homango, Lubiri, Kalambo ya Isemengeja na Mwawile, baadhi wamelipwa na baadhi bado mfano, awamu ya kwanza watu 38 shilingi 8,804,488, awamu ya pili watu 12 shilingi 2,677,290, awamu ya tatu ilikuwa na utata ambao watu 197 wamekuwa wakidai na bahati nzuri Serikali imeanza kuwalipa, matatizo bado yapo eneo la Mwawile pale walipojenga kituo na kuelekea Mwanashimba kupitia Mwanagili. Hawajalipwa, mthamini anasubiriwa na kuna shilingi 8,794,485 ambazo zipo Msiungwi na hazina maelekezo ya kuzitumia, Wizara itoe ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimwombe Waziri wa Miundombinu kufuatilia ujenzi wa barabara ya Misasi - Mbarika ilio chini ya *TANROAD* Mkoa, mjenzi alishapatikana, sasa ni zaidi ya miezi mitano wananchi wa vijiji vya Nduha, Kasololo wameshindwa kufikishiwa chakula kwa sababu ya uzembe wa makandarasi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba na muweza wa yote aliyetufikisha hapa na kutupa kila ambalo tumelipanga.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kushinda ushindi wa kishindo, lakini vile vile niwapongezeni, wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge

na baadaye kuchaguliwa kwa kura nyingi kushika wadhifa ulionao kuwa Spika wa Bunge la Tanzania. Pamoja nawe nimpongeze mama Anne Makinda kuwa msaidizi wako.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa nae baadaye kuthibitishwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri yetu ya Tanzania. Hii ni kuthibitisha imani kubwa tulionayo sisi na wananchi kwenu wote.

Mheshimiwa Spika, kazi kweli imeanza kwa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya. Sisi Wabunge na wananchi wetu wanayashuhudia hayo na kuyakubali. Katika kazi hii iliyoanza ya kuleta mabadiliko ya haraka pamoja kazi ya kuondoa maovu si kila mtu (hasa watu wabaya) wanalifurahia suala hili. Ndio maana kundi la majambazi na hata wale waliokoswa wanashabikia ujambazi na yawezekana wanashirikiana na wahalifu ili kutingisha hali ya usalama wa Watanzania. Wapo waliokosa nyadhifa na kwa maana hiyo kuwa maadui, badala ya marafiki na hawaipendi kazi nzuri ifanywayo na Mheshimiwa Rais, Makamu na Waziri Mkuu.

Katika hali hii nzito ya utumiaji wa silaha kwa raia wema na kwa wafanyabiashara, nachelea sana sana wimbi hilo lisije likageuka kwa viongozi wetu wapendwa. Kwa hilo basi, nashauri kuanzia sasa Mheshimiwa Rais na Makamu wake, Waziri Mkuu na wewe Spika mwende au mpewe ulinzi wa hali ya juu sio majumbani tu, bali hata katika misafara yenu mkiwa makazini. Raia wema hawana uwezo wa kuwapoteza wachapakazi kazi wazuri kama akilia ninyi. Hapa nakusudia kusisitiza kwa Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu walindwe na hasa wanapokuwa katika mahafali ya kuwatembelea wananchi kwenye masoko mitaani na kadhalika. Mimi binafsi sijaridhika na ulinzi uliopo. Watu wabaya ni wachache lakini azma zao ni dhaifu, hawajali juu ya madhara ya matendo wanayoyatenda.

Mheshimiwa Spika, tumeyaona yaliotokea India kwa Gandhi, tumeyaona yaliotokea *USA* kwa F. K. Kennedy, yaliyotokea Misri kwa Anwar Saadat na hata hapa Tanzania kwa Marehemu Mzee wetu Abeid Amani Karume mwaka 1972. Nasisitiza tena ulinzi kwa Waheshimiwa hawa. Ahsante.

MHE. FATMA ABDALLA TAMIM: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuandika mchango huu unaohusu hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Pili, nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu, Naibu Spika pamoja na Mawaziri wote Mwenyezi Mungu atakusaidieni na kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake iliyojaa falsafa inayooonesha dira ya mwelekeo wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Hotuba hii haikuacha kitu imechambua mambo yote. Kwa kweli ameanza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, kila sekta ameelezea kwa wakati uliopita kilichofanyika. Wakati wa sasa hivi tulionao na wakati ujao kwa kweli amechambua mambo mbalimbali kwa hotuba hii sina hata la kuchangia.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba kuchangia katika hotuba hii kuhusu majambazi yaliyoshamiri katika nchi yetu. Inasikitisha sana hakuna wa kulaumiwa ila tumwombe Mungu atusaidie ili tuondokane na mtihani huu.

Mheshimiwa spika, Mheshimiwa Rais ana nia njema na nchi yake, kila anapo jitahidi kutangaza kuliondoa tatizo hili kwa nguvu zote na wao wanakaza kamba kwa kujitahidi kufanya uhalifu. Namwomba Mheshimiwa Rais asichoke, ajitahidi kwa nguvu zake zote aendelee kupambana nao wahalifu na Mwenyezi Mungu atamsaidia na kila anaye jitahidi hakika Mungu yuko pamoja na yeye na *Inshallah* atashinda.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anayehusika na Wizara hii achukue juhudhi ya kukutana na Makamanda wa Polisi na pia afanye mabadiliko katika Jeshi la Polisi kwa mtazamo inavyoonyesha na wao wanachangia katika uhalifu japo kuna wengine wanafanya kazi vizuri lakini wanapoanza wenzao kwani watu wanasema, samaki akioza mmoja huoza wote.

Namwomba Mheshimiwa Waziri anayehusika na Wizara hii achukue juhudhi ya kuwashirikisha na raia wao ndio wanaozipata taarifa kwa haraka kwa sababu wao ndio wanaokuwa karibu mitaani.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri atoe tangazo atakayetoa taarifa ya kuwafichulia majambazi atapata zawadi mfano shilingi kadhaa na pia atalindwa kwa usalama wake na pia huyo atakayetoa taarifa isipelekwe kwa viongozi wa polisi, lakini wapelekwe moja kwa moja kwa Waziri ili isije ikarudi taarifa hiyo kwa majambazi na kuhatarisha maisha. Pia iwekwe namba ya simu ya siri ikiwa mtu hataki ajulikane na itangazwe kwenye vyombo ya habari. Namba hiyo pengine huenda ikasaidia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri angekutana na Jeshi la Polisi lote ili akawasiliza matatizo walijonayo kwani wao ni binadamu na pengine hawana vitendea kazi vya kutosha pengine ndio sababu inayopelekea kupata lawama nyingi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache niliyoyaeleza naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. BAKAR SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe, Naibu Spika na Waheshimiwa Mawaziri kwa kushika nyadhifa zenu mnazoshikilia sasa.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze mchango wangu pale Mheshimiwa Rais alipozipongeza Tume za Taifa za Uchaguzi ile ya Taifa na ile ya Uchaguzi Zanzibar. Kwa maoni yangu Tume ya Uchaguzi Zanzibar haistahili kupewa pongezi ya kufanya vizuri katika uchaguzi uliopita wa tarehe 30 Oktoba, 2005 bali inastahili kulaumiwa vikali sana kwa kuliaibisha Taifa kwa kufanya kazi yake kwa utashi wa kisiasa zaidi

kuliko jukumu lake halisi hadi kupelekea matokeo ya uchaguzi huo kutokubalika katika dunia nzima hasa zile nchi zinazojali haki na demokrasia ya kweli.

Mheshimiwa Spika, inakuwaje Tume inayosimamia Mikoa mitano tu kushindwa kutoa matokeo kwa saa 24 wakati Tume za uchaguzi katika nchi nyingine kubwa zenye maeneo makubwa huwa zinachukua si zaidi ya saa 24?

Mheshimiwa Spika, Tume hiyo ya Uchaguzi ilitoa matokeo mara mbili na mara zote hizo matokeo hayo hayakukubalika na waangalizi wa kweli na wapenda haki duniani.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uvunjifu wa uadilifu wa Tume hiyo, ndio uliopeleka Chama cha Upinzani cha *CUF* na baadhi ya nchi duniani kutoyakubali na kutomtambua Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa saba katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Rais ameeleza kwamba Wapinzani wasitafute mchawi kila wanaposhindwa uchaguzi. Kama kweli Mheshimiwa Rais anataka kuleta hali nzuri ya kisiasa lazima akubaliane na ukweli kwamba Upinzani unao wachawi wengi na ni lazima Mheshimiwa Rais asibeze kuwashughulikia wachawi hao ili kuweka mazingira mazuri ya kisiasa nchini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wachawi hao ni kwanza, vyombo vyatoka nchini bado vinaegemea zaidi upande wa Chama Tawala (CCM) kinyume na maadili ya kazi zao. Tumeshuhudia askari wanashabikia siasa na hata kufikia hali ya kuwanyanya Wapinzani.

Pili, vyombo vyatoka nchini navyo ni mchawi wa pili ambaye anavikandamiza vyama vyatoka upinzani. Tumeshuhudia katika kampeni jinsi vyombo hivyo vilivyosaidia Chama Tawala na kuviacha wakati mwengine hata kuacha kutaja kwamba mgombea wa Chama cha Upinzani yuko katika Mkoa gani licha ya kusema amewaeleza nini wananchi katika kampeni zake.

Tatu, mchawi mwengine ambaye nia yake ni kuvimaliza Vyama vyatoka Upinzani ni Tume za Uchaguzi. Tume za Taifa zapaswa ziangaliwe upya juu ya mjengeko wake na hata maadili ili iweze kufanya haki kwa vyama vyote na kuepusha malalamiko ambayo hayaleti picha nzuri kwa Taifa letu.

Katika ukurasa wa 18 wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Rais amesema kwamba anasononeshwa na mpasuko wa kisiasa kati ya Unguja na Pemba na hasa ulivyojiteza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Rais alieleza hivyo kwa kuwa CCM wamekosa Jimbo katika uchaguzi huo. Lakini kama ni hivyo mbona hasononeshwi kwa *CUF* kukosa Jimbo Dar es Salaam au Tanzania Bara kwa ujumla. Pia Mheshimiwa Rais kama hajui sababu zilizopelekea matokeo yale, basi afanye utafiti wa kina na sio kuchukulia maneno ya upotofu ya wana CCM wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda nichukue nafasi hii nimwelezee Mheshimiwa Rais baadhi ya sababu za mpasukowa kisiasa kati ya Unguja na Pemba.

Moja, ubaguzi uliokithiri wanaofanyiwa Wapemba na CCM na Serikali zake zote mbili lakini hasa ile ya Zanzibar mfano, angalia Baraza la Mawaziri la Zanzibar wote ni kutoka Unguja na mmoja tu kutoka Pemba naye hana Wizara eti amepewa kazi maalum. Lakini anapoulizwa ni kazi gani hiyo yeje haijui.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika, Jaji Mkuu, Makamishna wa Polisi, Mkuu wa Uhamiaji, Wakuu wa vikosi vya KMKM, JKU, Magereza na Valantia wote wanatoka Unguja. Hata kiongozi Mkuu wa Vijana wa *Janjaweed* ambao wanatuhumiwa kukubhu kwa kuwatendea Wapemba vitendo vya ukiukaji wa hali za binadamu pia anatoka Unguja.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo kwa nafasi za masomo kama ilivyotokea vijana zaidi ya arobaini waliokwenda Malaysia wote walitoka Unguja kana kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilisahau kuwa Pemba ni sehemu ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, miezi miwili tu iliyopita Tanzania Zanzibar ilipata mwaliko wa vijana zaidi ya 20 kufanya ziara ya masomo Uhlanzi, wote ni kutoka Unguja.

Pili, kunyanyaswa, kuporwa mali, kunajisiwa wanawake kila baada ya uchaguzi hasa huu wa mwaka 2005, askari kujichukulia hukumu mikononi mwao mfano walipoteswa na kupigwa virungu watu wa Piki na hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi, polisi walikiri kwamba askari wa JKU walikamatwa kwa kupora nyumba za watu Pemba lakini hadi hii leo hatujasikia kwamba wamefunguliwa mashtaka na pia askari wa JKU walimpiga askari polisi pale Piki (Ali Salim Faki) akiwa na vazi la uaskari kwa kuwa yeje ni Mpemba na mpaka leo hatujasikia hatua yoyote iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Rais aunde Tume huru ili ifanye utafiti wa kina wampatie Rais maelezo halisi juu ya mpasuko uliodumu miaka mingi sasa. Mheshimiwa Rais asije kufuata maelezo ya wana CCM, watampoteza na kuacha mpasuko uendelee.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante.

MHE. EMMANUEL J. LUAHULA: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi zangu nyingi kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushindi mkubwa alioupata. Nawapongeza Mheshimiwa Abeid Karume na Dr. Shein kwa kuchaguliwa kwao. Pongezi nazipeleka kwa Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kuwa kiongozi mkuu wa utendaji Serikalini.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa ushindi wa umma mliouputa. Nawapongeza pia Wabunge wenzangu wote wa Majimbo, Viti Maalum na wa Kuteuliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu hatimaye niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kwao kusimamia Wizara mbalimbali. Mwisho, natoa pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Bukombe wa itikadi mbalimbali kuniwezesha kushinda kwa kishindo na Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, napenda nichangie mchango wangu katika hotuba ya Rais katika nyanja zifuatazo:-

Kwanza, usalama wa raia na mali zao. Nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati wa uchaguzi na ukaisha kwa amani na utulivu. Hata hivyo jeshi la polisi tunaomba wapewe vitendea kazi vya kisasa ili kupambana na ujambazi unaotokea. Askari wapatiwe mavazi ya kuzuia risasi za moto, Jimboni kwangu hata ofisi ya upelelezi haina gari, wapewe madai yao, wanayoidai Serikali walipwe mapema mfano, fedha za uhamisho na madai mengine, mishahara yao itazamwe upya na idadi ya polisi haitoshelezi sehemu nyingi ikiwemo na Bukombe. Kwa upande mwingine askari polisi walio wabovu wafukuzwe kazi mara moja kwani wao ndio wamekuwa kichocheo cha ujambazi.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Bukombe askari wamekuwa na tabia ya kubambikiza kesi za mauaji wananchi na kesi za namna hii Bukombe ni nyingi sana ukifutilia hazina ukweli ndani yake. Naomba Serikali ichukue hatua za lazima kwa askari wa namna hii.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka tarehe 19 Januari, 2006, nilifanya kikao na askari wote wa Bukombe, mara baada ya kutoka pale wananchi waliokuwa na watu wao *lock-up* walifika pale wakaambiwa watoe shilingi milioni tatu, watu hawa walikuja kwangu wakiwa na Diwani wao ndipo nilipokemea tabia hiyo. Hata hivyo haikusaidia, pengine kwa kuwa askari wamekuwa na mazoea na kuona kuwa wao hakuna anayeweza kumuogopa Wilayani, hili nalo linaleta kero, naomba uhamisho kwa askari kama hawa uwepo.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu chakula. Jimbo la Bukombe silioni katika takwimu za mgawo wa chakula wakati Bukombe ina njaa na tathmini ambayo nilipewa na *DED*, tarehe 13 Januari, 2006 kwenye kikao changu na ye ye aliniambia tunahitaji takriban tani hamsini elfu. Bado akinamama na watoto wamekuwa wakiletwa nyumbani kwangu na ofisini kutaka niwapatie chakula au fedha. Leo hii Bukombe haipo kwenye mgao wa chakula, kweli huku ni kunifunga kitanzi ambacho sitapona kwa miaka yote hii. Pengine Wilaya haikutoa takwimu sahihi kwa wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, bado tarehe 08 Januari, 2006 nilipoongea na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya wakaniambia wamepeleka maombi yao ya tani 16,850 nazo hazionekani. Leo hii nimepokea simu toka nyumbani kwangu watu wanamsumbu mama watoto na familia wakimwambia awapatie chakula kwa sababu Mbunge ameambia Serikali hamna njaa, basi Mbunge anacho chakula atuhudumie.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifanye uchunguzi wa kina Bukombe ili wapelekewe chakula wananchi wangu, bei ya mahindi ni kati ya shilingi elfu sita hadi shilingi elfu saba kwa debe.

Mheshimiwa Spika, ninayo mengi ya kuchangia, lakini kwa sababu naandika nitajaza karatasi nyingi, acha niishie hapa, mengine tutahoji Serikali kuitia maswali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais inayotoa dira na mwelekeo. Ahsante sana.

MHE. RAMADHANI A. MANENO: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa ushindi mkubwa usio na mashaka. Pia nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika nakupongeza na Naibu wako Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kushika nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Rais kushika nafasi katika Wizara za Serikali ya Awamu ya Nne. Nawapongeza Wabunge wote waliopo hapa kwa ushindi walioupata.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru na kuwapongeza wapiga kura wangu wa Jimbo la Chalinze kwa kunichagua niwe Mbunge wao na naahidi kuwatumikia kwa hali na mali.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwanza kabisa suala la rushwa limekuwa kero katika maeneo yanayotoa huduma kwa wananchi, hasa Mahakama na Polisi, rushwa ni biashara, kwenye Jimbo langu Idara ya Mahakama hasa za Mwanzo kuna tabia kwamba wanaposhitakiana mkulima na mfugaji iwe, isiwe mfugaji lazima ashinde.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu suala la nidhamu. Nidhamu imeshuka sana, kila mtumishi anajifanyia atakavyo. Kwa kasi mpya, naomba Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa umma itazame suala hili kwa makini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo, tufikie mahali suala la kilimo litiliwe umuhimu, Wizara husika ilione hili. Kilimo cha jembe la mkono limeshapitwa na wakati, njaa iliyotupata kwa sasa imechangiwa na kilimo duni. Sasa ni wakati muafaka Serikali kwa makusudi isaidie sana jambo la kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la barabara. Barabara zetu ni mbaya sana huko vijijini, hazipitiki kwa gari wala pikipiki, mgonjwa hasa akinamama wajawazito wanapata taabu sana kupelekwa kwenye zahanati, naomba Wizara husika ilione hili.

Mheshimiwa Spika, suala la vijana hasa ajira ni muhimu sana. Kwenye kampeni tulitoa ufanuzi kuhusu ajira, nashauri tusilipuuze jambo hili, kwani vijana macho yao

kwetu sisi Wabunge na Serikali. Sio siri vijana walijiandikisha sana kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na hatimaye majibu tuliyaona kwani walijitokeza kwa wingi kupiga kura tarehe 14 Desemba, 2005, mategemeo yao ni ajira kwamba itapatikana, hili ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza na kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, napenda vile vile kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Micheweni kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa nyadhifa zenu. Vile vile nampongeza na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri na Naibu wao.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nampongeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa kuchaguliwa kuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na mwisho lakini sio kwa umuhimu nawapongeza Wabunge wote waliochaguliwa kihalali katika Majimbo, Viti Maalum na wa Kuteuliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nikianza kuchangia hoja ya Mheshimiwa Rais kwanza nataka kusema kuwa hotuba ni nzuri lakini hoja sio uzuri, hoja hii itatekelezwa?

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais amezungumza mambo mengi ya aina mbalimbali mimi sitozungumzia mengi ila nitazungumzia zaidi kwenye masuala ya kisiasa ambalo ndio hasa tatizo linaloikabili jamii yangu pamoja na wapiga kura wangu wa Jimbo la Micheweni.

Mheshimiwa Spika, nikianzia na shukrani za Mheshimiwa Rais namnukuu: “Nawashukuru watani zangu wa Kambi ya Upinzani kwanza, kwa ujasiri wao mkubwa wa kujitokeza kushindana na Chama cha Mapinduzi, maana kushindana na CCM sio mchezo.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hapa tu namuona Mheshimiwa Rais amesema kweli kwani ni ujasiri kweli kushindana na CCM, kwa sababu CCM ni Chama Tawala kweli, hakitaki kuondoka madarakani hata iwe vipi wapo tayari. Kwa vyovyyote vile lakini wasiondoke madarakani kwa mfano, sisi tunaotoka Visiwani tumeshuhudia vyombo vyote vya dola vya nchi hii vikishirikishwa katika Uchaguzi wa Zanzibar na sio kuwashiriki kikazi tu bali hata kuingilia kwenye Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa malori yaliojaa askari yalikuwa yakipelekwa kwenye vituo vya kura na wakapewa kura kinyume na sheria na wakapiga kura mara mbili, mbili na wengine zaidi. Kwa kweli kushindana na CCM sio mzaha kwani CCM ni chama dola kinatumia askari kujirudisha madarakani, kwani askari wote walishirikishwa kwenye uchaguzi wa Zanzibar. Majeshi, Polisi, Usalama wa Taifa,

KMKM, JKU, KVZ Mafunzo, Mgambo na vijana wa CCM maarufu kwa jina la *Janjaweed*.

Mheshimiwa Spika, sijui kwa huku Bara lakini kwa sisi Zanzibar siku zote hakuna Uchaguzi kwa sababu CCM hawakubali kushindwa na wakati Wazanzibar wameshaichoka imejiweka pale kwa kutumia nguvu za dola tu, leo hii ukifanyika uchaguzi wa huru na haki, CCM itaondoka madarakani. Ile kusema Rais Wazanzibar ameshinda ni kuudanganya umma ambao unafahamu.

Mheshimiwa Spika, napenda niufahamishe umma uelewe CCM wanavyoiba kura kule visiwani, wizi huu ambao nimeushuhudia mimi mwenyewe sio wa kuhadithiwa. Kwanza wanawaweka watu wao kwenye vituo vya kupigia kura yaani *PO* na *PC* wanahakikisha kwenye Tume ya Uchaguzi kuwa msimamizi lazima awaunge mkono CCM. Sasa wanapokuja watu wao ambao wameshazungumza nao basi huwapa kura hata ikiwa hawamo kwenye daftari hili. Nimeiona mimi mwenyewe nimewakamata watu na nimemkabidhi *OCD* wa polisi na hakuna chochote kilichotokea kubwa awaondoa pale kwenye uchaguzi tu. Wizi mwengine mtu kuchukua kitambulisho cha mtu mwengine akaenda kupiga kura ya mtu, aliyekufa, asiyekuwepo au cha mtu mwengine akaenda kwenye kituo kwa kuwa wasimamizi washafahamiana wakifika humpa kura akapiga na baadae ndio huenda akapiga kura yake ambayo huwa hajapiga, maana kwanza huwa anapiga ya wizi na baadae ndio anapiga ile yake halisi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa uchaguzi kama huu Vyama vya Upinzani vitakuja juu. Hii ni kwa Zanzibar na huku Bara Takrima ndio inayotumaliza Upinzani. Sisi kule Pemba *CUF* tunashinda kwa sababu hatuna CCM hata kidogo lakini hao hao kidogo huo ndio wizi wao wanaotumia na kubwa wanategemea kuwa askari ni wao hawawezi kufanywa chochote.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari navyo vyote vipigie debe Chama Tawala tu.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kuzungumzia kuhusu mpasuko uliotajwa na Mheshimiwa Rais. Ni kweli mpasuko upo, lakini mimi nauliza huu mpasuko umesababishwa na nani? Wao waliosababishwa si wanajulikana. Kwa mfano, hivi wewe uwe na watoto wawili, mmoja uwe unampa kila kitu na mmoja humpi chochote, mmoja anatumbuwa na mmoja anaishi kivyake vyake tu. Hawa watoto kweli watapendana na huyu mtoto asiyepewa chochote na mzee wake atampenda. Basi mfano huu ni wa Serikali ya Muungano kama mzee na watoto ni Serikali ya Zanzibar na mtoto anayependwa ni Kisiwa cha Unguja na wasiopendwa ni Kisiwa cha Pemba. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kila kitu inafanya Unguja tu na Pemba hakupelekewi maendeleo yejote na sote tunajua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amesema mpasuko huu umesababishwa na historia, lakini hakusema ni historia gani na sisi tukapata kuchangia. Mimi naomba tuambiwe ni historia gani hiyo?

Mheshimiwa Spika, napenda nimnukuu Mheshimiwa Rais katika sehemu hii: “Iweje leo Wapemba ambao ni hodari wa kutumia fursa ya Muungano wetu na kuishi na kufanya biashara na kuwekeza katika pembe zote za Jamhuri yetu wawe hao hao wanaonekana kama wanajitenga kiasi kwa kiwango tunachokishuhudia kwenye Uchaguzi Mkuu.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema Wapemba hawajajitenga, ila tu wanatumia haki yao ya Kikatiba. Hivi kama kuna mtu hakuchagua CCM ndio amejitenga, si vimeundwa vyama vingi ili mtu achague chama anachokipenda.

Mheshimiwa Spika, sisi Wapemba tumejitahidi kuimarisha Muungano kwani Wapemba wengi wameoa Bara na wameolewa na tumewekeza sehemu nyingi ila Serikali zetu ndio zinazotutenga. Hazitushirikishi katika shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amesema: “Umfika wakati wa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa mpasuko huo.”

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na Mheshimiwa Rais kuwa wakati umefika wa kuondoa tatizo hili na sisi tuko tayari kumsaidia kwa hali zote. Ila tunamfahamisha tu afahamu uchaguzi uliofanywa Zanzibar haukuwa huru wala wa haki, hili jambo alifahamu kisawasawa. Sasa katika kutafuta suluhu hiyo aelewé mahali pazuri. Kwa kuanzia asianzie mambo katikati aanze kwenye mizizi ya tatizo hili. Ahsante sana.

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO: Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kukupongeza kwa kuteuliwa na kwa uamuza wako wa busara wa kutupatia nafasi Wabunge kuijadili hotuba ya Mheshimiwa Rais alipolihutubia Bunge jipya tarehe 30 Desemba, 2005. Ni hotuba ya kujivunia.

Mheshimiwa Spika, ni mwongozo safi wa hatua za kuchukuliwa katika kukuza uchumi na kupambana na umaskini.

Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia katika maeneo mbalimbali, nimeamua kulenga mchango wangu kwenye matatizo ya maji na mazingira. Nakubaliana na Rais kuwa maji ndicho kilio kikubwa, si cha Watanzania wote mijini na vijijini tu bali hali ni mbaya sana katika Mji wa Kisarawe na vijiji vyote vya Wilaya ya Kisarawe.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ulipokuwa Waziri wa Maji, alifika Kisarawe na akajionea mwenyewe hali mbaya ya maji mjini na baadhi ya vijiji vya Kisarawe. Pamoja na misaada ya Serikali kutoa shilingi milioni 250 kwa upanuzi wa Bwawa la Minaki, shilingi milioni 9 kuchimba malambo matatu na fedha nyingine kukarabati vyanzo vya maji mjini Kisarawe, ukame uliofululiza miaka mitatu umeifanya hali ya maji Kisarawe kuwa mbaya zaidi.

Nimpongeze tena Mheshimiwa Rais na wewe mwenyewe, kwa kuweka uzito mkubwa kwenye masuala ya maji na mazingira. Kwenye hotuba ya Rais tatizo la maji limechukua nafasi kubwa. Katika hotuba hiyo Rais ameordhesha mambo 10 muhimu ya

kuzingatiwa, mojawapo namba 9 likiwa kupambana na uchafuzi dhidi ya mazingira ili kuweka misingi imara ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hoja yake ameodrodhesha mambo makubwa manne ya kutilia mkazo yafuatayo:-

- (i) Upanuzi wa Shule za Sekondari;
- (ii) Kilimo cha Umwagiliaji;
- (iii) Utunzaji wa mazingira; na
- (iv) Uimarishaji wa raslimali watu.

Kwa hiyo, mazingira umeyapa umuhimu. Pamoja na kuwapongeza kwa kuweka mkazo kwenye masuala haya muhimu ni bora niieleweshe Serikali kuwa huko Kisarawe vijijini mambo ni mabaya sana na hatua za dharura zinahitajika kuwaokoa wananchi wetu. Hakuna maji kwenye malambo wala visima vifupi. Akinamama wanashinda na kukesha mabondeni bila ya mafanikio. Maji kidogo yanapatikana kutoka masafa marefu si chini ya kilometra 20. Kwa hiyo, hata mikokoteni sasa haiwezi umbali huo. Maji yanaletwa kwa baiskeli yanauzwa kwa shilingi 200 hadi 500 kwa dumu moja. Gharama hizi wananchi hawaziwezi.

Mheshimiwa Spika, ukame umeletwa na mambo makubwa mawili, ukataji hovyo wa miti na misitu kwa ajili ya mkaa na kulima hovyo katika vianzio vya maji.

Mheshimiwa Spika, mkaa umekuwa nishati namba moja kwa Jiji la Dar es Salaam kwa matumizi ya nyumbani, lakini pia ni ajira. Ndiyo maana hii leo Kisarawe kuna wageni wengi hasa kutoka Mbeya na Usukumanini amba wanahamisha misitu yote kwa kupeleka mkaa Dar es Salaam. Naipongeza Serikali kwa kupiga marufuku biashara hii. Lakini hatua hii haitasaidia iwapo hatutatafuta nishati mbadala. Kwa yote haya mawili naishauri Serikali ifanye yafuatayo haraka.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ituchimbie visima virefu (*bore holes*) hata vichache, pili, ifuatilie miradi ya nishati mbadala kwa mfano makaa ya mawe ya Mchuchuma, nishati za juu na upopo na kadhalika na tatu, isimamie Sheria za Kuzuia Uharibifu wa Mazingira.

MHE. SALOME J. MBATIA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukupongeza wewe binafsi na Mheshimiwa Anna Makinda, kwa kupata kura nyingi sana za kuwania nafasi ya Uspika na Unaibu Spika. Hongereni sana.

Vile vile ninatoa hongera za dhati kwa Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi Jimboni kwake na kisha kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kupitishwa kwa kura nyingi na Wabunge kuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, niingie sasa katika hoja iliyo mezani. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na kummwagia sifa zisizo kifani kwa namna ambayo ameanza kutimiza majukumu yake kwa kutufundisha kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameamua kupita katika Wizara na kushirikisha viongozi wake wa juu kuainisha majukumu yao. Kwa utendaji huu uliotukuka Mheshimiwa Rais ametufunga kamba sisi tulio Wizarani, kamba ambayo tukifanya mchezo itatunyonga sisi wenyewe au tukichapa kazi haitatugusa.

Mheshimiwa Spika, nina hakika hakuna anayelala wala atakayelala. Tutafanya kazi kwa bidii, maarifa, ufanisi na kasi inayotakiwa ili tufanikishe kuendana na ushirikishi na mafunzo/maagizo aliyotuelekeza wakati alipotembelea kwenye Wizara zetu. Mimi binafsi nimehamasika na kujisikia ninawajibika zaidi na ari yangu ya kufanikisha imeongezeka. Mungu aendelee kumpa afya na kuzidi kumwongoza katika juhudii zake hizi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuwa sekta binafsi sasa ndiyo mhimili au injini ya kukuza uchumi. Serikali na sekta hii ni lazima kuwa wabia au wadau (*partners*) ili kufanikisha lengo hilo. Kwa namna hiyo, ni vema tukawa wepesi wa kung'amu mahitaji, kero na vikwazo ambavyo vinaweza kuzuia sekta hiyo kutoa mchango wake kikamilifu. Hivyo basi ni lazima kwa mfano upande wa biashara tuweze kuheshimu *ethical issues*, masuala ya kimaadili katika biashara kwa mfano haki za wabunifu mbalimbali wawe wasanii au wazalishaji katika viwanda au wafanya biashara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kwa mfano kiwanda kimoja cha nguo kila kikifanya ubunifu wa alama katika nguo zake, kiwanda kingine kiliweza kuiga na kutumia jasho hilo la kiwanda cha kwanza kufanya biashara ya haraka haraka na kadhalika. Iko mifano mingi, hata kwa wasanii, vijana wetu. Tatizo hili linaleta hasara pande zote na hususan kwa vijana linapunguza kasi ya ajira, linafukarisha juhudii na bidii ya vijana kujitegemea, linaongeza kutoaminiwa kama Taifa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunajitahidi sasa kuimarisha sheria na mfumo wa Mahakama zetu. Kwa mfano, tumeshakuwa na Mahakama ya Biashara na sasa Mahakama ya Ardhi. Lazima tufanye bidii zaidi ya kuimarisha na kukomaza taratibu zetu ili masuala ya Mahakama, hasa kesi mbalimbali kukamilika mapema.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ndani ya nchi yetu ni makubwa na hasa sasa tukiwa ndani ya dunia ya utandawazi hatuwezi kuepuka kwenda na wakati. Wakati mabadiliko haya ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na teknolojia hasa ya habari na mawasiliano yakija kwa kasi, miundombinu yetu ikiwemo mfumo wa sheria hasa za kusimamia soko huria haimaanishi na mabadiliko hayo na kadhalika. Hivyo *back up* ya mifumo yetu inakwamisha shughuli za uchumi. Ni muhimu *back up system* hizi zika-*match* na kasi ya maendeleo ya kiuchumi yanayotokea.

Mheshimiwa Spika, elimu ni kweli tunakazania. Lakini elimu hiyo ni sharti *i-match* pia na *activities of the day*. Katika mchakato mzima wa kukuza uchumi na kutaka kufikia upeo au *vision* yetu ya 2025 ni lazima elimu iwe ni ya ufundi zaidi na ya ujasiriamali zaidi. Elimu ya ufundi itaongeza kujitegemea hasa kwa vijana, lakini pia

elimu ya ujasiriamali itasaidia katika kuwa *aggressive*, kuthubutu, kuchakarika na kuchukua *risk* mbalimbali katika masuala ya uchumi. Wafanyabiashara wasio wajasiriamali ni wafanyabiashara nusu tu ! Hivyo ninapendekeza kwa nguvu masomo ya aina hii yaendelee kuwa katika *syllabus* za shule.

Mheshimiwa Spika, yapo mengi sana ya kuzungumza katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nizungumzie, kwa kumalizia, kuhusu kuimarisha Utaifa.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nimetiwa moyo mno kuona kuwa Rais amelijali na kuliweka katika kipaumbele. Hapa katika kipindi cha katikati vijana wetu wamekuwa wepesi wa sifa. Sifa hii uzito wake umepungua sana siku za karibuni. Labda ni kwa sababu tulijichimbia mno katika shughuli za kuhakikisha uchumi unaboreka tukasahau. Lakini jambo hili ni muhimu sana, sana. Suala hili linaendana na maadili vile vile. Naungana na Mheshimiwa Rais kwa mambo yaliyoainishwa ukurasa 19 hadi 21 ili kujenga Utaifa wetu. Nimeguswa sana na hotuba nzima ya Mheshimiwa Rais na ninaiunga mkono sana, sana.

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Spika, utunzaji wa Mazingira, ni tatizo kubwa Tanzania. Kwa kiwango kikubwa, Serikali imechangia katika uharibifu wa misitu ya asili, kwa kuruhusu uvunaji wa miti ya asili kama biashara. Uharibifu wa mazingira, hauwezi kufidiwa na pesa tunazopata. Kwa uuzaji wa magogo nje ya nchi. Serikali ipige marufuku kabisa uvunaji wa miti kwa biashara.

Mheshimiwa Spika, uvunaji wa misitu kwa ajili ya mkaa, unaathiri sana mazingira. Zaidi ya 80% ya wakazi wa nchi hii wanaka vijijini. Hawa hawatumii mkaa bali hutumia kuni ambazo hupatikana porini kutokanaf d na miti iliyokauka na hawaathiri mazingira. Watumiaji wakubwa wa mkaa, ni wakazi wa mijini. Hawa ndio waharibifu wakubwa wa mazingira. Lakini mijini kuna, umeme, gesi na mafuta ya taa. Ili kulinda mazingira, naiomba Serikali kwa makusudi kabisa, ipunguze bei ya mafuta ya taa, ili mafuta ya taa, yawe mbadala wa mkaa. Hii ndio njia moja ya kuokoa misitu yetu. Kama kodi ilio kwenye mafuta ya taa ikiンドolewa, matumizi ya mafuta ya taa kwa kupikia na kaadhalika itakuwa rahisi kuliko mkaa, wakazi wote wa mijini watatumia mafuta ya taa badala ya mkaa. Moja kwa moja hakuna mtu atatumia mkaa na moja kwa moja, huu ndio ufumbuzi wa kulinda mazingira.

Mheshimiwa Spika, upandishaji wa bei ya nishati unachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira. Ni ukweli, uchafuzi wa mazingira unachangiwa na Serikali kwa kuweka bei ya nishati kuwa ya juu sana. Kila mtu angependa kupika kwa umeme na gesi, kuliko mkaa, lakini bei ya hii nishati ni kubwa mno kwa hiyo watu wengi warudie mkaa. Ni vizuri Serikali iangalie upya namna ya kupata nishati kwa bei nafuu, iwe ni rahisi kuliko mkaa. Hii ni njia moja ya kulinda mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, kila mahali uendapo utakuta na watu wenye *CHAINSAW*. *Chainsaw* moja ikiingia porini kwa siku moja anavuna mbao lori zima. Siku hizi huhitaji Kiwanda cha Kupasua mbao. *Chainsaw* ni kiwanda peke yake na si rahisi kujuua ni wapi

Chainsaw inavuna. Hizi *Chainsaw* zinaharibu mazingira kwa kiwango kikubwa, zipigwe marufuku kwenye misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na umeme, nadhani sasa ni wakati muafaka wa kufungua milango wazi kwa yeьте anayependa kuzalisha umeme aweze kufanya hivyo, na isiwe lazima kuuzia umeme *TANESCO*. *Monopole* aliyopewa *TANESCO* ndio unafanya umeme uwe ghali.

Mheshimiwa Spika, sioni kwa nini Serikali inunue *IPTL*. *IPTL*, iruhusiwe iiuzie umeme wake moja kwa moja kwa wateja wake bila kupitia *TANESCO*. Kama Serikali itaamua kuinunua *IPTL*, itatumia pesa mara kumi kuliko kujenga mtambo kama huo huo. Huu mtambo, umekwishaingiza Serikali hasara kubwa na wananchi wamechoka na *IPTL* na Serikali isijiingize kununua mtambo huu, kwani wananchi hawaitaielewa Serikali yao. *IPTL* imekuwa kisirani, ni heri Serikali iondokane nao. Wabaki na mtambo wao na watafute wateja wa kuwauzia umeme wao.

Mheshimiwa Spika, sera ya nchi yetu ni soko huria kwa misingi hiyo, kila anayetaka kuingia kwenye biashara ya umeme awe huru na ukiritimba wa *TANESCO* uondolewe.

MHE. OMAR SHEHA MUSSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi chini ya Kanuni ya 49(7) na kwamba nakupongeza wewe kwa kuteuliwa kwako kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa mwaka 2005 hadi 2010.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Chumbuni kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kipindi hiki cha 2005 hadi 2010; na kwa jumla nawashukuru vile vile kukipa ushindi Chama cha Mapinduzi kule Jimboni kwangu Chumbuni kwa nafasi ya Rais na ya Mbunge katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 uliofanyika tarehe 12 Desemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kuchangia hotuba ya Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ukurasa wa 16 hadi 17 juu azma yake ya kuimarisha Muungano wetu pamoja na kuondoa kero za Muungano zilizobakia na kuiwezesha Zanzibar kupata maendeleo zaidi ya kiuchumi katika kipindi chake cha Awamu ya Nne ya Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kuteleleza azma hiyo ya kuondoa kero za Muungano na kuisadia Zanzibar ipasavyo, basi mambo yafuatayo yazingatiwe:—

(a) Uhushiano wa kifedha uliokuwepo baina ya iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kabla ya Muungano wa mwaka 1964 na baada ya Muungano wetu Aprili, 1964.

(b) Utaratibu wa sasa ulioleta kero, hasa kwenye eneo la kodi za Muungano (*Fiscal Policy*) ambapo nahisi ndio kero kubwa baina ya pande mbili.

(c) Kutekeleza na kufanya jitihada za kuondoa mambo ambayo ni vikwazo vyta Muungano wetu kama ilivyokwishaamuliwa kwenye taarifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, taarifa ya Kamati ya Shellukindo ya tarehe 27 Septemba, 1994, ambayo ni taarifa ya Serikali ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikifuatilia nini kilitokea baada ya Muungano wetu wa hiari, hasa mahusiano ya kifedha yalivyokuwa baina ya pande zetu mbili baada ya Muungano wa Aprili, 1964. Serikali zote mbili, ile ya Mapinduzi Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano, walikuwa ni Wanachama wa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki (*East African Currency Board*).

Mheshimiwa Spika, baada ya Uingereza (waliokuwa watawala wa eneo la Afrika Mashariki) kuzipa uhuru nchi zote nne za Afrika Mashariki - Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar mnamo kipindi cha miaka 1961 hadi 1963, nchi zetu mbili (ambapo sasa ni moja inayoitwa Tanzania), zilimiliki mtaji kwenye Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, ambao ulirejeshwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1992 hadi 1994 pande mbili za Muungano zilikubaliana kuwa *IMF*, Shirika la Fedha la Dunia, wapewe kazi ya kuchunguza uhusiano huo wa kifedha na katika ripoti yao ya Machi 1994, ilishauriwa kuwa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 1965 ibadilishwe ili Zanzibar nayo kupewa haki ya hisa zake kwa mujibu wa mtaji wake uliorejeshwa Tanzania kutoka Bodi hiyo ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1966 hadi 1972.

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi hiyo na Ushauri wa *IMF* ilikubaliwa na pande zetu mbili kuwa tusitazame nyuma kwa kuepuka kugombana, bali tupige mstari na kukubaliana yafuatayo kuanzia mwaka 1994 (Miaka 30 baada ya Muungano wetu):-

- (a) Tuwe na Benki Kuu moja, Sarafu moja;
- (b) Tuwe na Mamlaka Moja ya Fedha, Sera moja ya fedha; na
- (c) Tuwe na usimamizi mmoja wa Mabenki na vyombo au Taasisi za Fedha.

Mheshimiwa Spika, hayo yalitekelezwa na pande zote mbili na kuanzia Julai, 1995 sheria mpya ya *BOT* ilianza kutumika pande zote mbili za Tanzania na kuiwezesha Zanzibar kupata gawio la 4.4% pamoja na kufungua na kuweka hesabu zake ndani ya Benki hiyo hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, mgao huo wa faida ya *BOT* kwa Zanzibar, mwaka 1995 ulifanywa kwa *formula* ya muda tu na ripoti yenye ya *IMF* ya Machi/Aprili 1994 ilieleza hayo. Sasa ni miaka kumi na nne imepita bado gawio la Zanzibar limebaki pale pale. Hili ni kero kubwa la Muungano.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kero hiyo kubwa kuliko zote, Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*) iliyokwishaundwa chini ya kifungu cha 134 cha Katiba ya Tanzania, sasa imalize kazi yake ya kupendekeza kwa Serikali zote mbili, ili kuona mgao wa hisa wa Zanzibar unaboreshw na kufikia angalau ya 11% au zaidi, kama mtaji wa Zanzibar ulivyokuwa ndani ya Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, ambao umetajwa kwenye Ripoti ya *IMF (Appendix II)* ukurasa wa 16.

Mheshimiwa Spika, yakifanyika hayo kwenye eneo la uhusiano wa kifedha, basi Tanzania itakuwa imeondoa kabisa kero hiyo kubwa ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la Kodi za Muungano (*Fiscal Sector*) kero kubwa ni utaratibu wa sasa ambao uliwekwa tokea mwaka 1977. Utaratibu wa sasa ambao unatekelezwa na SMT na ambao unaumiza upande mmoja na utaratibu huo ni wa kubakisha kodi za bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara na ambazo hutumika kwa wananchi wa Zanzibar (*Consuming Area*) kodi hizo kubakia Bara. Bidhaa kama Sigara, Bia, Saruji, Soda na kadhalika, kodi za Viwandani *VAT* na *Excise Duty* ambazo ni kodi za forodha, ni vyema sheria zote husika zibadilishwe katika Awamu hii ya Nne, ili kero hii iondoke, kwani Zanzibar hainufaiki pamoja na kodi ya mapato (*PAYE*).

Mheshimiwa Spika, endapo Serikali ya Muungano itafanya mabadiliko hayo kwenye sekta ya fedha (*Monetary*) na sekta ya Kodi (*Fiscal*) basi Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne pamoja na Bunge lake hili, itawezesha Zanzibar kufaidika milele na kudumisha Muungano wetu kwa kuondoa kero hizi. Zanzibar nayo, itaweza kulipa mchango wake wa Muungano kutokana na Mapato yatokanayo na *Monetary/Fiscal Sector*.

Mheshimiwa Spika, yote hayo ili yatendeke, Tume ya Fedha ya Pamoja, ambayo sasa imanza kazi zake, iharakishe hayo na Wizara za Fedha na Muungano zishirikiane kusimamia hayo na mapendekezo ya awali yaanze kutekelezwa angalau kuanzia Julai, 2006

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 30 Desemba, 2005.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Rais. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia na kuzungumza katika Bunge lako Tukufu, naomba nami niungane na wenzangu kuwapongeza viongozi mbalimbali walioteuliwa na kuchaguliwa katika ngazi mbalimbali za uongozi.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii pia naomba kuwashukuru kwa moyo wa dhati wanawake wa Mkoa wa Manyara kwa kuonyesha imani yao kubwa kwangu na kunipa kura nyingi kuniwezesha kuwa Mbunge wao wa Viti Maalum.

Aidha, nachukua fursa hii pia kumpongeza na kumshukuru sana Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kuongeza idadi ya wanawake Bungeni, suala lililonipa

msukumo wa kugombea Ubunge na hatimaye kuingia Bungeni. Si hilo tu bali kwa niaba ya wanawake wa Mkao wa Manyara na wanawake wa Tanzania kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuteua Mawaziri na Naibu Mawaziri wengi kushika Wizara mbalimbali na tena Wizara nyeti katika uongozi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pondezi na shukrani hizo, naomba sasa nichangie hotuba ya Rais kama ifuatavyo:-

Kwanza niseme naiunga mkono hotuba hiyo nzuri na yenye changamoto kwetu Wabunge na watekelezaji wote wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia mawazo kuhusu suala zima la uvezeshaji wa jamii, kiuchumi, hususan wanawake na vijana na kwa hakika, tunampongeza na kumshukuru kwa kulipa suala hili kipaumbele katika Awamu ya Nne ya utawala wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea napenda, kwa niaba ya wanawake wa Jimbo la Monduli ambako nimefanya kazi ya kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa miaka 14 napenda kumpongeza sana na kumshukuru sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa. Leo hii ninapozungumza, Monduli kuna mfano wa kuigwa kutokana na jitihada za Waziri Mkuu, ambako jumla ya shilingi bilioni moja na milioni 962 zimetolewa kama mikopo kwa wanawake wapatao 5,000 hadi kufikia Desemba 2005. Kwa mfano huo wa Monduli basi, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kiongozi wa kuigwa, aliyevalia njuga maendeleo ya wanawake kuanzia Jimboni kwake na kwa nafasi aliyopewa ya kuwa Waziri Mkuu, sisi wanawake wa Tanzania tuna matarajio makubwa ya kuwa Mheshimiwa Edward Lowassa atakuwa mkombozi wetu.

Mheshimiwa Spika, suala la uvezeshaji wanawake kiuchumi hususan kwa kuwapa mikopo, ni njia mojawapo ya kuwakwamua katika lindi la umaskini. Lakini naomba shughuli hizi za kuwakopesha akinamama, zitanguliwe na kujenga mazingira ya kuruhusu ufanisi ili kusiwe na vikwazo katika urejeshaji. Kwa mfano, vijiji vingi Tanzania hakuna umeme. Huko Mkoani Manyara, ni Makao Makuu tu ya Wilaya, lakini ukienda kwenye Tarafa, Kata na Vijihi hakuna umeme, tatizo la maji ndilo halisemekii. Wanawake wanatumia muda mwingi kutafuta maji. Baadhi ya barabara za vijijini hazipitiki kuruhusu kufanya biashara kwa urahisi. Kwa kifupi, bila mazingira ya kuruhusu kufanya biashara ili mikopo iweze kurejeshwa kwa ufanisi, uvezeshaji huo kiuchumi utapata vikwazo kiutekelezaji.

Mheshimiwa Spika, bila chakula cha kutosha cha familia hasa watoto, wanawake watatumia hiyo mikopo kwa kununua chakula na hatimaye kutoweza kurejesha.

Mheshimiwa Spika, hii ni mifano michache ya mazingira ambayo, bila kushughulikiwa na hatimaye kuboreshwa ili wanawake waweze kufanya biashara ndogo ndogo, shughuli ya utoaji mikopo haitakuwa na ufanisi na hatimaye kuathiri pia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kurudia kuwa naiunga mkono hotuba ya Rais wetu na nina hakika imeonyesha dira ya kuifuata ili nchi yetu iendelee kwa ari, nguvu na kasi mpya. Naomba kuwasilisha.

MHE. MOHAMED ALI SAID: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe binafsi na pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na wananchi wa Majimbo wanayoyawakilisha kwa ushindi mkubwa. Mimi pia niwashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo langu la Mgogoni kwa heshima kubwa sana walionipa kwa kunichagua mimi kuwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, nichangie mambo mawili, kwanza, suala la kilimo, suala la kilimo lipewe kipaumbele katika nchi yetu. Tunaiomba Serikali ielekeze nguvu zake zaidi, zile sehemu ambazo ni zenye kupata mvua na zilizo na mito na maziwa, kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwa vile nchi yetu ni yenye ardhi nzuri, hivyo basi, tulime kilimo cha umwagiliaji na zile sehemu zenye mvua basi ni vyema pia tujenge mabwawa kwa wingi ili tuhifadhi haya maji ya mvua yasipotee, na tuyatumie kwa shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kuchangia, ni kuhusu mpasuko wa kisiasa Zanzibar. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuliona hilo. Hii inatokana na umahiri, busara na hekima alizo nazo.

Mheshimiwa Spika, Wapemba hawana ugomvi na CCM kwani hivi sasa wako Wapemba ambao ni CCM. Lakini hata hao walio CCM na wao itafika wakati watachoka. Hii inatokana na ubaguzi mkubwa uliomo ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ya kuwabagua Wapemba.

Mheshimiwa Spika, SMZ imewabagua Wapemba na kuwafanya kuwa hawana haki hata kidogo katika Serikali hii ya SMZ. Kwa mfano, katika mgawanyo wa madaraka, ilikuwa ni vyema basi Waziri Kiongozi atoke Pemba au katika Mawaziri waliomo Serikalini, basi japo Mawaziri wanne angalau watoke Pemba. Wakuu wa Mikoa ni watano basi wawili watoke Pemba. Makatibu Wakuu na Wakurugenzi pia pangkuwa na mgawanyo japo mdogo kwa Wapemba. Kutokana na hao hao CCM waliomo Pemba.

Mheshimiwa Spika, ubaguzi kwenye elimu, wanafunzi wa Pemba hawawezi kupata uhamisho kwenda Unguja. Lakini mwanafunzi wa Unguja anapata uhamisho kwenda Pemba. Ubaguzi kwenye mawasiliano, mfano barabara nydingi sana zinajengwa Unguja na sekta zote zina ubaguzi mtupu.

Mheshimiwa Spika, ninaliomba Bunge lako Tukufu kama wazee, pamoja na watu wengine wenye hekima, wamsaidie Mheshimiwa Rais, kuuondosha mpasuko huu wa kisiasa uliopo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa kutoa pungezi kwa kuchaguliwa kwake na kuunda Baraza la Mawaziri lenye matumaini makubwa ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Pia nakupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge letu na Mheshimiwa Anne Makinda, kuwa Naibu Spika, natoa pungezi za dhati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Rais kwa asilimia mia moja.

Kwa kuwa katika hotuba ya Rais amesisitiza kuboresha sekta ya afya na kuleta afya bora kwa kila Mtanzania, Mkoa wa Mtwara ni mionganoni mwa mikoa ambayo huduma za afya ziko nyuma kwa kuwa na zahanati chache na hospitali za Wilaya zenyne watumishi wachache na wataalam kidogo ukilinganisha hali ya magonjwa mbalimbali na yanayohitaji madaktari wenye ujuzi kwa kukosa wataalam watu wengi wanapoteza maisha kwa kukosa uwezo wa kwenda Hospitali za Rufaa. Hivyo tunaomba watu wa Mkao wa Mtwara tufikiriwe kupata Hospitali ya Rufaa ili kuweza kunusuru maisha ya wananchi ambao hali zao ni duni.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara ni mionganoni mwa Wilaya ambazo ina tatizo kubwa la maji mjini na vijiji. Tatizo ambalo linapelekea kuwa na magonjwa ya matumbo mara kwa mara kwa kutumia maji ya kuokota. Pamoja na Serikali kuwa na mpango wa mradi wa maji Mbwinji, lakini bado tuna vijiji vya Kata ya Lukuledi, Chingulungulu, Namajani, Lisekese ambavyo ndiyo tegemeo la vijiji vyenye maeneo ya kilimo na ndiyo wanaovuna kwa kiasi kikubwa na kulisha mji wa Masasi. Lakini ndiyo vijiji ambavyo vina shida kubwa ya maji. Kwa mfano, Chiwale, Mpanyani, Mihima, Mraushi, Nambawala kwa sehemu kubwa kuanzia mwezi wa nane hutumia chakula kubadilishana na maji na baadae kuwasababishia kuwa na upungufu mkubwa wa chakula, hivyo basi kwa kuwa Chiwale kuna bwawa la asili ambalo linahitaji ukababati na Mihima kuna bwawa ambalo lilianza kujengwa na *Red Cross* na hawakuweza kumalizia kwa kwisha mkataba tunaomba Wizara isaidie ukarabati wa mabwawa haya mawili ili kuweza kunusuru hali mbaya ya maji iliyopo katika vijiji hivyo kwani ni kero ya miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, ili kuharakisha maendeleo ya jamii inabidi kuwe na utawala bora na mtawala awe na eneo ambalo anaweza kuwafikia wananchi ili kuhamasisha maendeleo. Katika Wilaya ya Masasi kuna Kata ambazo ni kubwa sana ambazo unaweza kuzigawa zikapatikana hata Kata tatu na Kata hizo ni Kata ya Lukuledi , Kata ya Lisekese na Kata ya Nangomba.

Mheshimiwa Spika, ni kipindi kirefu zimeombewa kugawanywa lakini Wizara haijachukua hatua yoyote ya kuzigawa. Ikumbukwe kwamba Madiwani hawana usafiri hivyo kutumia baiskeli katika kutembelea vijiji vyao na kuwawia vigumu katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Kwani Halmashauri huwa haizingatii ukubwa wa Kata

katika kugawa miradi ya maendeleo hivyo kuonekana kutotosheleza huduma katika Kata hizo. Hizi Kata ni sawa na Tarafa au Majimbo katika maeneo mengine, hivyo tunaomba Wizara iangalie umuhimu wa kuzigawa hizo Kata tatu zilizopo Wilayani Masasi ili kuleta ufanisi katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante kwa kupokea hoja zangu.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kupata na kushinda kwa kura nyingi sana na vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na kupita kwa kura nyingi za Bunge. Natoa pongozi kwa Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kushinda kwa kura nyingi. Nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri na Wabunge wote.

Naanza kwa kuchangia katika kilimo katika Jimbo la Solwa bado wananchi wanatumia zana za zamani sawa na katika sera na Ilani yetu ya CCM tuliahidi kwamba watapata mikopo na ikumbukwe wakulima ni waoga kuchukua mikopo kwenye mabenki hata kama wana hatimiliki na vile vile mabenki yako mbali sana na wakulima. Naomba Wizara husika ijaribu kufikiria mikopo itoke moja kwa moja lazima kuitia Halmashauri na Serikali iwe mdhamini katika kutoka mikopo kwa wakulima.

Vile vile kwa kuwa kila inapotokea ukame Shinyanga na Wilaya zake hukumbwa sana na baa la njaa, naomba Wizara husika izingatie hasa katika kujenga *dam* zitakazoweza kufanya wakulima walime kilimo cha umwagiliaji vyanzo vya maji viko na maeneo ambayo hakuna basi tuchimbe visima kwa umwagiliaji.

Sasa naomba nichangie katika barabara za vijiji ni kwani inachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza masoko kwa wakulima wakati wanapotaka kupeleka mazao yao kuuza kwenye masoko au wakati wanunuza wataweza kuja kiurahisi kwa wakulima kununua mazao. Naomba Wizara husika izingatie sana kwani karibu miaka 40 barabara hizo hazijatengenezwa, nina vijiji 116 katika Jimbo la Solwa.

Naomba nichangie katika elimu hasa shule za sekondari za Wilaya ya Shinyanga Vijiji wapo wanafunzi wengi wameshinda lakini wamekosa nafasi ya kwenda sekondari kwa sababu sekondari ni chache mno. Kwa sasa tunakihitaji sekondari 10. Naomba Wizara husika iangalie na kuchangia kwa kiasi kikubwa kwani sasa hali ya ukame imewafanya wananchi wakose hata mchango wa kuchangia kujenga sekondari. Elimu ya sekondari inasaidia kutoa elimu ya kupunguza mauaji ya bibi vizee wanaouliwa hovyo.

Mwisho naomba nichangie kwa kuwa sasa bomba la maji linajengwa kuja Shinyanga kuitia Solwa na kwa kuwa barabara ya lami inajengwa kuja Shinyanga na Mikoa mingine, naomba sasa Mkoa wa Shinyanga uchaguliwe na utengwe, uwe Mkoa wa viwanda wa Mikoa ya Kanda Ziwa. Shinyanga iko katika sehemu nzuri ambayo imezungukwa na mikoa jirani hivyo kufanya mikoa hiyo kufika na kutoka Shinyanga

ikizingatiwa tuko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, itakuwa imesogeza huduma na bidhaa kufika haraka Kenya na Uganda, soko la ndani ni kubwa sana ambalo inaweza kukidhi na kununua bidhaa zitakazozalishwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna soko kubwa sana la nchi jirani kama vile Burundi, Rwanda, Kongo na sehemu ambayo inaweza kufaa kutenga eneo la viwanda ni Wilaya ya Shinyanga Vijijini kwa sababu ya kuepuka msongamano wa magari mjini na vile vile itakuwa karibu na bomba la maji. Kama nitahitajika niko tayari kushirikiana kuandaa ripoti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais na ahsante sana.

MHE. FRED M. TUNGU: Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambazo Serikali inatakiwa kuchukua ili kuboresha sekta ya maji ni kuimarisha ofisi za maji za mabonde kwa kuongeza wafanyakazi. Wafanyakazi ni wachache, lakini pia maslahi ya maafisa wa maji wa mabonde ni hafifu.

Aidha, upotevu wa maji kwenye Mamlaka za Majisafi na Majitaka upunguzwe. Kwa sasa kati ya asilimia 30 hadi 61 ya maji yanayochukuliwa kutoka kwenye vyanzo yanapotea kabla ya kuwafikia walengwa. Upotevu huu upunguzwe.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira kwa vijana, wakati wa Kampeni Mheshimiwa Makamu wa Rais aliwaahidi wananchi wa Kishapu juu ya Serikali kujenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Kishapu. Kupitia Bunge lako Tukufu naomba kuikumbusha Serikali juu ya umuhimu wa kutekeleza ahadi hii, kwa mtazamo wa dharura vijana katika Wilaya ya Kishapu hawana ajira. Kujengwa kwa chuo cha *VETA* kitawasaidia kupata elimu ya ufundi na kuweza kujajiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, Kishapu ni moja ya Wilaya kame nchini, lakini yapo maeneo ambayo yanafaa kwa kilimo mfano Kata za Itilima na Talanga ambazo kilimo cha umwagiliaji kinaweza kufanyika. Wananchi wa Kata hizi wasaidiwe kuboresha mitaro ya umwagiliaji ambayo wamechimba. Aidha, tatizo la barabara lishughulikiwe. Kata hizi zina matatizo ya ubovu wa barabara ili ziwasaidie wananchi kupeleka mazao.

Bila mawasiliano mazuri, maendeleo mahali popote yatasuasua. Wilaya ya Kishapu ina tatizo la barabara ambazo nyingi hazipitiki wakati wa masika. Naomba Serikali ishughulikie barabara ya kutoka Bunambiyu kupitia Bubiki, Seke, Wishiteleja, Idukilo hadi Mhunze. Barabara hii ni muhimu kwa maendeleo ya Wilaya ya Kishapu. Aidha, naomba Serikali itekeleze ahadi iliyotoa ya kujenga barabara ya lami kutoka Maganzo kupitia Mhunze kwenda Maswa.

Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa makusudio yake ya kulipa suala la Hifadhi ya Mazingira kipaumbele. Kweli miti inakatwa na misitu inateketea na kuleta ukame. Lakini ukame huu inawezekana unasababishwa na kuongezeka kwa joto duniani (*global warming*). Kutokana na kuongezeka kwa gesi za *carbon dioxide* na *Methane* (*CO₂* na

CH4). Kwa mtazamo huu, yapo maeneo yatapata ukame kwa muda mrefu. Serikali ichimbe malambo na mabwawa maeneo haya na Wilaya Kishapu ikipewa upendeleo. Kuna maeneo yatapata mvua nyngi. Maeneo haya yalime mazao yanayostahili mvua nyngi.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Serikali ilitazame suala la uchafuzi wa mazingira unaotokana na taka za sumu zinazotokana na bidhaa zilizotengenezwa na madini ya mionzi. Taka za sumu zinazotokana na bidhaa au vifaa vyenye madini ya mionzi zinaongezeka kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya vifaa hivyo kwa mfano betri za magari, betri za simu za mkononi, vifaa vya Kompyuta, televisheni. Taka za sumu zinatokana na madini ya mionzi zikiingia kwenye mazingira na mfumo wa chakula zitaleta athari kubwa kwa afya ya binadamu, mfano magonjwa ya kansa, ulemavu, mtindio wa ubongo na kadhalika. Serikali iangalie utaratibu wa kutupa kitaalam taka hizi.

MHE. FELIX N. KIJKO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kabla sijaongea lolote, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi wa kishindo alioupata kutoka kwa Watanzania katika Uchaguzi Mkuu uliopita. Pongezi zaidi naziwasilisha kwa ushindi wa Spika pamoja na Naibu Spika. Pongezi zaidi zimfikie Waziri Mkuu kwa ushindi mkubwa alioupata kwa kuungwa mkono na Wabunge baada ya jina lake kupitishwa ama kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa basi nichukue nafasi hii kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Muhamwe walionichagua kwa kura nyngi na vile vile niwashukuru wananchi wa Jimbo la Buyungu ambao wote kwa pamoja wameweza kutuchagua sisi Wabunge wawakilishi wao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi na mwenzangu ambaye ni Mbunge na Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kibondo yeny Majimbo mawili ya Muhamwe na Buyungu ni mionganini mwa Wilaya za Mkoa wa Kigoma ambazo wananchi wake wanaishi kwa kutegemea kilimo cha mikono.

Mheshimiwa Spika, ni kwa mantiki hiyo Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake zinajitosheleza kwa chakula kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya hiyo yeny Majimbo mawili niliyoyataja wanakabiliwa na matatizo yafuatayo:-

(i)Barabara za Vijijini kwa ajili ya kusafirishia mazao ni mbaya. Hiyo ni kutokana na fedha kidogo inayotolewa kwa Halmashauri za Wilaya na *TANROAD* ni kidogo mno. Aidha, usimamizi wa matumizi ya fedha na ubora wa kazi ni duni sana. Nashauri Halmashauri ziongezewe fedha za kutosha kukidhi matengenezo ya barabara hizo ili mazao yaweze kutoka vijijini hadi kwenye *centres* za mauzo.

(ii)Ulinzi na Usalama, ni tatizo lingine linalochangia hali ya usalama kwa Majimbo hayo kuwa mbaya zaidi. Mipaka bado inapitisha wahamiaji haramu ikiwa ni

pamoja na silaha. Udhibiti unaofanywa na polisi hautoshi na matokeo yake mauaji ya kila wakati yanayotokana na ujambazi hujitokeza.

Mheshimiwa Spika, nashauri vyombo vyao ulinzi viongezewe watumishi wa kuweza kukabiliana na hali hiyo.

(iii) Wilaya inakabiliwa na tatizo kubwa la kutokuwa na maji.

(iv) Wilaya haina umeme tangu Wilaya hiyo ilipoanzishwa miaka 44 iliyopita.

(v) Makundi ya vijana, wajane na walemvu wanaishi maisha magumu kutokana na kukosekana kwa mikopo ya fedha.

(vi) Nimepigwa simu na wananchi kuhusu wananchi na Wilaya kuzuiwa kuchoma mkaa pamoja na kuuza kuni kwa matumizi ya nyumbani kwa madai waliyoelezwa kuwa ni amri kutoka Wizarani. Naomba Waziri aingilie kati jambo hili kwa sababu vyote hivyo ni vitu muhimu kwa matumizi ya nyumbani badala ya umeme ambao haupo.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuunga mkono hoja ya Rais.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi, Naibu wako, kwa ushindi wa heshima mlioupata wakati wa kura za uchaguzi kwenye Majimbo yenu. Pili kwa kuchaguliwa kuongoza Bunge hili kwa kura nyingi sana.

Nampongeza kwa dhati Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa ushindi wake wa *Tsunami*. Sote tunajivunia ushindi huo pamoja na ushindi wa Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu kwa kura nyingi sana za kumthibitisha! Nawapongeza pia Mawaziri, Manaibu, Wakuu wa Mikoa na kadhalika walioteuliwa. Tuwatake mfanye kazi ya nchi kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais katika hotuba yake Bungeni.

Nawashukuru wapiga kura wangu wa Mjini Sumbawanga kwa kuniamini tena kuwaongoza. Naomba kati ya yote yalizungumzwa nishauri yafuatayo:-

Kwanza, Ilani ya Uchaguzi isambazwe kwenye Taasisi zote za Umma na ipewe mpangilio wa utekelezaji wake na kila baada ya mwaka, taarifa ya utekelezaji wake ionyeshwe.

Pili, barabara zilizoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi kwa kuwekewa lami ni pamoja na ile ya Tunduma - Sumbawanga. Ilani imeiweka barabara hiyo kipaumbele kuliko mingine yote! Nashauri tuanze na hilo.

Mheshimiwa Spika, tatu, barabara ya kuunganisha Uvinza, Kasuku, Kibondo hadi Bukoba ipewe kipaumbele ili iungane na jirani zetu wa Uganda.

Nne, barabara ya kwenda Kasanga kwenye Ziwa Tanganyika ili tufanye kazi ya biashara na Kongo, Rwanda, Burundi na Zambia. Barabara hizi zipewe pia kipaumbele kwenye mpango wa barabara za Afrika ya Mashariki!

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge lako likubali *IPTL* inunuliwe na Serikali ili tuwe na uwezo wa kudhibiti gharama zake zisizo za lazima. Pia nashauri tuiangalie upya *Songas* na mikataba yake. Fedha zilizotumbukizwa ndani ya mradi huu na ni hisa kiasi gani tulizonazo katika mradi huu na nini hatma ya mchango huo kwa maendeleo ya baadaye ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, bado suala la kupitia upya baadhi ya miradi na mikataba yake ili kuondoa wasi wasi unaojitokeza!

Mheshimiwa Spika, tupange mkakati wa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi haraka iwezekanavyo ili kusiwe na kisingizio cha kutoelewa tafsiri ya Ilani!

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais, isiishie hapa Bungeni lakini taasisi zote na vyuo mbalimbali wakiwemo Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi wakutane na kujadili kero za Muungano na mbinu za kuleta maendeleo ya uhakika katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kuimarisha ulinzi wa wananchi wenyewe ili kusaidiana na askari katika ulinzi wetu. Mgambo na sungusungu waanze kufufuliwa na mafunzo yaendelee! Polisi wasiposaidiwa na wananchi hawawezi kukabiliana peke yao na wimbi hili la ujambazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hifadhi ya Mazingira katika Mkoa wa Rukwa upewe uzito unaostahili, tutake, tusitake, lazima tuonyeshe hatari iliyo mbele ya Mkoa huo baada ya wafugaji kuingia na kuvamia Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mkoa wetu uangaliwe kwa macho mawili kwa suala la elimu. Tupewe kila aina ya msaada ili walimu wapatikane wa kutosha, sekondari ziongezwe za kutosha na vyuo vya ualimu vianzishwe!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Rais kwa nguvu zangu zote!

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi za dhati kwa ukubwa alioupata Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Waheshimiwa Wabunge, Wawakilishi na Madiwani wote wa CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kutoa pongezi maalum kwa Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Samuel Sitta, Mheshimiwa Anne Makinda, Mawaziri na Naibu Waziri wote, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Wakuu wote, Wenyelevi wa Kamati za Bunge na viongozi wengine wote waliochaguliwa au kuteuliwa kushika dhamana za uongozi katika ngazi za juu. Ninawataenia kheri, mshikamano mwema na mafanikio

mema. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkinga, napenda kuwahakikishia ushirikiano wetu kamili.

Mheshimiwa Spika, naomba fursa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mkinga kwa kunipa ushindi mkubwa na ridhaa kwa CCM kuendeleza kuongoza jimbo hilo. Napenda kuwaahidi kwamba nitawatumikia kwa uwezo wangu wote ili kuleta maendeleo ya kasi kubwa Jimboni humo na nchini kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkinga, napenda kuishukuru sana Serikali ya CCM kwa kuidhinisha Wilaya mpya ya Mkinga. Ni matumaini yangu kwamba Wizara na taasisi mbalimbali zitatoa ushirikiano kamilifu katika kujenga miundombinu, kuboresha huduma na kuipatia mahitaji yake yote muhimu Wilaya hii changa na nyenye kiu kubwa ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla, naomba sasa nijikite katika hoja ilio mbele ya Bunge lako Tukufu. Hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, Bungeni tarehe 30 Desemba, 2005 ni tafsiri fasaha na mwongozo thabiti kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Hotuba hiyo inaelekeza kwa umahiri mkubwa kuhusu utekelezaji sahihi wa maeneo yote yaliyo katika Ilani pamoja na ahadi mbalimbali zilizotolewa wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hotuba hiyo sio tu ina mvuto mkubwa bali pia ni changamoto nzito kwa viongozi wa ngazi mbalimbali na wananchi kwa jumla. Hotuba hiyo imeleta matumaini makubwa kwa wananchi. Waheshimiwa Wabunge wengi wameijadili hotuba hiyo kwa kina na takribani masuala yametolewa michango ya kutosha, hivyo mimi ningependa kuwekea mkazo masuala matatu ambayo hayakupata msisitizo wa kutosha.

Kwanza ni utekelezaji thabiti na wa kisayansi kuhusu mwongozo ultolewa na Mheshimiwa Rais ndio tegemeo pekee la kuleta tija na ufanisi unaotarajiwa. Sera, mikakati na programu zinazotokana na dira, Ilani na mwongozo zielekezwe kwa Wizara, Taasisi, Mikoa, Wilaya, Kata na hata katika kaya kwa malengo yaliyowazi kwa vipindi maalum pamoja na vigezo vya kupimia matokeo. Mbinu ya ushindani ikitumika vizuri ni kichocheo kizuri cha kuongeza ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Ni kwa utaratibu huu ndiyo malengo makuu mawili ya kujenga uchumi wa kisasa wa nchi inayojitegemea ya kuwawezesha wananchi kumiliki uchumi wa nchi yao na hivyo kuwawezesha kila Mtanzania kuwa na maisha bora. Utaratibu niliodokeza hapo juu utaleta mafanikio ikizingatiwa kuwa Tanzania ina neema tele.

Mheshimiwa Spika, pili, katika kitabu cha Sera ya Wananchi kiuchumi imenorodhesha mifuko saba, si wananchi wengi na pengine hata viongozi wengi wenye ufahamu kuhusu MKUKUTA, MKURABITA na mipango mingineyo inayokusudiwa kuwafaidisha wananchi. Uwazi zaidi, elimu na utekelezaji bora ni muhimu kwa kufanikisha matarajio.

Tatu, mara nyingi wananchi wanakatishwa tamaa kwa kucheleva kufika kwa fedha au vifaa kwa wakati. Aidha, upungufu mkubwa wa watumishi, kama vile

madaktari au walimu, baada ya miradi kama hospitali, zahanati, nyumba zinakamilika bila wanaotarajiwa kuhusika na miradi kuwasili kwa muda mrefu. Ni vyema hatua thabiti zichukuliwe kurekebisha hivi. Aidha, wataalamu wa kilimo, uvuvi, misitu na kadhalika wasibaki mijini bali wafike vijijini kusaidia wakulima, wavuvi wafugaji na kadhalika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia ningependa kugusia kwamba Wilaya changa ya Mkinga ina kero nyingi sana zikiwemo maji, miundombinu, kiwango kidogo cha elimu, umaskini wa mapato, maradhi na mengineyo mengi ambayo yanaifanya Wilaya hiyo kupata vipaumbele maalum. Ni matumaini yangu hali hii itatazamwa kwa kipaumbele kinachostahili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI: Napenda kumpongeza Rais Jakaya Kikwete kwa hotuba yake nzuri, aliyoandika wakati akiwa na nia ya kutumikia nchi hii, akiwa na nia ya kuona kama walivyotulia wananchi walioko Kisiwa cha Ukerewe, Ukara na Kisiwa cha Mafia basi aonekana angependa Visiwa vya Unguja na Pemba viwe katika utulivu wa aina moja.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais alivyovipongeza vyombo vya ulinzi kwa kazi nzuri waliofanya wakati wa uchaguzi. Naomba kuuliza hivi vyombo vya ulinzi ni pamoja na vile vilivyoletwa kule Unguja na Pemba au askari walioletwa kule sio hawa wetu? Kwa sababu walikuwepo Pemba kazi kubwa waliofanya ilikuwa ni kuwapiga wananchi, kuwabaka vizee na watoto amba ni dogo sana kiumri. Je, hongera anazotoa Rais kwa vyombo vya ulinzi ni kwa kufanya kashfa na kuwapiga Wapemba na Waunguja?

Mheshimiwa Spika, tunayo mifano ya watu wa kawaida waliouliwa, askari waliouliwa na hata kiongozi wa nchi (Marehemu Abeid Karume) lakini hawakuteswa wananchi wa mji mzima au kuwekewa visasi waliokuwa Vyama vya Upinzani. Wale waliotiliwa mashaka walikamatwa na upelelezi ulifanyika. Mwisho wa kesi waliokuwa wahalifu walihukumiwa.

Mimi nakumbuka aliwahi kuuliwa mwanachama wa Chama Tawala katika eneo ambalo ilikuwa ni *stronghold* ya Chama cha Upinzani (enzi hiyo ni *Afro Shirazi*) Chama Tawala hakikichukua hatua ya kuteketeza kijiji kizima ambacho mwanachama wao aliuliwa. Serikali hiyo ya ZNP (*HIZBU*) ilijaribu kufanya upepelezi na waliposhindwa waliagiza askari wataalam kutoka Ulaya amba wakiitwa *Scotland Yards*. Wakati wa upepelezi watu wanne waliwekwa ndani na mwisho mtu mmoja alitiwa hatiani na watatu wakaachiwa huru.

Mheshimiwa Spika, Mpemba sasa akisema heri wakati wa Ukoloni, je, atakuwa amekosea? Mheshimiwa Rais katika hotuba yake amesema anataka kujenga demokrasia ya kweli. Kama hivyo ndivyo, basi namshauri Rais aunde Tume ikachunguze kama askari yule kweli aliuliwa na wanakijiji cha Piki? Pili, Tume pia ikaone kama ni kweli

watu wamepigwa, kuumizwa na kubaka wasiokuwa na hatia katika sehemu za Mji Mkongwe, Bumbwini, Tumbatu na Piki huko Pemba.

Mheshimiwa Spika, naamini Rais Jakaya Kikwete anayo nia ya kweli katika kuleta maendeleo ya nchi hii. Maana rushwa iliyoota mizizi katika nchi hii inamuudhi kama alivyoonesha katika ukurasa wa 8 wa hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, rushwa imekithiri kiasi kwamba Watanzania sasa hawaiangalii rushwa kama ni kosa la jinai. Rushwa ilitiliwa mbolea na utawala uliopita na mwisho sisi Wapinzani tukilalamika, tunaambiwa tuna wivu wa kike na Waandishi wa magazeti wakiitwa waongo.

Mheshimiwa Spika, yote hiyo kuupa mwanya mkondo wa rushwa uendelee. Lakini enzi ya Baba wa Taifa aliwachukia sana wala rushwa na Baba wa Taifa mtu yejote akiomba uongozi basi alikuwa akifuatilia historia ya mwombaji uongozi na endapo akigundua kwamba ana utajiri ambaa hauelezeki, basi huyo hatapewa nafasi hiyo na Baba wa Taifa alikuwa anatoa hadharani kwa nini fulani hafai kupewa uongozi, maana mtu kama huyo ataiangamiza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna sheria ambayo unapochaguliwa na kuwa Mbunge au ukishika nafasi ya uongozi huwa unatakiwa kujaza fomu na uweke bayana mali uliyonayo.

Mheshimiwa Spika, viongozi wanapoondoka madarakani lazima, napendekeza wapewe fomu za kuweka bayana mali aliyopata wakati wa uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, napendekeza hivyo kwa sababu alipoingia madarakani Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa aliweka bayana mali aliyokuwa nayo. Nakumbuka ilitoka katika magazeti kwamba ana nyumba moja Dar es Salaam shamba la korosho lenye ekari 10 na shamba moja ambalo halijaendelezwa. Lakini hivi sasa tunasikia mitaani kuwa Mstaafu huyu ana mali ya kutosha, nje na ndani ya nchi, eti ana kijiji Lushoto ambacho amejenga hadi *Air strip*. Haya yanaweza kuwa ni uongo, lakini laiti angeweka bayana mali yake wakati alipotoka, basi jamaa wa mitaani wasingekuwa na nafasi ya kumpaka matope Mstaafu huyo.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 18 wa hotuba yake Mheshimiwa Rais amesema kuna mpasuko kati ya Unguja na Pemba na hata kati ya Pemba na sehemu nydingine za Bara na mfano aliota ni kwamba katika uchaguzi uliopita eti kwa sababu CCM hawakupata kitu.

Mheshimiwa Spika, je, CCM wangepata viti vyote Pemba Rais angesema kwamba kuna mpasuko? Kigoma kuna CHADEMA, Bariadi kuna UDP, Moshi na Karatu wamechukua CHADEMA. Je, mbona hasemi kuwa huko kuna mpasuko? Mbona Mheshimiwa Rais Wapemba wamezagaa Bara. Mheshimiwa Rais asisahau kwamba Wanyamwezi na Wasukuma wamejaa Pemba. Sasa mbona tena kunatumika lugha ya kibaguzi?

Mheshimiwa Spika, swali la UKIMWI ni nyeti na napendekeza sisi Wabunge na viongozi wengine tujitolee bila ya uoga tupimwe ili ikiwa bahati mbaya kiongozi amekutwa *positive*, basi apewe dawa za kusaidia kuongeza kinga za mwili na kurefusha maisha.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka msisitizo kuhusu suala la UKIMWI, ni bora hili litungiwe sheria.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili alikuwepo mbunge mmoja aliiwa Mbatia, naye alipendekeza kwamba Wabunge wanapoingia Bungeni ingekuwa ni busara wapimwe vichwa vyao. Sio ukubwa wa kichwa bali ndani ya kichwa mna nini? Sasa ndio naona umuhimu wa Wabunge kupimwa afya zao.

Mheshimiwa Spika, Rais Jakaya Kikwete ajitayarische kuja kuwaomba radhi CCM wa Pemba, maana nao pia walipigwa, watoto walibakwa, mali zao pia ziliibiwa ili mwaka 2010 Rais asije akalalamika juu ya mpasuko kuwa umepanuka, maana wapo CCM waliokula kiapo baada ya watoto wao kubakwa, hawataipa tena kura CCM.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, amani na utulivu katika nchi yetu ni jambo la kulindwa kwa nguvu zetu zote. Yeyote anayejaribu kuvunja amani na utulivu inabidi achukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, licha na hali iliyodhahirishwa na Mheshimiwa Rais katika hotuba yake juu ya amani na utulivu uliopo nchini bado katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 katika Jimbo langu la Mkoani wakati wa uandikishaji wa wapigakura vikosi vya SMZ katika kituo cha Ngombeni kwa kutumia risasi walimuwa mwanafunzi Juma Omar na kuwajeruhi Bakar Ali Bakar na Shaibu Abeid.

Mheshimiwa Spika, vikosi hivyo vilifanya ukatili huo kwa kutaka kuwalazimisha waandikishwe watu walioletwa kwa meli ya *MV Mapinduzi* kutoka Unguja kwa kisingizio kuwa wao ni KMKM.

Mheshimiwa Spika, mtindo huu wa kusafirisha watu kwa makundi kwenda kuijandikisha maeneo mbalimbali ni wa kawaida katika chaguzi za Zanzibar. Mwaka 2000 Jimbo la Mkoani kwa kisingizo cha kituo cha KMKM Makombeni ambacho ni kawaida huwa wakizidi askari 20 waliletwa watu wasiopungua 1,800. Watu hao waliletwa kwa meli wakaandikishwa na kurejeshwa Unguja siku ya pili yake.

Mheshimiwa Spika, mpaka ninapotoa mchango wangu huu kwenye hotuba ya Rais wa Awamu ya Nne waliosababisha mauaji na majeruhi hawajachukuliwa hatua yoyote ya kisheria. Kitendo hicho kinaashiria kuwa maisha ya binadamu si chochote si lolote.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi na wananchi wa Jimbo langu wanategemea makubwa kutoka kwa Rais wa Awamu ya Nne kuhusiana na tukio bayaa kama hilo. Ni

vyema Serikali ya Awamu ya Nne ikaunda Tume kuchunguza ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu hususan wakati wa mchakato wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali ya Awamu ya Nne katika kuwarejeshea imani ya uhai wao ifanye mambo yafuatayo:-

Kwanza, wale wote waliouwa na kujeruhi wapelekwe katika vyombo vyamini ya pili, wale waliojeruhiwa, Serikali iwalipe fidia na yule aliyefariki wazee wake walipwe fidia.

Katika ukurasa wa 7 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ameahidi kuwa hana nia ya kuviuva vyama vyamini ya siasa na pia katika ukurasa wa 8 Mheshimiwa Rais ameonesha kuwa ipo haja sasa Tanzania tuwe na maadili yatayotawala shughuli za kisiasa, ambayo hayategemei hiari ya viongozi wa kisiasa walioko madarakani.

Mheshimiwa Spika, kuwa na maadili ni jambo zuri lakini tufanye subira mpaka hapo tutapofanya uchunguzi juu ya utekelezaji wa sheria zinazoambatana na mfumo wa vyama vingi. Kwa uzoefu wangu inaonesha sheria hizo zipo kwa vyama vyamini ya upinzani katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, waliofukuzwa kazi, kuonywa kwa kisingizio cha kushiriki siasa mpaka sasa ni wale wanaoshukiwa huwa ni wapinzani. Wakati wafanyakazi ambao ni CCM wanashiriki katika siasa wazi wazi. Mfano katika jimbo langu wako wafanyakazi wa Serikali walikuwa mawakala wa CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama wa Taifa katika jimbo langu ni kawaida kuwepo katika matawi ya CCM kana kwamba ndizo ofisi zao. Vyombo vyamini ya vimetolewa kwenye siasa wao wamezama. Lakini kwa sababu wamezama katika CCM si hoja.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ndio iliyonifanya kwanza tufanye uchunguzi juu ya utekelezaji wa sheria hizo, dosari na marekebisho yake. Vinginevyo bila ya kufanya hivyo maadili hayo yatakuja kutumiwa kuwa vyama vyamini ya upinzani kinyume na matakwa ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Ninapendekeza iundwe Tume Teule itakayovishirikisha vyama vyamini ya siasa ili ifanye uchunguzi huo.

Mheshimiwa Spika, rushwa haiwezi kuondoka nchini kwa kuwashughulikia wala rushwa wadogo. Ninashauri ili wananchi warudishe imani kwa Serikali yao basi hatua za makusudi zichukuliwe kwa wala rushwa wakubwa. Wananchi washirikishwe na wahamasishwe huwataja kwa njia ya siri watumishi ambao kwa mali zao na mishahara wanayolipwa hayalingani.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nawashukuru wapigakura wangu wote wa Jimbo la Mkoani kwa kuniwezesha nikawa Mbunge. Pia ninaishukuru Kamati ya Kampeni iliyokuwa chini ya Meneja wake Mheshimiwa Amin Othman Sharif.

Mwisho zaidi ninaiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante.

MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kupata fursa ya kuingia katika Bunge hili. Pia kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Tumbe kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwawakilisha katika Baraza hili muhimu la kutunga sheria. Aidha, nawapongeza wote waliochaguliwa na au kuteuliwa kushikilia nyadhifa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe pamoja na Naibu Spika wako, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuongoza shughuli za Bunge. Baada ya utangulizi huo sasa naomba kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 30 Desemba, 2005 katika ufunguzi wa Bunge Jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ni hotuba ambayo kimuundo imegusa nyanja zote muhimu kwa maendeleo na usalama wa Jamhuri yetu na watu wake. Kwa hili nampongeza lakini uzuri wa hotuba hii, hata hivyo, hautakamilika endapo hautakuwa na utekelezwaji.

Mheshimiwa Spika, hotuba imegusa maeneo mengi lakini ambayo ningependa kuyachangia ni rushwa, kilimo, elimu, ajira, hifadhi ya mazingira, michezo na nishati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa rushwa pamoja na njia kadhaa ambazo Mheshimiwa Rais ameziainisha kuchukuliwa ili kupambana na rushwa, naomba kupendekeza kwamba Tume ya Maadili ya Viongozi iwe inahoji juu ya mali za viongozi wanaopata nafasi mwanzo wanapoanza utumishi wao na mali watakazokuwa nazo pale muda wao wa utumishi unapokoma. Serikali isisite kuwachukulia hatua wale amba mali walizozichuma katika kipindi hicho zitakuwa hazilingani na mapato ya halali waliyopangiwa kuyapata.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kilimo ningependa kuchangia kwa kuanza kusema kwamba pamoja na kuwa nchi yetu inakitegemea sana kilimo kwa uhai wa wananchi wake bado hakijapewa kipaumbele unaostahili. Bajeti ya Wizara ya Kilimo bado ni ndogo sana ambayo haiwezi kukidhi haja ya kufanya Mapinduzi katika suala la kilimo. Wataalamu wa kilimo ni wachache sana. Pembejeo za kisasa hazipo au hazitoshi pia tuna tatizo sugu la kukosa mbegu bora. Haya yanawapelekea wakulima bado kuendeleza na kilimo cha jadi ambacho hakitoshelezi licha ya kupata ziada. Serikali ielekeze au itoe fungu kubwa la fedha za Bajeti kwa Wizara ya Kilimo na mkazo uelekezwe kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa mikoa inayoruhusu kilimo hicho. Hii itaongeza uzalishaji na kusaidia ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Serikali imejitahidi kutoa elimu kwa Watanzania lakini elimu inayotolewa hata kwa wale wahitimu wa Vyuo Vikuu bado kwa kiasi kikubwa inaonekana haiwasaidii. Ni wengi amba wanabaki na shahada zao bila

kuwasaidia katika kupata ajira au kujajiri. Ni vyema sasa mitaala yetu ikalenga kutoa mafunzo ambayo mhitimu atakapomaliza mafunzo yake akaweza kujajiri badala kungoja ajira ya Serikali.

Suala la ajira limezungumzwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Hili ni muhimu sana na nathubutu kusema kwamba ukosefu wa ajira ndio shule inayofunza majambazi. Kukosekana kwa ajira kunawapelekea vijana kukimbilia maeneo ambayo wanajikuta ili kumudu maisha wanalazimika kuingia katika harakati za ujambazi. Tatizo hili litaondoka kwa kiasi kikubwa kwa kuanzisha shughuli zitakazowaajiri vijana. Tuwekeze kujenga viwanda vitakavyoshughulikia mazao ya baharini, vya kusindika matunda na nafaka mbalimbali, pia viwanda kwenye sehemu za migodi.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira limezungumzwa ili kutunza mazingira ni lazima pawepo sheria kali ya kuhifadhi mazingira itakayolinda kukata miti kiholela na itakayolazimisha watu kupanda miti.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya na michezo ni ajira. Tunapaswa Watanzania tusiichukulie kuwa michezo ni burudani tu. Ili tusiwe nyuma katika michezo, itabidi tujaze fikra kwa vijana wetu kuwa michezo pia ni sehemu ya ajira katika dunia ya leo hivyo tuwaandae kufikia lengo hilo kwa kuwawezesha kupitia Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa nishati katika maeneo mengi kumepelekea pia kupungua kwa uzalishaji na uwekeaji hasa katika maeneo ya vijijini. Vijijini ndiko ambako tatizo la ukosefu wa ajira umejichimbia. Ili kupunguza tatizo na uhamaji wa nguvu kazi ni vyama kwa awamu hii mkazo wa nishati ukaelekezwa vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Rais nikitegemea mawazo haya yatasaidia.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwashukuru wapigakura wote wa Jimbo la Musoma Vijijini kwa kunirudisha tena Bungeni bila kupingwa. Najua kwa dhati kabisa kwamba kupita kwangu bila kupingwa kunatokana na ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya iliyojitokeza Jimboni tangu niwe Mbunge wa Jimbo hilo kwa mara ya kwanza mnamo mwezi Oktoba, 2000.

Mheshimiwa Spika, ni nia yangu kuendeleza ari, nguvu na kasi hiyo tena katika kipindi hiki cha pili kinachoishia mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kwa niaba ya wapigakura wangu wa Musoma Vijijini nikupongeze wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa ushindi mkubwa mlioupati kwanza katika Majimbo yenu na pili ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na vile vile Rais wa Zanzibar

Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa ushindi mkubwa waliopata katika Uchaguzi Mkuu uliopita.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge katika Bunge lako Tukufu. Hali kadhalika nawapongeza viongozi wote ambao wameteuliwa kuwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wakuu wa Mikoa ambao wote kwa pamoja watamsaidia Mheshimiwa Rais kuendesha Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini pongezi maalum zimwendee Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania na baadae uteuzi huo kuungwa mkono kwa kishindo na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi Mheshimiwa Edward Lowassa, ni rafiki yangu wa karibu lakini mbali na urafiki wetu, najua ni mchapakazi, sote humu tunafahamu majukumu aliyonayo ni mazito na anahitaji ushirikiano wa karibu kutoka kwa Wabunge wote wa Bunge hili. Mimi ninamwombea afya njema ili aweze kuzimudu kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sijawasahau Wabunge wenzangu waliomo humu katika Bunge lako Tukufu. Kila mmoja wenu nampongeza kwa ushindi aliopata Jimboni kwakwe. Nasema hongereni sana!

Mheshimiwa Spika, kutohana na muda kuwa mfupi nitagusia jambo moja tu la muhimu katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu. Hili ni suala la elimu.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 30 Desemba, 2005 Mheshimiwa Rais wetu alitoa hotuba rasmi katika Bunge lako Tukufu wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge hili hapa Mjini Dodoma.

Wakati Mheshimiwa Rais anazungumzia huduma ya jamii, alizungumzia mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Nne kuhusu elimu kuanzia ukurasa wa 40 hadi 42. Katika utangulizi wake Mheshimiwa Rais alisema na namnukuu: “Hakuna Taifa lililopata maendeleo bila kuendeleza elimu. Hivyo kuendeleza elimu nchini itakuwa *agenda* muhimu ya Serikali ya Awamu ya Nne.”Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tangu enzi za ukoloni, Watanzania wamekuwa wakidai elimu iliyo bora. Lakini kwa muda mrefu hatujakoma kutafakari ni kwa nini tunaitaka na ni nini iwe madhumuni ya elimu hiyo tunayoihitaji.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba, ninukuu aliyosema Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1967 katika kitabu chake *Freedom and Socialism* (Uhuru na Ujamaa) ukurasa wa 268: “Tunapotafakari kuhusu suala la elimu huwa tunafikiria elimu kwa misingi ya kupata walimu, mainjinia, makarani, watumishi wa Serikali na kadhalika kwa mtu mmoja mmoja na kwa ujumla wetu tukiififikiria elimu kama mafunzo ya kutuwezesha kuajiriwa na kupata mishahara mikubwa.”Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tokea enzi za awamu ya kwanza, nchi yetu imekuwa ikitumia asilimia kubwa ya pato lake kila mwaka kuendeleza elimu. Katika hotuba yake Rais wetu pia amesisitiza nia yake kufanya hivyo tena kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya (Soma Ukurasa wa 41 – 42 ibara ya 3,5,6,9 na 11 ya hotuba yake. Lakini ni elimu ipi tunayoitaka?

Katika nchi maskini kama yetu ambapo tunatumia asilimia kubwa ya pato la nchi kila mwaka kwa ajili ya kuelimisha watoto wetu, hivi sasa ni wakati muafaka wa kuangalia upya suala zima la elimu katika namna ambavyo elimu itolewavyo iwanufaishe watoto wetu kuwa na uwezo wa kujiajiri na kujitegemea kwa mujibu wa jamii ambayo tunayotaka kuijenga.

Mheshimiwa Spika, muundo na madhumuni ya elimu hutofautiana katika jamii mbalimbali kutokana na jamii zenyewe kutofautiana kwa sababu siku zote elimu huwa ina nia na madhumuni fulani ya kufundisha kizazi kijacho, elimu ambayo itawawezesha kujitegemea katika jamii yenye maendeleo endelevu. Elimu tunayoihitaji kwa nchi yetu iwe ni elimui ambayo itamuwezesha atakaye hitimu awe na uwezo wa kujiajiri na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake mbele ya Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Rais wetu alizungumzia hatua kumi na moja ambazo Serikali ya Awamu ya Nne itazichukua ili kuendeleza elimu nchini. Katika hatua ya 9 na ya 10, Mheshimiwa Rais alieleza kama ifuatavyo:-

Hatua ya tisa ni: “Kujenga angalau Chuo Kikuu kingine kipyta na kumi, kuhakikisha kuwa mafunzo ya ufundi stadi yanaendelezwa na kuimarishwa kama mkakati wa kupambana na tatizo la ajira. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na hoja hizo za kujenga angalau Chuo Kikuu kingine kipyta na ya kuendeleza mafunzo ya ufundi stadi kama mkakati wa kupambana na tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hotuba hiyo, Mheshimiwa Rais wetu ukurasa wa 29-30, pia amezungumzia suala la kuendeleza kilimo kama njia/mkakati wa kupambana na tatizo la ajira katika nchi yetu kama ifuatavyo:- Nanukuu: “ ... kwa muda mrefu ujao, kilimo kitaendelea kuwa mhimili wa uchumi wa uchumi wetu. Sekta hii ndiyo inayoajiri watu wengi na ndiyo inayotuhakikishia upatikanaji wa chakula, bidhaa za kuuza nje na malighafi za viwandani.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa ninaomba kutumia fursa hii kuishauri Serikali kupitia Bunge lako Tukufu kwamba pamoja na hatua inazokusudia kuchukua kujenga angalau Chuo Kikuu kingine kimoja na mpango wa kuendeleza elimu ya ufundi stadi kama njia mojawapo ya kupambana na tatizo la ajira, Serikali pia iwe na mpango /mkakati madhubuti wa kujenga angalau Chuo Kikuu kingine cha Kilimo ambacho kitafundisha misingi ya elimu ya kujitegemea. Chuo Kikuu ambacho wanafunzi wake

watajifunza nadharia lakini kwa asilimia kubwa zaidi ya muda wao wote watakapokuwa chuoni hapo watatumia kwa kufanya kazi kwa vitendo wakishirikiana na wananchi, wakulima wadogo wadogo na wakubwa walio katika maeneo ya jirani na chuo chao na hata kwingineko. Mafunzo ambayo yatatumia utaratibu wa kujifunza kwa (kushiriki) kutenda kazi halisi na wakulima.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba gharama za kujenga chuo kikuu kimoja tu ni mzigo mkubwa kwa Serikali yetu kulingana na hali ya uchumi wetu. Lakini jawabu ya jinsi mojawapo ambapo Serikali inaweza ikafikia lengo hili imefafanuliwa vema katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 41, Ibara ya 7 kama ifuatavyo, nanukuu: "... Kutoa fursa na motisha kwa sekta binafsi, taasisi za dini na mashirika binafsi yanayowekeza katika elimu." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ni maoni yangu na Watanzania wenzangu wengi pia ambao wanaitakia mema nchi yetu kwamba kuwekeza katika chuo kikuu chenye kutoa elimu ya kilimo kwa utaratibu wa kujifunza kwa kutenda ni mkakati wa uhakika wa kukabiliana na tatizo la ajira kwa wananchi wetu katika siku za usoni. Sekta nyinginezo za binafsi za biashara na ajira Serikalini pekee haziwezi kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu. Vijana wetu wanaohitaji ajira hawawezi wakaajiriwa wote mijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba pia kutumia fursa hii kutoa ufanuzi kidogo wa dhana ya kujifunza kwa kutenda.

Mheshimiwa Spika, elimu ya kujifunza nadharia na kuirithisha kwa watoto wetu kwa vitendo ndiyo elimu ya jadi, si kwa nchi yetu pekee bali kwa Bara zima la Afrika. Katika hilo, Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere katika kitabu chake *Education for Self Reliance*, ukurasa wa 45 kilichochapishwa takribani miaka 6 tu baada ya kupata uhuru mwaka 1961 alielezea kama ifuatavyo, nanukuu: "... ingawa Bara la Afrika halikuwa na shule nyingi wakati wa utawala wa kikoloni haikumaanisha kuwa watoto wetu hawakuwa na elimu." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, watoto wetu walifundishwa majumbani mwao na mashambani mambo mbalimbali ambayo yaliwawezesha kujitegemea na jinsi ambavyo jamii ilitegemea kuwaona wanavyojiheshimu katika jamii. Walijifunza kwa kuishi na kutenda kwa vitendo.

- Walifundishwa aina mbali mbali za mimea na matumizi yake;
- Kazi ambazo zilipaswa kufanya katika mazao walipokuwa shambani kwa mfano jinsi ya kuchagua mbegu bora kwa ajili ya mazao;
- Jinsi ya kuchunga na kulea mifugo kwa kushirikiana na wazazi na wakubwa wao katika kazi za uchungaji na kuhudumia mifugo; na
- Walifundishwa historia ya makabila yao na mahusiano yaliyokuwepo baina yao na makabila ya jirani kwa kusikiliza simulizi kutoka kwa wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, ingawa hakukuwa na miundombinu ya shule na vyuo kwa wakati huo, haikumaanisha kwamba watoto wetu hawakuwa na elimu. Elimu walikuwa nayo kwa sababu kila mzazi au mtu mzima alikuwa mwalimu kwa namna moja au nyingine kwa watoto wetu na elimu waliyopata ilizingatia kwamba wataweza kujitegemea na (huenda) hii ndio ilikuwa ni elimu ambayo watoto wetu waliyoihitaji ili waweze kukabiliana na maisha.

Mheshimiwa Spika, ninachosisitiza sasa, kulingana na hali ya mabadiliko ya maendeleo ya ulimwengu wetu wa sasa pamoja na utandawazi, ni vema na ni sahihi kabisa kujenga chuo kikuu cha kilimo cha kisasa ambacho kitafundisha elimu ya kujitegemea kwa mtindo wa kujifunza kwa kutenda kwa kushirikiana na wananchi walio vijiji vya jirani na kwingineko. Chuo Kikuu ambacho kitazalisha wahitimu ambao wanajua na wana uwezo wa kujitegemea na kujiajiri katika maeneo ya vijijini ambako wanaishi badala ya kufikiria kuhamia mijini kama njia kuu ya kuwawezesha kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu katika Bunge lako Tukufu. Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili Tukufu, napenda nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi wa kishindo na pia kwa *speech* ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya aliyanza nayo baada ya kuwateua Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuwatemebelea katika Wizara zao na kubaini matatizo na pia kutoa maelekezo ya utendaji katika Wizara hizo.

Nampongeza sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za kishindo Jimboni kwake na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe kwa imani waliyoonyesha kwako wananchi wa Urambo Mashariki kukuchagua kuwa Mbunge wao. Nakupongeza kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu. Nampongeza sana Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili Tukufu. Nawapongeza pia Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kuongoza Wizara zao. Aidha, nawapongeza Wabunge wenzangu kwa kwa ushindi waliopata katika Majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Dodoma kwa kunichagua na pia Jumuiya ya Wanawake Tanzania kwa kuitisha jina langu katika mchakato mzima wa uchaguzi. Nawaahidi wananchi wa Mkoa wa Dodoma ushirikiano mkubwa katika shughuli za maendeleo ya ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa kuanza na suala la mazingira. Maeneo mengi ya nchi yetu mazingira yake yameharibiwa sana. Sisi wanadamu tumekuwa na uadui na miti kwa kufyeka mapori bila kujali athari zake na hii ndiyo sababu kubwa ya ukame. Mito mikubwa imekauka, mabonde mazuri yametoweka.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuanza zoezi la kushindanisha Vijiji katika Mikoa yetu upandaji wa miti ya matunda na vivuli. Wananchi wahamasishwe katika ushindani huu hadi ngazi ya mkoahini ya usimamizi wa viongozi wa vijiji husika na asiyetii zoezi hili awajibishwe na Serikali ya Kijiji. Viongozi wa vijiji wahakikishe wanatoa taarifa ya upandaji miti kwa mamlaka husika aidha, Kata au Tarafa.

Mheshimiwa Spika, kwa ushindani wa upandaji miti tunaweza kurudisha mandhari ya nchi katika suala la mazingira .

Mheshimiwa Spika, naamini ni wakati muafaka kwa Serikali kuanza kufikiria kuwaelimisha wananchi manufaa ya matumizi ya *Biogas*. Serikali inaweza kuteua au kuchagua mikoa michache ya mfano kwa matumizi ya *Biogas*. Hii itapunguza matumizi ya kuni na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itapunguza ushuru kwa vifaa vya *Biogas*, naamini wananchi wengi watahamasika na kupenda matumizi ya *Biogas* kwani matumizi ya mafuta ya taa yatapungua na wanawake wengi wanoshinda juani wakitafuta kuni watapata ahueni na kupata muda wa mapumziko.

Mheshimiwa Spika, nichangie sasa kuhusu elimu ya watu wazima. Naiomba Serikali kuangalia upya suala la elimu ya watu wazima kwani wananchi wengi vijijini hawajui kusoma wala kuandika na hili nimelishuhudia wakati wa kampeni.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya 1970 Serikali ilitilia mkazo suala la elimu ya watu wazima kwa kuhakikisha kuwa kila kitongoji kina darasa la elimu ya watu wazima kwa wale wasiojua kusoma na kuandika. Mkakati huu uliwasaidia sana wananchi wengi kujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Ni hivi karibuni tu niliona kwenye luninga wananchi wa Mkoa wa Arusha vijijini wakiiomba Serikali iwasaide kupata walimu wa kuwafundisha kusoma, kuandika na kuhesabu. Nilifurahishwa sana na kuona wananchi hao walivyotambua umuhimu wa elimu.

Mheshimiwa Spika, siyo Arusha tu ambako kuna wananchi wasiojua kusoma na kuandika. Kuna maeneo mengi nchini na hasa vijijini elimu hii inahitajika sana. Naishauri Serikali kuanza mkakati huu mapema zaidi kwani nchi haiwezi kuendelea au kuondoa ujinga, umaskini na maradhi kama wananchi waliowengi vijijini hawajui kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Spika, nichangie sasa kuhusu Jeshi la Kujenga Taifa. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake mzuri wa kuimarisha JKT. Hili ni Jeshi la Kujenga Taifa. Narudia kwa kusema ni Jeshi la Kujenga Taifa. Pamoja na malengo na madhumuni mazuri ya kuanzishwa kwa JKT, naiomba Serikali sasa iwatumbu vijana hao kikamilifu

katika Ujenzi wa Taifa letu. Naiomba Serikali, Jeshi hili liwe chuo cha mafunzo ya taaluma mbalimbali ili wanaomaliza JKT wasiwe wazururaji katika maeneo wanamokaa. Mafunzo ya ufundi yanayofundishwa *VETA* sasa yafundishwe kwa vijana wa JKT ili liwe Jeshi la Kujenga Taifa kikweli.

Mheshimiwa Spika, vijana hao baada ya kupata mafunzo ya ufundi wakiwa JKT watarudi uraiani na kuweza kuunda vikundi vidogo vidogo nya uzalishaji kutokana na utaalam watakaoupata. Kwa sasa vijana wanaomaliza JKT hurudi katika maeneo yao na kukaa bila kazi yoyote ya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutilia mkazo suala la kilimo kwani kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika karne hii ya 21 bado wananchi wetu tena walio wengi wanaendelea kutumia jembe la mkono. Nchi yetu ina ardhi nzuri na yenye rutuba kwa ajili ya kilimo lakini wananchi bado wanatumia vifaa duni nya kilimo. Naiomba Serikali kwa kuwatumia maafisa kilimo wananchi waelimishwe kutumia jembe la kukokotwa kwa ng'ombe kwani wananchi wetu wengi ni wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kilimo cha jembe la kukokotwa na ng'ombe pia kwa kupanda mazao yanayoendana na hali ya hewa ya mikoa yao, Watanzania wengi watajikomboa kutokana na umaskini unaowakabili. Nitoe mfano mzuri tu kwa Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Dodoma kutokana na ukame unafaa sana kwa kilimo cha alizeti. Wananchi wakielimishwa vizuri kulima alizeti na kisha kuwa na viwanda vidogo vidogo nya kukamulia mafuta ya alizeti wangeondokana na umaskini uliokithiri kwani mafuta ya alizeti yana soko sana katika nchi yetu na nje ya nchi. Ninaamini wananchi wa Mkoa wa Dodoma hawajalijua hili. Ni changamoto kwa Serikali yetu kuwaelimisha wananchi wake, na sisi Wabunge tutashirikiana na Serikali yetu katika kuwahimiza wananchi.

Mheshimiwa Spika, naamini wananchi walio wafugaji wengi hawajajua kilimo cha jembe la kukokotwa na ng'ombe au punda kilivyo rahisi kwani mtu analima ekari zaidi ya moja kwa siku. Elimu hii iwafikie wananchi ili waondokane na kilimo cha jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, nichangie sasa kuhusu michezo: Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Rais kuwa michezo ni muhimu kwa afya zetu na afya za watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, michezo isipotiliwa maanani kuanzia shule za msingi kwa kuwatambua watoto wenye vipaji maalum na kuwaendeleza, tutaendelea kudumaa kimichezo kama ilivyo sasa. Naiomba Serikali kuanzisha vipindi nya michezo katika shule za msingi na kuhakikisha kuwa kila shule kuna walimu wa michezo waliofuzu kwenye fani.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali irejeshe mashindano kwa shule za msingi na sekondari ili kubainisha watoto wenye vipaji maalum kwa michezo mbali mbali ili waendelezwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwajali wananchi wake kwa kuchukua hatua za haraka kuhusu suala la njaa. Kwa niaba ya akinamama wa Mkoa wa Dodoma wanaoteseka na njaa na watoto wao, naiomba Serikali iendelee kuwaangalia kwa jicho la huruma wananchi wa Mkoa huu wenye ukame kila mwaka.

Namwombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema Rais wetu, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, pamoja na Mawaziri na Naibu Mawaziri wote bila kuwasahau Wabunge na watendaji wote wa Serikali ya Awamu ya Nne. Mungu Ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia mia moja.

MHE. OMAR ALI MZEE: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote afya njema.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakupongeza wewe Mheshimiwa Samuel Sitta, kwa kuchaguliwa katika Jimbo lako na kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pili, nampongeza Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika, umahiri wake katika kazi hii ni wa kipekee.

Mheshimiwa Spika, pongezi za dhati zimfikie Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Uchapaji wake wa kazi ndiyo kielelezo tosha.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote. Vile vile nawashukuru wananchi wa Jimbo la langu la Kiwani walionichagua na ambao hawakunichagua kwani wametimiza haki yao ya kidemokrasia. Nawaomba tuungane kuiletea maendeleo nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba yake nzuri, mororo na mwanana ambayo imetaja maeneo muhimu yenye kutafakari mwelekeo wa nchi hii katika uongozi wake. Mwenyezi Mungu ampe busara njema kwa yote aliyokusudia kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Kitaifa, Tanzania ni moja pamoja na raia wake, tofauti yetu ni makabila tu. Kuwepo kwa vyama vingi vya siasa siyo kutofautiana, lengo ni kuikosoa Serikali na kuilekeza, haina maana sehemu moja iwe bora na nyininge kuwa dhalili au mwingine awe na sauti ya kusema na mwingine asiwe nayo. Tushirikiane kutatua matatizo yetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza Mheshimiwa Rais aliposema ataendeleza kwa dhati mfumo wa demokrasia ya vyama vingi. Ni matarajio yangu atavisaidia vyama vyote, kuviedeleza, kuvipatia nyenzo na maslahi bora zaidi ili

ionekane kwamba kweli Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna mfumo wa vyama vingi vya siasa na vyenye ushindani wa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgogoro na mpasuko ambao unamsononesha Mheshimiwa Rais kuhusu Uunguja na Upemba, nashukuru sana kwamba mpasuko huo ameuona, kwa mfano muafaka wa kwanza uliofanyika, matokeo yake ukabewa. Muafaka wa pili ukajenga imani na matumaini ya Wazanzibari, matokeo yameonekana. Kwa mfano, uchaguzi wa Zanzibar matokeo yalichukua zaidi ya siku tatu kutangazwa kwa watu wasiozidi laki tano, Baraza zima la Mawaziri kumi na watatu, Mpemba ni mmoja, tena Waziri asiye na Wizara Maalum (Waziri Kazi Maalum), Makatibu Wakuu, Wapemba ni wawili tu, Wakuu wa Mikoa, Mpemba ni mmoja tu, nafasi za uteuzi za Rais, Mpemba ni mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, kwa mifano hiyo ni dhahiri mpasuko mkubwa upo kwani hakuna Wapemba ambao ni Chama Tawala? Lakini yote ni kwa sababu Mpemba yeoyote anaonekana hana thamani.

Mheshimiwa Spika, nampongeza tena Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wake katika Serikali yake hii Tukufu kuona Wapemba nao wameshirikishwa katika nafasi za juu. Ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Rais anawathamini watu wote wa Jamhuri ya Muungano. Ni matarajio yangu kwamba ule msemo usemao, chanda chema huvikwa pete, ni dhahiri Mheshimiwa Rais atalitatua tatizo hili kwa udhati wa moyo wake ili kufanikisha azma yake ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais.

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Bukene kwa kunichagua kwa kura nydingi, 75% kuwa Mbunge wao, hasa wanawake kwa kuniunga mkono.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hii ninawaahidi kufanya kazi kwa uwezo wangu wote kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM nikishirikiana na Rais na Serikali ya Chama Tawala CCM. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pili nawapongeza kwa kumpa kura nydingi Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, 85% na Madiwani wote wa Kata 16 CCM na hasa kukomboa Kata ya Bukene. Hongera sana na shukrani ziwafikie kupitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba niwapongeze wale wote walioteuliwa na Rais kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri. Hongereni sana. Namshukuru Rais na kumpongeza kwa kuteua wanawake wengi na hivyo kututambua kwamba wanawake tunaweza. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru sana Serikali kwa kupeleka chakula cha msaada wa njaa haraka kweli, kwenye Jimbo langu ilikuwa sheshe. Debe moja la mahindi lilifikia kuuzwa kwa bei ya shilingi 7000/= na ng'ombe alishuka bei hadi

shilingi 30,000/= ng'ombe ambaye alikuwa anauzwa kwa shilingi 180,000/=. Sasa mwananchi anauza kwa shilingi 30,000/= ili mradi aweze kupata debe moja au mbili za chakula.

Mheshimiwa Spika, naamini na naishukuru Serikali kwa kuchukua hatua za haraka kusambaza chakula. Ninaomba Serikali kufuatilia kwa makini ili wasipatikane wajanja (*middle men*) ambao si wazalendo wanaotaka utajiri wa haraka kwa shida kama hii.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, naiomba Serikali iwe makini zaidi ili wananchi wapate chakula cha msaada ipasavyo yaani kwa bei poa na wale ambao hawana uwezo wapewe bure.

Mheshimiwa Spika, kama alivyokumbusha Mheshimiwa Rais kwenye Mkutano wake wa shukrani hapa Dodoma wiki iliyopita, naomba nami niwakumbushe zile ahadi ambazo alizisema kwenye Jimbo langu la Bukene ili ziorodheshwe ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, umeme, Mheshimiwa Rais aliahidi umeme Bukene (Jimbo la Bukene) na Ndala (Jimbo la Nzega) ikiwa ni ahadi ya Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ye ye alisema *ata-carry forward* na kusema kweli, pesa zilishatengwa, iliyobaki ni utekelezaji. Hivyo ninaomba ahadi hii itekelezwe upesi kwani nami niliahidi kusukuma kwa nguvu ahadi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, maji, katika kuomba kura nami nilisema *long term* maji ya Ziwa Victoria na *short term* ni visima vifupi na virefu.

Mheshimiwa Spika, maji yanayotoka Ziwa Victoria yakifika Kahama, ni jirani sana na Jimbo langu. Wananchi hawataelewa maji yasipite kabisa Jimbo la Bukene yakiwa yanaenda Nzega Mjini.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri maji haya yapite Wilaya ya Nzega yaani Majimbo mawili Bukene na Nzega na kwa kuwa tatizo la maji ni la Taifa, napendekenza au nashauri na kuomba hasa kwamba ijenge *reserve* kama ilivyo *Transfoma (TANESCO)* ili maji yakinotoka Kahama yafuate njia ya barabara Kahama – Mpera – Igusule – Itobo - Nzega. *Reserve* ijengwe Mwamala kwa kupeleka maji Mwangoye, Bukene na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu najua umuhimu wa maji Mwangoye na Mwamamala kwa sababu ya kilimo cha Mpunga. Maji yakifika Mwangoye, maana yake yamefika Tinde. Kwa kweli naomba masuala ya maji na umeme tuyashughulikie Kiwilaya yaani Wilaya ya Nzega karibu na Kahama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliahidi pia juu ya barabara ya kutoka Tabora- Bukene inayounga Wilaya hizi mbili kwa kiwango cha changarawe. Barabara inayotoka Nzega - Itobo - Kahama, nami niliendelea kuzipigia debe. Kwa kweli ni aibu kwa mtu mzima kuja sutwa. Kwa misingi hiyo, naomba ahadi hizi ziwekwe ipasavyo. Mimi nakumbushia tu. Ni wazi nitafurahi sana zikitekelezwa maana ahadi ni deni.

Mheshimiwa Spika, mengine tutajitahidi wenyewe kubuni na kutimiza miradi na ajira kwa vijana na wanawake kutokana na mazingira yetu, mfano kutengeneza *juice* za maembe, ngoma za utamaduni na kaadhalika. Ila naomba ushirikiano wa Serikali, *NGOs* kama *SIDO*, *promoters* kwa nyimbo au ngoma za jadi ili mwisho wa siku kila Mtanzania awe na maisha bora. Naomba kuwasilisha.

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY: Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri, safi na yenye malengo mazuri ya kuiendeleza Tanzania yetu ikiwa kweli watendaji watakuwa na nia nzuri kama ilioonyeshwa na Mheshimiwa Rais mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa katika maeneo machache tu, kwa lengo la kuboresha zaidi hotuba hiyo au pengine katika kupendekeza nini tufanye ili yale matatizo ambayo Mheshimiwa Rais hayampi usingizi yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nimeutoa kutoka hotuba iliyomo ndani ya *Hansard*, maana hotuba hiyo imeongeza mambo ambayo kwenye kitabu hamna. Ukurasa wa 49 wa hotuba hiyo inazungumzia mpasuko uliopo baina ya Unguja na Pemba. Ni kweli na mpasuko ni mkubwa, mpasuko ambao umesababishwa kwa makusudi na viongozi waliopo au kwa maana pana unasababishwa na Serikali iliyopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mkakati wa makusudi wa kuifanya Pemba kana kwamba ni kisiwa cha watoto yatima. Nichukue mifano miwili, mitatu kuanzia kipindi cha miaka mitatu nyuma: Bajeti ya Serikali ya mwaka 2003/2004 na 2004/2005 ilionyesha dhahiri upendeleo uliopo katika Visiwa hivyo, mfano katika Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano itenga asilimia 93 kwa ujenzi wa barabara za Kisiwa cha Unguja wakati Pemba ambako barabara zake ni mbovu zaidi walipewa asilimia 7 tu .

Mheshimiwa Spika, zingatia uteuzi wa Baraza la Mawaziri la kipindi hiki, kati ya Mawaziri 14 walioteuliwa ni Waziri mmoja tu kutoka Pemba tena Waziri ambaye hana Wizara Maalum. Tena ameambiwa ofisi yake iwepo Pemba. Hii ina maana mikutano mingi ya Baraza la Mapinduzi ambayo ndiyo *cabinet* hatapata na uamuzi utachukuliwa tu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara ya Elimu (Serikali) imepitisha sera ambayo mtoto wa Pemba au wa Kiunguja atasoma kwao kuanzia darasa la kwanza hadi la 12 bila ya kukaa *boarding* au kupangiwa shule nyingine kama vile zamani yaani unatoka darasa la 7 Pemba na unakwenda darasa la 9 Unguja na huko unakaa *dakhalia*.

Mheshimiwa Spika, tizama hotuba ya Mheshimiwa Kikwete alipoashiria umoja na kuahidi kuwepo kwa mchanganyiko wa wanafunzi kutoka mkoa mmoja hadi mwingine kwa kuwaweka wanafunzi hao *dakhalia*. Mheshimiwa Kikwete aliyaeleza haya katika hotuba yake ukurasa wa 50.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara moja ya vikosi vya Serikali ilipewa bilioni 14, wakati Wizara tano kwa moja zilipewa fedha kiasi cha bilioni 12.5. Wizara hizo ni Afya, Wanawake na Watoto, Maji, Ofisi ya Rais na moja nimeishahau. Pemba hospitali ni mbovu, hakuna dawa wala madaktari, hakuna maji, ajira ni mbovu na kadhalika. Lakini hiyo haikuonekana na wakapewa vikosi kwa kuajiriwa vijana wengi wa Unguja na hao hao kutumiwa katika vitendo viovu vya kuwapiga Wapemba, kuwaibia, kuwavunjia, kuwanajisi na kufanya kila aina ya *idhilate* kwa Wapemba hao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Naibu Waziri Kiongozi anawaita na kuwasifia kwa kazi yao nzuri wanayoifanya huko Pemba.

Mheshimiwa Spika, huu si mionganoni mwa mipasuko iliyopo? Hata baada ya huo ushindi wa nguvu, vurugu, hamkani bila ya utaratibu uliopatikana (maana kishindo kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili maana yake ni hiyo) basi haionekani kwamba kunahitajika uwakilishi uliosawa baina ya Unguja na Pemba yaani *proportional representation*, (Wete, Chake, Mkoani na Michenzani) hakuna wana CCM wa kuteuliwa kuwa Mawaziri kama walivyoteuliwa Adam Mwakanjuki, Ramadhan Abdulla Shaaban na Asha Abdulla chini ya kifungu cha 66 cha Katiba ya Zanzibar? Huo si ubaguzi unaoleta mpasuko?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 46 anazungumzia Usalama wa Raia. Usalama wa Raia ni suala la Kitaifa. Vifungu vya 14,15 na 16 vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinazungumzia haki ya kuwa hai, haki ya uhuru wa mtu binafsi na haki ya faragha na Usalama wa mtu vinahusika. Vifungu hivyo pia vimo katika Katiba ya Zanzibar. Kwa mujibu wa Katiba hizo hizo Rais wa Jamhuri, kifungu 33(2) cha Katiba ya Jamhuri, ndiye Amiri Jeshi Mkuu waUlinzi na Usalama. Hivyo anawajibika Kikatiba kuhakikisha usalama wa kila raia kuanzia Mtwara hadi Kagera na kutoka Kigoma hadi Visiwa vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, kama Mkoo wa Usalama wa Raia, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Rais kuwa Unguja na Pemba usalama huo haupo. Watu tena kwa ushahidi nilionao wanateswa, wanaibiwa, wanapigwa, wananyanyaswa, wanavunjiwa vitu vyao. Ni nani wanafanya hivyo? Ni Polisi na vikosi vya SMZ kama vile KMKM, JKU, Mafunzo, *Volunteer*, Zimamoto na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni kweli vikosi hivi vingine ukiacha Polisi vimeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu 121 ambapo Rais wa Zanzibar chini ya kifungu 123(i) ndiye Kamanda Mkoo wa vikosi hivyo .

Mheshimiwa Spika, huyu Kamanda Mkoo inaonyesha hawajibiki vizuri, basi kama Mheshimiwa Rais ndiye Amiri Jeshi Mkoo hawezi kumwajibisha Kamanda wake?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Mheshimiwa Rais anaweza akaunda Tume kuchunguza vifo vya watu wanenye, wakati Unguja kuna watu walioibiwa na kupigwa, kuna waliobakwa na kuna waliodhalilishwa?

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wa Zanzibar wanauliza, huku Zanzibar Rais wa Jamhuri hahusiki au hakerwi na uvunjifu wa amani kwa usalama wa raia? Mimi binafsi ninaamini anakerwa na ninaamini suala hili atalichukulia hatua madhubuti, ama kwa kuunda Tume ya kuchunguza hayo au kwa kuiongezea nguvu Tume aliyokwisha kuiunda kuchunguza vifo vya watu wanne ili iweze kufanya kazi kuchunguza dhuluma na *idhilal* hizo zilizoko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika suala la Tume za Uchaguzi ambazo Mheshimiwa Rais amegusia katika ukurasa wa 42. Mheshimiwa Rais alizisifu Tume za Uchaguzi. Sina uhakika mkubwa kama Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) iliharibu uchaguzi. Lakini nina uhakika mkubwa sana zaidi ya asilimia 90 kuwa *ZEC* haikuwa huru.

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo tu ni yale maelezo ya Mwenyekiti wa *ZEC* ndani ya barua yake *TUZ/33/05/06/52* ya tarehe 1 Novemba, 2005 aliyompelekea Mgombea Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya *CUF*, Mheshimiwa Seif Sharif Hamad. Katika barua hiyo ukurasa wa mwisho, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (*ZEC*) alisema na ninaomba kunukuu: "Hivyo hakuna dosari zozote katika uchaguzi isipokuwa labda ile ya kuvamia vituo na watu ambao hawakujandikisha kupiga kura na wakapiga kura." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, nina ushahidi kamili wa watu wengi waliopiga kura mara mbili. Kwa mfano Makame Mcha Mkanga alijiandikisha na kupiga kura Matemwe namba ya kadi yake namba 0050220 na baadaye kujandikisha tena Chubuni Mjini kwa jina la Mkanga Mcha Mkanga, kadi ya kupigia kura namba 00411192. Lakini kadi zote hizo mbili zikiwa na picha ya mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa watu wengi na ninao kama ushahidi. Hawa Mbaruk Ali akawa Mwajuma Mbaruk Ali namba 00502094 na namba 0015780 Matemwe na Chumbuni, Nassir Ali Khalid (Nkurma) namba 0267863 na kuipiga tena Welezo kama Khalid Ali Nassir namba 0054535 na wengi wengineo.

Mheshimiwa Spika, hii si Tume huru, bali ilikuwa ikisindikizwa na matakwa ya watu fulani na chama fulani.

Mheshimiwa Spika, ninayo mengi lakini kwa leo yanatosha. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe mchango wangu katika hotuba ya Rais. Kwanza kabisa, nakupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuitishwa na Bunge bila kupingwa. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais pamoja na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushindi mkubwa walioupati katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake na Rais na baadae kupitishwa na Bunge kwa zaidi ya asilimia 99. Vile vile napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri pamoja na Wakuu wa Mikoa kwa kuteuliwa na Rais kushika nyadhifa zao.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapongeza Wabunge wote kwa ushindi waliopata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 na wengine kuteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu, napenda kuwashukuru wananchi wa Mtwara kwa kunilea vizuri na baadaye kunipa ridhaa ya kuwa mmoja wa wawakilishi wao katika Bunge lako Tukufu kupitia Chama cha Mapinduzi. Kwa namna ya pekee nakishukuru Chama cha Mapinduzi ambacho ndicho kilichonipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumshukuru Mungu kwa mema yote aliyotujalia, pia namwomba azidi kutujalia Watanzania wote afya njema ya roho na mwili ili tuweze kushirikiana vizuri katika kuliendeleza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri na ilioandaliwa kisayansi. Naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100 na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tuzingatie kama ndio msingi na rasilimali ya kwanza kabisa katika utekelezaji wa sera za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia mengi lakini kutokana na muda nitazungumzia suala la maji, kilimo na kuboresha uchumi. Rais wetu ametueleza mambo yote muhimu tunayotakiwa kuyafanya kwa ajili ya maendeleo yetu, lakini amedhihirisha wazi kuwa tatizo la maji ndio kero ya kwanza miongoni mwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba tulipe suala hili kipaumbele katika utekelezaji wa sera zetu. Kwa kweli tatizo hili linaathiri jamii hasa akinamama katika ushiriki wa shughuli nyingi za maendeleo kwani hypoteza muda mwingi wakitafuta maji kutoka maeneo ya mbali na makazi. Kwa mfano, katika miaka ya 1995/1996, kiasi cha dola za Kimarekani 40,000 zilirudishwa kwa wafadhili kwani walengwa wa mradi wa wahamiaji hawakupata nafasi ya kuonana na kuongea na wafadhili kutokana na tatizo la maji. Tatizo la maji vile vile linaathiri kipato cha wananchi kwani kwa mfano Wilayani Tandahimba na Newala maji huuzwa kwa shilingi 500/= kwa litu 20. Kwa kifupi, ni kwamba kwa yale maeneo yenye shida kubwa ya maji si rahisi sana kukwamua wananchi kiuchumi hata kama watakopeshwa mitaji. Rais wetu ameonyesha nia yake kubwa ya kuleta mapinduzi ya kilimo kwa mbinu mbalimbali. Naona pia iko haja ya kuangalia upya aina ya wataalam wa kilimo kwa kuzingatia mahitaji na hasa kuhusiana na suala la usalama wa chakula katika kaya. Usalama wa chakula huathiriwa na mambo mengi yakiwemo magonjwa na wadudu waharibifu, upungufu wa rutuba, uhaba wa mvua na mvua zisizoaminika na utumiaji wa nyenzo hafifu za kilimo na pengine mbegu zisizo bora.

Mheshimiwa Spika, napendekeza wataalam wa udongo, wadudu na magonjwa, hifadhi ya chakula, umwagiliaji na bustani, wafanye kazi kama timu na wafike vijijini au mashambani ili kusaidia kupunguza tatizo la uhaba wa chakula litokanalo na matatizo

mengine mbali na ukame. Kwa kuwa mazao ya mizizi husaidia kuimarishe uhakika wa chakula, naiomba Serikali ijithidi kuziba ufa kwa kuboresha mazao hayo. Nakumbuka mnamo miaka ya tisini kulitokea njaa kali Mkoani Mara kutokana na mdudu wa muhogo (*Cassava Mealy Burg*). Lakini baada ya wataalam kumdhiliti mdudu huyo kumetokea tena ugonjwa mwinge unaofikiriwa kuwa ni *Cassava Bacterial Blight* kuanzia miaka ya 1994/1995. Kwa mara ya mwisho nimeshuhudia mkulima akipoteza muhogo zaidi ya nusu shamba Septemba, 2005 Mkoani Mtwara kutokana na dalili za ugonjwa wa *Cassava Bacterial Blight*. Muhogo huo ulikuwa na umri usiozidi miezi tisa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchumi, naomba nirejee hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 13 ambapo majukumu mawili ya msingi yametamkwa bayana kuhusiana na uchumi wa nchi yetu. Nadhani hapa Mheshimiwa Rais anatalika Waheshimiwa Wabunge tusaidie Serikali yetu ni jinsi gani tutainua uchumi wetu maana mambo yote yanahitaji fedha. Taswira hii imejitokeza pale ambapo kila Mbunge aliyesimama kuchangia au kuuliza swali aligusia maeneo yaliyohitaji fedha. Majibu sahihi yaliyotolewa pia yalielezea ufinyu wa Bajeti kama kikwazo kitu ambacho nadhani kinaweza kupunguza kasi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Fedha kwa kuongeza Pato la Taifa kuititia *TRA* katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tat. Kutokana na malalamiko ya wananchi na ushuhuda wangu binafsi, bado Pato la Taifa linaweza kuongezeka maradufu zaidi. Bado ukwepaji kodi upo kwani wafanyabiashara wengi wamekuwa hawatoi risiti, huambiwa aongezee asilimia 20 ya *VAT*. Hivyo nashauri bidhaa ziwekewe *label* za bei ili kuepukana na tatizo hili na tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wabunge waliochangia juu ya matumizi bora ya rasilimali zote tulizonazo yaani madini, nishati, misitu, mbuga za wanyama, ardhi, samaki na watu kwa manufaa ya Watanzania ikiwa ni pamoja na kuwa waangalifu kwenye mikataba. Naungana nao pamoja na Mheshimiwa Rais. Naongeza pia kuiomba Serikali iwawezeshe wananchi kufanya biashara za aina mbali mbali kama alivyosema Rais wetu kwani kwa sasa biashara nyingi ni mpishano wa mama ntilie, machinga au machinga mama ntilie. Je, wote wakifanya biashara ya aina moja ni nani atanunua kwa mwenzake? Tatizo ni kwamba mazingira hayaruhusu huko vijijini ambapo ndipo mahali palipo na wananchi wengi zaidi. Hali hii husababisha vijana na akinamama wanaopata mafunzo ya ufundi na kuhitim, kwa mfano mafundi cherehani hukimbilia Mijini ili waweze kutumia vifaa vya umeme kwa kazi zao. Lakini wakati mwinge tunapiga kelele kuhusu *rural urban migration*. Je, ni kosa la nani? Kwa ujumla matatizo ya kiuchumi yanayoikibili nchi yetu kuanzia ngazi ya kaya hadi Taifa yanahusisha sekta mbalimbali kwa mfano wa utando wa buibui.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba niseme kwamba kwa Tanzania yenye neema tele, kila Mtanzania anaweza kupata maisha bora endapo tutajipanga vizuri, kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante!

MHE. EPHRAIM N. MADEJE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuiongoza nchi yetu, pili, nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Rais wetu na kuthibitishwa kwa kura za kupindukia na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu. Ninawataenia afya njema na maisha mrefu viongozi wetu hawa ili waliongoze Taifa letu kuelekea kwenye ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kutoa pongezi za pekee kwako, wewe kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili katika kipindi kijacho, vile vile nampongeza Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuwa mwanamke wa kwanza kukalia kiti cha Naibu Spika. Ninawataenia nyote kila la kheri katika nyadhifa zenu hizi mpya.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete ili kuiongoza Serikali. Hatimaye nawapongeza Wabunge wenzangu wote kwa ama kuchaguliwa na kuteuliwa ili kuutumikia umma wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia hoja, naitumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Dodoma Mjini kwa kunichagua kwa kura nyingi niwe mwakilishi na mtetezi wao katika Bunge hili Tukufu. Naahidi kuwatumikia kwa juhudhi na uwezo wangu wote ili nikidhi matarajio yao. Hotuba ya Rais aliyoitao tarehe 30 Desemba, 2005 licha ya kuchukua muda mrefu ilikuwa ni ya kusisimua na ilizingatia *agenda* muhimu katika maendeleo ya Taifa letu. Nampongeza Rais kwa hotuba yake mahiri ambayo mimi binafsi (bila shaka na wengine) ilinikumbusha enzi za Hayati Mwalimu Julius Nyerere. Sisi wakazi wa Dodoma tunafarijika kutokana na jinsi Rais aliviyolizingatia suala la kilimo cha kisasa na cha umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Spika, licha ya Dodoma kuwa na ukame wa asili, wakazi wa vijiji vinavyozunguka mji huu hujuhishwa na kilimo cha umwagiliaji maji wakati wa kiangazi kwa kutumia visima vifupi vya kwenye makorongo. Kwa kiasi kikubwa kilimo cha mizabibu na cha nyanya na mboga mboga kinategemea sana umwagiliaji huu. Kwa hiyo, wakulima hawa watafaidika sana na mipango itakayopangwa ya kukarabati mabwawa yaliyopo, ujenzi wa mabwawa na malambo mapya na uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji kwa ujumla. Tutahimiza ukarabati wa bwawa la Mauhumbulu, Kata ya Mpunguzi na lile la Hombolo ili wakulima waweze kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa 31, Mheshimiwa Rais amesisitiza umuhimu wa ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati katika kuongeza Pato la Taifa na ajira pia. Ni matumaini yetu kwamba sheria iliyokuwa inatoa upendeleo kwa wawekezaji ili wavutike kujenga viwanda Dodoma itahuishwa haraka iwezekanavyo. Aidha, tutaomba uwekezaji uelekezwe kwenye viwanda vya kusindika mazao hasa zabibu, nyanya, mbegu za mafuta (karanga, ufuta, alizeti) nafaka na kadhalika. Ombi maalum tunalolitoa Serikalini ni juhudhi zifanywe kukamilisha uuzaaji wa kiwanda cha vigae Zuzu

ili uzalishaji uanze mara moja kwa manufaa ya wote wawekezaji, waajiriwa na watumiaji wa bidhaa hii.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru pia kwamba suala la upatikanaji wa maji ya uhakika na yaliyo safi kwa matumizi ya wananchi limepewa kipaumbele kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Amefanya hivi pamoja na kwamba suala la maji tayari lipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ili kuonyesha umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, sisi wakazi wa Dodoma Mjini tunashukuru kwamba upatikanaji wa maji unaridhisha kwa kiwango kikubwa. Tatizo liko kwenye Kata za Dodoma Mjini ambazo kwa kweli ni Vijiji (*perse*) halisi. Vijiji hivi ndivyo vyenye matatizo makubwa ya maji na bado havijapata huduma ya *Dodoma Urban Water and Sanitation Authority (DUWASA)*.

Mheshimiwa Spika, hata kama *DUWASA* ingeweza kuvifikia baadhi yao, bado wananchi wangeshindwa kumudu gharama zake kubwa. Kwa hiyo, wanavijiji hao wana matumaini makubwa sana na mpango kabambe wa maji uliobuniwa na hasa hasa wale wa vijiji vya Mchemwa (Makutupora), Chitogolo (Nghongonha), Mhande (Nghongonha), Mapinduzi (Nghongonha), Chizomochi (Mbabala) na vinginevyo vingi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nzungumzie suala la janga la njaa ambalo ni matokeo ya kilimo chetu duni na ambacho Rais amekizungumzia kwenye ukurasa wa 29. Tunashukuru kwa hatua zilizokwishachukuliwa na Serikali kulikabili tatizo hili. Azma ya Serikali ni kwamba hakuna Mtanzania ambaye atakufa kwa njaa. Hii ni nia njema kabisa lakini kama hatua za haraka hazitachukuliwa kurekebisha tathmini ya mahitaji halisi ya chakula hasa yale ya bei nafuu na ya msaada (bure), majuto anaweza kuwa mjukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya kabisa Jimbo la Dodoma Mjini limeathirika kuliko mengine yote kutokana na tathmini isiyo sahihi. Inawezekana kutokana na jina Dodoma Mjini, wanaohusika wanatufananisha na miji mingine kama Dar es Salaam au Tanga ambayo watu wake hawategemei kilimo.

Mheshimiwa Spika, kati ya Kata 30 za Dodoma Mjini, 18 ni Vijiji halisi vya wakulima ambavyo vimekosa kabisa mvua katika msimu uliopita. Licha ya hali hiyo ya uhitaji mkubwa wa chakula cha njaa, Dodoma Mjini haikupata chochote katika mgao wa kwanza na hivi sasa imepata tani 185 tu ambazo zimesambazwa katika mazingira magumu sana ya malalamiko.

Kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali itumie pia takwimu zilizotayarishwa na Manispaa ambazo zimejumuisha wadau wa ngazi zote katika ukusanyaji wake na tunaomba kazi hiyo ifanyike haraka iwezekanavyo ili tunusuru maisha ya baadhi ya wananchi ambao wana hali duni sana. Kwenye ukurasa wa 54, Rais amegusia umuhimu wa kuendeleza makao bora kwa kuheshimu dhana ya mipango miji.

Mheshimiwa Spika, Mji wetu wa Dodoma una bahati kuwa kati ya miji ambayo ina mpangilio mzuri. Kati ya kazi nzuri sana ambayo ilifanywa na *Capital Development*

Authority (CDA) katika miaka ya nyuma, ni kutengeneza *master plan* ya Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukiukaji wa mpango huo wa hapa na pale, bado ni mfano wa kujivunia na ni dira nzuri ya maendeleo ya mji huu. Ni matumaini yetu wananchi wa Dodoma ya kwamba Mamlaka zinazohusika zitasimama imara kuhakikisha *master plan* hii haikiukwi kiholela.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie mchango wangu kwa kuzungumzia suala la maendeleo ya michezo. Tunakubaliana na Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia kuhusu umuhimu wa maendeleo ya michezo kuanzia ngazi ya chini kabisa yaani shule za msingi. Kuna umuhimu wa kutengeneza mpango kabambe utakaohusisha yafuatayo:-

(a) Utoaji wa Elimu kwa walimu watakaosimamia michezo;

(b) Upatikanaji wa nyenzo na vifaa vya michezo; na

(c) Uainishaji wa maeneo/viwanja vya michezo ya kila aina kwa kila shule katika ramani (*school land use plan*). Hii itahakikisha kwamba maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo hayamezwi na matumizi mengine jinsi shule zinavyokua.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Rais kwa hotuba yake nzuri sana. Hata hivyo ninaomba nichangie machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, Serikali ichukue hatua madhubuti na haraka za kuondoa upungufu mkubwa wa walimu katika shule za msingi na sekondari, Serikali itekeleze ahadi zake za kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Kwa mfano katika Jimbo la Kondoa Kusini Serikali iliahidi kuchangia fedha kwa ajili ya madarasa 16 katika shule za sekondari Sikwakwa, Farkwa na Msakwalo. Lakini mpaka sasa imechangia madarasa sita tu. Tunaomba ikamilishe mchango wa madarasa 10 yaliyobaki. Aidha, kuna madarasa zaidi ya 80 yanayosubiri kukamilishwa katika shule za msingi Jimboni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi hawana uwezo wa kujenga maabara katika shule za sekondari zinazojengwa kwa nguvu za wananchi, Serikali ichukue jukumu la kujenga maabara katika shule hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya Afya, tatizo la upungufu wa watumishi wa afya lishughulikiwe haraka, vituo na zahanati zilizojengwa kwa nguvu za wananchi zifanyiwe utaratibu wa kufunguliwa haraka. Mfano Kituo cha Makorongo na Zahanati za Mwaikisabe na Jongolo Wilayani Kondoa na kigezo cha sasa cha kujenga Zahanati kwa ajili ya watu katika ya 6,000 hadi 10,000 kiangaliwe upya na badala yake kila kijiji kipatiwe Zahanati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya maji, ninakubaliana kabisa na kauli ya Rais kuwa kero *number one* nchini ni maji. Pia ninakubaliana na pendekeso lake la kuanzisha mpango kabambe wa maji kwa nchi nzima. Hata hivyo ninashauri katika mpango huo uvunaji wa maji ya mvua hususan wa mabwawa makubwa katika Mikoa kame kama Dodoma upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora, naomba utaratibu wa kushughulikia watuhumiwa wa sasa uangaliwe ili kuondoa gharama anazoingia mlalamikaji wakati wa kuendesha kesi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache naomba nikushukuru tena na kutamka kuwa naunga mkono hotuba ya Rais. Ahsante kwa kunisikiliza.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu katika hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akifungua rasmi Bunge jipya hapa Dodoma tarehe 30 Desemba, 2005 ambayo kwa sababu za wakati sikuweza kumalizia katika mchango wangu niliyoutoa Bungeni siku ya Ijumaa tarehe 10 Februari, 2006.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusoma vizuri na kuelewa ukurasa wa 18 na 19 wa hotuba ya Rais nimepata tafsiri zifuatazo, kwanza, mpasuko kwa sababu *CUF* haikupata kiti katika Majimbo ya Tanzania Bara?

Pili, mpasuko kwa vile CCM haikupata kiti Pemba? tatu, kwa aina ya chaguzi zote zilizofanyika Zanzibar au kwa hizo sababu za kihistoria?

Mheshimiwa Spika, Wabunge wametoa sababu za ubaguzi baina ya Unguja na Pemba, wengine baina ya Pemba na Tanzania Bara. Mimi naamini Wapemba si wabaguzi lakini wao wanabaguliwa na ninazo sababu nyingi. Mfano wa kwanza Wapemba tangia zama za zamani wameingiliana na watu wa makabila mbalimbali katika ndoa, Waarabu, Wanyamwezi, Wasukuma, Wachaga, Wahaya, Wadigo, Wanyakyusa na wengineo na zilipokuja ndoa za *forced marriage* wao hazikuwaathiri hata kidogo, lakini Unguja ziliathiri maana hawakuzizoea. Huo ulikuwa wakati wa Marehemu Abeid Amani Karume, Rais wa kwanza wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Marehemu Abeid Amani Karume alifuta suala la makabila na halikutumika katika shughuli yoyote ya kiserikali ikiwa ya kuandikishwa shule, kuajiriwa kazini kwenda masomoni na kadhalika. Lakini hivi leo tokea mwaka 1995 mambo hayo yanahitajika katika shughuli yoyote ya Kiserikali Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa huo wa 18 katika hotuba yake Mheshimiwa Rais amesema: “Iweje Wapemba hawa ambao ni hodari wa kutumia fursa ya Muungano wetu kwa kuishi na kufanya biashara na kuwekeza katika pembe zote za Jamhuri yetu wawe hao hao wanaojitenga kisiasa kwa kiwango tulichoshuhudia kwenye Uchaguzi Mkuu?” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Wapemba hawakujitenga, bali wametengwa na baada ya kutengwa UNGUJA na kwa vile wanakubali Muungano ndio sababu ya kwanza iliyowafanya watumie fursa hiyo.

Sababu ya pili, kwa vile hawana *god father* wamekuwa wahangaikaji kimaisha baada ya kukosa fursa nyingi kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sababu ya tatu, fursa za kuwekeza Pemba hakuna na sababu ya nne ni ya kidini inayomruhusu mtu kuhamia popote katika ardhi ya Mwenyezi Mungu endapo hapo unapoishi pana shida na matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Wapemba wanaamini kwamba chama cha siasa cha CCM ni kimoja kwa Tanzania nzima. Ni chama cha Kitaifa, iweje leo mambo na hotuba na matendo ya CCM iwe tofauti baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, je, kuna sera tofauti? Lahasha! Ni kwa sababu Wapemba wanabaguliwa Visiwani. Ni wakati wa Marehemu Abeid Amani Karume tu na wakati wa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi ndipo tuliposhuhudia angalau kwa kiasi fulani kuna *equal distribution of resources* za nchi. Angalia wakati wa uchumi wote kwa wakati huo mpaka hivi sasa kwa kiwango fulani unategemea zao la Karafuu kutoka Pemba.

Mheshimiwa Spika, sitaki haya maoni yangu yaaminike moja kwa moja bali ningombwa yatizamwe maoni waliyoyatoa Bungeni Waheshimiwa wafuatao, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo na Mheshimiwa Jackson Makwetta, wote wamechangia suala la mpasuko pamoja na maoni yangu haya yafuatayo iwe ni moja kati ya dira ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kupata pa kuanzia kutafuta ukweli na hatimaye kuondosha mpasuko huu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni kwamba kuundwe Tume Huru itakayokuwa na Wabunge wachache wa pande zote, wawakilishi wachache wa pande zote, wanasheria wasiofungama na upande wowote, viongozi wa kidini na vyama huru vinavyopigania haki za binadamu pamoja na hadidu za rejea watakazopewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, wakachunguze Zanzibar haya yafuatayo:-

- (i) Wafanyakazi wangapi waliotolewa kazini ambao ni Wapemba na wangapi ni Waunguja.
- (ii) Walioingizwa kazini Wapemba na Waunguja.
- (iii) Waliokimbia nchi, Wapemba na Waunguja.
- (iv) Walioko masomoni Kiserikali, Wapemba na Waunguja.
- (v) Waliuwawa Wapemba na Waunguja.

(vi) Walioathirika kwa risasi, mapanga na marungu Wapemba na Waunguja.

(vii) Waliofunguliwa kesi za kubuni Pemba na Unguja.

Mheshimiwa Spika, kuna ajira za Polisi, Jeshi, Usalama, Magereza, KMKM, JKU, Zimamoto na kadhalika. Wangapi Wapemba na wangapi Waunguja.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kukuarifu kwamba katika ajira ya vikosi vya Muungano, mara nyingi wanatolewa watu kuja Pemba na *ma-god father* ili ionekane wametoka Pemba wakati wa uandikishaji. Naamini hayo yakinendeka ukweli utajulikana dhahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupatikana ukweli iwepo Tume ya maridhiano na shughuli zote za Zanzibar ziwe za pamoja maana mimi na wengine hatujui siku iliyounganishwa Pemba na Unguja kama ilivyounganishwa Tanganyika na Zanzibar ambayo sisi Wapemba tunajisikia huru kuliko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa vile pia yapo matatizo ya Muungano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, mimi ushauri wangu ni kuwa wakati umefika sasa kufuata mapendekezo ya Tume ya Jaji Nyalali na Jaji Kisanga bila kuingia gharama nyingine zozote maana kwa upande wa Zanzibar na misimamo ya vyama vya upinzani ni kuwa na Serikali tatu. Ikumbuke kwamba wapo watu Unguja wanaovaa koti la Muungano lakini ukweli ni wachache wanaojiita wana CCM ambao ni wepesi kuwaita Wapemba wanataka kuvunja Muungano lakini kumbe wao ndio wenye hofu ya roho ikiwa patakuwa na Serikali tatu na ufanuzi mzuri wa mambo. Wao wanataka eti Serikali mbili ili kuendeleza ubaguzi wao.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja lakini si kwa asilimia mia moja, bali ni kwa kiwango cha asilimia 99. Ahsante.

MHE. DORAH H. MUSHI: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii pia na kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuliongeza Bunge letu. Nampongeza Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kupata ushindi wakishindo. Nimpongeza pia kwa kumteua Mheshimiwa Waziri Mkuu, naye nimpongeze pia kwa kuchaguliwa kwa kura zote isipokuwa tatu tu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Rais wetu kwa kuwateua Wabunge akinamama kwa kuwapa uongozi wa juu, Mawaziri na Manaibu Waziri, hongereni sana. Bila kusahahu Wabunge waliochaguliwa kwenye Majimbo yao. Nawapongeza sana pia Wabunge wa Viti Maalum na Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais inaonyesha dira ambayo italeta mabadiliko ya uchumi wa Taifa letu hususan kwa kipindi hiki cha dunia ya utandawazi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba hii kwa sababu ndiyo utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2005, yenyewe majukumu na mikakati ya Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba yote kama ilivyotolewa na kusisitiza yafuatayo:-

Kwanza, elimu na mafunzo ya mara kwa mara mionganoni mwa wananchi na wanachama hasa viongozi wa vyama vyaya siasa kwa lengo la kuweka wazi maana halisi ya demokrasia ili kutetea na kulinda sera za kutoligawa Taifa letu. Napendekeza pawapo na sera za Kitaifa kwa jumla ambazo vyama vyaya siasa vitafuata ili kuweka wazi maslahi ya watanzania. Kwa mfano sera za uwekezaji kwenye maliasili kama vile madini ambazo zitalinda maslahi ya Watanzania na kamwe kutokuingiliwa na siasa za uchumi kwa lengo la kuhujumu.

Mheshimiwa Spika, pili, naunga mkono Serikali kwa kuwa na malengo mahususi ya kuindoa Tanzania kwenye uchumi tegemezi na kutokomeza umaskini kuanzia katika ngazi ya kaya hadi Taifa. Hii imeonekana dhahiri pale Rais wetu alipounda Wizara kwa kuzingatia mikakati aliyoainisha ili utekelezaji wake ufanyike kwa wepesi na haraka na kupima matokeo yaliyokusudiwa ambayo kwa vyovypote vile yatakuwa na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono uboreshaji wa miundombinu ambao umefanyika nchi nzima hususan katika huduma za jamii ikiwepo barabara, elimu na maji.

Kwa kupitia hotuba hiyo, naomba Serikali iangalie tena upya uwezekano wa kusambaza huduma ya barabara hasa pale ambapo uzalishaji wa kuongeza Pato la uchumi wa Taifa unakuwepo. Kwa mfano, katika maeneo ya uchimbaji wa madini hususan *Tanzanite* madini yanayochimbwa Mererani, Simanjiro Mkoani Manyara (madini hayo hayapatikani mahali pengine duniani).

Mheshimiwa Spika, madini ya *Tanzanite* yana thamani kubwa na hasa katika soko la nje na Serikali inapata mapato makubwa kutokana na kuuzwa kwa madini hayo. Barabara inayounganisha eneo hilo la uchimbaji ni takribani kilometra 40 kutoka njia panda ya Moshi - Arusha. Kama ilivyo tangu zamani barabara hiyo imekuwa ni kero kubwa kwa watumiaji na zaidi sana wanawake na watoto wanaoishi eneo hilo huathirika vibaya hasa pale ambapo wanawake wanakwenda kujifungua kwani hakuna hospitali karibu isipokuwa *KCMC*, Moshi au *Mt. Meru*, Arusha.

Mimi mwenyewe nimeshuhudia vifo vyaya akinamama waliojifungulia njiani kwa sababu ya umbali na barabara kuwa mbaya wakienda Hospitali. Dharura yoyote inapotokea huko migodini ni lazima mchimbaji apelekwe *KCMC* au *Mt. Meru*. *Mt. Meru* kwa *X-Ray* pale anapovunjika au huduma ya kuongezewa damu. Kwa sababu barabara ni mbaya, wengi hufia njiani, naomba suala hili liangaliwe na kupatiwa ufumbuzi kama hotuba hii ya Rais inavyositisiza kwa ujumla uboreshaji wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kusimamia kikamilifu huduma za jamii na hasa suala la elimu, mpango wa MEMKWA na *MMEM*, kwa sababu mpango huu unazaa matunda, umepunguza sana mlundikano wa watoto madarasani ambapo madarasa mengine yalikuwa na zaidi ya wanafunzi 100. Napongeza pia mpango wa *MMES* na ushauri mzuri wa kuanzishwa shule katika kila Kata. Lakini je, watoto ambao watafaulu watasuburi mpaka shule hizo zijengwa? Naunga mkono kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana lakini napenda kusisitiza yafuatayo:-

(a) Kwa sababu watoto wengi bado wako mtaani na mijini wenye umri wa kusoma na hawapo darasani basi ningependekeza madarasa ya MEMKWA yaanzishwe na jamii pale ambapo watoto wanaishi na wanaonekana ni wazururaji hawana shughuli rasmi za kufanya katika vijiji au Kata. Serikali isaidie kulipa walimu posho ili iwe kama motisha. Tafiti za mtazamo zinaonyesha kuwa watoto wengi kati ya umri wa miaka 14 hadi 18 ambao hawakuweza kumaliza elimu ya msingi kujiunga na madarasa ya MEMKWA.

Mheshimiwa Spika, wanaona aibu na aidha, hakuna madarasa ya kutosha ya kuwafundishia. Madarasa hayo yakianzishwa nje ya shule ya msingi na kwa vile yatafundisha stadi za msingi za kazi basi yatatoa matunda mazuri na watoto wanapohitimu wanakuwa tayari na ujuzi wanaweza kujiufigi wenyewe ili kuepuka uzururaji na ajira kwa watoto wakiwa na umri mdogo.

Mheshimiwa Spika, vijana wajunge na JKT kwa mujibu wa sheria pindi wanapomaliza elimu yao na hasa ile ya msingi kwa lengo la kuwatayarisha katika kuwajibika kupata ujuzi kabla ya kuajiriwa kwa mfano, endapo mtoto atamaliza darasa la saba akiwa na umri wa miaka 14 na hakuweza kuendelea na elimu ya sekondari basi ajiunge na Jeshi la Kujenga Taifa na huko ajengwe kiufundi stadi na hatimaye baada ya miaka mitatu au minne atakuwa amekomaa na akitoka huko akiwa na stadi za kazi ambazo zitamsaidia kujiufigi mwenyewe. Hii itapunguza uzururaji na ajira zisizo rasmi kwa watoto katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono ulinzi wa mali za raia na kupambana na uhalifu wa kila aina hapa napendekeza yafutayo:-

(i) Jeshi la Polisi liangaliwe upya kwa misingi ya kuwaondoa wale ambao hawapo tayari kulinda maadili ya kazi yao.

(ii) Kuwepo na vitendea kazi vya kutosha kwa Jeshi hilo la Polisi nchini ambavyo vinakwenda na wakati kwa sababu vifaa vingi wanavyotumia hii sasa vimepitwa na wakati.

(iii) Watendaji (Polisi) wapewe marupurupu ya kuridhisha ili isiwe rahisi kurubuniwa kutokana na mazingira magumu walijonayo kazini hii ikiwa ni pamoja na kujengewa nyumba nzuri za kuishi pamoja na kuongezewa mishahara na motisha wanapofanya kazi nzuri.

(iv) Ulinzi wa jadi (Sungusungu) uimarishwe na walinzi hao wafanye kazi mchana na usiku wakishirikiana na jamii na polisi kwa sababu askari wa jadi wanafahamu mambo yote yanayoendelea katika maeneo yao hivyo si rahisi njama mbaya zifanyike bila kufichuliwa.

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Rais kwa hotuba nzuri na nachangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazingira, kuwe na sheria mahususi ya kusimamia upandaji miti katika Halmashauri zetu zote. Liwe ni jambo la lazima si kwa kusubiri siku ya kupanda miti. Pia kuwe na idadi ya miti iliyopandwa na iliyokua, suala la kupanda bila kujua inayoangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora, viongozi katika Wizara waone jambo la muhimu kwa Rais kufanya ziara kila Wizara na watendaji wasikae ofisini, watoke.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ulinzi, kuwepo na makubaliano ya mikataba mbalimbali kuhusu makampuni ya ulinzi na usalama ili kupunguza ujambazi hapa nchini. Uboreshaji wa huduma ya nyumba za polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta, ongezeko la bei ya mafuta liangaliwe sana maana kila siku bei inaongezeka kiholela, kwa nini hakuna utaratibu mzuri na waufafanue kuhusu suala la upandaji wa bei ya mafuta na kwa nini imepanda?

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, shule za binafsi ni nyingi sana, gharama kubwa, sheria ipi inayowaruhusu kufanya hivyo. Cha kushangaza Waziri wa Elimu kipindi kilichopita katika Mkoa wake kuna shule ya binafsi na mkewe ni Mkurugenzi, wataka kuniambia maana ya kuanzishwa shule hiyo hakubaliani na shule za Serikali kama zina mchepuo wa maendeleo ya elimu bora? Tubadilike, sasa tujikosoe ili nchi yetu ipate mafanikio makubwa kielimu.

Mheshimiwa Spika, wasichana kupata mimba kwa kasi sana, suala hili liangaliwe na wasichana hao waweze kuendelea kielimu kama Zanzibar. Linawezekana huku kumezidi nini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwako binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu, nampongeza sana Mama Anne Makinda, kwa kuwa Naibu Spika hivyo kuwa mwanamke wa kwanza Mtanzania kushika wadhifa huo hapa nchini. Kwa wanawake tumefarijika sana. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteua wanawake wengi kushika nyadhifa za juu Serikalini.

Pili, nakishukuru Chama cha Demokrasi na Maendeleo (CHADEMA) kwa kunitfea kushika wadhifa huu. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Freeman Mbwe,

Mwenyekiti wa CHADEMA kwa jinsi alivyofanya kampeni za kisayansi hivyo kuweza kuongeza idadi ya Wabunge kutoka watano hadi kumi na moja. Kwa heshima niliyopata nawaahidi wana CHADEMA kuwa sitawaangusha, nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu wote.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais kama alivyoitoa katika Bunge hili tukufu tarehe 30 Desemba, 2005. Kwa uhakika hotuba hii ni nzuri kwa maana ya kwamba imegusa sehemu zote zinazohusu maendeleo ya nchi hii. Hii ni pamoja na huduma za jamii, miundombinu, nishati, madini na maliasili. Tatizo ninaloliona lipo katika utekelezaji kwa maana ya kuwa hotuba hii haikuonyesha waziwazi ni lini mikakati iliyoainishwa na Rais itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa utekelezaji wa kitu chochote unategemea muda au *time frame*. Najiuliza hivi ni lini mipango hii mizuri ya Rais itatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala zima la vipaumbele. Katika hutoba hii haielezi wazi wazi Serikali ina kipaumbele gani? Haiwezekani mambo yote aliyoyaorodhesha Rais katika hotuba yake yawe na kipaumbele. Tutakuwa tunagusa hapa na pale katika kila jambo hivyo kutokuwa na ufanisi katika utekelezaji. Ningeshauri Serikali iweke vipaumbele vichache ili viweze kutekelezwa kwa ufanisi na umakini.

Mheshimiwa Spika, tuchukue mfano wa nchi za India na China ambazo zilijiwekea kipaumbele cha mapinduzi ya elimu. Waliona elimu ndiyo njia pekee ya kukuza uchumi. Baadaye walijikita kwenye miundombinu na sasa hivi nchi hizi zina uchumi mzuri usioteteleka. Kwa kweli tusipokuwa na vipaumbele vichache hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nichangie katika suala la utawala bora. Mheshimiwa Rais ameongelea sana suala hili na akakazia suala la rushwa. Rushwa ni chanzo cha kurudisha nyuma uchumi na pia kupunguza ufanisi na uwajibikaji. Rushwa inakuwa mbaya zaidi pale inapogusa vyombo vyta dola kama polisi, kwani wananchi wanakosa imani na watumishi hao hadi inafikia wananchi kujichukulia sheria mikononi yaani *mob justice*.

Mheshimiwa Spika, hii inafanyika kwa sababu wananchi wanapeleka mhalifu polisi, baada ya siku mbili wanamwona mtaani zaidi ya hapo hata wale raia wema wanaopeleka taarifa kwa polisi wamekuwa wakiwapa taarifa hizo wahalifu. Wahalifu hao huwarudia wale raia wema na kuwatambia kwamba hawana lolote.

Mheshimiwa Spika, sasa nichangie katika suala la amani na utulivu. Amani na utulivu ni jambo la msingi sana na imesaidia sana nchi yetu kupata marafiki wengi ikiwa ni pamoja na wawekezaji wengi. Lakini amani na utulivu itadumu tu kama wananchi watasikilizwa matatizo yao. Nchi kama Burundi, Rwanda na Siera Leone zilikuwa nchi zenye amani na utulivu wa hali ya juu lakini sasa hivi nchi hizo hazikaliki kwa kuwa zina vita za wenywewe kwa wenywewe. Uvumilivu huwa na mwisho wake kutegemeana na jinsi wananchi wanavyonyimwa haki zao za msingi. Wito wangu ni kuwasikiliza wananchi, tusiyapuuze madai ya msingi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la umaskini. Nchi yetu ni maskini na ni tegemezi, tunategemea kiasi kikubwa cha fedha za Bajeti yetu kutoka nje ya nchi. Inasikitisha zaidi kuona viongozi wetu kutozingatia umaskini wa wananchi. Kwa nini nasema haya.? Tukiangalia Baraza la Mawaziri, Makatibu Wakuu na Manaibu, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Manispaa pamoja na Wakurugenzi wote hawa wamepatiwa magari ambayo thamani ya gari moja ni zaidi ya shilingi 80,000,000. Hivi kweli ni lazima kwa Waziri kuwa na Magari ya 4x4 katika Jiji la Dar es Salaam? Siamini kama *4x4 cars* zinahitajika.

Nijuavyo mimi *four wheel drive* zinaendeshwa katika barabara mbovu, hivyo hizi gari ni muhimu sana kwa Wabunge kwani barabara Majimboni ni mbovu sana. Hivi Waziri anayetoka *Oysterbay* kwenda ofisini katikati ya jiji la Dar es Salaam ana haja ya gani ya kuwa na *VX GX* au *Prado*? Kwa nini asiwe na *Toyota Mark II* au *Chaser* mayai inayogharimu shilingi milioni 7? Kama suala la kuja Bungeni Dodoma kwa Mawaziri kwa nini tusiwe na mabasi *very luxurious* kama yalivyo kwa Wabunge?

Mheshimiwa Spika, India Mawaziri wanatumia vigari vidogo tu. Hivi ni utajiri gani tulionao wa kuwa na magari ya gharama kubwa huku wananchi wetu wana hali mbaya sana? Wafadhili wanatushangaa jinsi baadhi ya Watanzania wanavyoishi maisha ya anasa kuliko hata wale wanaotoa misaada hiyo. Hii siyo sifa nzuri kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni elimu. Elimu ndiyo msingi na ufunguo wa maisha. Kwa bahati mbaya sana Serikali haijatilia mkazo suala hili hii ikiwa ni pamoja na kutoa Bajeti ndogo sana hivyo kufanya elimu ya msingi kuzidi kudorora. Ni kweli ubora wa elimu unategemea walimu na vitabu ikiwa ni pamoja na mazingira mazuri na sio wingi wa madarasa na wanafunzi wengi.

Mheshimiwa Spika, Shirika lisilo la Kiserikali la Haki Elimu lilijitahidi sana kukosoa Wizara ya Elimu ili iweze kuboreka zaidi. Cha ajabu Shirika hili limepigwa marufuku. Sasa tunajiuliza hivi ni kweli imefikia kuwa viongozi wetu wanataka wasifiwe tu hata pale wanapoboronga? Shirika hili limejitahidi kuelezea matatizo ya walimu ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya mishahara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, elimu imekuwa mali ya Wizara ya Elimu, mitaala imekuwa inaandaliwa na maofisa wa Wizara bila kuwashirikisha walimu ambao ndio wadau wakuu matokeo yake mitaala imekuwa haiendani na utaalam wa walimu. Kwa mfano, somo la stadi za kazi, walimu wanaambiwa wafundishe utengenezaji wa redio yeye mwewewe hajafundishwa somo hilo. Je, atawezaje kufundisha? Wanafunzi wenyewe wakimaliza darasa la saba bado hawataweza kufanya matengenzo ya redio kwa kuwa somo hilo linafundishwa kinadharia na sio *practical*. Hii inamfanya mwanafunzi mhitimu wa darasa la saba kushindwa kabisa kufanya ufundi wa redio mtaani.

Mheshimiwa Spika, wakati fulani Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema kulangua elimu ni dhambi. Sasa hivi elimu inalanguliwa na hivyo hivyo kuweka matabaka ya waziwazi. Karo ya elimu ya *nursery* hadi shilingi

milioni moja, shule hadi shilingi milioni 1.5, sekondari hadi milioni moja. Kwa Mtanzania wa kawaida ni ngumu mno.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali isimamie ada ili kupunguza *gap* kati ya Watanzania maskini na matajiri katika suala la elimu.

MHE. MWADINI ABASS JECHA: Mmeshimiwa Spika, mimi naelekeza mchano wangu katika suala la kuwepo kwa mpasuko wa kisiasa kati ya Unguja na Pemba na pengine kati ya Pemba na sehemu nyingine ya Jamhuri yetu.

Kama anilivyosema Mheshimiwa Rais suala hili lipo na limekuwepo kwa muda mrefu sasa kiasi ambacho linamsononesha kila mtu mwenye kuiona hali hii.

Mheshimiwa Spika, mpasuko huu utaendelea kukua iwapo hatua za dhati na za maksudi hazitachukuliwa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa mpasuko huu na kwa hivyo nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuliona tatizo hili na kwamba linamsononesha na kwamba sasa anaona upo umuhimu wa kuandaa mikakati madhubuti ya kuiondoa hali hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa ushauri wa nini kifanywe naomba nidokeze kidogo baadhi ya sababu ambazo zimepelekea kuwepo huo mpasuko na kuendelea kupasuka na kufikia hali iliyopo hivi sasa. Miongoni mwa sababu hizo nitazigawa katika mafungu mawili makubwa.

Fungu la kwanza ni la maendeleo ya kiuchumi na eneo la pili ni la kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu Visiwa vya Zanzibar kwa miaka mingi sana uchumi wake unategemea zao la Karafuu. Asilimia 90 ya zao hili linalimwa Pemba lakini ni jambo la kusikitisha sana jinsi mgao wa mapato yatokanayo na zao la Karafuu yanavyogawiwa katika shughuli za maendeleo baina ya Unguja na Pemba. Haya yanaweza kuthibitishwa na mpango wa matumizi ya Serikali ya Zanzibar yanayopitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Spika, ni jambo lililodhahiri kwamba kwa kiasi kikubwa ujenzi wa barabara, upanuzi wa gati na uwanja wa ndege, viwanda na kadhalika yanafanyika Unguja. Aidha, huduma za elimu, afya na umeme wa uhakika zinatolewa zaidi Unguja kuliko Pemba.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaleta mkanganyiko wa mawazo jinsi ambavyo Serikali ya Zanzibar inavyoendeleza ubaguzi wa kimaendeleo baina ya visiwa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kisiasa nako pia kuna ubaguzi wa hali ya juu. Aidha, upandishaji vyeo Serikalini, ugawaji wa nyadhifa za kiutendaji Serikalini nao pia hauzingatii uwiano kati ya Visiwa hivi. Ubaguzi wa wanafunzi mashulen ambao unapelekea wanafunzi walioko Unguja wasome Unguja na walioko Pemba hawana

ruhusa kusoma shule za Unguja. Ubaguzi huu unuaa umoja wa kitaifa na kukuza uhasama katika kizazi kipyä.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni jambo la kawaida kuwasikia baadhi ya viongozi wa Serikali pamoja na baadhi ya jamii ya Waunguja wakisema kuwa Mpemba kuingia Ikulu ni sawa na mbwa kuingia msikitini na kama Wapemba wanataka kuingia Ikulu basi wajenge yao. Kauli kama hizi zinatisha, ni za kibaguzi na zinakuza chuki ya Wapemba na Waunguja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mchakato wa kisiasa uliopita, Zanzibar imejengwa dhana kwamba Wapemba ni Waarabu na kwamba azma kubwa ya kutaka uongozi ni kuwarejesha Waarabu watawale tena nchi. Dhana hii nayo inakuza uadui kati ya jamii ya Wapemba ama Waarabu na jamii ya Waunguja.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa kushauri yafuatayo:-

Kwanza, ni vyema sasa miundombinu ya Pemba kama vile barabara, uwanja wa ndege wa Karume, gati za Mkoani na Wete viganuliwe ama kujengwa upya ili kuleta uwiano katika kukuza shughuli za kiuchumi katika kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Spika, aidha, mgawanyo wa madaraka na upandishaji wa vyeo kwa watumishi wa Serikali uzingatie elimu, uwezo na uzoefu na sio wapi mtu anatoka.

Mheshimiwa Spika, mchanganyiko wa wanafunzi mashulenii uwe kama uliviyokuwa katika awamu ya tatu ya uongozi wa Serikali. Shule hususan za sekondari na vyuo kuwe na mchanganyiko wa wanafunzi kutoka Pemba na Unguja.

Mheshimiwa Spika, unyanyasaji wa Wapemba unaofanywa na vyombo vya dola, Vikosi vya SMZ pamoja na makundi ya *Janjaweed* ukomeshwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na tukawenza kuwepo hapa leo pamoja.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kutokana na ushindi mkubwa alioupata katika uchaguzi mkuu wa 2005 na kupata kura za kishindo. Vile vile nampongeza kwa hotuba aliyoitoo Bungeni tarehe 30 Desemba, 2005. Hotuba ambayo imekusanya nyanja mbalimbali za kuleta maendeleo ya Tanzania nzima. Pia simsahau Makamu wake Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, nawaombea kwa Mungu wazidi kuwa na ushirikiano katika juhudii za kuiletea maendeleo nchi yetu.

Pia nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo kuwa Rais wa Awamu wa Sita Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuongoza Bunge hili. Nampongeza pia Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge hili kuwa Waziri Mkuu. Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa mbalimbali. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na wale walioteuliwa wote kuingia Bungeni kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, lakini pia nichukue nafasi hii kuwapongeza wanachama wa CCM wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kunichagua kwa mara ya kwanza kuingia ndani ya Bunge hili nikiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais katika vipengele vyote. Mheshimiwa Rais amegusa mambo mbalimbali katika hotuba yake na ikiwa tutaifuata kwa vitendo basi ndipo itakapojengeka sera ya maisha bora kwa kila Mtanzania kwenye Tanzania yenye neema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kipengele cha amani na utulivu, nataka kusema kuwa amani na utulivu ndio dira sahihi katika nchi yetu itakayotuongoza ikiwa tutaifuata. Napenda kusema kuwa tutafanikiwa ikiwa tutaondoa tofauti zetu za kisiasa na kuangalia zaidi maendeleo ya nchi kwani bila amani hakuna maendeleo.

Mheshimiwa Spika, watoto, vijana wetu wanahitaji elimu na malezi bora ya kutosha ambayo yatawawezesha kuwa viongozi imara wa baadaye. Pia tuwe na tabia ya kuwapa historia ya nchi sio kuwapotosha ili waweze kuwa na uchungu wa nchi yao. Tuepukane na tabia ya kuwajengea jazba vijana wetu na kuhatarisha maisha ya raia. Bila kuwepo na amani hakuna kijana wala mtoto atakae kuwa na muda wa kupata elimu na wazee pamoja na wasiojiweza watahanganya na kufa bila ya kuhudumiwa. Vijana watapotea kabisa, nchi itakuwa yenye giza. Hivyo napenda kuwatahadharisha viongozi wa vyama vya siasa kuwaweka chini vijana wao na kuwapatia elimu sahihi ya historia ya nchi yetu na kuwalenga katika masuala ya maendeleo ya nchi bila tofauti zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kuwa Mheshimiwa Rais aliyaona mengi ndio maana akaweza kutuandalia hotuba ile Bungeni na kama tutafuata yale yote aliyoyasema ndani ya hotuba ile basi ndiyo pale tutakapokuwa na nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya. Lazima tuangalie sana amani ndiyo msingi wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujambazi na rushwa, ujambazi umekithiri sana Tanzania imefikia hadi mtu anajiamini kutembea kifua mbele awe kwa miguu, pikipiki au hata gari. Kumejitokeza vijana waporaji hovyo na wezi waliokithiri na unapotoa taarifa polisi baadhi ya askari polisi wanapokea rushwa na kusababisha kuendelea kwa hali hii ya ujambazi. Napenda tuungane na Mheshimiwa Rais katika maagizo aliyoyatoa katika hotuba, aliyowahutubia wananchi wa Dodoma katika Uwanja wa Jamhuri kuwa tushirikiane katka kupambana na hali hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mipango miji, kwa upande wangu napenda nichukue fursa hii kuelezea suala la ukarabati wa Ikulu ya Wete ambayo tunavyojuwa Ikulu hiyo iko katika hali mbaya na inajulikana kwa jina la Ikulu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivi sasa Mheshimiwa Rais anapofanya ziara Kisiwani Pemba inatisha kusikia Mheshimiwa Rais atapata mapumziko mafupi katika Ikulu ya Wete. Tunamwomba Mheshimiwa Rais kuliona suala hilo kwani wakati wa ziara zake aweze kuwa na mahali pazuri katika Ikulu hiyo kwa mapumziko. Matengenezo yanayohitajika hapo ni ukarabati wa jengo, ujenzi wa barabara ya kuelekea Ikulu hiyo na kuwepo wafanyakazi wa bustani wakutosha. Namwomba Mheshimiwa Rais kulitupia macho suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo mafupi naunga mkono hoja.

WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi walishiriki katika kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, wakizungumzia masuala yanayohusiana na Wizara ya Usalama wa Raia. Waheshimiwa Wabunge wapatao 32 walipata nafasi ya kutoa ushauri na maoni mbalimbali juu ya utendaji kazi katika Jeshi la Polisi. Napenda kuwashukuru kwa michango yao ambayo naamini itasaidia kuliimarisha Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, siyo rahisi kuelezea kila hoja ya Mheshimiwa Mbunge mmoja mmoja. Hivyo, Wizara yangu inakubali maoni, ushauri maelezo na hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge na kuwaahidi kwamba tutazitafakari na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo juu ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, napenda kutoa Taarifa fupi juu ya hali ya uhalifu nchini kuanzia mwaka 2004 hadi Januari mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu Jeshi la Polisi limekuwa likifanya kazi nzuri sana. Likijitahidi kulinda raia wake na mali zao hapa nchini. Hii inadhihirishwa zaidi ukiangalia takwimu kwa miaka miwili ya nyuma yaani 2004 na 2005. Kwa mujibu wa takwimu za matukio ya jinai yaliyoripotiwa Polisi kwa mwaka 2005 zinaonyesha kuna upungufu wa matukio 9,956 ikilinganishwa na mwaka 2004. Upungufu huu ni sawa na asilimia 16.2. Hata hivyo, kwa mwezi Januari, 2006 takwimu hizo zinaonyesha kuna ongezeko la asilimia 8.3 kwa matokeo ya ujambazi wa kutumia silaha peke yake. Ongezeko hili ni kwa Mkoa wa Dar es Salaam peke yake Mikoa mingine ambayo ilikuwa na matokeo mengi ya ujambazi kwa kutumia silaha ni Kigoma, Kagera na Arusha.

Mheshimiwa Spika, baada ya taarifa hiyo, naomba sasa kutoa ufanuzi katika maeneo machache ambayo yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa ujambazi, Waheshimiwa Wabunge katika suala hili waliongea kwa uchungu sana. Ni kweli usiofichika katika mwezi wa Januari,

2006. Matukio na yenye kuvuta hisia za wananchi yametokea katika Mikoa yetu hususan Dar es Salaam, Kagera na Arusha. Matukio haya yamevuta hisia kwa vile yametokea mchana katikati ya mji na yamelenga taasisi za fedha, maduka ya fedha na biashara.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limebuni mikakati yenye lengo ya kukabiliana na wimbi hilo la ujambazi hapa nchini. Ninaamini mikakati hiyo ikitekelezwa kikamilifu wimbi hilo litapungua kwa kiasi kikubwa. Mikakati mbalimbali imeshaanza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kufanya operesheni maalum ya kuwasaka majambazi na silaha zao. Jeshi la Polisi limeanza kutoa ulinzi kwa Mabenki yote ya *NBC* hapa nchini. Pia tunafanya mawasiliano na Benki Kuu Tanzania kuandaa utaratibu wa kisheria utakaowalazimisha wamiliki wa Benki kuweka mifumo ya ulinzi inayotumia teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wananchi, tumezingatia hoja za Waheshimiwa Wabunge juu ya namna bora ya kuwashirikisha wananchi katika suala zima la ulinzi na usalama. Suala hili ni la muhimu sana kwani tunaelewa kwamba wao ndiyo wenye kuweza kutupatia taarifa sahihi za uhalifu na wahalifu ambazo tunaweza kuzifanyia kazi na kufanikiwa kupunguza wimbi la uhalifu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wananchi ambao wamejitokeza kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu na tunaomba wananchi wengine waige mfano huu ili hatimaye tuweze kufanikisha zoezi zima la kupambana na uhalifu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu inafanya maandalizi kwa kutungwa kwa Sheria itakayodhibiti kampuni binafsi za ulinzi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa kampuni hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nidhamu ya Askari Polisi, Wizara yangu inatambua kuwepo kwa Askari wachache ambao wamekuwa wakikiuka maadili mema ya utumishi wao kiasi cha kuharibu sifa nzuri ya Jeshi la Polisi. Juhudi zinafanyika za kudhibiti matendo maovu ya Askari hao wachache ikiwa ni pamoja na kuwafukuza kazi wale wasiofaa. Tunaomba ushirikiano wa wananchi juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa vitendea kazi, Serikali inatambua mapungufu yanayokwamisha utendaji na ufanisi wa Jeshi la Polisi na inaendelea kuchukua hatua za dharura na zile za muda mfupi na muda mrefu kwa lengo la kuliwezesha Jeshi la Polisi kufanya kazi yake kwa ufanisi na kukidhi matarajio ya wananchi. Mapungufu hayo ni pamoja na vitendea kazi, maslahi ya Askari, mishahara, posho, makazi, motisha na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Wizara yangu inashughulikia tatizo la deni sugu la posho za Askari ili hatimaye Askari wote wanaodai posho waweze kulipwa. Kama alivyozungumza Naibu Waziri hapa Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, sasa hivi Askari wanadai bilioni 8 na suala hili tulikwishalifikisha katika vikao vya juu na linashughulikiwa. Ni matarajio yangu kwamba kulipwa kwa posho hizi kutaongeza

ari ya utendaji kazi kwa Askari hawa na hivyo kuongeza tija katika utendaji. Wizara yangu pia inaangalia upya utaratibu wa ajira ya Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia juu ya kushirikisha Jeshi la Wananchi Tanzania katika suala la kupambana na ujambazi. Napenda kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba Jeshi la Polisi bado linao uwezo wa kukabiliana na hili tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muundo wa Wizara, Wizara yangu ni Wizara mpya hivyo hivi sasa tunaandaa muundo wa Wizara ambapo dhana ya usalama wa raia itaangaliwa kwa makini sana. Aidha itaandaliwa Sera ya Usalama wa Raia itakayoendana na wakati tulio nao.

Mheshimiwa Spika, baada ya Sera ya Usalama wa Raia kukamilika, Sheria za Usalama wa Polisi zitatungwa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopo za Jeshi la Polisi. Wizara yangu itafanya mabadiliko katika utendaji wa Jeshi la Polisi ili kulifanya liwe la kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, pamoja na maelezo hayo, napenda kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yao yatazingatiwa kwa faida ya wananchi wanaowatumikia na Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia. Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia ameweka mfano mzuri, amezungumza ndani ya dakika 15. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA (MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA): Mheshimiwa Spika, nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameunga mkono hoja hii kwa kutamka kwamba nami naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia hoja hii hasa waliogusa eneo la mazingira na wamezungumza kwa uchungu sana.

Mheshimiwa Spika, waliochangia moja kwa moja kuhusu eneo la mazingira walikuwa Waheshimiwa Wabunge kama 27 hivi. Wengine wengi wamechangia kuhusu mazingira lakini mengi yamegusa Wizara nyingine kwa mfano Wizara ya Maliasili na Utalii, Maji hata Elimu. Kwa maana hiyo, baadhi ya hoja zao sitaweza kuzijibui kwa sababu nina uhakika zitajibwi na Mawaziri wenzangu kwa sababu kama mnavyojua suala la mazingira ni suala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, hali ya mazingira ya nchi yetu ni mbaya. Miti inakatwa ovyo, vyanzo vya maji vinakauka, mabwawa yanakauka. Maeneo owevu au maeneo

chepechepe yanaingiliwa na kukauka. Mifugo sehemu nyingi inazidi uwezo wa malisho, kina cha maji kwenye Maziwa yetu kinapungua kwa mfano Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Kwa kipindi cha miaka 35, takwimu za vituo 21 ya Hali ya Hewa zimeonyesha kuna kupungua kwa mvua nchini hali iliyopelekeea ukame. Migogoro katika matumizi ya ardhi, tatizo la umeme ambalo tumelisikia sasa hivi ni tatizo la mazingira kwa kweli. Bioanuai viumbe, miti adimu inayopatikana Tanzania tu nayo imepotea. Kwa hiyo, hali ya mazingira ya nchi yetu ni mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge inaonyesha kwamba hatuna sababu ya kukata tamaa. Ni michango mizuri na imejikita katika maeneo makuu mawili. Umuhimu wa kuwa na programu madhubuti wa hifadhi ya mazingira nchini na vile vile umuhimu wa usimamizi na utunzaji wa mazingira hususani utunzaji wa vyanzo vya maji. Lakini vile vile Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia masuala mengine kama vile ya taka ngumu, taka za plastiki na suala la mazingira maalum ya Visiwa vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu programu ya mazingira ya Kitaifa, labda tukubaliane kwamba kila Wilaya itakiwe na itatakiwa kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi, ikitainisha pamoja na mambo mengine maeneo mahsus kwa ajili ya kilimo, mifugo ikiwa ni pamoja na kubaini uwezo wa malisho, maeneo ya misitu, makazi na maeneo yanayohitaji uokoaji ambayo yameharibika pamoja na kuainisha vyanzo vya maji katika miji muhimu. Itabidi tuzingatie mipango miji, tupande miti mijini, tutenge maeneo maalum katika miji yetu yawe mashamba ya miti kwa ajili ya nishati na kwa ajili ya biashara kama vile mbao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kampeni ya Taifa ya kupanda miti na kutunza miti iende katika gia ya haraka zaidi. Kila Wilaya iainishe maeneo na aina ya miti ya kupandwa. Tupande miti ya asili, maeneo yatengwe kwa ajili ya Hifadhi ya misitu zaidi ya yale ambayo yametengwa Kitaifa kwa ajili ya nishati, maeneo yaliyoharibika yatengwe ili uoto wa asilia uanze upya, vyanzo vya maji tuvitambue, tuyainishe na pale inapobidi tupande miti inayokubalika kupandwa kulinda vyanzo vya maji. Shule za Msingi na Shule za Sekondari na Taasisi mbalimbali ziwe vitovu vya kuendeleza mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, programu hii ni vema iwe shirikishi ikihusisha vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya kwa maana Halmashauri na Wakuu wa Wilaya na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali. Kama nilivyosema hapa leo asubuhi nikijibu swali la Mheshimiwa Mbunge mmoja, sekta binafsi ina nafasi kubwa sana katika hifadhi ya mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuonyesha mfano na kwa vitendo, Mheshimiwa Rais katika suala la kuhifadhi mazingira mbali na kuanzisha kampeni ya upandaji miti, tarehe 1 Januari, Rais amekubali ianzishwe Tuzo ya Rais ya Kupanda Miti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mikoa itashindanishwa katika Tuzo hiyo. Tuzo hiyo itatolewa katika kila tarehe 5 Januari ambayo ni siku ya Mazingira Duniani. Samahani tarehe 5 Juni ambayo ni siku ya Mazingira duniani. Kila Mkoo wa Mkoaa naye ataanzisha

Tuzo ya Mkuu wa Mkoa ya Hifadhi ya Mazingira ikihusisha utunzaji wa vyanzo vya miji, ufugaji endelevu, kilimo endelevu pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi ya mazingira, nalikumbushia Bunge lako Tukufu kwamba Sheria Namba 7 ya Mwaka 1982 na Sheria Na. 8 ya mwaka 1982 zinatoa mamlaka kamili ya usimamizi na hifadhi ya mazingira kwa Halmashauri za Wilaya, Halmashauri za Miji, Halmashauri za Manispaa na Halmashauri za Jiji. Kama tunavyojuua Halmashauri zimeanzisha Kamati za Kudumu za Mazingira. Tuzitumie kikamilifu Kamati hizo katika vita hivi vya kuhifadhi mazingira ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sheria Na. 20 ya mwaka 2004 inampa madaraka Waziri mwenye dhamana ya mazingira kutambua na kutangaza eneo au maeneo nyeti ya kiikolojia. Maeneo ambayo inabidi yapewe hifadhi na sheria hiyo na maeneo ambayo hayajapewa hifadhi na sheria nyininge za nchi yetu, anawenza vile vile akakasimu usimamizi wa eneo hilo kwa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema na kusisitiza ni kwamba sheria zipo kwa hiyo kila mhusika kwa mamlaka aliyopewa atekelze sheria hizo. S vizuri Katibu Kata alalamike kuhusu mazingira, Katibu Tarafa alalamike, *DC* alalamike, Mkuu wa Mkoa alalamike, Waziri mwenye dhamana ya mazingira naye alalamike, Bunge lilalamike, Rais alalamike, tufanye kazi.

Mheshimiwa Spika, michango mingine ya Waheshimiwa Wabunge tumeichukua. Tumeichukua kama ushauri mzuri na pengine ni kama maelekezo ya kuzingatiwa katika mipango ya hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Kwa ujumla imedhihirisha kwa mara nyininge tena kwamba Waheshimiwa Wabunge ni wana mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wahenga wanasema hatujarithi ulimwengu huu kutoka kwa babu zetu bali tumekopeshwa na wajukuu zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa maelezo ya ufanuzi kuhusu hoja za Waheshimiwa Wabunge zinazohusu Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Mufindi Kaskazini na wananchi wenzangu wote wa Wilaya ya Mufindi kwa kunichagua kwa mara ya saba kuwa Mbunge wao katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge 58 waliochangia katika maeneo mbalimbali saba yanayohusu sekta ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Sasa naomba nichukue fursa hii kutoa maelezo kwa yale maeneo saba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza linahusu programu ya kuendeleza sekta ya kilimo ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 13. Kwa kuzingatia Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 kuanzia 2005 – 2010 kilimo kinatakiwa kikue kwa asilimia 20 kutoka asilimia 6 ya mwaka 2004. Ili kufikia lengo hilo programu ya kuendeleza sekta ya kilimo yaani *Agricultural Sector Development Programme (ASDP)* ambayo tayari ipo itahuishwa ili iweze kukidhi maelekezo ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, programu hii inaiwezesha Serikali kuongeza uwekezaji katika kuendeleza kilimo. Karibu asilimia 75 ya fedha yote ya Serikali itakayowekezwa katika kilimo itaelekezwa katika Wilaya na Vijiji kupitia uwekezaji katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo na Wilaya yaani *District Agricultural Development Plans* yani DADP. Kila Wilaya itakuwa na mpango wa aina hii wenyе fedha za uhakika.

Eneo la pili linahusu kilimo cha umwagiliaji ambalo tumepokea mawazo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge 14. Mpango kabambe wa Taifa wa Kilimo cha Umwagiliaji yaani *Irrigation Master Plan* umebaini kwamba Tanzania ina eneo la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa umwagiliaji maji mashambani yenye viwango mbalimbali vya uwezekano wa kuendelezwa ikiwemo hekta milioni 2.3 zenye uwezekano mkubwa yaani *high potential* na hekta milioni 4.8 zenye uwezekano wa kati yaani *medium potential* na hekta milioni 22.3 zenye uwezekano wa chini yaani *low potential*.

Mheshimiwa Spika, Wizara imelenga kuendeleza hekta milioni 2.3 hizo zilizomo katika *high potential* mapema iwezekanavyo kwa kuzingatia gharama na mahitaji ya uendelezaji. Aidha, Wizara inapanga awamu mbili ya kufikia lengo hilo. Katika awamu ya kwanza tufikie hekta milioni moja na awamu ya pili, tufikie hekta zote milioni 2.3. Ili kuyafikia malengo hayo inatarajia kutekeleza mapendekezo ya kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji yaani *National Irrigation Development Fund* utakaotumika kama ilivyo kwa maendeleo ya barabara kwa kutumia Mfuko wa Barabara yaani *Road Fund* au kama ilivyo kwenye mpango wa MMEM na MMES katika elimu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji utahusu ujenzi wa mabwawa, matumizi ya teknolojia rahisi za uvunaji wa maji ya mvua, pampu zinazotumia dizeli, mionzi ya jua na nguvu za upemo, matumizi ya maji ardhini na umwagiliaji kwa njia ya matone yaani *drip irrigation*.

Eneo la tatu linahusu matumizi ya zana bora ya kilimo. Katika eneo hili, tumepata mawazo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge 24. Malengo ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 ni kuhakikisha kuwa Serikali inawasaidia na kuhimiza watu binafsi wenyе uwezo wa kukopa matreka yatakayotumika kukodishwa kwa wakulima mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2005, Serikali itaendelea kuhamasisha watu binafsi wenye uwezo wa kukopa matrepta na kuanzisha vituo vya kukodisha matrepta kwa kuweka dhamana mali zao zinazokubalika kisheria. Watapewa pia utaalam wa kuendesha vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana chini ya mpango huu, vilianzishwa vituo vitatu Songea Mjini, Masasi na Moshi Mjini. Vituo vya matrepta vinavyotarajiwa kuanzishwa mwaka huu ni vitano. Majina ya vituo hivyo vitano bado hayajawa tayari kwa sababu jambo hili lipo katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaendelea kufanya ukarabati wa vituo vya wanyamakazi na kuipatia zana mbalimbali kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wakulima. Zana hizo ni pamoja na plau, majembe ya palizi, majembe ya matuta, ripa, jembe tindo, mashine za kupanda mbegu na mikokoteni.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia mfuko wa pembejeo itawakopesha wakulima zana hizi ili waweze kuzitumia kuendeleza kilimo. Aidha, itatolewa mikopo ya kununulia matrepta madogo ya mikono yaani *power tillers* ambayo inahitajika sana kwa wakulima wa mashamba ya mpunga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea ambayo pia Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia, hapa Tanzania bado matumizi yetu ya mbolea ni wastani wa kilogram 7 za virutubisho vya mimea kwa hekta. Tukilinganisha na wenzetu Malawi wanatumia wastani wa kilo 27 kwa hekta, Afrika ya Kusini kilo 53 kwa hekta, India kilo 103 kwa hekta, China wastani wa kilo 279 kwa hekta. Matumizi madogo mno ya mbolea yanachangia kwa kiasi kikubwa nchi yetu kukumbwa na upungufu wa chakula mara nyangi.

Mheshimiwa Spika, kitaalam ni muhimu matumizi ya mbolea yafikie angalau wastani wa kilogram 100 za virutubisho kwa hekta ndipo uwepo uhakika wa chakula cha kutosha na kasi nzuri ya kukua kwa kilimo. Kwa hiyo, ipo haja kubwa ya kuongeza utumiaji wa mbolea kutoka hizo kilogram 7 za virutubisho kwa hekta za sasa hadi kufikia angalau kilogram 50 za virutubisho kwa hekta mapema iwezekanavyo. Kiwango hicho ni sawa na matumizi ya takriban tani 700,000 za mbolea za viwandani. Kwa hiyo, ni muhimu tuongeze matumizi ya mbolea kutoka tani 120,000 za sasa hadi kufikia hizo tani 700,000 ifikapo mwaka 2010. Baada ya hapo, itabidi tuenze awamu ya pili ya kuelekea kwenye kilogram 100 kwa hekta ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo hayo mazuri, itabidi kuongeza sana ruzuku ya mbolea kama inavyoelekezwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Aidha, Serikali itahamasisha sekta binafsi hususan makampuni makubwa ya usambazaji wa mbolea katika soko la dunia kama vile Kampuni ya Yara ya Norway kuleta mbolea nchini kwa wingi. Tayari wamekwishakubaliana na Wizara kuwa na mbolea ya kutosha katika maghala yao ambayo wanayafungua katika maeneo muhimu kama vile Dar es Salaam, Makambako, Arusha na Mwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakulima walio wengi wanatumia mbegu kutokana na mavuno yao ya msimu wa awali. Mara nyingi mbegu hizo siyo bora kwani zimechanganyika au hazijafanyiwa *selection*. Aidha, upatikanaji wa mbegu bora na kwa bei nafuu si mzuri. Kwa wastani upatikanaji wa mbegu bora ni tani 10,825 ambayo ni sawa na takriban asilimia 36 tu ya mahitaji ya tani 30,000 za mbegu bora kwa mwaka. Mpango wa kuongeza uzalishaji wa mbegu utatekeleza mambo yafuatayo: Kwanza, utapanua na kufanya umwagiliaji kwenye mashamba ya mbegu ya Serikali hekta 5,000 kwa mwaka na kuzalisha tani 10,000 za mbegu bora. Pili, utatekeleza/kuendeleza mpango wa uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya chakula unaotekelizwa na wakulima vijijini. Tatu, tunatarajia kuanzishwa kwa Wakala wa Mbegu (*Agricultural Seed Agency*) utakaomiliki mashamba ya mbegu ya Serikali na nne, kuhamasisha sekta binafsi kuzalisha takriban tani...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)

SPIKA: Samahani Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, utaendelea tu kwa sababu tumeokoa muda kama wa dakika 10 kwa wenzio. Nadhani mambo ya kilimo ni mazito zaidi, basi sasa endelea. (*Makofii*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne linahusu usalama wa chakula. Eneo hili limekuwa na wachangiaji 27. Ili kuhakikisha usalama wa chakula kwa wananchi, Wizara hutathmini hali ya mazao mashambani kila mwezi wa 5 na kukiwepo upungufu Wizara hutoa tahadhari za awali (*early warning*) ambazo hufuatiliwa na tathmini za kina kubaini ukubwa wa tatizo. Aidha, Wizara hununua mahindi kutoka kwa wakulima na kuyahifadhi katika maghala ya hifadhi ya chakula ya Taifa kwa ajili ya wakati wa upungufu wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara yangu kuhusu usalama wa chakula yameainishwa kwenye Sheria ya Usalama wa Chakula (*Food Security Act*) Na. 10 ya mwaka 1991 katika kifungu cha 8. Idara ya Maafa ya Ofisi ya Waziri Mkuu hununua chakula hicho na kukilipia gharama za usafirishaji hadi Makao Makuu ya Halmashauri zenye upungufu wa chakula. Majukumu ya Idara ya Maafa yameainishwa kwenye Sheria ya Maafa (*Disaster Relief Coordination Act*) Na. 9 ya mwaka 1990 katika kifungu cha 8. Halmashauri za Wilaya huchukua chakula kutoka Hifadhi ya Chakula ya Taifa na kukigawa kwa walengwa kwa kutumia Kamati za Maafa za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Wilaya na Halmashauri za Wilaya zinatakiwa kutoa taarifa sahihi kuhusu mwenendo wa bei na hali ya chakula katika maeneo yao. Ikithibitika dalili ya upungufu, tathmini ya kina hufanywa. Tathmini hiyo inahuisha wadai wote katika masuala ya chakula ikiwemo Wizara ya Kilimo na Ushirika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Maafa, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani na Shirika la Kilimo la Chakula la Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuwa na chakula cha aina tatu. Kwanza, chakula cha bei nafuu cha Shilingi 50 kwa kilo ya mahindi. Pili, chakula cha bure kwa wananchi wasio na uwezo wa kununua na tatu, chakula kinachouzwa kwa wafanyabiashara kiushindani.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano na la mwisho linahusu usindikaji wa mazao. Nchi yetu imebahatika kuwa na aina mbalimbali za matunda, viazi, mboga na viungo, lakini ni chini ya asilimia 10 ya mazao hayo ndiyo yanasisindikwa. Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya usindikaji kwa kuweka vivutio vya uwekezaji. Aidha, Wizara itakuwa na jukumu la kutoa takwimu za mazao yanayoweza kusindikwa yaliyoko kwenye maeneo mbalimbali ya nchi. Viwanda vitajengwa kwenye maeneo yanakolimwa mazao ili yasindikwe kwenye maeneo hayo kabla ya kusafirishwa. Kwa mfano, hivi sasa kiwanda cha kukamua machungwa kinajengwa Morogoro kutoakana na wingi wa matunda hasa machungwa katika Mkoa huo na Mikoa jirani kama vile Mkoa wa Tanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wizara vile vigeo itaendelea na utoaji wa mafunzo ya uendeshaji wa mashine ndogo za usindikaji wa mazao kwa mfano, mashine za kubangua korosho, kukamua mafuta na kusindika mihogo. Wastani wa bei za mazao makuu ya biashara katika soko la dunia zimekuwa zikiendelea kushuka tofauti na bei za baadhi ya mazao mapya yanayohitajika katika soko hilo hususan mazao ya viungo, matunda, maua na mimea ya kuzalisha dawa za kutibu magonjwa ya binadamu. Mazao hayo yanayostawi vizuri hapa nchini kwa mfano, mazao ya viungo kama vile *vanilla* na *paprika*, mazao ya mapambo kama vile maua ya waridi, mazao ya matunda kama maembe, ndizi mbivu na matunda yaitwayo *passion fruit* na mmea wa dawa mbadala kwa *quinine* katika kutibu ugonjwa wa malaria uitwao *Artemisia*.

Mheshimiwa Spika, Wizara inao mpango wa kuwapatia vipando bora na mafunzo wakulima wa mazao hayo. Mpango huo unatekelezwa kwa kushirikiana na sekta binafsi chini ya utaratibu wa *Public Private Partnership (PPP)*. Mbinu muhimu inayotumika kuendeleza mazao hayo ni pamoja na kilimo cha mkataba (*contract growing*) ambacho kinawahakikishia wakulima soko na mafunzo ya kanuni bora za uzalishaji pamoja na pembejeo.

Mheshimiwa Spika, eneo la sita linahusu ushirika na limechangiwa na Wabunge watatu. Serikali inatambua umuhimu wa vyama vya ushirika ikiwa ni pamoja na *SACCOS* katika kutoa fursa kwa vikundi vidogo vidogo vya wananchi kujiajiri na kuboresha hali yao ya kiuchumi kwa kuchangia kwenye pato la Taifa.

Serikali itatekeleza *program* kabambe ya mageuzi na *modernization* ya ushirika ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kuibua vyama vya ushirika imara zikiwemo *SACCOS* katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa kilimo, maendeleo ya kilimo yanategemea sana ushiriki wa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Wilaya na wataalam kuhimiza na kusimamia maendeleo katika Wilaya zao.

Baadhi ya sheria na kanuni zitarekebishwa ili kuweka mazingira mazuri na uwekezaji katika sekta ya kilimo na kufikia malengo ya kupunguza umaskini na kuwa na maisha bora yenye neema kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuwapa uhakika wa masoko wakulima wa mazao ya chakula, inatarajiwa kuanzishwa Bodi ya Chakula na Nafaka (*National Food and Grains Board*). Itatangaza mapema bei za mazao ya nafaka katika kanda maalum yanakofaa kulimwa, lakini wanunuzi wa soko huria wataruhusiwa kununua kwa bei zaidi ya ile iliyotangazwa kama soko linaruhusu kufanya hivyo. Yaani kuanzishwa kwa bodi hakutaleta ukiritimba.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia yatajitokeza katika bajeti ya mwaka ujao ya Wizara yangu. Tumefaidika sana na mawazo mengi mazuri tuliyoyapokea katika mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie dakika moja kumpongeza Mheshimiwa Rais na Bunge hili kwa ushindi katika uchaguzi uliopita. (*Makofi*)

Pili, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa wananchi wa Bunda kwa kunirudisha katika Bunge hili bila kipingwa baada ya kupata likizo ya miaka 10. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hotuba tunayojadili hapa ambayo ndiyo hoja ya Waziri Mkuu na ambayo mimi naiunga mkono, imetilia mkazo sana juu ya suala la upatikanaji wa maji mijini na vijijini. Kwa ajili ya kutaka kuilewa zaidi hotuba hii na umuhimu wa sekta ya maji, ningependa kunukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais katika ukurasa wa 42 ambapo alisema: “Tatizo la maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania mijini na vijijini, ndiyo kero nambari wani. Serikali ya awamu zote zimefanya jitihada kubwa kukabiliana na tatizo hilo. Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia kulikabili tatizo hili kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Serikali itaweka msukumo mpya katika kuwawezesha wananchi wengi zaidi mijini na vijijini kupata maji safi na salama.” Hayo ndiyo maneno ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, tunapojadili hoja hii, tunajadili juu ya namna gani tutatekeleza maelekezo ya Rais ambayo ndiyo agenda ya Serikali ya Awamu ya Nne kuhusu sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge 25 wametoa mawazo yao kuhusiana na sekta ya maji. Wengi wamezungumzia zaidi maji vijijini kwa sababu maji vijijini ndiyo tatizo kubwa tulilonalo mpaka sasa. Lakini wako wachache ambao wamezungumzia maji mijini hususan katika mji wa Dar es Salaam na vile vile wako ambao wamezungumzia juu ya hifadhi ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, majukumu pamoja na mikakati ya kuwapatia wananchi maji yanaweza kugawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni hifadhi ya vyanzo vya maji. Haiwezekani tujiridhishe kwamba tunaweza kuwapatia wananchi maji na yakawa endelevu bila kulinda hifadhi ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, tunao ushahidi juu ya uharibifu wa vyanzo vya maji na Waheshimiwa Wabunge waliochangia suala hili wamedhihirisha ukweli huu. Uchomaji moto, uchungaji wa mifugo katika maeneo ya vyanzo vya maji, ukulima karibu na vyanzo vya maji, malisho ya mifugo na ukataji ovyo wa miti, vyote vinachangia katika kuleta ukame katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, tunayo mifano katika milima ya Uluguru ambako moto inachomwa na hifadhi ya maji inaharibika. Tuna ushahidi wa ukataji miti katika mlima wa Kilimanjaro ambao unaharibu kabisa mazingira na kuhatarisha vyanzo vya maji. Tunao ushahidi wa kuharibika kwa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya Mto Ruaha ambapo ndiyo chanzo cha Bwawa la Mtera na ambapo kusema kweli vyote vinasababisha kuwepo kwa uharibifu wa vyanzo vya maji na hata kule ambako tuna maji ya uhakika kama Ziwa Victoria. Kuna uchafuzi mkubwa sana wa mazingira katika Ziwa Victoria. Maji machafu yanamwagwa katika Ziwa lile na viwanda hasa katika Mkoa wa Mwanza na Musoma ambavyo vinahatarisha usalama wa maji na usafi wa maji katika Ziwa hilo. Haya ni mambo ambayo yote kwa pamoja tunatakiwa kuyachukulia hatua ili kuboresha zaidi huduma ya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, mkakati ambao tunaufanya katika kushughulikia suala hili la uharibifu wa vyanzo vya maji ni wa aina mbili na ambao unashirikisha karibu kila mtu. Kwanza, ni lazima tuwaelimishe wananchi waelewe umuhimu wa kutunza vyanzo hivi vya maji kwa sababu vina uhusiano mkubwa sana na uhai wetu sisi wote. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote pamoja Serikali, Wakuu wa Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Taasisi zisizokuwa za Kiserikali, ni wito wangu wa kuomba tushirikiane katika kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji na usafi wa maji ili yaweze kutupa huduma katika siku zinazokuju.

Mheshimiwa Spika, wataalam wanaonyesha kwamba kadri watu wanavyoongezeka ndivyo huduma ya maji inavyopungua. Wanatwambia kwamba, ifikapo mwaka 2025 kama kasi ya uharibifu wa vyanzo vya maji itaendelea kama ilivyo, basi huduma ya maji na vyanzo vya maji vitapungua kwa asilimia 45 ambapo idadi ya watu inakadiriwa kufikia milioni 59.8. Kwa hiyo, ni vizuri tujihakikishie kwamba vyanzo vya maji vinatunzwa ili kukidhi idadi ya watu inavyoongezeka ili huduma hii ya maji isije ikafika mahali ikafanya nchi ikawa jangwa.

Mheshimiwa Spika, ziko nchi duniani ambazo hazina vyanzo vya maji kama vyetu, wanahangaika sana. Rafiki zetu wa Egypt wanategemea mto mmoja tu wa Nile na siku zote tunazungumza nao juu ya namna watakavyoendelea kupata maji kutoka mto ule. Kwa hiyo, sisi tuna vyanzo vingi, tukivihifadhi tutakuwa salama zaidi, tukiendelea na uharibifu tutaharibikiwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala hilo lilizungumziwa zaidi na Waheshimiwa Wabunge kama wanne. Nadhani majibu hayo yanatilia nguvu maelezo ambayo tayari wameyatoa.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine wa kuhifadhi vyanzo vya maji ni sheria. Hivi sasa Wizara yangu inatazama upya Sheria Na.42 ya mwaka 1954 kwa nia ya kuiboresha. Matumaini yangu ni kwamba tukiishakamilisha kazi hiyo tutaleta sheria hiyo katika Bunge lako Tukufu ili ifanyiwe marekebisho kwa nia ya kuweka nguvu zaidi juu ya hifadhi ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine inayohusiana na huduma ya maji ni huduma za maji vijijini. Takwimu tulizonazo zinaonyesha ya kwamba asilimia 54 ya watu wa vijijini ndiyo peke yao wanaopata maji. Lakini vilio vya maji ni vingi kwa kweli. Ushahidi wenyewe uko hapa hapa Bungeni. Tangu Bunge hili limeanza nimekwishashikwa shati na watu wengi tu, kila mtu anataka maji. Mimi nikauliza, hivi huko ambako sisi tunatoka ni wapi yapo na wapi ambapo hayapo? Huu ni ushahidi ya kwamba hili ni tatizo kubwa na labda ndiyo maana Mheshimiwa Rais alisema ndiyo tatizo namba moja katika nchi yetu. Kwa hiyo, tunafanya nini katika suala hili la kueneza maji vijijini?

Mheshimiwa Spika, kwanza, ipo miradi inaendelea huko vijijini ambayo Waheshimiwa Wabunge wakati wowote wanakaribishwa Wizarani ili tujadiliane na miradi inayohusiana na maeneo yao. Iko miradi ya kukarabati yaani huduma ilikuwepo, watu wameongezeka, sasa ile huduma imepoteza maana yake kwa hiyo inahitaji kurekebishwa ili watu wengi zaidi waendelee kupata maji. Lakini vile vile, tunayo *program* ya Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira. *Program* hii iko kila Wilaya na tumekwishapokea mapendekezo kutoka kila Wilaya ya miradi isiyopungua 10 ya kushughulikia suala la maji. Miradi hii itasimamiwa na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kuzishawishi Halmashauri za Wilaya ambazo ndizo zitakazosimamia mradi huu kuajiri Wahandisi amba wanaweza kuisimamia kazi hii. Tuna Wilaya kama 52 ambazo hazina Wahandisi wenyewe ujuzi. Ukikabidhi fedha kwa watu amba hawana uwezo wa kusimamia kazi, fedha hizi zitapotea na maji hayatakuwepo. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane na Halmashauri zetu tupate Wahandisi. Wizara yangu iko tayari kusaidiana na Halmashauri kuwapata Wahandisi amba watakwenda kufanya kazi katika Halmashauri za Wilaya ili kusimamia mpango huu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kusema kwamba, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu sisi kazi yetu ndiyo hii hasa ya kusimamia maendeleo na kwa sababu tatizo la maji ni kubwa na kwa kuwa wote tunapenda kurudi hapa mwaka 2010, basi tusimamie kwa ukamilifu sana kule chini ili kuhakikisha mahali palipo na mradi tuwe na uhakika unatekelezwa na watu wanapata maji. Sisi tuko tayari kuwasiliana na Wabunge wote wanaosimamia kazi hii kule ili tupate maelezo na sisi tuko tayari kutembea nchi nzima kukagua miradi hii ili kuhakikisha kwamba kweli wananchi wanapata maji kama ambavyo tumekusudia chini ya huu Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mbinu tutatakazozitumia itakuwa ni uchimbaji wa visima virefu. Tutatilia mkazo zaidi uchimbaji wa visima virefu kwa sababu visima vifupi vimetuletea mchezo wa kukauka. Ukitokea ukame vinakauka kwa wingi kabisa. Tumeshuhudia katika Mikoa ya Ziwa chini ya mpango wa *HESAWA* ambao ulitekelezwa kwa miaka mingi, sasa hivi visima vile vilivyokuwa vifupi vyote vimekauka na tumeanza upya. Kwa hiyo, tutatilia mkazo zaidi suala la visima virefu. Maji ya maziwa vile vile yatapewa nafasi.

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, mwisho, kama utanivumilia kwa dakika mbili nitazungumzia suala la maji katika mji wa Dar es Salaam. Maji ya Dar es Salaam ni tatizo kubwa. Dar es Salaam ndiyo mji wetu mkubwa kuliko yote na ndiyo mji ambao hauna maji. Tunategemea chanzo kimoja tu cha maji katika Mto Ruvu na kule Ruvu hatuna *reserve*, yaani ni kwamba tumeweza mashine zetu tunategemea hali ya mtiririko wa maji katika mto. Kwa hiyo, mazingira ya Dar es Salaam ni magumu, halafu miundombinu imechakaa. Kwa hiyo, tunachukua hatua gani katika kusaidia suala hili?

Mheshimiwa Spika, kwanza kuna mpango unaogharimiwa na Benki ya Dunia na *ADB* kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam, lakini vile vite tunaweka pampu mpya Ruvu Juu. Hatua za kuziagiza pampu hizo zimeanza kuchukuliwa na tunadhani zitaweza kufika hapa wakati wowote ili tuimarishe usukumaji wa maji kutoka Ruvu Juu ambayo inahudumia sehemu fulani ya jiji la Dar es Salaam. Huduma inayotoka Ruvu Chini bado ni nzuri na mitambo yake bado ni mizuri. Kwa hiyo, hizo ndiyo hatua tunazochukua. Lakini vile vite tunapendekeza kwamba, tujenge bwawa katika eneo la Ruvu ili tuhifadhi maji badala ya kuyaruhusu kwenda baharini yote. Tuyahifadhi ili inapotokea ukame tuwe tunaweza kutumia ile kama *reserve* na kwa hiyo tunaweza kuupa mji wa Dar es Salaam maji bila matatizo makubwa hata kama ukitokea ukame. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ya muda mrefu ambayo tunaififikiria ni uwezekano wa kutoa maji Mto Rufiji. Tumekwishaanza kufanyia kazi suala hilo. Tunatazama njia hiyo kama njia mbadala ya kuupatia mji wa Dar es Salaam maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuwapa wananchi maji ni kazi ngumu na kubwa. Lakini kwa kutumia bajeti ya kawaida pengine ni tatizo ambalo linaweza kuchukua muda mrefu. Kwa sababu hiyo, tunapendekeza kuanzishwa kwa Mfuko wa Maji wa Taifa (*National Water Fund*). Hili si wazo jipya, ni wazi ambalo lilikwishazungumzwa huko nyuma na liliwahi kufika Bungeni. Tunataka sasa tuanzishe mfuko ule ili utusaidie katika kufikisha huduma ya maji vijijini kwa kasi mpya, nguvu mpya na kwa ari mpya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia niungane naye Mheshimiwa Waziri Mkuu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri hapa Bungeni. Hotuba yenye upeo, dira na mwelekeo wa hatma ya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, nami napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kibaha kwa kunichagua kuwa Mbunge wao. Kwa kweli hili Jimbo jipya wamenichagua mara ya kwanza, lakini wananchi hawa hawa waliishanichagua mara tatu huko nyuma wakati lilipokuwa ni Jimbo la Kibaha nzima kama Wilaya. Niliwaahidi kuwatumikia kwa uadilifu na naamini nitafanya hivyo, niwatumikie kwa uadilifu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 28 wamechangia mambo yanayohusu Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza kabisa, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na wale waliosikiliza pia michango hii inayohusu Wizara ya Nishati na Madini. Napenda niwaahidi tu kwamba, yote waliyoyasema yana maana na yote waliyoyasema tutayafanya kazi kuhakikisha kwamba tunapeleka mbele gurudumu la maendeleo la nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hao wamechangia katika maeneo mawili. Kwanza, nishati na pili madini. Kama ambavyo Mheshimiwa Rais amewahi kusema katika hotuba yake, nishati ni sawa sawa na chembechembe za damu mwilini. Ni muhimu sana. Hatuwezi kuzungumzia maendeleo ya nchi yetu bila ya kuzungumzia nishati. Hatuwezi kuzungumzia kupambana na umaskini bila ya kuzungumzia nishati. Madini ni raslimali yetu na ni lazima tuitumie kuhakikisha kwamba nchi hii inanufaika ipasavyo na inaondokana na umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, katika Wabunge 28 ambao wametoa hoja, isingekuwa rahisi kuweza kumjibu kila Mheshimiwa Mbunge hoja kwa hoja. Lakini tunaahidi kwamba tutawajibu kwa maandishi hoja kwa hoja wote waliochangia. Isipokuwa hapa nitakachofanya ni kutoa maeneo machache kulingana na muda tuliopewa ili kuweza kutoa ufanuzi tu. Baadhi ya maeneo haya tayari tumeishayatolea kauli hapa Bungeni au tumeishayajibu kwa njia ya maswali. Lakini si vibaya basi kuyarejea kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo walichangia Waheshimiwa Wabunge karibuni 11 ilikuwa inahuwa upanuzi wa uzalishaji wa umeme ili kupata nishati ya uhakika. Napenda kusema kwamba, nakubaliana moja kwa moja na hoja hii ya Waheshimiwa Wabunge juu ya umuhimu wa kuwa na nishati ya uhakika na huwezi ukawa na nishati ya uhakika kama huna vyanzo vya uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa ikitegemea uzalishaji wa umeme kwa kutumia maji. Ni chanzo rahisi, ni chanzo endelevu na kikitunzwa kwa kweli inakuwa ni chanzo cha kuaminika. Tumepata matatizo hapa katikati kutokana na

ukame lakini kama ambavyo Waheshimiwa Mawaziri waliopita na hususan Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia mazingira na Mheshimiwa Waziri wa Maji hivi punde wakati alipokuwa anachangia hapa ni kwamba, vyanzo hivi vya maji vimeharibika kwa kiwango kikubwa kutokana na uharibifu wa mazingira. Kama ambavyo Waheshimiwa Mawaziri waliopita walivyosema, Serikali katika ujumla wake inashughulikia suala hili la utunzaji wa mazingira na sisi kama viongozi na ndugu wananchi sote tunapaswa kuungana na Serikali katika kuhakikisha kwamba tunatunza vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa ikizalisha umeme kwa zaidi ya asilimia 80 kwa kutegemea maji. Kwa kutambua kwamba hali hii ya ukame imetufikisha mahali tunakuwa na matatizo ya umeme, Serikali imechukua jitihada ya kuhakikisha tunaanzisha vyanzo vingine mbadala ambavyo vitaungana na hivi vyanzo vya maji katika kutupatia umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika miaka mitano iliyopita, Serikali imefanya jitihada kubwa ya kuanzisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia Gesi ya *Songosongo*. Pia ipo Gesi ya *Mnazi Bay* ambayo inashughulikiwa hivi sasa kwa kujaribu kuzalisha umeme kwa kupitia gesi. Lakini je, Serikali imechukua hatua ya kuanzisha miradi ambayo itatufikisha mahali ambapo uzalishaji wa umeme utakuwa ni wa uhakika kwa kuwa na vyanzo mchanganyiko au *mixed generation regime* ya umeme ambayo inatokana na maji, makaa ya mawe na gesi.

Mheshimiwa Spika, asubuhi hii wakati natoa taarifa juu ya hali ya uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini nilitoa mifano ya kazi ambayo Serikali imenuia kuifanya kwa dhati kabisa na kazi hiyo inafanyika kwa haraka hivi sasa kuhakikisha kwamba tunachukua hatua za muda mfupi na hatua za muda wa kati na muda mrefu ili mpango wetu wa kuzalisha umeme uwe na vyanzo vingi, tunapata umeme wa uhakika kwa matumizi ya ndani lakini pia pale tutakapopata akiba na tunaamini tukivitekeleza vyote hivi tutapata akiba basi tuwe katika nafasi nzuri ya kufanya biashara na nchi zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, huo ndio mtazamo ambao tunakwenda nao, lakini napenda niongeze tu kwamba hapo nyuma mara nyingi katika uwekezaji katika suala la nishati tulikuwa tunategemea sana wawekezaji kutoka nje au Serikali marafiki, taasisi za Kimataifa au watu binafsi kutoka nje. Kwa kiasi fulani tumenufaika na hili lakini kutokana na hali jinsi ilivyo hivi sasa Serikali imeona pia ni vizuri tukashawishi vyanzo vya ndani ambavyo vinaweza vikachangia katika uwekezaji, uzalishaji na usafirishaji wa umeme. Nafurahi kusema kwamba baadhi ya taasisi zetu muhimu za hapa ndani zimeweza kujitokeza na kuweza kuona kwamba kuna umuhimu katika kuchangia uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo limezungumzwa sana pamoja na suala la uzalishaji kwa sababu umeme una sehemu tatu uzalishaji, usafirishaji na usambazaji. Suala la usambazaji umeme hasa suala zima la kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya zilizobaki kama 15 hivi na kwenye vijiji vyetu mbalimbali kama nilivyosema mwanzo bila ya kuwa na umeme wa uhakika hata mipango ya Serikali ya kupiga vita

umaskini haitakuwa madhubuti sana pale ambapo inabidi nishati hii itumike kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 - 2010, Serikali inaendelea kusisitiza au kutoa kipaumbele katika kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya zote. Wilaya hizi 15 kwa sasa zinaonekana nydingi kwa sababu hapa katikati Mheshimiwa Rais aliunda Wilaya mpya lakini kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 1995 na 2000 kazi kubwa ilifanyika hapa katikati kiasi ambacho wakati fulani zilibaki kama Wilaya nane tu ambazo zilikuwa hazina mpango wowote ule wa kufikisha umeme katika kipindi cha hivi karibuni. Lakini hizi zimeongezeka idadi yake kutokana na Wilaya nydingine kuweza kuundwa. Pamoja na hayo, napenda nichukue nafasi niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba azma ya Serikali ya kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya iko pale pale na tunaifanya kazi kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, zipo baadhi ya Wilaya sasa hivi ambazo kazi hii inafanyika kule Serengeti, Ukerewe na Urambo lakini pia kuna Wilaya ambazo hivi karibuni kazi hii pia itafanyika kwa mfano Wilaya ya Simanjiro ambayo tunategemea ufadhili kutoka Serikali ya Sweden. Wafadhili kutoka Serikali ya Sweden wataanza kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Lakini pia ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba Mikoa hii ambayo haijaunganishwa na gridi ya Taifa na hasa Kigoma na Ruvuma kazi ya kufikisha umeme kwenye maeneo haya inafanyika. Tunaposema gridi ya Taifa ni pamoja na Mikoa ya Mtwara na Lindi lakini nilisema pale mwanzo kwamba huku Mtwara na Lindi kuna mradi wa umeme ambao tunataka tuutazame vizuri zaidi ili nao uwe ni umeme ambao unaweza kuwa manufaa kwa eneo lile lakini pia kwa nchi nzima. Ningependa niseme tu kwamba tunafanya kazi kuhakikisha kwamba umeme unafikishwa kwenye maeneo haya muhimu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu kubwa inayohusu umeme inahu Menejimenti ya *TANESCO* ya *Netgroup*. Jana nilitoa taarifa wakati najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge mmoja juu ya Menejimenti ya *Netgroup* nilisema kwa ufupi na ninapenda nirejee maelezo yale. Ni kweli sasa hivi yapo matatizo ya uendeshaji wa Shirika la *TANESCO*. Serikali inatambua na Serikali inashughulikia tatizo hili. Pale mwanzo kampuni hii walipoingia walionyesha dalili za kufanya vizuri kwenye upande wa ukusanyaji mapato kwa mfano walilikuta Shirika likikusanya shilingi bilioni 11 kwa mwezi, sasa hivi wanakusanya shilingi bilioni 22, lakini hicho hakiwezi kuwa ni kigezo pekee.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba kwa maeneo mengine ambayo yametajwa kwenye upande wa madini, yamezungumziwa masuala ya mikataba ya madini, suala la madini katika ujumla wake, nililisema hata asubuhi wakati najibu swali la nyongeza kwamba ni suala ambalo limeamsha mjadala mzuri tu Kitaifa mpaka kupelekeea Serikali kuunda kamati iliyongozwa na Dr. Jonas Kipokola. Taarifa hiyo tunayo, tunaifanya kazi na kama nilivyosema asubuhi mimi nadhani suala hili tungesubiri mpaka wakati Serikali itakapoanza kuchukua hatua juu ya mapendekezo ya mambo ambayo yametajwa katika taarifa ile.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu Wizara yangu, linahusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira na jinsi gani utunzaji wa mazingira unahusiana kwa karibu kabisa na suala zima la nishati. Kama nilivyosema awali naungana na Waheshimiwa Mawaziri waliopita katika kusema kwamba Serikali inatarajia kuchukua hatua na hatua nyingine amezitaja Waziri Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya juu ya suala hili na hata mwezi uliopita tulipokwenda Mtera kutizama hali ya Bwawa la Mtera na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia mazingira Mheshimiwa Waziri wa Maji na mimi pia suala hili la utunzaji wa mazingira lilijitokeza waziwazi kwamba bila ya kulishughulikia hili suala la ukosefu wa maji ya kutosha katika Bwawa la Mtera na kwa kweli siyo Mtera tu na katika mabwawa mengine pia itakuwa suala linalojirejea au linalorudia mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo ni wazi kwamba sasa Serikali imedhamiria kuchukua hatua kwenye sehemu hii.

Lakini pamoja na hayo Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumzia masuala ya nishati mbadala na mimi nakubaliana nao na kama nilivyosema ni kwamba hili ni eneo ambalo tunapaswa kushirikiana sote. Kuna vyanzo vingi vya nishati mbadala. Watani zangu wale Wasukuma wanaelewa na kuhusu suala la *tariffs* au bei ya umeme niliwhi kusema hapa Bungeni kwamba ni jambo ambalo lina mambo mengi kwa hiyo inabidi lishughulikiwe katika ukamilifu wake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati naanza hizi hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge tutawajibu kwa maandishi mmoja mmoja na kama nilivyosema awali pia nawashukuru sana kwa hoja hizi nzito, nzuri. Napenda kurejea kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninawashukuruni sana kwa kunisikiliza. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, la pili tunakusudia kuzungumza na Waandishi wa Habari, Wahariri na wamiliki wa vyombo ili tujenge uhusiano mzuri kati ya Waandishi, Wabunge na Bunge kwa sababu sote tunafanya kazi moja ya kuwahudumia Watanzania. Kwa hiyo, ninapenda kusema kwamba kwa hili tutajitahidi ili msuguano huo uliotokea usitokee tena ili tuwe sote wamoja, sote za wazalendo tujenge nchi yetu kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kwamba tumezungumza kuhusu Kiswahili na sisi tunaahidi kwamba Wizara yetu inajiandaa kutumia Kiswahili kama sehemu ya ajira kwa Watanzania. Tunahitaji Walimu wengi katika nchi za Afrika Mashariki na Kati, tunahitaji Waandishi wa Habari, Watangazaji wa *radio*, Wakalimani nakadhalika. Kwa hiyo, tunaahidi kwamba tutalivalia njuga jambo hili ili Kiswahili ili litoe ajira kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, la nne tumezungumza kwamba tunaffikiri viwango vyetu vya michezo vimeshuka sana nchini na tunaahidi tutajitahidi kuweka mikakati ili viwango vyetu vya michezo viwe vya juu na tushinde katika mashindano mengi ya Kimataifa na Kitaifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho tunaahidi tutajitahidi kuomba Serikali yetu tuwe na ukumbi wa kisasa wa sanaa na michezo. Wakati mwagine tunaona aibu tunakwenda pale kwenye ukumbi ule wa *Diamond* ni mafeni chungu mzima kama vile nchi hii haina uwezo wa kujenga. Tumeweza kujenga kiwanja kikubwa cha Kimataifa cha mpira kwa nini tushindwe kujenga ukumbi mzuri wa kisasa ambao utajenga hadhi ya nchi yetu. Tutaomba Serikali isaidie ili tuwe na ukumbi kama huo ili kujenga hadhi ya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia kuhusu hali ya Pemba na kutoendelea. Nimejaribu kupata takwimu hapa na mifano halisi kuonyesha kwamba kiasi kikubwa sawa na Serikali ya Zanzibar imesaidia sana maendeleo ya kule Pemba. Kuna maeneo matatu, eneo la kwanza ni la barabara na nina takwimu hapa kwamba barabara sita zimejengwa kule Pemba ya Mkoani Chakechake, Chakechake Wesha, Kilindi Micheweni, Chanjani Uwanja wa Ndege, Mtahaliwa Chokocho, Macho Manne Vitongoji na jumla ya shilingi bilioni 9.1 zimetolewa kwa ajili ya barabara za Pemba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia Vituo vya Afya, Serikali imefanya matengenezo Vituo vya Afya vitano navyo ni Tandauwa, Ndagoni, Wingwi, Makangale na Bogoa. Jumla ya shilingi milioni 398,150 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya ukarabati Vituo vya Afya.

Pia kuna barabara ambazo zimejengwa kipindi hiki cha 2006 nazo ni sita Mtambile Kangani, Mtambile Kengeja, Kenya Chambani, Itandawo Pujini, Mzingani wa Mbaa, Mgagadu Kiwani jumla ya milioni 8 za U\$ zitatolewa kwa ajili ya barabara hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna matanki ya maji ambao yamejengwa kule Pemba na Serikali ya Zanzibar nayo ni Mtemani mawili, Chakechake mawili, Bahamasa moja, Mtambile moja, Pujini moja, Gandwe moja imegharimu shilingi milioni 321 kwa ajili ya Pemba. Kwa hiyo nafikiri si kweli kwamba Serikali haishughulikii. Hofu yangu ni kwamba matanki haya wasije wakatia vinyesi watu wa kule Pemba. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nizungumzie lingine la mpasuko ambalo limezungumzwa hapa. Nafikiri mpasuko huu uliozungumzwa hapa kweli upo lakini tuangalie chimbuko lake limeanza lini na kwa nini ikatokea? Sababu zake ni kwamba mpasuko huu kwa kweli ni masuala ya kitabaka ya mvutano wa matabaka mawili ya wanyonge, maskini ya Mungu na wale wanaotaka kutawala wenzao. Mwaka 1957 wakati Chama cha *ASP* kinaundwa ndio mwanzo wa msuguano huo. Baadaye kikaundwa Chama cha Zanzibar *National Party* na Chama za *ZPP*. Kwa hiyo nasema mvutano huu kati ya CCM na *CUF* kule Unguja haukuanza leo ndugu zangu Wabunge hasa wale wapya, siyo wa leo huu ni wa zamani. Ni mpambano wa kihistoria ya kupambana katika masuala ya kitabaka na kila mmoja anataka ashike Serikali kwa ajili ya maslahi yake. Sasa kwa nini mnafikiri kule Pemba wanachama wengi wa *CUF* bado hawapendi CCM sababu pia ni ya kihistoria.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa mwaka 1961 kule Pemba Chama cha *ASP* kilipata viti viwili, Chama cha *ZNP* na *ZPP* viti saba. Mwaka 1961 Juni uchaguzi mwingine *ASP* viti viwili, *ZNP* na *ZPP* viti nane. Mwaka 1963 *ASP* viti viwili, *ZNP* sita. Kwa hivyo jumla ya wapinzani vilikuwa viti 12 na *ASP* viti viwili. Kwa hiyo sasa hivi ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge msidanganyike mambo haya hayakuanza leo yameanza zamani haya na mpambano wa kitabaka ya makundi mawili kundi la Waafrika, wanyonge maskini ya Mungu na wale ambao wanataka kuonyesha utawala wa Kisultani na Umwinyi kule Zanzibar. Ndio maana mwaka 1963 Serikali ile ya Mseto ya *ZPP* na *ZNP* ikatimuliwa na Chama cha *Afro-shiraz Party*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe mfano kwa nini tunafarakana matabaka mawili? Yako mambo ya msingi matatu. La kwanza wako watu kule Zanzibar wana haki yao, wanaona Chama cha *ASP* ni Chama cha watwana na wajakazi, hiyo ndio asili yake na sasa hivi CCM imerithi *ASP* au siyo jamani? CCM imerithi *ASP* na *TANU* kwa hiyo watu wapo bado wana-CCM ni *ASP* wale wale tu waliochukua Serikali na kumpindua mfalme, hii ni sababu ya kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili na tofauti ya pili ni mapinduzi Zanzibar. Chama cha *CUF* kinaamini mapinduzi kule Zanzibar ni udhalimu na si halali, wana-*ASP* na CCM wanaona kwamba mapinduzi yale ni ya halali yalikuwa lazima yatokee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sababu ya tatu Muungano wa Tanzania. Sisi wana-CCM tunaamini kwamba Muungano ulikuwa halali na ulikuwa muhimu kwa ajili ya Umoja wa Afrika wa Tanzania lakini wenzetu Muungano ule hawautaki. Kwa hiyo nataka tuzungumze kwamba mambo matatu makubwa haya ndio sababu ya mvutano siyo u-Pemba, siyo u-Unguja, siyo Uarabu wanatumia haya kwa ajili ya kujenga imani watu

muone hivyo. Mfano mwingine, kule Zanzibar kulikuwa na Bwana mmoja alikuwa akiitwa Ally Mussin Baruani, picha yake hii.

(*Hapa kielelezo husika kilionyeshwa Bungeni*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Huyu ndio kiongozi wa *Hezul Wasal*, mpe Waziri Mkuu hamjui. (*Makofi/Kicheko*)

(*Hapa kielelezo husika pia kilionyeshwa Bungeni*)

WAZIRI WA HABARI, UTADUNI NA MICHEZO: Huyu alikuwa kiongozi wa Chama cha *Hisbul* kule Zanzibar na sisi ndio tunaohusisha *CUF* na *Hisbul* kwa sababu ya huyu Bwana mambo yao yanafanana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano ukurasa wa 241 ukifungua Waziri Mkuu hapo, Ally Mussin anasema hivi, Januari 12 ni siku nyeusi kwa wa-Zanzibar anasema yule bwana, ukurasa wa 241 utaona hapo ni siku nyeusi kwa wa-Zanzibar yeze anaona hivyo, sisi kwetu ni mkombozi kwake ni nyeusi. Kwa hiyo je, angalia mawazo ya huyu bwana na mawazo ya *CUF* hayafanani kuhusu Mapinduzi ya Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, vile vile hawatambui kuhusu *ASP*. Huyu bwana ukurasa wa 33 anasema hivi, kitendo hiki kiovu cha kuunda *ASP* kimetokea katika mwaka 1957 ni maafa makuu katika tarehe ya nchi yetu. Miongoni mwa matunda ya kitendo hiki ni maafa ya kuangamiza nchi yetu, anasema huyu bwana kuhusu *ASP* kwamba ni maafa kwake yeze sisi ni ukombozi.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 33 soma Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu muungano huyu bwana anasema na hii *ASP* baada ya mvamizi wa nchi yetu Zanzibar katika Aprili 34 kwa yale makubaliano ya Nyerere na Karume kwamba Karume kaiiza Zanzibar kwa Nyerere, anasema huyu bwana na mawazo hayo hayo ndio mawazo ya *CUF* kuhusu muungano, hawautaki.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo ndugu zangu nasema tusibabaike kwamba matatizo yetu si ya Uarabu, si ya u-Pemba masuala ya kitabaka na kiitikadi na kimwelekeo. Sisi tunathamini Waafrika walio wengi, tunathamini mapenzi yetu, tunathamini muungano na tunaona kwamba kuwepo kwa mfalme ilikuwa maumivu kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitabu hiki cha mwingine huyu bwana Prof. Haroub Othman huyu CCM anasemaje kuhusu *CUF* msimamo wake, ukurasa wa 184 kitabu cha taarifa kamili kutoka kwa wafuatilaji wa uchaguzi anasema hivi, *CUF* katika kampeni zake ilidhihirisha mambo matatu. Kwanza ilikuwa inatilia mashaka uhalali wa mapinduzi Zanzibar tarehe 10 Januari, 1964. Pili litangaza au itairejesha au kuwalipa fidia wale ambaao mali zao pamoja na ardhi zinataifishwa kutoka mapinduzi hayo. Tatu *CUF* ilisema kwamba itawasiadia wale wote ambaao wanataka kufungua mashtaka mahakamani dhidi ya watu wanaohusika na mauaji au mateso ya ndugu zao, wazee wa umri na kadhalika

wakati wa awamu ya kwanza ya Karume. Kitabu hiki ameandika Haroub Othman wa Chuo Kikuu , *Professor* simfichi mimi anazungumza mawazo ya *CUF*.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba sisi CCM hatuwachukii Waarabu, *ASP* haichukii Waarabu kwa sababu katika Serikali ya Mapinduzi Katibu Mkuu wa kwanza Baraza la Mapinduzi alikuwa Salum Rashid, Mwarabu mweupe, singa mpaka hapa chini. Kulikuwa na Ally Sultani nywele ndefu mweupe. Kulikuwa na Babu wote hawa ni Waarabu wakati wa mapinduzi ya mwanzo. Kwa hiyo hatuwachukui Waarabu sisi wale rafiki wa Pemba lakini la msingi tunatofautiana katika muelekeo, mtizamo.

Sasa ndugu zangu ombi langu Wabunge wa Muungano hasa wale wapya msidanganyike na lugha za ulaghai za *CUF* hatuwachukii Waarabu wala wa-Pemba hapa kuna mvutano wa wazi wazi wa msuguano kati ya matabaka mawili ambayo nafikiri ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba Serikali ya *SMZ* ni Serikali ya CCM, mueewe hivyo. *SMZ* ni ya CCM kwa hivyo itapotukanwa na kunyanyaswa nyinyi mnanyanyaswa na Serikali yenu watu wa Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo CCM pia imerithi mambo yote mazuri ya *ASP* na *TANU*, CCM hii ina wajibu mkubwa wa kutetea mapinduzi ya Zanzibar, muungano wa Zanzibar kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa na mimi ni mara ya kwanza kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu, naomba na nichukue nafasi hii fupi sana kumshukuru kwanza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunipa nafasi hii ya Uwaziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kabisa kwa kuchaguliwa kwa kishindo akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika na Naibu Spika hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia sitawatendea haki wanawake wenzangu kwa kupitia Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wao ndio walioniwezesha kufika hapa, nawashukuru sana. Lakini pia ninawashukuru wafanyakazi wenzangu na Walimu kwa ujumla wao ndio wameniwezesha kuwa hapa Bungeni, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge wapatao 50 wamechangia hoja hii katika eneo la elimu na mafunzo ya ufundi. Hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge zinagusa hasa maeneo makuu manane yakiwemo upungufu mkubwa wa madarasa, nyumba za Walimu,

maabara, maktaba, hosteli hasa za wasichana na samani, upungufu mkubwa wa Walimu mashulenii hasa katika ngazi za sekondari, upungufu mkubwa wa vifaa vya kujifunza, kufundishia vikiwemo vitabu, kuboreshwa kwa mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa MMES, kutazama upya mtaala hasa wa elimu ya sekondari iliyorekebishwa kwa lengo la kurejesha masomo yaliyoondolewa, kuboreshwa kwa miundombinu katika shule zenyenye wanafunzi wenye ulemavu ili ikidhi mahitaji ya wanafunzi hao, pia huduma ya chakula katika shule za bweni na masuala ya mtambuko ambayo ni elimu kwa wasichana na kujenga Utaifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea ushauri wote uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Napenda kutoa ufanuzi wa jumla kwa maeneo yaliyochangiwa kama ifuatavyo. MMEM na MMES ni mipango inayotekelawa kwa ubia baina ya Serikali na Halmashauri, wananchi pamoja na wahisani. Ili kusaidia juhudzi za wananchi, Serikali hutoa Ruzuku ya Maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, nyumba za Walimu, maabara, maktaba, hosteli kwa wasichana na samani. Hata hivyo fedha hizi ni kidogo zikilinganishwa na mahitaji makubwa yaliyopo. Pia uzoefu huonyesha kwamba fedha za wahisani hutolewa kwa kuchelewa na wakati mwingine hupatikana pungufu kuliko matarajio. Kutokana na hali hii ni vema Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla tukaelewa kwamba sehemu kubwa ya mafanikio ya mahitaji haya yatategemea moyo wa kujitolea na hasa kwa ushiriki mkubwa wa wananchi na Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, ukichukulia kwa mfano mwaka huu tuna uhaba mkubwa sana wa madarasa kutokana na kundi kubwa la vijana wetu ambao wamefaulu mtihani wa darasa la saba, wanasubiri kuingia kidato cha kwanza. Tungependa kutoa ushauri ufuatao. Ili kukabili uhaba huu mkubwa uliojitokeza Halmashauri kwa kushirikiana na sisi wote Wabunge na wananchi kwa ujumla tuangalie vifungu vilivyopo katika Halmashauri ambavyo vinawenza kutusaidia kwa hatua ya dharura. Kwa mfano kuna fungu la fedha linalojulikana kama *Development Capital Grant* lakini pia kuna fungu lingine ambalo ni *General Purpose Grant* na wakati huo tunaweza kuangalia katika Halmashauri mafungu mengine ambayo yako kwa ajili ya miradi mbalimbali ambayo tunaweza kutumia wakati huo wa dharura lakini kwa tahadhari kwamba tusiathiri miradi ili yopo. Lakini naamini kabisa Halmashauri kama walivyofanya Halmashauri za Dar es Salaam tulipokutana nao waliahidi kwamba wanaweza kutumia fedha hizo ambazo vifungu vyake nimevitaja ili kukabili huu uhaba mkubwa uliojitokeza hasa wa madarasa na vifaa vingine vya kujifunza na kufundishia.

Mheshimiwa Spika, ipo mikakati ya muda mfupi ambayo inaweza pia kusaidia kukabili shida ya uhaba wa madarasa kwa mfano kutumia *double session* ambayo inaweza kufundisha wanafunzi wengi kwa kutumia madarasa machache yaani wengine wanakuja asubuhi na wengine wanakuja mchana hasa katika maeneo ya mjini ambayo tunaamini yana idadi ya Walimu ya kutosha. Wakati huu utatuwezesha kutumia vyumba madarasa kwa ajili ya vya *double session* ili kukabili uhaba wa vyumba vya madarasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la upungufu wa Walimu, Wizara inalitambua tatizo hili na kwa sababu hiyo imekuwa ikitekeleza kwa mafanikio utoaji mafunzo ya Walimu Tarajali kwa ngazi zote za msingi na sekondari. Lakini kutokana na kasi ya

ongezeko ya shule za sekondari ni wazi kuwa Walimu wanaoandaliwa wa vyuo vilivyopo hawakidhi mahitaji. Hivyo Serikali inafikira kuchukua hatua za muda mfupi ili kukabili tatizo hilo kama ifuatavyo.

Kwanza kujaribu kutambua Walimu wengi ambaao walishapata mafunzo lakini wapo tu hawafanyi kazi yoyote kutokana na urasimu uliopo katika utaratibu walioutumia wa kusaili, utaratibu wa kusaili umesababisha urasimu mwingi na hivyo tumepoteza Walimu wengi sana.

Kwa hiyo, tutajaribu kutambua Walimu waliopo ambaao wameshapata mafunzo lakini hawajaajiriwa mpaka sasa na pia kuendelea kuwapanga wahitimu wa ngazi ya Stashahada na Shahada moja kwa moja bila usaili. Tunategemea mwezi Mei mwaka huu kupata wahitimu 3,500 wa Stashahada ambaao tutawapeleka moja kwa moja kwenye shule za sekondari bila usaili. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Spika, usaili wa Walimu hautakuwepo tena. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo kuwatumia wahitimu wa Vyuo Vikuu ambaao hawakusomea Ualimu bali hupewa leseni ya kufundisha. Pia kuendelea kuwatumia wahitimu wa Kidato cha Sita waliofaulu si chini ya kiwango cha Daraja la Tatu na kuwapatia mafunzo ya muda mfupi kama vile wiki nne. Pia kutumia Walimu wenye Stashahada wanaofundisha katika shule za msingi hasa kwenye maeneo ambayo hayana uhaba mkubwa wa Walimu. Serikali pia itaangalia uwezekano wa kuwatumia Walimu wastaafu ambaao bado wana uwezo wa kufundisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, ninawashauri Waheshimiwa Wabunge, Halmashauri na viongozi wa tarafa, kata na wakuu wa shule na wananchi kwa ujumla, washirikiane kuwapatia mapokezi mazuri Walimu wapya na pia ujenzi wa madarasa uende sambamba na ujenzi wa nyumba za Walimu. Hili tunalisemea wazi tu kwamba kuna shule nyingi ambazo zimeshajengwa lakini Walimu hawakai kule kwa sababu wanakosa nyumba hasa maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, ingekuwa ni vizuri sana tunapojenga madarasa mapya yaende sambamba na ujenzi wa nyumba ili Walimu wapate mahali pa kuishi palipo salama, nadhifu na karibu na shule wanazofundisha.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Walimu kubaki katika ajira hasa kwenye maeneo yenye mazingira magumu Serikali inaangalia uwezekano wa kutoa posho maalum kwa Walimu wanaofundisha katika maeneo hayo. Wakati huo huo, Serikali inaangalia namna ya kuondoa urasimu katika ajira ya Ualimu kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia fedha za Ruzuku na za Uendeshaji, Wakuu wa Shule na Bodi za Shule wahakikishe wanununa vifaa muhimu wanavyovihitaji kwa ajili ya kufundishia vikiwemo vifaa vya maabara na vitabu vya kiada, ziada na rejea pamoja na miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya shule za sekondari za Serikali, Wizara inaangalia maeneo ya madaraka yanayoweza kupelekwa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ili kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shule hizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabadiliko ya mitaala hasa mtaala wa shule za sekondari na hasa kwa upande wa michepoo na masomo yaliyounganishwa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu imeyasikia maoni yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, wadau wengine wa elimu na wananchi kwa ujumla. Suala hili linafanyiwa kazi kwa makini hasa baada ya mafunzo ya ufundu kurejeshwa kwenye Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, elimu maalum ni moja ya vipaumbele vya MMEM na MMES. Wizara inaendelea kuongeza nafasi za wanafunzi wenyewe ulemavu na kutoa Ruzuku ya Maendeleo na ya Uendeshaji ili kuboresha miundombinu na kuimarisha uendeshaji wa shule.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa chakula hasa kipindi hiki cha njaa, huduma ya chakula kwa wanafunzi wa bweni, Wizara yangu imewasiliana na ofisi ya Waziri Mkuu ili shule za Serikali za bweni ziuziwe chakula cha bei nafuu kutoka maghala ya hifadhi ya Taifa ya chakula. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, yapo pia masuala ya mtambuko ambayo yamejadiliwa na Waheshimiwa Wabunge mojawapo ikiwa ni elimu kwa wasichana. Serikali inatambua umuhimu wa elimu kwa wasichana na kwa msingi huo kwa kushirikiana na wadau wengine wa elimu inategemea kujenga hosteli na kuongeza nafasi katika hosteli zilizopo ili wanafunzi wa kike wasome kwa ufanisi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kujenga Taifa ambalo Wabunge pia wamelijadili sana, suala hili Serikali inategemea kuongeza shule zaidi za bweni na kuongeza nafasi katika shule zilizopo ili zichukue wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wapatao 50 waliochangia nikiamini kwamba watapatiwa nafasi maalum ya kutambuliwa hususani wajulikane na wapiga kura kwamba walichangia masuala haya muhimu na imekuwa kwangu vigumu kuwataja lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuzidi kushirikiana kuwashamasisha wananchi ili kukamilisha kazi ya kuimarisha utoaji wa elimu iliyo bora kwa ngazi zote tukiamini kwamba shule hizi ni kwa manufaa ya watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Wizara hii ni mpya na kwa njia nafuu sana ya kuelewa hili jambo bila kupata ugonjwa wa kichwa, ni kufikiria tu Mwandsosya + Magufuli = Mramba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hiyo ni njia rahisi sana ya kuelewa Wizara hii na niseme nimebahatika kwamba nimekuta wenzangu wameniandalia mambo, kuna mpango wa maendeleo ya miaka kumi, kuna wataalam waliobobe, kuna miradi mingi inayotekelizwa, kuna matatizo mengi yaliyobaki ambayo ndio hasa kazi ninayoshughulikia na mapya ambayo nitabuni. Mambo yote haya nitaeleza kwenye mwezi wa saba wakati wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba kwa kweli kazi iliyombele yetu ni kubwa kwa sababu kikwazo kikubwa katika maendeleo ya uchumi wetu sasa ni miundombinu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mambo ya *macro-economic parameters* na nini na nini yameshawekwa vizuri lakini miundombinu ni kikwazo kikubwa na hasa kama tukijumlisha umeme na maji kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, napenda tu niseme kwamba hayo nimeyatambua na tunayawekea mpango, tuna mpango wa miaka kumi wa kuendeleza miundombinu wa dola 5.8bil. Kwa kutekeleza mpango huo tuweze kuondoa vikwazo vilivyopo katika kukuza uchumi na tuweze kuboresha maisha ya wananchi na hasa tuweze kufanikisha utekelezaji wa MKUKUTA (Mpango wa Kuondoa Umaskini na Kuinua Uchumi).

Mheshimiwa Spika, mipango hiyo itakuwa katika maeneo gani? Kwanza, barabara za Mikoani na Taifa. Hivi sasa Rais ametuongeza tuangalie uwezekano wa kujihusisha zaidi kwenye barabara za Wilaya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili, lazima tuwekeze zaidi kwenye barabara za Wilaya, Miji na barabara zinazounganisha barabara kuu na barabara za vijijini (*feeder roads*). (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lazima tuwekeze zaidi kwenye bandari zetu na lazima tuwekeze zaidi kwenye bandari za kwenye maziwa kwa mfano Kasanga liliulizwa swali hapa juzi, Kigoma, bandari za Ziwa Victoria na kadhalika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwekeze zaidi kwenye maeneo ya usafiri wa anga na hususani Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania* na kuzingatia usalama wa anga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwekeze zaidi kwenye reli zetu tuangalie uwezekano wa kupanua reli ya kat, kuboresha utendaji na ufanisi katika *TAZARA*, uwezekano wa kujenga reli ya kuunganisha Tanga – Arusha na Musoma, uwezekano wa kujenga reli ya kuunganisha Mchuchuma na Bandari ya Mtwara ambayo iko kwenye Ilani ya Uchaguzi na wakati huo huo kuboresha hali iliyopo sasa hivi ya reli zetu. Ni lazima nikiri kwamba hairidhishi kwa sababu tu kwamba huko nyumba hatukuwekeza kwa wingi katika eneo hili la reli. Ni lazima tuwekeze zaidi vile vile kwenye maeneo ya kuendeleza utumishi na vile vile tuangalie uwezekano wa kutumia teknolojia mpya katika maeneo haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, *last but not least*, uwezekano wa kuwekeza kwenye eneo la mawasiliano (*ICT*) mambo yanayohusiana na *TTCL* na simu za mkononi na kadhalika. Maeneo hayo ambayo maandalizi yake yamekamilika ndio tunayowekaweka umuhimu wa na mwisho tutaleta hapa wakati wa bajeti ili tuweze kutekeleza.

Kwa hiyo, kwenye barabara naweza kusema tu liko jipya kwamba Mheshimiwa Rais juzi alipokuwa anahutubia mukutano hapa Dodoma alisema kwamba kuna baadhi ya maeneo ambapo aliahidi barabara na madaraja. Nawaomba Wakuu wa Mikoa wanilet ee orodha za ahadi hizo za Rais za madaraja na barabara ili niweze kuziwekea mkakati kati ya sasa na miaka mitano ijayo. Pia na wenyewe huko kupitia Kamati za Barabara za Mikoa waweze kuziwekea umuhimu, hizi za umuhimu wa kwanza, wa pili, umuhimu wa tatu, ili na mimi niweze kuzingatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye madaraja, nimesikia sana maswali hapa kuna wasiwasiliano kwamba gharama za madaraja haya ni kubwa kuziachia Serikali za Vijiji au Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, hiyo ni *point* nimeshaichukua hapa katika kuangalia eneo la madaraja, nitaangalia uwezekano wa Serikali Kuu kujihusisha zaidi katika utengenezaji wa madaraja ya Wilaya na Vijiji pale ambapo kweli hawana uwezo kwa sababu barabara bila daraja sio barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na reli niongezee kwa kusema kwamba sasa hivi imeamuliwa katika Serikali kwamba reli yetu ya kati tutakodisha hatutai-*privatize* kwa maana ya kuiuza. Kwa kweli kwenye eneo lote hili la miundombinu hatutauza moja kwa moja kama tulivyouza viwanda. Kwenye eneo hili tutakodisha, uamuzi wa kukodisha umeshafanywa, tunafanya tu maandalizi ya mwisho ya kuamua ni nani na mimi nafikiri kabla ya mwisho wa mwezi tutakuwa tumetangaza ni nani atakayekodishwa hiyo reli ili aweze kuiendesha hasa kwa kuongeza idadi ya mabehewa na kutengeneza maeneo katika reli ambayo ni mabaya.

Mheshimiwa Spika, tutaongeza reli mpya na *studies* zimeshaanza tayari kati ya Isaka na Kigali kule Rwanda na vile vile kuunganisha kwa barabara Bandari ya Kigoma na nchi ya Burundi. Barabara hiyo itawekwa kwenye bajeti ijayo kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa ndege, ni kweli kama magazeti yanavyosema kwamba pamejitokeza matatizo kati ya ubia wa Shirika la Ndege ya Afrika ya Kusini na Shirika la Ndege la Tanzania. Serikali zetu tumekubaliana kwamba hawa waachane kwa amani lakini kuna taratibu za kisheria ambazo zinaendelea ili *Air Tanzania* iweze kujiimarisha tena upya na Serikali imeamua kwamba ni lazima kujiimarisha Air Tanzania ili iweze kuwa kile kilichokuwa kinazungumzwa hapa kwamba tuwe na ndege ya Taifa. Lakini niseme tu kwamba tafsiri ya *National Carrier* imebadilika. *National Carrier* ni ndege ya Serikali kwa sehemu kubwa au mali ya wananchi wa nchi fulani kwa sehemu mradi Serikali ya nchi ile itamke hivyo. Sisi tumeamua kwamba tutaendelea kuwa na *Air Tanzania* ambayo imeimarishwa na ambayo itakuwa kwa sehemu kubwa ni mali ya Serikali ya Tanzania pekee au na wananchi, hilo litaamuliwa baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuna mpango wa kutengeneza na kuimarisha viwanja 10 vya ndege pamoja na kukamilisha kiwanja cha ndege kule Songwe, Mbeya. Kwa sasa hivi tunashughulikia kiwanja cha Mwanza ili kiweze kuwa ni *center* ya kwenda kwenye eneo la Maziwa Makuu. Kwa hiyo, tutaendelea kuimarisha viwanja 10 katika miaka mitano ijayo na lengo ni kabla ya miaka mitano ijayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Shirika letu la *TTCL* ambalo liliyumba sana baada ya ubinafsishaji, sasa limeanza kuimarika baada ya kuelewana upya na yule mwekezaji na tumelipa kazi kubwa, litaendelea kuimarisha simu za kawaida lakini kwa teknolojia mpya lakini vile vile litashughulikia hasa mkonga wa simu wa Taifa ambaao unaweza ukasema ndio uti wa mgongo wa simu Kitaifa. Kazi hiyo wameshaanza na kwa mujibu wa sera iliyopo sasa ya *ICT (Information and Communicaton Technology)* tutashirikisha watu binafsi katika eneo hili na tumeshaanza kupata watu wengi binafsi ambaao wameonyesha nia ya kuwekeza zaidi katika eneo hili na sio hivyo tu lakini katika eneo la simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoolewa simu za mkononi sio za Serikali. *TTCL* bado Serikali ina hisa nyngi zaidi lakini simu za mkononi ni za watu binafsi isipokuwa Celtel ambayo karibu theluthi ya hisa ni za Serikali. Lakini bado tuna uwezo nao kwa sababu sisi Serikali ndio *regulators* siku zote tutaendelea kuwabembeleza ili wasogee zaidi vijijini na bahati nzuri tumepata watu ambaao wako tayari kusogea huduma za simu za mkononi hadi vijijini. Kwa hiyo msiwe na wasiwasi hilo tunalo na tutaendelea kufanya kazi hii kwa umakini mkubwa ili kusudi maslahi ya Taifa yasije kupotea. Hilo naweza kuwahakikishieni kwamba nitalisimamia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya miundombinu, hizi ninazotawala zina matatizo makubwa ya uwezo. Kwa mfano ingawa sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo ya Serikali inatokana na Wizara hii lakini Watanzania wanaofaidika na bajeti ile ni wachache. Nitatangaza baadaye wakati wa bajeti hatua ambazo nataka kuchukua za kuwezesha Watanzania, kampuni ndogo za Tanzania ziweze kukua ziwe kubwa na zichukue kandarasi kubwa kubwa ili mzunguko wa fedha uendelee kubaki kwa Watanzania. Hilo ni moja ya uwezeshaji wa Watanzania katika eneo hili la ujenzi wa barabara, madaraja na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, kutumia Wizara hii kuongeza utajiri vijijini kwa mfano kama unatengeneza barabara ni kwa namna gani wanakijiji wa eneo lile barabara inamopita watafaidika na kandarasi ile? Jambo hilo sasa hivi nalishughulikia mwezi wa saba tutatangaza *in details* namna gani Serikali za vijiji, mwananchi mmoja mmoja ndani ya vijiji, Halmashauri za Wilaya zinavyoweza kufaidika na kandarasi za barabara na madaraja yanayojengwa katika maeneo hayo ili kusudi nao wapambane na umaskini kutoptaka na baraka zilizotoka *center*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengi ya namna ile ambayo kwa kweli tunafikiri Wizara yangu hii ingeyafanya itasaidia *physically* kupambana na umaskini na vile vile itasaidia sana kuwawezesha Watanzania wasomi, wahandisi, ma-*architects*

kufaidika na bajeti tunayotenga na vile vile kujisikia kwamba wao wenyewe ndio wanajenga nchi hii kwa kutumia elimu waliyonayo na kwa kutumia uwezeshaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, unajua mimi ni sawasawa na mtu aliyeingia kwenye nyumba, bado sijajua kona zote za Wizara hii. Lakini hivi sasa nakamilisha muundo mpya wa Wizara; itakuwa Wizara ndogo lakini yenye wataalam wazuri wenyewe utendaji. Sawasawa kabisa na Jeshi la Wananchi, Jeshi dogo linaloendeshwa kitaalam na hii itakuwa Wizara ndogo inayoendeshwa kitaalam na mtakuja kuona matokeo baadaye kama Mungu akitujalia. Tukishakamilisha nadhani nitakuwa na mimi nimeshafahamu kona zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo nataka kusema ni kwamba katika Wizara hii zinahitajika fedha nyingi sana na hata kama bajeti nzima ya Taifa ingepewa Wizara yangu, haingetosha. Kwa hiyo tumelewana na Mheshimiwa Zakia kwamba kiasi atanitafutia hela, kiasi nitatafuta mwenyewe. Mimi nashukuru sana kwa kutokea huko kwa sababu najua barabara zote za kwenda kwenye fedha. Kwa hiyo, tutasaidiana, matumaini yangu ni kwamba Mungu akitujalia tunaweza tukaonyesha matokeo kwa ari mpya na nguvu mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa nitamwita mchangiaji wa mwisho kwa asubuhi hii ambaye ni Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge mkumbuke kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu atajibu hoja kama mtoa hoja hapo saa 11. Nawaombeni wote tuwahi tuweze kumsikiliza.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza kwenye Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu kama Waziri wa Fedha, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwanza kwa kunateua kuwa Mbunge na baadaye kunipa wadhifa huu mzito sana wa kuwa Waziri wa Fedha. Namshukuru sana kwa imani aliyionionyesha. Napenda kumtaka hapa kwamba kwa kweli nitajitahidi kwa uwezo wangu wote na naomba Mwenyezi Mungu anipe afya niweze kufanya kazi kwa kulitumikia Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Basil Mramba alipokuwa anazungumza mwishoni, alisema kwamba tumekubaliana juu ya fedha. Najua kwamba wakati ule Mheshimiwa Mramba alikuwa mchungu kweli kweli wa fedha sasa na yeye asitarajie mimi sitakuwa mchungu wa fedha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kuunga mkono hoja aliyotoa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa maelezo mafupi ya waliochangia katika sekta hii ya fedha. Napenda kusema kwamba mengi yaliyochangiwa tutayachukua na kwa kweli yatatusaidia sana katika utendaji wa siku kwa siku ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema pia kwamba Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara ya Fedha alitamka bayana kwamba Wizara ya Fedha ni kama moyo wa Serikali kwa hiyo una umuhimu mkubwa sana. Kwa yale Waheshimiwa Wabunge waliyozungumza karibu yote yamezungumzia juu ya mapato, matumizi na pia juu ya suala zima la kuimarisha sekta hii ya fedha katika makusanyo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika uchangiaji mmojawapo alizungumzia juu ya Benki Kuu iweze kuangalia juu ya utoaji wa leseni katika maduka haya ya fedha za kigeni (*bureau de change*) na kwamba aliona maduka mengi sana yamezagaa sehemu za Kariakoo na kadhalika. Alieleza kwamba kuna haja ya kuangalia zaidi juu ya utoaji wa leseni hizi. Niseme kwamba Benki Kuu ambayo inasimamia shughuli za fedha za kigeni kwa mujibu wa kanuni za uendeshaji wa shughuli za kubadilisha fedha za kigeni za mwaka 1999 (*foreign exchange bureau de change regulations, 1999*), kanuni hizi zimewека vigezo ambapo vigezo hivi vinatumika katika utoaji wa leseni kwa maduka ya kubadilisha fedha zote za kigeni. Maduka haya hutoa huduma hiyo kwa wateja wake ambaо wametapakaа sehemu zote ikiwemo sehemu hiyo Kariakoo ambayo ameitaja.

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaka kwamba Benki Kuu itafutilia kwa karibu sana utekelezaji wa sheria na kanuni za uendeshaji wa maduka haya ambayo yamesajiliwa. Pale ambapo pataonekana na dalili za uvunjaji wa sheria au inaonekana kwamba kanuni kwa kweli hazifuatwi basi Benki Kuu hazitasita kuwanyang'anya leseni maduka haya yenye kuhusika na *bureau de change*. Kwa hiyo, Benki Kuu itafutilia hilo na pale ambapo inaonekana utaratibu haifuatwi basi itanyang'anya leseni hizi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa juu ya udhibiti wa matumizi mabaya ya Serikali kama vile kutorejesha masurufu ya safari mapema na bila wahusika kuchukuliwa hatua. Napenda kusema kwamba kuna taratibu na sheria ambazo zimewekwa katika uchukuaji na urudishaji wa masurufu. Lakini tunajua kwamba mara nyingi sana sheria na taratibu hizi hazifuatwi na ndio maana tunapata matatizo makubwa sana ambayo hata Mheshimiwa Rais aliyaeleza hapa. Napenda kusema kwamba tutaweka msisitizo na kuhakikisha kwamba sheria na taratibu zilizowekwa zinafuatwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutaja baadhi ya sheria na taratibu hizi zilizowekwa. Kwanza msisitizo juu ya kutoa masurufu kwa mtumishi ambaye hajarejesha masurufu ya awali. Yaani yule mtumishi ambaye amepewa masurufu amekwenda safari akarudi na hakurudisha masurufu haya basi hapaswi kupewa masurufu mengine. Hili nasema kwa uhakika tutalisimamia na mimi binafsi nitahakikisha kwamba ninauliza kila mara juu ya jambo hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili kuweka utaratibu wa kuwakata mishahara yao watumishi ambao watashindwa kurejesha masurufu waliyopewa kwa wakati unaotakiwa baada ya safari au kukamilika kwa shughuli maalum. Kwa sababu kuna muda wanaopewa inawekezekana kabisa mtu amechukua masurufu akakaa nayo mwaka mmoja na kadhalika kwa hiyo tunasema kwamba muda ule ambao anatakiwa kurudisha ukipita basi fedha hizi zitakatwa kwenye mshahara wa yule mtumishi.

Tatu, ili kuweza kupunguza ukubwa wa kiwango cha masurufu anayopewa mtumishi katika masurufu maalum tutaweka msisitizo katika kulipa moja kwa moja gharama kwa watoa huduma kwa mfano hoteli na kumbi za kuendesha mikutano. Kuna baadhi ya watendaji labda kuna semina na mikutano ambapo wanabeba fedha nyingi labda kulipa fedha kwa ajili ya hoteli, kumbi za mikutano, tunataka kufanya utaratibu kwamba fedha hizi kwa kweli ziweze kulipwa moja kwa moja badala ya mtumishi huyu kubeba masurufu haya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilihusu msamaha wa madeni. Suala hili lilisema kwamba Serikali ililipa deni la nje kwa kutumia kiasi cha dola za Marekani 500mil kwa kila mwezi na kwa sasa Serikali imesamehewa deni lake je, hizi fedha zinapelekwa wapi? Pili, kwa nini malipo yanafanyika kwa kutumia fedha za kigeni yaani dola badala ya kutumia fedha zetu yaani shilingi ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, msamaha wa madeni umepatikana mwanzoni mwa mwaka 2001 baada ya Tanzania kufikia ukomo wa *HIPIC* chini ya mpango wa kusamehe madeni kwa nchi maskini yaani *enhance HIPIC initiatives*.

Chini ya mpango huo Tanzania ilipewa ahadi ya kufutiwa dola za Kimarekani milioni tatu toka nchi pamoja na mashirika ya fedha za Kimataifa. Mara tu baada ya ahadi hiyo ya kufutiwa madeni hayo, Serikali imefanya juhudu kubwa ya kukamilisha mikataba ya kupatikana kwa misamaha. Takwimu zinaonyesha kuwa hadi kufikia Desemba, 2005, Serikali ilikuwa imeshapata unafuu wa madeni wa dola za Marekani bilioni 2.2.

Mheshimiwa Spika, msamaha huo kwa kweli umetuwezesha kutoongezeka sana kwa deni letu ingawa tunaendelea kukopa toka kwa vyanzo nafuu. Hivyo ikilinganishwa kwa mwaka 2001, deni limepungua sana kwa kipindi hiki. Fedha zilizopatikana ndizo ambazo zinatumika katika utaratibu mzima wa bajeti ambao unalenga kama tulivyoeleza katika MKUKUTA (Mkakati wa Kuondoa Umaskini na Kukuza Uchumi).

Mheshimiwa Spika, hili litakuwa jambo muhimu sana kama tunavyosema 41% ya bajeti yetu mpaka sasa ni tegemezi. Kwa hiyo mkakati huu ukiwekwa kwa kweli tunategemea kwamba bajeti itapunguza utegemezi wake.

Mheshimiwa Spika, suala la kufanyika kwa malipo kwa fedha za nje na siyo fedha za Tanzania, haya yanatokana na makubaliano ya wale ambao wanatukopesha. Wale wanaotukopesha ndiyo ambao wanaamua ni fedha za *denomination* gani ambayo tunapaswa kulipa.

Kwa hiyo, wengine wanaweza kutaka dola, wengine *Euro* au wengine fedha za kwo wenye na kwa sababu fedha zetu bado hazijawa na nguvu Kimataifa mara nyingi sana fedha ambazo wanazotaka ni fedha za nje. Lakini sisi tunakuwa tunalipa fedha za hapa Tanzania kwa *BOT* halafu *BOT* ndiyo ambao wanalipa fedha za kigeni kwa wale ambao wanatukopesha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni suala la *pension* ambalo limekuwa likileta usumbufu mkubwa kwa wazee na kwamba ni kidogo sana zingeweza kuongezwa. Ni kweli kabisa kwamba watu wengi sana wamekuwa wakilalamika juu ya suala zima la *pension*. Serikali inafuatilia suala hili lakini katika kuongeza fedha za *pension* itategemea sana uchumi wetu. Mtakumbuka kwamba kuna wakati ambao wazee walichukua *pension* ya mkupuo fedha zote lakini ikaonekana kwa kweli hali zao zilikuwa taabani na kwa maana hiyo ikabidi warudishwe katika kuchukua fedha zao kwa kila mwezi. Kwa hiyo fedha za pension mpaka sasa hivi kiwango cha chini kabisa ni shilingi 21,000/= kwa mwezi lakini kama ninavyosema kwamba kila uchumi unavyokuwa ndivyo ambavyo suala hili la *pension* nalo litawenza kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya kuchelewa kwa fedha kufika kwenye Halmashauri za Wilaya na kwamba tuhakikishe zinafika kwa wakati muafaka. Labda nieleze fedha zile ambazo zinakwenda kwenye Halmashauri kwanza ni fedha ambazo zinapitia kwenye bajeti ya Serikali. Pili, fedha chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi yaani MMEM kule PEDEP. Tatu fedha chini ya Mfuko wa *Local Government Capital Development Ground System* ambao fedha hizi hupitia TAMISEMI na pia ...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri una muda wa kutosha kwa kweli usifuate kengele.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru sana.

Nne, ni fedha zile za *Road Fund* ambapo nafikiri juzi au jana Mheshimiwa Selefii alisema kwamba asilimia ile 30 anapendekeza iongezeke iwe asilimia 40 na tukasema kwamba Serikali italiangalia suala hili. Tumeshazungumza na *Accountant General* kwamba fedha zinachelewa lakini kabla *Accountant General* hajapeleka fedha hizi, kuna mtiririko mzima wa fedha ambazo zinaweza zifike kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, tatizo ambalo lilikuwepo tumeshalionna na mimi nasema kwamba tutalishughulikia ili kuhakikisha kwamba fedha zile za bajeti zinafika kwa wakati.

Lakini pili fedha hizi za miradi kama nilivyosema kuna fedha ambazo zinalipwa na wahisani kwenda kwenye miradi mbalimbali. Juzi Jumamosi tulipokuwa na semina hapa tulikuwa tunasema kwamba tulikuwa tumewataka wahisani wakubali kuingiza fedha moja kwa moja kwenye bajeti ya Serikali yaani kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Utaratibu huu wa kuingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ina maana kwamba mkishapitisha bajeti fedha za wahisani zinakuwa zimeingia. Utaratibu huu ni kwamba wanaleta fedha lakini wakati mwagine hawaleti kwa wakati. Kwa hiyo, badala ya *quarter* ile ya kwanza wanaweza kuleta *quarter* ya pili au ya tatu. Nafikiri fedha za MMEM safari hii pia zimechelewa na hivi sasa ndio zinaanza kuingia. Kwa hiyo

uchelewashaji wakati mwingine unakuwa kwa sababu ya ucheleweshaji wa fedha za wahisani wanazozileta na ndiyo maana tunajaribu sana kuzungumza nao ili angalau asilimia kubwa ya fedha zao ziende moja kwa moja kwenye Mfuko wa Serikali. Tukifanikiwa hili basi tutaweza kuendesha *program* zetu vizuri zaidi lakini *of course* ni kufanikiwa kwa makusanyo ya fedha kwa sababu kama makusanyo yataweza kuwa makubwa zaidi basi bajeti yetu itakuwa hatutegemei nje kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba kwa upande wa MMEM hata hii ya *Local Government Capital Development Ground System* ambayo ameitaja sasa hivi Mheshimiwa Waziri wa Elimu, *Road Fund* na kadhalika hizi ni fedha sehemu kubwa zinatoka kwa wahisani sisi tunazo fedha zetu kidogo lakini huwezi kuleta kwa sababu ya mpango inabidi uongojee fedha zile za wahisani. Tutazidi kuzungumza na wahisani ili kuhakikisha kwamba kwa kweli walete fedha hizi kwa wakati muafaka..

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni kuhusu kuwawezesha kiuchumi wananchi wa hali ya chini wakiwemo vijana na wanawake. Suala hili nalo pia limezungumzwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba tufanye utaratibu ili kuwawezesha wananchi ambao wanakuwa na kipato cha chini waweze kuwa na uwezo ili kuondoa umaskini. Niseme kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi itatekeleza Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi. Hivi sasa kuliwa na mpango ule ambao najua kwamba haujibu moja kwa moja suala hili, mpango ule wa *Credit Guarantee Scheme*, Mpango wa *Bank of Tanzania* yaani *BOT* ambao unadhamini mabenki. Kwa hiyo wewe ukiwa mteja kwenye *bank* unaweza kudhaminiwa ukachukua mkopo. Dhamana siyo kwako wewe lakini wanadhamini ile *bank* ukachukua mkopo na baada ya hapo ukaweza kurudisha mkopo. Utaratibu ni kwamba kama *in case* hujaweza kurudisha mkopo mzima basi inabidi *Bank of Tanzania* ibebe *percentage* ile ambayo huwezi kurudisha.

Sasa tunachotaka kufanya hivi kwa kweli ni kuweza kuzungumza pia na *National Micro Finance Bank* yaani *NMB* ambayo ina mtandao wake nchi nzima na ambayo Serikali ina asilimia 51 na wawekezaji wengine asilimia 49 lakini kwa taarifa tulizonazo ni kwamba wale asilimia 49 wana *experience* kubwa sana katika masuala haya ya kutoa mikopo hasahasa kwa wananchi wa vijijini. Kwa hiyo tunachotaka kufanya sasa hivi kwa kushirikiana na *BOT* yaani *Bank of Tanzania* tuangalie ni jinsi gani ambavyo tutaweza kuimarisha aidha *SACOS* ili waweze kupata mikopo kupitia *NMB* na kwa maana hiyo kuimarisha uwezekano wa wananchi huko vijijini kuweza kupata mikopo. Nasema hili tutalifanya kazi kwa sababu hili ni jambo ambalo tumetoa ahadi kwa wananchi wote na sisi kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi tunasema tunafanya yale ambayo tuliahidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba kama kutakuwa na mawazo zaidi ya Waheshimiwa Wabunge basi ninapenda sana wanilettee kati ya sasa au miezi miwili au mitatu lakini isichukue muda mrefu sana. Tuleteeni mawazo na tutaangalia ni jinsi gani ambavyo tutaingiza katika suala hili la kuwasaidia wananchi maskini waliokuwepo huko vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo narudia tena kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu kwa kweli naweza kusema *speed* yake ni kali sana, nampongeza sana. Ninawashukuru sana Waheshimwa Wabunge. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kusitisha shughuli za Bunge kwa asubuhi hii, bado nimeendelea kupata malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge hasa Wabunge wanawake kwamba hali ya hewa humu ndani ni ya baridi sana. Sasa jana ilikuwa afadhali lakini leo sijui Wahandisi kumetokea nini lakini kwa kauli hii ya Spikaawaomba Wahandisi waheshimu malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge tusiwe na joto kabisa watu watoke jasho lakini pia isiwe baridi ambayo inawafanya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kumwandikia Spika kutoa malalamiko yao.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11:00 Jioni.

(*Saa 06:38 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11:00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nihitimishe mjadala tulioanza siku kadhaa zilizopita.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imechangiwa kwa kuzungumza na Wabunge 133 na Wabunge, 47 kwa maandishi. Kama ulivyo utamaduni wetu, nivumilieni niwatambue wote waliochangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Dr. Harisson G. Mwakyembe, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Hazara P. Chana, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Anna M. Komu Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Grace S. Kiwel, Mheshimiwa Eliatta N. Switi, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Dr. Omari Nibuka, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mheshimiwa Hilda Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Zuleikha Y. Haji na Mheshimiwa Janet B. Kahama. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Jacob D. Shibili, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Zubeir A.

Maulid, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Jakson Makwetta, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Ali S. Salim, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mheshimiwa Luhanga J. Mpina, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Lucas L. Selelili Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri na Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Joyce L. Machimu, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Kidawa H. Salehe, Mheshimiwa Benedict K. Losolutia, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Ponsiano B. Nyami, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Ibrahim M. Sanya, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Mwanne I. Mcchemba, Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Halima Omari Kimbau, Mheshimiwa Capt. John D. Komba. Mheshimiwa Willam J. Kusilla, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Margaret A. Mkanga, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Mwanju S.O. Msambya, Mheshimiwa Dr. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Athuman S. Janguo, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki na Mheshimiwa Juma A. Njwayo. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Eustace O Katagira, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Balozi Hamis S. Kagasheki, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, Mheshimiwa Godwin F. Kimbita, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Diano Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Harith B. Mwapachu, Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandosya, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Stephen Wassira, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Zakhia H. Meghji. (*Makofi*)

Waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:-Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Mwinchumu A. Msomi, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Fatma A. Tamim, Mheshimiwa Bakari S. Faki, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Athuman S. Janguo, Mheshimiwa Salome J. Mbatia, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Martha Umbula na Mheshimiwa Mariam R. Kasembe. (*Makofî*)

Wengine ni Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbiri, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Anastasia J. Wambura, Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji na Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wote kwa michango yao. Napenda kuwashakikishia kwamba tumezingatia michango yao na nitakapokuwa najibu siwezi kuwajibu wote. Lakini niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, ambao asubuhi hii walinisaidia kujibu sana hoja ambazo zimejitokeza kwenye mjadala huu. Napenda kuwaahidi kama tulivyotangulia kupatana kwamba kila Mbunge, kila Wizara itamwandikia majibu ya maswali yake ambayo ameuliza katika kikao hiki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niwashukuru Katibu Mkuu wa Wizara yangu na Naibu wake na wataalam wote pamoja na wataalam wa Wizara mbalimbali ambao wamekuwepo hapa wakichukua mazungumzo haya na kuyaandikia majibu, nawashukuru wote kwa michango yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamekwishazungumzwa na kwa kweli mengi yalikuwa ni kutuimarisha katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ni ushauri, tutauzingatia na sehemu kubwa imejibiwa na Waheshimiwa Mawaziri. Mimi nitachukua maeneo machache sana ya kusisitiza tu ambayo nafikiri ni vizuri yamejitokeza na vizuri kuyatolea msimamo.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni Tume ya Uchaguzi. Kumekuwepo na maneno mengi sana juu ya Tume ya Uchaguzi ambayo mimi sihitaji kuyarudia. Lakini naomba kuweka bayana mambo mawili. Kwanza, Tume za Uchaguzi ziko mbili, iko Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na iko Tume ya Uchaguzi ya Muungano. Tume zote hizi zimefanya kazi nzuri. (*Makofî*)

Ningependa kuweka bayana kwamba ni vizuri Waheshimiwa Wabunge, kama kuna hoja zinazohusu mambo ya Zanzibar, yazungumzwe kwenye Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Tukiulizwa habari ya Askari wa KMKM hapa Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu hana majibu. Lakini nina hakika katika Baraza la Wawakilishi, wapo watu wanaoweza kujibu vizuri hoja hizo. Kwa hiyo, naomba tutofautishe hoja za Zanzibar zilengwe Zanzibar, hoja za Muungano zilengwe ndani ya Muungano. Narudia kusema Tume za Uchaguzi zimefanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Watanzania tuna tatizo la kutokupenda na kusifu mambo yetu. Wamekuja wageni wa nje wa Ulaya, wa Afrika wamesema uchaguzi umeendeshwa kwa haki na huru. Wamesema Tume hizi zimefanya kazi nzuri na angalieni vifaa vimekwenda mpaka kijiji cha mwisho cha nchi yetu, vifaa vimefika na uchaguzi umefanyika. Leo tupo hapa ingekuwa uchaguzi haukuwa haki na huru tungekuwa tunapigana makofi hapa. Lakini kila mtu anakiri kwamba uchaguzi ulikuwa wa haki na huru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hata idadi ya (*petition*) waliopinga matokeo hii ni wachache sana kwa sababu mambo yalikuwa shwari sana. Ndiyo maana Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, anaweza akasimama akasema mimi ni wa kwanza Tanzania kwa kupata kura nyingi kwa sababu uchaguzi ulikuwa umeandaliwa vizuri, kura zimepigwa vizuri na zimehesabiwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, badala ya kuwalaumu Tume na kusema tuwabadilishe na kusema walipendelea Chama Tawala, kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Bunge hili napenda kuipongeza Tume ya Uchaguzi chini ya Jaji Lewis Makame na Mheshimiwa Kiravu. Walitufanyia kazi nzuri wamejengea heshima nchi yetu, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni suala la Muungano. Limesemewa sana, mpasuko ndani ya Muungano wetu. Maneno yamekuwa mengi na makali. Sina hakika kama ndicho alichotaka Mheshimiwa Rais. Lakini Mheshimiwa Rais, alisema: “Anasononeshwa na mpasuko uliopo”. Tumeendelea kusema sababu za mpasuko huo na kadhalika na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, asubuhi ametukumbusha historia ya mpasuko huo. (*Makofi*)

Lakini mimi napenda kusema yafuatayo; Muungano huu uko imara. Muungano huu ni wa kupigiwa sifa Afrika. Nasononeshwa sana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wanaochukua Kurani Tukufu, Biblia wanaapa mbele ya dunia nitaitetea na kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akitoka pale anasema siitambui Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Anaapa nitaitetea na kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mle katika Katiba ile ndimo imo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofi*)

Mimi naamini kila mtu mwenye dini yake anajua maana ya dini yake. Kila mtu mwenye busara anajua maana ya kiapo. Tule kiapo tunachokiamini, tutetee na kuilinda

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuulinda Muungano wetu na kutambua Serikali halali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofî*)

Haitusaidii sana kuzunguka duniani kusemana, kusengenyana na kuzuia misaada kwa ajili ya maendeleo ya watu. Haisaidii sana baada ya uchaguzi kuishi kuendelea na maneno. Uchaguzi umeisha Mheshimiwa Amani Abeid Karume, ndiye Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, najua kuna kero kwenye Muungano lakini hata nyumbani una kero, haziishi siku moja. Tusaidiane, nia njema ya Rais ya kumaliza kero hizo zimalizike kwa uungwana na kwa mahusiano mazuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, juzi hapa tulipokuwa katika mchakato wa uchaguzi ndani ya chama chetu kuna watu walitaka kutuletea mpasuko huo. Lakini Wabunge, walijibu kwa kauli kubwa hatutaki mpasuko na mtu akapata kura nyingi sana. Wabunge hawautaki mpasuko na nina hakika Watanzania, hawataki mpasuko ndani ya Muungano wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ujambazi, suala la ujambazi limezungumzwa kwa kirefu sana. Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, ametoa maelezo mazuri sana. Najua na Waheshimiwa Wabunge mpaka wamefika mahali wanasema tuite Jeshi la Wananchi. Lakini natahadhari mbili, jamani hali siyo mbaya kiasi hicho. Nenda *SOWETO* pale unaingia mlangoni begi linachukuliwa mbele ya watu. Unavaa saa wanavunja dirisha wanachukua, Tanzania hatujafika hapo, bado nchi hii ina amani na utulivu ndani ya nchi yetu. Bado nchi hii leo ni kisiwa cha amani ndio maana wawekezaji wanakuja kwa wingi sana kwa sababu ni nchi ya amani hata walioko Afrika Kusini wanakuja wanashangaa yaani nchi kuna amani kiasi hiki hawaamini, matukio haya madogo yatapita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema hali siyo mbaya kiasi hicho. Lakini lazima tupambane na ujambazi hawawezi kutushinda. Mimi nashukuru mapendekezo mengi yametoka hapa. Mheshimiwa Rais, alipohutubia aliwaomba wananchi na akawaambia jamani eeh majambazi wanakaa humo mitaani, tuleteeni majina. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwapongeza wananchi waliotuandikia barua. Sasa hivi ziko mafaili na mafaili wananchi wakitaja majambazi. Wametajwa majambazi na baadhi ya viongozi ndani ya Jeshi la Polisi, wanatajwa na wananchi. Sasa Jeshi letu lina watu wengi lakini lina wabaya vile vile. Lakini hatuwezi kusema Jeshi lote ni baya, hapana. Jeshi letu liko imara na tutalisaidia tutashinda majambazi hawa katika muda mfupi sana. Haitusaidii sisi kulumbana juu ya Jeshi la Polisi, suala ni kwamba tuondoe na tuutokomeze ujambazi ndani ya nchi yetu na tusaidiane kama alivyoelekeza Rais wote kwa pamoja tuchukue hatua zinazopasa. Mimi narudia kusema nawapongeza sana wananchi hawa ambao wanaandika kwa ujasiri kusema nani jambazi, nani anatokea wapi, nani ndani ya Jeshi la Polisi, tunawapongeza na waendelee kutufanyia kazi hiyo. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, jambo moja ambalo linajitokeza ni kwamba baadhi ya majambazi hao siyo Watanzania, wanatoka nje ya nchi yetu kuja kutuharibia. Sasa

tunaomba Watanzania tusikubali tuwataje na wakamatwe, tuwatoe tuwapeleke ndani ya vyombo vyaa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la Madiwani, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge mlivyolizungumza suala hili, mmeonyesha matatizo yaliyopo. Ni kweli hawa ni viongozi wenzetu katika ngazi ya Kata, ni wawakilishi wazuri sana, maslahi yao ni duni. Yote mliyoyasema tunakubaliana. Ila napenda kuwashakikishieni kwamba Serikali haikukaa kimya. Tumeunda Tume chini ya Mheshimiwa George Lubeleje ya kutazama maslahi ya Madiwani na taarifa yao tunaitegemea muda wowote. (*Makofi*)

Tutakapopokea taarifa ile tutaichambua tutaangalia nini cha kufanya ili na wao kwa kweli waweze kufanya vizuri kazi za uwakilishi ambazo wananchi wamewachagua nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa suala la njaa na ukame. Mheshimiwa Naibu Spika alisema Wabunge wapya alitarajia watasema kidogo, lakini akagundua wanasema kweli kweli. Mheshimiwa Anne Makinda, nakubaliana na wewe.

Lakini kubwa nadhani wanaotusikiliza wameshuhudia kwamba Wabunge hawa ni wawakilishi wa wananchi na wasemaji wa maslahi ya wananchi. Hakuna Mbunge aliyesimama hapa awe Mbunge wa Jimbo, Mbunge wa kuteuliwa au wa Viti Maalum ambaye hakuzungumza juu ya tatizo la njaa na ukame katika nchi yetu. Tena likazungumzwa kwa umahiri na umakini wa hali ya juu sana. Nawapongezeni sana, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri wananchi wakajua kwamba wawakilishi wao wanajua tatizo, wawakilishi wao wanashirikiana na Serikali ili kupambana na tatizo ambalo limetupata katika nchi yetu. Kana kwamba ukame peke yake hautoshi tumepata tatizo la viwavi jeshi katika Mikoa ya Kusini, vimeanza kula mahindi na mazao kule na dalili zilizopo ni kwamba wataelekea Kaskazini pale mvua za mwezi Machi zitakapoanza kunyesha wavamie maeneo hayo na mazao hayo. Lakini nashukuru jana tumepeleka maombi yetu na nitaeleza baadaye naamini yatashughulikiwa. Nataka kusema nini kutohana na ukame huu, tutategemea kwamba tutawalisha Watanzania wote, Waheshimiwa Wabunge ni jambo gumu sana. Nia yetu njema, dhamira njema, lakini tumuomba Mwenyezi Mungu jamani tupate mvua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo usiku nimesikia katika sehemu kubwa sana za nchi mvua zimenyesha. Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu tupate mvua kwa sababu ndiyo suluhisho la matatizo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulieleza kwenye *briefing*, hali ilivyo sihitaji kuirudia. Lakini nirudie kusema tunacho chakula nchini, tutakisambaza. Wafanyabiashara binafsi wanasantazachakula na kile cha Serikali kina mafungu matatu, kipo kile ambacho tutauza kilo Shilingi 50 kipo kile ambacho tutaomba watu wenye nguvu lakini hawana pesa wafanye kazi ni chakula cha kazi. Mzee John Malecela, ananikumbusha kila siku

chakula cha kazi. Kipo pale ambacho mtu hana uwezo kabisa na wanakijiji wanasema huyu hana uwezo tutampa chakula bure. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mahitaji ni makubwa, jana tulizungumza na Mabalozi. Sasa naona kuna gazeti moja linatupiga vijembe hivi, wanasema hatimaye Serikali yaomba chakula, ndiyo, ni kweli hatimaye, kwa sababu Rais wetu alisema si vizuri kuomba chakula, si heshima, unavunja heshima ya nchi yako kwenda kuombaomba chakula, tukiamini kwamba kwa Bajeti yetu tungeweza kushughulika na tatizo hili. Lakini tumeona tatizo ni kubwa mno ndiyo maana tunasema jamani sasa tupige kelele, tuombe dunia itusaidie. Sasa wasiseme kana kwamba hatukuwa makini, tulikuwa makini sana lakini tulitaka kujenga heshima yetu wenyewe kwamba kwa Bajeti yetu tusingeweza kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeomba chakula tani 100,000 lakini ni zaidi hiyo kwa sababu kama tulivyozungumza siku ile hapa Waheshimiwa Wabunge, mlisema kufikisha chakula Makao Makuu ya Wilaya peke yake, Vijijini hakifiki kwa sababu uwezo wa Halmashauri zetu ni mdogo. Kwa hiyo, katika maombi yetu tumeunganisha vile vile na suala la usafiri. Kwa hiyo, jumla ya maombi kwa *donors* ni dola za Kimarekani milioni 50 kwa ajili ya chakula na usafirishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mabalozi wale wametuahidi kwamba wanalishughulikia lakini wametukumbusha jambo moja kwamba jamani ninyi mnashindana na wengine, Kenya kuna njaa, Ethiopia kuna njaa, Somalia kuna njaa na tulianza kuwasaidia huko kabla ninyi hamjaja. Lakini hata nchi za jirani ingawa mvua zimeanza *Congo DRC*, Malawi imeanza na Zambia, lakini bado hali yao vile vile ya chakula siyo nzuri. Kwa hiyo, katika eneo zima hali ya chakula siyo nzuri, hata hao wanaoagiza hawaagizi kutoka *South Africa* kwa sababu *South Africa* hawana chakula. Wanaagiza kutoka *Mexico* na Marekani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nasema hali ndiyo hivyo lakini tunaamini tutapata chakula na sisi tutaendelea kununua. Rais ameigiza tuagize haraka tani 42,000 na Wizara ya Kilimo inatusaidia kufanya hivyo mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mambo mawili, kwanza naomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane, hicho chakula kidogo kinachokuja kwenye maeneo yenu, tutahakikisha kwamba taarifa tunayompelekea Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi vile vile na Mheshimiwa Mbunge, anapata ili sote hili liwe jukumu letu la kwanza kuhakikisha wananchi wanapata chakula. Hilo ombi langu la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu la pili, Waheshimiwa Wabunge, huenda mvua zikaja. Tunaomba msimamie kilimo cha mazao ya muda mfupi. Inawezekana kabisa tukipanda mtama, tukipanda fiwi, tukipanda viazi vitamu kwa mvua kidogo tunaweza tukapata chakula. Mazao ya kupanda mnafahamu lakini wote tusaidiane kuhimiza kilimo cha muda mfupi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika maombi yetu kwa (*donor*) wafadhili, tumeomba vile vile mbegu. Lakini mbegu, hiyo isipowahi mvua zikianza itabidi kwa kweli kuendelea kuziomba Halmashauri, nilisema siku ile kule Shinyanga, Bariadi, Maswa na Shinyanga Vijijini wamekwisha tafuta mbegu zao wameziweka tayari wanangojea mvua zikianza wawapelekee wananchi. Naomba Halmashauri zote nchini ziige mfano huo, wafanye kama Shinyanga, Bariadi na Maswa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, sasa msaada huu tunamuomba kila mmoja, kila kijiji mtu aliye na uwezo kuliko mwenzake amsaidie mwenye njaa. Taasisi za kidini, *NGO* na wengine watusaidie msaada wa chakula cha njaa kunusuru maisha ya watu wetu. (*Makofi*)

Nafurahi kuwajulisha kwamba jana baada ya maombi yale (*Vadacom*) *South Africa*, wamemkabidhi Mheshimiwa Rais Shilingi bilioni moja, kuchangia tatizo hilo la njaa. Vile vile Serikali ya Ubelgiji wametupigia simu wametupa *Euro 250,000/=*. Kwa hiyo, natoa wito na kuomba wengine wote wanaotaka kuchangia jithada hizi za kuokoa maisha ya watu wetu tunawakaribisha saa yoyote watusaidie michango hiyo. Nategemea Makampuni makubwa yale ya madini na wengine wote watajitokeza saa hii kufanya *cooperate responsibility* ya kusaidia watu ambao wana njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa jana Mheshimiwa Anne Malecela, aliuliza swalí zuri ambalo nilijibu. Lakini napenda kurudia swalí lake lile na majibu yangu yale. Tuliulizwa kama tutaiga mfano mzuri ambao Mheshimiwa Rais wetu ameanza kuonyesha wa kutoka ofisini na kwenda kwenye matatizo na kuyashughulikia huko yaliko. Nilijibu na narudia majibu yetu kwamba sisi Mawaziri, tutamuiga Rais kuhakikisha na sisi tunakwenda kwa kasi ya Rais.

Hatutakaa kwenye Ofisi za viyoyozi tukasahau matatizo ya watu tutakwenda kwa watu na kushughulikia matatizo ya watu huko waliko. Simtegemei Waziri ye yote labda yule wa Waziri wa Mambo ya Nje, abaki ofisini nategemea Mawaziri wanakwenda Vijijini kushughulika na matatizo ya wananchi papo kwa papo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, gazeti moja limesema nimetema cheche, mimi sijatema cheche aliyetema cheche ni Rais mwenyewe alituambia kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya. Lakini na nyinyi tusadieni alisema Rais siku ile, mkiona tunasinzia tuchangamsheni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nisome Azimio la Bunge kuhusu Hotuba ya Rais aliyoitao tarehe 30 Desemba 2005 wakati akizindua Bunge jipya.

Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea na kujadili hotuba hiyo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba sasa Bunge lako lipitishe Azimio lifuatalo:-

KWA KUWA, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais, alifafanua kwa kina kwa mapana na uwazi Sera za Serikali ya Awamu ya Nne na kuainisha kwa undani na kwa uhakika majukumu yanayolikabili Taifa letu na Bunge hili linalowakilisha wananchi wote katika kipindi cha miaka mitano ijayo;

KWA HIYO BASI, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa pili uliofanyika Mjini Dodoma, baada ya kuichambua hotuba yake, ninamuomba Mheshimiwa Spika awasilishe kwa Mheshimiwa Rais salamu za Bunge na taarifa kwamba Bunge hili kwanza linampongeza kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofî*)

Pili, linampongeza kwa dhati kwa kutoa hotuba nzito, yenye msimamo thabiti na yenye upeo wa hali ya juu kwa masuala yote muhimu yanayolikabili Taifa hili. (*Makofî*)

Tatu, linamhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba, Bunge litafanya kazi pamoja naye, kwa ushirikiano wa karibu sana na kumpatia kila msaada utakaohitajika ili kufanikisha jukumu la uongozi wa Taifa hili kwa kipindi chake cha uongozi.

Nne, Bunge litashirikiana naye katika kulinda na kudumisha amani na kutetea Muungano wa Tanzania. Aidha, Bunge wakati wote litahakikisha linaimarisha demokrasia ya kweli na kuhakikisha utawala wa sheria unadumishwa nchini kwetu. (*Makofî*)

Mwisho, Bunge linamtakia Mheshimiwa Rais afya njema, maisha marefu na kila la kheri katika uongozi wake. (*Makofî*)

Na kwa hiyo basi Bunge linawaomba Watanzania wote wamuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipitishe Azimio la Bunge kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 30 December, 2005 wakati akizindua Bunge jipya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Hoja ya Kujadili Hotuba ya Rais Pamoja na Azimio lililosomwa liliridhiwa na Bunge*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa wa Mwaka 2006
(The National Leaders Funeral Bill, 2006)

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi mchana huu ili niwasilishe Muswada huu mbele ya Bunge hili uweze kujadiliwa na hatimaye pengine kupidishwa.

Sasa kabla sijaingia kwenye hilo, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo au Wilaya ya Tunduru kwa imani kubwa ambayo wamenionyesha kwa mara ya nne mfululizo. (*Makofî*)

Nitaendelea kujitahidi kukaa nao karibu. Nashukuru kwa upendo waliouonyesha kwa sababu niliporudi Jimboni au Tunduru safari hii mapokezi yale makubwa hayajapata kutokea hata kidogo. Nawashukuru sana. (*Makofî*)

Pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunteua ili niwe mmojawapo katika Baraza lake la Mawaziri. Namshukuru sana kwa kunipa nafasi ya kufanya naye kazi kwa karibu san.

Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa. Mheshimiwa Lowassa ni mtu makini sana, hodari sana na mimi naamini nitajifunza sana kutoka kwake. Mheshimiwa Waziri Mkuu wote hapa tumethibitisha ni mtu mwenye ari, nguvu na kasi mpya kweli kweli. (*Mkaofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwasilisha Muswada ambao unahu kupidishwa kwa Sheria ya Mazishi ya Viongozi ya mwaka 2006 (*The National Leaders Funeral Act*) mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya Muswada wa Sheria wa Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa wa mwaka 2006 yamekamilika sasa. Muswada huu pamoja majedwali na marekebisho unawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu ili kusomwa kwa mara ya pili na hatua nyingine zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wale wote walioituwezesha kutekeleza majukumu yote yanayohusu ukamilishaji wa Muswada huu. Nawashukuru wataalam na wadau wote waliohusika katika utayarishaji na utoaji wa maoni na mapendekezo ambayo yaliboresha maeneo mbalimbali ya Muswada huu. Baadhi ya wadau hao ni pamoja na hawa wafuatao:-

Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA). Jumuiya ya Wakristo Tanzania (CCT), Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC). *Shree Hindu Mandal*, viongozi wa madhehebu ya Bhudha na wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, shukrani zangu

ziwafikie Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa uchambuzi na ushauri wao wa makini chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Makamu wake Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula ambaye kwa niaba ya Mwenyekiti, aliongoza kikao chake vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii. Nichukue nafasi hii kukupongeza sana wewe na Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana. Muswada huu unapendekeza kuwa na Sheria inayolenga kuwa na utaratibu wa mazishi ya viongozi wa Kitaifa pamoja na utaratibu maalum wa namna ya kushughulikia mazishi ya viongozi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hajjawahi kuwa na mfumo rasmi wa kushughulikia kifo cha kiongozi kinapotokea. Uzoefu uliotokana na mazishi ya viongozi wetu wa Kitaifa wakiwemo aliyejewa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine, mwaka 1984; Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mwaka 1999 na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Omar Ali Juma, mwaka 2002 umeonyesha matatizo mbalimbali yakiwemo kutokuwa tayari na hivyo kusababisha kuchukua muda mrefu kufanya maamuzi ya Wajumbe wanaostahili kuunda Kamati. Pia mahali na taratibu za mazishi na utaratibu wa kupata fedha haraka ili kuweza kushughulikia mazishi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfumo rasmi unaopendekezwa na Muswada huu wa Sheria utaliwezesha Taifa kujenga uwezo na kuwa tayari wakati wote kuweza kufanya mazishi ya viongozi wake kwa mujibu wa taratibu tutakazojiveke. Aidha, utaratibu huu utawezesha kuwa na vifaa, vitendea kazi, miundombinu na huduma bora kukidhi mahitaji ya shughuli za aina hii kwa haraka bila kuathiri utendaji wa shughuli zingine za Serikali. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza yenye ibara ya kwanza mpaka ya tatu. Sehemu hii inapendekeza mambo ya awali ambayo yanajumuisha jina la sheria itakayopendekezwa, tarehe ya kuanza kwa sheria, matumizi ya sheria na tafsiri ya msamiati uliotumika katika sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ina ibara ya nne mpaka ya sita. Sehemu hii inapendekeza masharti ya ujumla kuhusu utaratibu wa mazishi, viongozi wanaohusika na utaratibu wa mazishi chini ya sheria hii ambaeo ni viongozi wa Kitaifa na Viongozi Maalum. Imefafanuliwa kuwa viongozi wa Kitaifa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Waziri Mkuu. Viongozi Maalum ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jaji Mkuu. Viongozi hao watajumuisha wale wote waliostaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii imebainisha pia aina na taratibu za mazishi ambazo zitatumika kwa viongozi kutegemeana na nyadhifa zao. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyejewa madarakani na aliystaafu wanastahili mazishi ya Kitaifa yaani *State Funeral* wakati viongozi wengine walijotajwa na sheria wanastahili mazishi ya Kiserikali. Sehemu ya tatu ina ibara ya saba mpaka ya kumi na moja. Sehemu hii inapendekeza kuundwa kwa Kamati mbili za mazishi na majukumu ya Kamati hizo.

Chini ya mapendekezo haya, kutakuwepo na Kamati ya Kitaifa ya Mazishi ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Waziri Mkuu na Kamati ya Utendaji ambayo itaongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi. Kamati ya Utendaji itatekeleza majukumu yake kama yatakavyopendekezwa na Kamati ya Taifa ya Mazishi. Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anapendekezwa kuwa Katibu wa Kamati zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne, Ibara ya 12 mpaka ya 24. Sehemu hii inapendekeza utaratibu mzima wa mazishi ya viongozi katika ngazi mbalimbali. Aidha, sehemu hii imetoa utaratibu wa kutoa tamko rasmi la kifo cha kiongozi. Matumizi ya bendera na gwaride maalum wakati wa mazishi na mahali pa kuzika. Sehemu hii inaonyesha kuwa Rais ndiye anayehusika kutoa tamko la kifo kwa viongozi wote wa Kitaifa. Mazingira mbalimbali yamezingatiwa ili jukumu hili liweze kutekelezwa iwapo Mheshimiwa Rais hatakuwepo nchini au vinginevyo. Sehemu hii pia inapendekeza kuwa eneo la makaburi kwa ajili ya viongozi wa kitaifa litakuwa Dodoma. Aidha, kiongozi ambaye hatazikwa Dodoma kutokana na wosia au jinsi kifo kilivyotokea, mnara wa kumbukumbu yake utajengwa katika eneo la makaburi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii pia imeweka wazi kuwa mazishi ya viongozi hao yatazingatia mila, desturi, dini na wosia utakaothibitishwa kuachwa na kiongozi husika. Sehemu ya tano ina Ibara ya 25 hadi 29. Sehemu hii inahusu mambo mengine ya kijumla yakiwemo fedha zitakazotumika kugharamia mazishi ya Kitaifa, adhabu kwa kukiuka matakwa ya sheria hii na kupendekeza madaraka ya Waziri kutunga kanuni zitakazowezesha utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba sasa kuwasilisha rasmi Muswada wa Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa wa mwaka 2006 pamoja na jedwali la marekebisho ya Muswada kwa ajili ya kusomwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu kwanza kuwasilisha maoni ya Kamati Bungeni, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kuwa Makamu wa Rais.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu na kuthibitishwa na Bunge kwa kura nyingi. Aidha, napenda nichukue fursa hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Anne Makinda kuwa Naibu Spika. (*Makofî*)

Tatu, napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuwatumikia wananchi kwa kipindi hiki cha miaka mitano. Hali kadhalika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata nyadhifa za kuwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wakuu wa Mikoa katika kipindi hiki. Vile vile nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpwapwa kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao na nawaahidi kuwatumikia kwa uadilifu na uaminifu mkubwa kwa uwezo wangu wote kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. Aidha, natumia fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wao katika kipindi hiki. Naahidi kushirikiana nao kikamilifu katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni ya Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa wa mwaka 2006. Baada ya Muswada kuletwa kwenye Kamati, Kamati ilikutana tarehe 13 mwezi wa pili mwaka 2006 mjini Dodoma kuupitia Muswada huu. Katika kikao chake, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu azma yake ya kuleta mapendekezo ya Muswada wa Sheria hiyo kama ilivyoelezwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo ya Serikali, Kamati ilikuwa na maoni na mapendekezo kadhaa katika maeneo mbalimbali. Aidha, pale ambapo Kamati haikuelewa vema maudhui ya Muswada huo tuliomba kupewa ufanuzi, Serikali ilijitahidi kutoa majibu ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na yale ya jumla, ni kwamba Kamati inauona Muswada huu ni mzuri. Hata hivyo pamoja na kuwa mapendekezo ya Sheria yanakusudia kuwahuishwa viongozi waliopo sasa, Kamati inashauri kuwa ni vema pia Sheria hii ingeweka kumbukumbu za waasisi wa Taifa letu, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Aman Karume katika kuuthamini mchango wao mkubwa ambao wameutoa katika Taifa hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa waasisi hawa walizikwa maeneo mengine, Kamati inashauri kuwa uwepo utaratibu wa kuweka minara ya kumbukumbu zao katika eneo la Dodoma iliyokusudiwa kwa ajili ya mazishi ya viongozi wa Kitaifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la Dodoma, Kamati inashauri kuwa Muswada huu uweke kifungu kitakachowatoa viongozi wakuu wa Kitaifa kutoka Zanzibar waliotajwa katika Muswada huu wasiwe mionganoni mwa viongozi wakuu watakaolazimika kuzikwa Dodoma. Kamati imezingatia kwamba mbali ya Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia ina Serikali yake. Hivyo, imeona ni busara wasilazimike kuzikwa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la jumla linahusu suala zima la mazishi ya viongozi kwa kuzingatia itikadi na imani zao za kidini. Kamati hii inaona kuwa Kamati ya Kitaifa ya Mazishi kama ilivyoelezwa katika sehemu ya tatu ya Muswada haina uwakilishi wa viongozi wa kidini, jambo ambalo Kamati inadhani kuwa inaweza kuleta

utata wakati wa mazishi kwa kuzingatia imani na dini ya kiongozi anayehusika. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa ni vema utaratibu ufanywe ili viongozi wa dini wahusishwe kwa namna moja au nyingine kila inapobidi na Muswada utamke wazi kuwepo kwa wawakilishi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 7 ya Muswada unatamka kuwepo kwa Kamati ya Taifa ya Mazishi, Kamati imeona kuwa idadi ya Wajumbe wa Kamati ya Taifa ya Mazishi ni kubwa mno. Hivyo, inashauri kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza baadhi ya Wajumbe walijotajwa katika Kamati hii. Zaidi ya hayo Kamati inashauri kwamba uwakilishi wa Wajumbe kutoka Zanzibar uongezwe kwa idadi itakayoonekana inafaa badala ya kuwa na Wajumbe watatu kama ilivyotajwa katika ibara hiyo. Kuhusu Ibara ya 9(3)(A) Kamati inashauri kuwa neno *approve* liondolewe na badala yake lisomeke neno *endorsed*. Kamati inapendekeza hivyo kwa kuwa jukumu la kuidhinisha bajeti si la Kamati ya Utendaji kwani tayari kuna chombo kilichopewa kazi hiyo. Kuhusu suala la fedha za mazishi ya viongozi kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, Kamati iliyohoji juu ya sababu za msingi inazofanya mazishi haya yagharamiwe kutoka Mfuko huu. Wasi wasi wa Kamati unatokana na uzoefu kwamba mfuko huo huwa haukaguliwi. Hivyo Kamati iliona kuwa kufanya hivyo kunaweza kutoa mwanya wa matumizi mabaya ya fedha za mazishi kwa baadhi ya Watendaji watakaohusika. (*Makofi*)

Pamoja na ufanuzi uliotolewa Serikali kuhusu suala hili, Kamati yangu inashauri kuwa kuwepo na kiwango maalum kitakachotengwa kwa ajili ya kugharamia shughuli ya mazishi ya viongozi hao. Maeneo mengine yalihusu ushauri wa Kamati katika Muswada katika masuala machache yaliyohusiana na uandishi wa Muswada ambayo Serikali iliahidi kuyafanya kazi. Kwa ujumla haya ndiyo maeneo ambayo Kamati yangu iliyatolea maoni na mapendekezo. Natumaini kuwa yale ambayo hayakuguswa, Wajumbe wa Kamati yangu watachangia pindi watakapopata fursa ya kuchangia. Napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kuwasilisha maoni ya Kamati. Pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Juma Akukweti, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge na Uratibu kwa kuwasilisha vema maelezo ya Serikali mbele ya Kamati yangu. Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Manajimenti na Utumishi wa Umma, kwa kushirikiana na Mtoa Hoja pamoja na Wasaidizi wake.

Mwisho, nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa michango yao mizuri iliyoboresha Muswada kufikia hatua iliyopo hivi sasa. Ushahidi wa kuwepo kwa Jedwali na marekebisho ni matokeo ya kazi hiyo nzuri. Ninaomba niwatambue Wajumbe wa Kamati yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti. Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Hazara P. Chana, Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athuman S. Janguo, Mheshimiwa Rajab Ahmad Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbiri, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa

Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Dr. Ferdinand S. Mpanda, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa na Mheshimiwa Salim Yusuf Mohamed. (*Makofi*)

Aidha, Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Charles Mloka, Ernest Zulu na Athuman Hussein kwa kuihudumia vema Kamati hii na kutayarisha maoni kwa wakati muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naiunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (k.n.y. MSEMAJI WA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kutoa maoni kuhusu Muswada uliotajwa hapo juu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa Muswada huu kwa viongozi wakuu wa Taifa letu na hasa katika uzito kwenye sura ya ulimwengu, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa hata viongozi wakuu wa Vyama vyta Siasa kwa maana ya Mwenyekiti, Makamu na Katibu Mkuu wake nao wangeweza kuingizwa kwenye Sheria hii ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa. (*Makofi*)

Hivyo basi Ibara ya 2(1) ifanyiwe marekebisho na kuongeza mapendekezo yetu. Kifungu cha kwanza kinachosema viongozi wa Kitaifa, Muswada hauonyeshi ni wapi Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wale waliomtangulia wanapopewa heshima kama wanavyopewa viongozi wengine wa Kitaifa waliopo na wale waliokwishastaa fu pamoja na Spika wa Baraza la Wawakilishi. Kambi ya Upinzani inashauri kabla ya Bunge lako Tukufu kuitisha Sheria ni bora marekebisho haya yawe bayana ili kuondoa manung'uniko yanayoweza kujitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uanzishwaji wa Kamati ya Kitaifa ya Mazishi kama inavyosomeka katika kifungu cha 3(2) inaundwa na Wajumbe 16, Mawaziri na wengine wakubwa katika Serikali. Kwa mtazamo wetu ukubwa wa Kamati siyo uzuri wa utendaji. Hivyo basi Kamati hiyo inatakiwa kuwa na Wajumbe wasiozidi watano chini ya Uwenyekiti wa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Hii vile vile itapunguza baadhi ya matumizi yasiyo ya lazima kwa Serikali. Kama nilivyosema hapo juu wingi wa Wajumbe siyo utendaji. Suala la muhimu ni uwajibikaji. Hivyo basi hii Kamati Tendaji (*Executive Committee*) inatakiwa nayo iwe na Wajumbe wasiozidi watano. Kambi ya Upinzani imetoa ushauri huo kwa kuzingatia wingi wa watendaji inawezekana kabisa kuwa wakatumia robo tatu ya mazishi kabla ya mazishi yenye. Suala la msingi zaidi katika hili ni kuongeza tija na nidhamu ya matumizi ya fedha za walipa kodi. Katika Ibara ya 25(1) inayosema kuwa fedha zote zitakazotumika

kwenye msiba wa Kitaifa zitatoka katika *Consolidated Fund* ninavyoilewa mimi mfuko huu hauna Mkaguzi wa Mahesabu hivyo uwezekano wa matumizi mabaya kutokana na idadi ya washiriki ni mkubwa mno. Kambi ya Upinzani inashauri fedha zote zitakazotumika katika msiba wa Kitaifa zitoke katika Ofisi ya Waziri Mkuu au Ofisi ya Waziri Kiongozi, hii itatoa nafasi kwa Mkaguzi wa Hesabu kufanya kazi yake. Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Sheria hii aweke utaratibu wa Kanuni ya Sheria hii kwani hakuna kipengele kinachozungumzia ni VIP familia za marehemu zitakavyoishi kwani tumeshuhudia familia za baadhi ya viongozi wetu zikiwa omnia omnia na zingine kutimuliwa katika nyumba na kunyang'anywa vitu. Mifano hai ipo na inaeleweka kwa viongozi wetu. Kwa kuwa nchi yetu ina watu wa dini tofauti na kimsingi hawa viongozi wetu ni wafiasi wa dini hizo. Tunashauri hilo eneo lililotengwa lioneshe maeneo ya maziko kwa dini tofauti wala si madhehebu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maoni yetu, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja. Nashukuru sana. (*Makofî*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kwanza kuchangia Muswada huu. Mimi nakubaliana kabisa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, lakini nina suala kidogo la nyongeza. Kamati zote zinazoshughulika na mazishi sijaona kabisa familia ikiwa inahusishwa, hamna mjumbe yoyote kutoka katika familia ya marehemu. Naamini hata akiwa kiongozi wa Serikali huwa anatokana na familia. Kwa hiyo, nilikuwa nategemea kabisa kwamba *at least* mmoja au wawili *members* wa familia ya marehemu wangehusishwa katika Kamati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye *file*, kifungu namba 25(t) kuna suala la ndugu la marehemu. Kamati itashughulikia kuwasafirisha ndugu wa marehemu lakini hajasema idadi na tunajua Watanzania wengi tuna-*extended families*. Sasa tunauliza je, ni wote? Ni 100, ni 20 au watano? Kwa hiyo tulikuwa tunaomba ufanuzi, ahsante. (*Makofî*)

MHE. PHARES K. KABUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ninayo maneno machache ya kusema juu ya Muswada huu. Kwanza nilipokuwa nausoma nilikuwa najiuliza hivi kweli *priority* ya Watanzania ndio hii na hii ndiyo kasi mpya? Kweli ndilo hitaji la kwanza la Mheshimiwa Rais wetu kuanza nalo? Kwanza kwa kuwa tumeanza na mabalaa, tumeanza na njaa halafu tena tunaanza na Muswada wa kuzika wenzetu. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri yalikuwepo mengi ya kufanya lakini kwa kuwa Muswada umeshakuja

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa nadhani hausomi.

MHE. PHARES K. KABUYE: Kwa kuwa Muswada umeshakuja, hatuna la kufanya. Lakini hata hivyo naomba niseme hivi, sisi Watanzania kwa kawaida mtu huwa ni mtu wa ukoo, huwa ni mtu wa kabilo. Sasa tunaposema wewe nenda uwe kiongozi si

kwamba tumekutoa kabisa bado ni mtu wetu hata unapokufa na maiti ni yetu. Mimi nikiwa mtoto nilikuwa naambiwa mtu akiwa Padre tunaanza kufanya matanga kwa sababu atakwenda huko na akifa anazikwa huko hatumuoni tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kufanya hivyo Rais amepewa kazi ana ukoo, ana kabilia, ana jamaa kazi inapokuwa imeisha bado anarudi ni mali ya hao watu, lakini sasa akishakuwa Rais basi hata maiti si ya hao watu na wala siyo ya Watanzania. Kwa kweli nadhani si maudhui ya Watanzania ni mambo ya kuigaiga hatuna hilo katika Tanzania, sijalionia katika kabilia lolote lile na kama ni mambo ya kuiga tusingeiga hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba niseme jambo zuri, Dodoma tangu tuamue kuwa Makao Makuu Serikali haijahamia Dodoma, sasa Dodoma itakuwa ni Makao Makuu ya Bunge pamoja na makaburi ya viongozi. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunakimbilia hili, hivi ni kero? Kama ni kero inamkera nani? Kwa nini kero lisiwe ni kuhamia Dodoma ili Dodoma ikawa ni Makao Makuu Ikulu ikaja na Wizara zote. Sasa Dodoma imekuwa ni Makao Makuu ya Bunge pamoja na makaburi ya Waheshimiwa. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina tatizo na idadi ya wazikaji lakini nina tatizo kwa nini wawe ni wataalam na Mawaziri tu, kwa nini wananchi wengine maarufu kama hawa wanaokufa wana viongozi wa kabilia kwa nini asisemwe yaani wanazikwa na Mawaziri na wataalam. Kule ni kutaka hata mtu asije, akishakuwa huko utasikia amefia London anatoka London anakwenda Uwanja wa Kimataifa akitoka huko anaenda Dodoma. Angekuwa Msibi mngepata taabu kwa sababu sisi Msibi akifa hawezি kwenda kuzikwa mpaka kwanza aje aage nyumba yake akae kwenye kitanda akaage nyumba, lakini akifia Ujerumanu anakwenda Uwanja wa Taifa anatoka huko anakuja kwenye makaburi Dodoma, mimi nadhani tuangalie mila na desturi za watu (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna kuzuru makaburi huwa watu wana desturi zao kwamba wanatoa heshima kwa makaburi kwa kipindi fulani. Sasa niambieni huyu kiongozi kama alikuwa Musoma jamaa zake wataletwa na nani kila mwaka au kwa kipindi chao kuja kutoa heshima kwenye makaburi hapa Dodoma, nani atagharamia hiyo gharama? Naomba hayo myuaangalie. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika *combination* ya hawa wanaozika, mimi naona madhehebu ya dini yetu tuliyonayo makubwa sana ni mawili Wakristo na Waislamu. Wangetamkwa wakawa mionganoni mwa hii Kamati kwamba kifo cha kiongozi ni janga kwa hiyo janga linapotokea basi watu wa aina fulani waungane na Kamati siyo unakuja tu hapa, wewe Sheikh fulani utakuja kusalia maiti, wewe Askofu fulani utakuja kuombea. Ningemba Kamati iungane na viongozi wa dini kama ni mmoja kila dhehebu ili matatizo yatakopokuwa yanatokea tusiwe na haja ya kuhangai ka hangaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo kwa upande wangu yalikuwa ni maoni kwa hiyo ningemba yazingatiwe. Naunga hoja mkono. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano kidogo nataka niutoe, sasa sijui ule ulikuwa umeshaingia katika mambo ya Kitaifa au baada ya kuonekana makosa yale ndio ukatungwa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nime-experience kidogo mazishi mawili katika Tanzania yaliyotokea. Mazishi ya kwanza ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere na mazishi ya pili ni ya marehemu Dr. Omar Ally Juma. Mazishi haya yote mawili kwangu mimi nimeona yamekuwa na desturi moja ambazo si sahihi na siku nyingine desturi hii imekuja baada ya kukabidhiwa Kamati ya Mazishi ya Kitaifa. Sasa kwa Kamati hii tunayotaka kuiunda hivi sasa pamoja na mambo mengine watakayoyazingatia basi na desturi nayo ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia kuhusu kaburi, kaburi alilozikwa marehemu Baba wa Taifa aliteremshwa kwa ngazi, lile kaburi jeneza lake lilifungwa kwa kamba na wapokeaji walikuwa chini unawaona lakini mbali kidogo.

Sasa kwangu mimi nilihisi kwamba labda kwa upande ule ilikuwa ni desturi yake lakini tulipokwenda kwa marehemu Dr. Omar Ally Juma halikadhalika mambo yalikuwa yale yale. Sasa hapa pana desturi kwa sababu kwa sisi Waislamu kaburi uteremke wa ngazi bado hatujaona mambo kama hayo sasa labda tuje tuambiwe nini sababu yake? Tunaogopa mbwa asiingie wasifukue, tembo labda akija asifukue kaburi hili au wanyama gani?

Sasa kwa kwetu sisi Zanzibar makaburi tumezoea ya kawaida sana, sasa kama kuna kifungu kinachozungumza hivyo basi labda tuje tufahamishwe lakini ninachozungumzia desturi lazima zifuatwe hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni sehemu ya kuzikiana Kitaifa imeamuriwa Dodoma, tuna viongozi wa Kitaifa mbalimbali lakini kwenye Muswada huu ukiupitia sana utaona kwamba kuna kipengele kinasema watu wa familia ya marehemu wanaweza wakaamua asizikwe katika makaburi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ulikuwepo katika viongozi wa Kitaifa tulionao, waliopita na watakaokuja hakuna hata mmoja ambaye atakuwa hana kwao na familia hii mara nyingine haitakuwa tayari kumuondosha mtu kwao akazikwe kwingine. Sasa kipengele hiki kinanitia wasiwasi makaburi haya yatakuwa hayapo, labda kiongozi wa Kitaifa atokee Dodoma. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu ameshapewa nafasi ya kuchagua wapi pa kuzikwa, mtu wa Shinyanga, Mwanza, Tabora mathalani atokee kiongozi wa Taifa katika sehemu hizo basi familia haitakubali achukuliwe kutoka Tabora aletwe Dodoma haiwezakani, kwa sababu kwanza kutakuwa na mtiririko mzima wa masafa na tabu ya kuja kuangalia kaburi lile. Sasa sijui waandaaji wa Muswada huu walikuwa wanadhamiria nini? Lakini hapa patakuwa na matatizo makubwa ya makaburi haya

kuwapo kama alivyozungumza mzungumzaji aliyepita kwamba Makao Makuu yatakuwa Dodoma basi na makaburi ya Taifa yatahamia Dodoma nahisi kutakuwa hakuna hata moja atakayezikwa hapa labda kiongozi atoke Dodoma. Sasa kipengele hiki hakina faida kama tunaamua kuweka makaburi ya Taifa Dodoma kipengele hiki tusikiweke kwa sababu hata mimi sikubali baba yangu kama Rais au Makamu wa Rais nimtoe kwetu nimlete Dodoma hiyo haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini linginge ni suala la viongozi wa kidini ambao wametakiwa kupewa nafasi ya kuingia katika Kamati. Kwangu mie uundwaji wa Kamati ya Mazishi ya Kitaifa imejitosheleza. Imejitosheleza kwa sababu ndani ya Kamati ile ndimo atakapokuwa anatafutwa Padre anayefaa kwa dini ya mtu aliyekufa, ndipo atakapotafutwa Sheikh anayefaa kwa mtu aliyekufa. Sasa hatuna haja sasa hivi ya kuingiza tena Padre na nani katika Kamati ile, Kamati iachiwe ifanye kazi yake wakati ukifika wao wataamua nani anafaa kuingia katika sehemu ile ya maiti muhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho katika mchango huu ni suala la sehemu mbili za mazishi ya Kitaifa kwa sababu tunazungumzia viongozi wa Kitaifa na tumo ndani ya Tanzania. Kule Zanzibar basi kama tunaamua kuwa sehemu ya viongozi wa Kitaifa tuseme basi viongozi wa Kitaifa Zanzibar watazikwa wapi ndani ya Jamhuri ya Muungano. Kwa sababu ninachokifahamu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wanao utaratibu wao wa mazishi ya Kitaifa kwa viongozi wa Zanzibar lakini kuna viongozi wa Zanzibar wamo ndani ya Jamhuri ya Muungano sasa hawa wanaowekewa utaratibu wao wapi hawa wazikwe? Ndio ninarudi kule kule hatuwezi tukawa na Makamu wa Rais yuko Zanzibar akaletwa Dodoma haiwezekani, haiwezekani hata siku moja. Sasa basi Muswada utamke kwamba Zanzibar kwa viongozi wa Kitaifa makaburi yake yatakuwepo wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. CHACHA Z. WANGWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuchangia Muswada huu. Kwa kweli mimi mengi ambayo nilitaka kuyasema naona yamesemwa na wenzangu lakini naungana nao hasa Mheshimiwa Phares Kabuye kwa sababu ninaona cha kuzingatia zaidi hapa ni kujifahamu ya kwamba sisi ni nani, tunatoka wapi na tuko wapi? Ninaamini kwamba sisi bado ni Waafrika sana na hatuna nafasi ya kuweza kubadili mila na desturi za mababu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nkinukuu kipengele cha 16 cha Muswada huu. Hiki kinakinzana na dhana yote ambayo imependekezwa hapa yaani ni *self contradictory* kabisa. Kinasema, *the funeral rites of the national leader or specified leader shall be conducted according to the religion, custom and traditions of the deceased depending on the cause of death.* Kwa hiyo, hiyo inaonyesha kabisa kwamba huu Muswada hauna mahitaji wala umuhimu kwa wakati huu. Pengine baada ya karne kadhaa basi watakuja kufanya wanavyotaka kwa sababu tukichukua mfano wa marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere yeye nasikia alikataa makusudi kabisa hata kwa kuulizwa akasema mimi nataka nizikwe nyumbani. Kwa kweli ukienda pale Butiama utaona panapendeza hata wale wananchi wa pale waliomzaa na kumkuza basi inawapa faraja na moyo kwamba nao vile vile walikuwa na mpiganaji ambaye anakumbukwa. Wengi wanatoka hata nchi za nje wanakwenda mpaka pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo suala la kujenga sehemu ya kuwazika viongozi, kwa Ulaya kwa sababu kwanza wana matatizo ya *space* na vile vile *orientation* ya kijamii ni kama imeshapotea nadhani kwao ni sawa, lakini kwetu sisi naona kila mtu aendelee kuzikwa nyumbani kwake. Kwa watu wao na kawaida ya Waafrika siku hizi wanaanda kabisa sehemu na hata unapokuwa unakuja Bungeni unawaambia kwamba kama kutatokea tatizo mimi mahali pa kuzikwa ni pale, wanakaa wakijua. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama mtu atatolewa nyumbani kwao aje kuzikwa Dodoma, kwa mifano iliyopo sasa hivi watu wa Afrika ya Kusini wenye asili ya Kiafrika wamekuwa na mahusiano na Wazungu kwa zaidi ya miaka 400 sasa, lakini sasa hivi kuna mgogoro mkubwa unaendelea ambapo kiongozi wa zamani ambaye ndio baba yake Rais wa Taifa lile marehemu Govan Mbeki marehemu anataka kuondolewa pale alipozikwa akazikwe kwenye eneo kama hili tunalopendekeza, lakini kuna mgogoro tayari na unaelekea Mahakamani familia yake hawataki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kenya bado kuna mgogoro. Wengine wanadai kwamba ule mwili wa Hayati Kenyatta bado upo barabarani. Kwa hiyo mila za Kiafrika ni zile zile na nadhani kwamba kitu ambacho ningeweza kukubaliana nacho hapo ni kusema kuwe na sehemu ya kujenga minara ya kumbukumbu kwamba aliquwepo kiongozi wa aina hiyo na maelezo yake pale, kama itakuwa ni *museum*. Lakini tutakuwa tunapingana na tunavuruga kabisa mila na desturi za Kiafrika kwa kusema ya kwamba watu wasizikwe makwao eti kwa sababu walikuwa viongozi. Vinginevyo pengine tungefanya *a national referendum* tuwaulize na wananchi nao tusikie wanasesmaje kwa sababu nao wana haki ya kuchangia haya mawazo kabla hatujapitisha huu Muswada. Mimi siungi hoja hii. (*Makofit*)

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, naomba kwa kifupi na mimi pia nichangie kama wenzangu. Kwa kweli nashukuru sana, kwa Serikali kufikiria kuleta Muswada huu ambao ni Muswada muhimu isipokuwa kitu cha kusikitisha umechelewa sana, kwani tumekwishazika viongozi wanne nchini maeneo mbalimbali kabla Serikali haijaamua, lakini hata hivyo mimi nakubaliana na wengi waliozungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ninaelewa sana umuhimu wa mtu kuwa na mtu wake au maiti yake karibu na nyumbani, ndio maana makabila mengine wanazika mbele ya nyumba au kwenye mashamba yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka watu wengine walipiga kelele kuwa Mheshimiwa Baba yetu wa Taifa alipofariki azikwe Dar es Salaam, lakini walikaa na kukutana na viongozi wakamua kuwa yeye mwenyewe alikuwa ammeamua azikwe Butiamu na ikafuatiwa na Serikali. Mimi sipingani na hilo na ninakubaliana nalo kabisa. Vile vile naomba tukumbuke kuwa kuzikwa kwa pamoja ndugu zangu kuna umuhimu wake, kuna umuhimu wa utambulizi ili kutambua viongozi wetu lakini pia kuna umuhimu wa kuwakaribisha wageni waende sehemu moja, makaburi yote yakiwa kwa pamoja likatengwa eneo kubwa la *heroes acre* pia siyo mbaya. Lakini jambo muhimu kwanza ni familia kukubali jambo hilo. Familia nyingine wanaweza wakakubali lakini familia nyingine wakakataa tunawenza tukaheshimu uamuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tukumbuke ndugu zangu ni kwamba tunazungumzia mashujaa, wetu tunazungumzia viongozi wetu kwa sasa, labda ingefaa pia tukawafikiria wale mashujaa wetu ambao ni mashujaa wengi wengine ambao walikuwa Kaboba wakati wa Nduli Idd Amini wamezikwa huko huko. Najua kuna wakati wanakumbukwa, lakini pia siyo mbaya majina yao yakawepo katika hii *heroes acre* sehemu mojawapo ambayo najua kwa mwaka wa 1975 eneo hilo kubwa lilikuwa tayari limetengwa Dodoma sehemu ya Isanga, Mlima wa Isanga hapa Dodoma. Naomba tuwakumbuke mashujaa wengine ambao walikuwepo ma-Chief wetu muhimu kabisa wa zamani wakina Chief Mirambo, Chief Mkwawa wakina Omukama Mtatembwa na wengine wengi ambao tunajua walifanya kazi ngumu, wamepigana na Wakoloni lakini pia wamepigana na Mataifa mengine kutoka nchi za jirani. Mimi naomba hao nao wakumbukwe kwani ni muhimu sana, wakumbukwe angalau majina yao yawekwe katika eneo hilo ambalo litakuwa na mazishi ya viongozi. Kwa sababu wao walikuwa ni viongozi wetu kabla hatujapata Uhuru, wao walikuwa ni viongozi wetu kama Marais, kama Mawaziri Wakuu na kadhalika kwa hiyo tuweke umuhimu sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nimeona ni lazima nilizungumzie ni kwamba tuwakumbuke wanawake viongozi wa zamani waliopita tusiwasahau. Wakati tulipopigania Uhuru kuna wanawake ambao wamekwishafariki na wenyewe wakumbukwe angalau hata kama miili yao haikuwekwa pale lakini minara yao iwekwe kuwe na utambuzi wao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia siyo viongozi wanawake peke yao lakini tukumbuke hata wanawake ambao walikuwa wake wa viongozi na wanawake ambao walikuwa wakipigania, wakisaidiana na waume zao wakati wa mapigano hayo ya kivita au ya ukombozi. Mfano mmoja mzuri niliokuwa nao ni wa ndugu marehemu mama Sally Mugabe ambaye alipigana na mume wake alikaa Tanzania mpaka akazaa mtoto Tanzania kwa bahati mbaya mtoto yule akaja kufarikia alipokuwa *West Africa*, alirudi akaishi na mume wake na huko Harare amezikwa *heroes acre* kwa utambuzi wa kazi alizofanya akiwa katika kupigania Uhuru yeche na mume wake. Kwa hivyo basi wanawake wa aina hiyo ambao watakuwa walipigana pamoja na waume zao angalau majina yao yatambuliwe au minara yao iwekwe ikumbukwe.

Ndugu zangu sikupenda kutumia muda mrefu sana, nilitaka maeneo hayo tuyazingatie na tuyakumbuke lakini mimi ninaafiki kabisa tena kwa asilimia mia moja kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwa na eneo la maziko kwa viongozi wetu, ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU(MHE. JUMA J. AKUKWETI): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza ningependa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameshiriki katika mjadala huu, awali ya yote ningependa tu niseme wakati nilipopewa kazi ya kuwasilisha Muswada huu yuko rafiki yangu mmoja akanifuata akasema umepewa Muswada wa uchuro, nikamwambia hapana hiyo ni imani tu mtu ana imani yake. Makabila mengi watu wengi wanajiandalia namna ya kuzikwa wengine wanajinunulia sanda anaweka, wengine wanajichongea sanduku huu si uchuro ni utaratibu wa maisha ya binadamu kwa sababu wote tunajua tumezaliwa na wote lazima siku moja Mwenyezi Mungu atatuita huko ambako tumetoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia naomba kwanza niwataje kwanza Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa George Lubereje ninamshukuru sana, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Hafidh Tahir, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Janet Kahama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote hawa wametoa mapendekezo mazuri, mawazo mazuri na kwa kweli niliyapokea mengi kutoka kwenye kamati ile na nia yao nadhani wote ilikuwa ni kuboresha namna nzuri ya kuweka haya mambo sawasawa. Siamini kwamba katika mmojawapo yoyote katika hapa alikuwa ana nia ya kupoteza historia ya Taifa letu. Taifa lisilo na historia haliwezi kwenda vizuri, Taifa lina historia katika hiyo historia ni historia ya watu, watu mbambali, watu maarufu kwa hiyo lazima mjiwekee utaratibu wa kuwa na historia ambayo baadaye katika karne na vizazi vijavyo wanaweza wakafuata historia yetu kwa urahisi. Yale ambayo yamesemwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani mmoja alisema viongozi wa kidini washirikishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo mara ya kwanza tunazika viongozi wetu kama alivyosema Mheshimiwa Hafidh Tahir alishuhudia mazishi tukiyafanya katika maeneo mbalimbali baada ya kuondokewa na viongozi wetu na wakati wote huu tulishirikisha

viongozi wa dini, kwa wale ambao wanakumbuka mazishi kwa mfano ya hivi karibuni ya marehemu Mheshimiwa Dr. Omar Ally Juma kule Pemba mimi nilijaliwa kuwepo wote tulishuhudia kwamba wale wanajeshi pamoja na mizinga na mbwembwe zote za kijesha lakini inapofika kwenye shughuli za kidini waliwaachia Mashekhe na Maimamu waendeshe taratibu zote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hiyo ndiyo taratibu inayofuatwa kwa hiyo kila wakati viongozi wa kidini wanahusishwa na wataendelea kuhusishwa.

Kamati hii iliyosemwa hapa ni ile ya Kitaifa inayosimamia Kitaifa lakini Muswada huu umetambua viliyyo kwamba utafuata mila, desturi na dini. Kwa hiyo, viongozi wa dini ile watashirikishwa na hakuna litakalo haribika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wajumbe kuwa wengi, hii mara zote inakuwa dharura, mmepata msiba mnahitaji kuzika. Sasa mkiweka Wajumbe wachache mnawenza kuwaacha wale waliokuwa muhimu kufanya maamuzi ya papo kwa papo. Kwa mfano unamwacha Waziri wa Fedha kwenye Kamati ile na ninyi mnahitaji fedha. Mnamwacha Waziri wa Miundombinu, mnahitaji ujenzi wa namna fulani. Kwa hiyo, hawa wamechaguliwa kwa makini sana kuhakikisha kwamba maamuzi yanafanyika pale na kazi ile inakwenda kwa haraka na kwa wakati. Badala ya kusema tumekwama hapa kamtafute fulani Wizara fulani wote wamewekwa hapa na si kazi ya muda mrefu sana maana kwa kawaida hatuchukui muda mrefu kuzika. Kwa hiyo, ni vizuri hawa wote waliopo wakawepo kwa ajili ya uharaka wa kufanya maazimio.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo lingine limetoka kwa Mwenyekiti wa Kamati wanasema iwekwe kiwango maalum cha fedha. Sasa sijui ni kiasi gani maana leo tunaweza kupata msiba wa kiongozi anayetoka sitaki kutaja mahali lakini tuseme anatoka mbali na Dodoma kwa mfano au amefia mbali sana, namna ya kumleta na yeye aliamua kuzikwa Dodoma matumizi yake yatakuwa tofauti na kiongozi mwengine. Kwa hiyo, ukipanga kwamba lazima utumie kiasi hiki basi unaweza kupata tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu uwoga ambao umejitokeza kwamba kwa sababu Muswada huu unasema pesa zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na ule hauwi *audited*, sio sahihi. Pesa zitatoka pale lakini kule zitakakokwenda kwa matumizi lazima ziwe *audited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *source* ya fedha hizi tupate wapi? Wazo lililoletwa ilikuwa ni kwamba zitoke Ofisi ya Waziri Mkuu. Ofisi ile ina matumizi yake na bajeti yake kwa mwaka ule, jambo hili tumepata la dharura ukizikata pale sasa Serikali katika maeneo yale itakwendaje? Ndio maana tumefikiri ni vema pesa hizi zitoke mfuko ule. Lakini nataka kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba pesa zile zikitumika zitakuwa *audited* kama pesa nyingine zote za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani ameleta wazo jipya kwamba katika ile orodha ya viongozi kama nilimsikia vizuri anasema na Wenyeviti wa

Vyama wajumuishwe, sijui kama nimemsikia vizuri. Maana nina mashaka kama nimemsikia vizuri kwa sababu siamini kama amesema hivyo, ndio maana nina mashaka. Kwa sababu vyama vinaanzishwa leo kesho kinaanzishwa kingine na inawezekana mtu akaamua nizikwe Dodoma kwa utaratibu ule naanzisha chama kesho basi huendi kwenye uchaguzi unangoja ukifa uzikwe Dodoma kwenye makaburi ya Kitaifa, hii haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli waliolengwa katika Muswada huu ni wale viongozi wetu wa Kitaifa ambao ni kweli wanaweza kuwa Wenyeviti wa Vyama vyao lakini amepita kwa wananchi wamemchagua kuwa kiongozi wa Taifa lao. Kwa hiyo, yule ndiye anayejumuishwa katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ye ye pia amezungumzia ukubwa wa Kamati, nadhani hili nimelijibu. Kuhusu mashaka yake ya kutoka fedha kwenye *Consolidated Fund* nadhani hilo nimelijibu kwamba zitakuwa *audited* bila mashaka yote.

Mheshimiwa Susana Lyimo, ye ye anawaza kwamba ni vizuri wana familia wakashirikishwa. Hili ni kweli lakini sio kwenye Kamati ya Mazishi. Watakuwa karibukaribu haiwezekani wa kwao umzike bila familia kuwa *around* ni kama wale viongozi wa dini, hawa watashirikishwa. Ni kweli ni mzazi wao, mjomba wao, shangazi yao, baba yao, kwa hiyo hawa watashirikishwa kwa namna Fulani. Lakini ile Kamati ya Kitaifa, Kamati inayosimamia mazishi Kiserikali, Kitaifa lazima wawe watu wa Serikali na uzoefu umetuonyesha kwamba hawa wanashauriwa mara kwa mara na Muswada huu hauwaondoi kupata ushauri kutoka kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya ushauri ni kwamba wametajwa hapa kwamba ule wosia ambaa atauandika yule kiongozi kabla hajafa utawasilishwa na wana familia kwamba baba yetu, mjomba wetu, shangazi yetu aliandika wosia huu kwamba anapenda kuzikwa sehemu fulani. Kwa hiyo, huu ni ushiriki mmojawapo wa kifamilia lakini Watanzania wote ni Waafrika tunajua namna tunavyoguswa tunapopata msiba, wote hawa watahakikisha kwamba hakuna atakayenung'unika atakavyotendewa marehemu wao na kiongozi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Kabuye, sijui niseme nini maana amekuja na *scenario* ya ajabu sana kwamba aah basi Dodoma itakuwa ni makao makuu ya Bunge na makaburi na kwamba mambo mengine yote nyie mmeona la kuanzia ni hili? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tufanyeje, tuliache? Kuliacha haiwezekani maana ni utaratibu. Hii inaonyesha jinsi gani uongozi huu inavyojali wastaifu. Unavyojali viongozi wa Taifa letu na hiyo ndiyo heshima kwamba isije tukahangaika lazima tuweke utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni namna nzuri tumeizoea Watanzania, wazee wetu, wastaifu wetu, viongozi wa Taifa hili tunawaheshimu sana. Kwa hiyo, tunaanzia na hapa

ili tusije tukababaika likitokea anapata mazishi ya heshima, mazishi anayostahili. Huu Muswada umeanza mashauriano muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kabuye, namfahamu vizuri, tumekuwa Bungeni miaka mingi, ana namna yake ya kusema jambo na mojawapo ni hii. Anafahamu kwamba si kweli alichokisema...

WABUNGE FULANI: Mmh! (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU: Lakini ni vizuri akalisema, ni namna ya uhuru wa Bunge na Bunge hili hili limefanya mengi tumeanza kujadili hotuba ya Rais. Kuna Miswada mingine inakuja, lakini huu ni Muswada mmojawapo kuhakikisha kwamba wazee wetu, viongozi wetu wa Taifa hili wanapewa heshima wakiwa hai na katika hali ya umauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kabuye amesema namna ya kushirikisha viongozi wa kikabila. Nadhani alikuwepo wakati tunamzika Mwalimu, aliona kiongozi pale wa kimila, heshima aliyopewa na Muswada huu haukusudii kuwapuuza kabisa hata kidogo. Inaweza kupatikana tabu kidogo katika hilo ambalo alilisema kutegemeana na mila kwamba lazima akaonyeshwe kitanda, akakalishwe pale. Lakini kutakuwa na mjadala mzuri na wale wanaohusika ili kuwe na utaratibu mzuri na kuona kwamba kabilalile au familia ile hainung'uniki. Lakini pia Watanzania wakubali kwamba wamemzika kiongozi wao wa muda mrefu kwa heshima anayostahili.

Mheshimiwa Kabuye pia alizungumzia juu ya kujumuisha Kamati ya Kiongozi wa Kimila kama nilivyosema, anajumuishwa pia kiongozi wa dini lakini katika kutoa ushauri tu, sio ile Kamati yenye ya Kitaifa ya Mazishi.

Mheshimiwa Hafidh Ali anasema ye ye ameshuhudia katika mazishi makaburi yanakuwa marefu mpaka unateremka kwa ngazi. Daah, sasa sijui ni semaje. Humu ndani hatukuweka *standard* ya urefu wa kaburi kwamba kaburi hili liwe hivi na nini. Lakini muwe na uhakika atazikwa kwa kufuata taratibu za dini yake. Kama dini ya Kiislam inasema kaburi ni futi fulani na Sheikh au Mufti akathibitisha kwamba kwa maandiko ya dini hiyo kaburi inakuwa urefu wa kiasi hiki, basi taratibu zitafuatwa bila wasiwasi. Nia ni kumjengea heshima marehemu kiongozi huyo katika hali yoyote ile. Kwa hiyo, hatapelekwa futi 40 chini au futi moja, nadhani kutakuwa na utaratibu wa kawaida wa kuzika.

Suala la kuzikwa kwao, hili limezungumzwa sana, lakini Muswada huu kama mlivyoona Waheshimiwa Wabunge umetoa nafasi zote hizo. Kama ameacha wosia basi atazikwa pale alipoamua mwenyewe marehemu akiwa hai, lakini kama hajaacha wosia basi Taifa litamzika Dodoma, litamzika kwenye makaburi ya Kitaifa. Humu umewekwa utaratibu nani atawakilisha huo wosia maana katika kifo wote tumeshuhudia anawenza kuja mtoto wa kwanza akasema mimi nasema baba azikwe mahali fulani, akaja mtoto wa pili akasema hapana, baba akazikwe sehemu Fulani. Sasa katika hali ya mabishano hayo, itatazamwa wosia na wosia ule utapelekwa pale kwenye Kamati kwa utaratibu na

utaletwa na yule ambaye ametakiwa aulete nao utakuwa *authenticated*, utathibitishwa kwamba ni kweli saini ni ya kwake, maana tumeona maeneo mengine watu wanagombea maiti. Maiti huyu lazima nimpeleke huku akazikwe, mwingine naye anasemwa azikwe huku. Muswada huu umeweka *clear* kabisa kwamba hapatakuwa na matatizo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo limejitokeza hapa ni suala la viongozi ambalo Mheshimiwa Hafidh Ali amelieleza kuhusu viongozi wa Zanzibar. Muswada huu kama nilivyosema, umeweka nafasi ya wosia. Leo tunasema kiongozi wa Zanzibar sharti azikwe Zanzibar, sawasawa. Lakini Taifa kama Taifa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka utaratibu wa kuzika viongozi wake Dodoma, wataendelea kuzikwa Dodoma. Kama kuna suala la kiongozi yejote kuzikwa pengine popote, basi wosia utaandikwa na utakuwa wa wazi. Pengine hapa nisemee viongozi wengine ukiondoa Rais wa Zanzibar ambaye amekuwa *covered* na Muswada huu. Wao wana sheria yao kule na watafuata hiyo sheria yao. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na makaburi sehemu moja (*National Cemetery*) moja ambayo ni Dodoma. Kwa hiyo kiongozi ambaye pengine asizikwe Dodoma, hawesi kulazimishwa kupelekwa Dodoma lakini kutakuwa na wosia ambao unasema mimi ningependa kuzikwa sehemu fulani na sehemu hiyo inaweza kutokea Zanzibar. Hilo wala halina mgogoro kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mengine ambayo yameelezwa, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Janet Kahama ambaye amesisitiza kwamba yeye anaafiki sana Muswada huu, lakini pia anakubali kuwe na sehemu moja ya kuzika viongozi wetu. Waheshimiwa Wabunge, Mataifa mengine ya Kiafrika hapa hapa wanayo maeneo hayo. Zimbabwe ipo. Kwa wale waliofika Zimbabwe kuna *Heroes Acre*, Msumbiji wanayo maeneo hayo na yamefanya kazi vizuri. Hawa ni Waafrika wenzetu wala hawana tofauti na sisi, lakini wao wameanza mwanzoni tu baada ya kupata uhuru wao wakaona umuhimu wa kuzika viongozi wao sehemu moja kwa faida ya watoto na vizazi vijavyo. Hili ni jambo la msingi sana. Leo sisi hapa tunaweza kusema kwa masihara, lakini fikiria miaka 100, 200, 300 ijayo, haya yatakuwa muhimu sana. Wengine wanaona raha kwa mfano ukienda Marekani, mnakwenda kuonyeshwa mahali ambapo wanazikwa viongozi wao na unakuwa kama mtalii unapitapita mle, aah huyu alizikwa hapa! Lakini wao waliamua kufanya hivyo. Sisi wakati ndio huu tufanye maamuzi. Ni kweli tunaweza kuwa na *statement* zetu, lakini ni vizuri tuanze kuanza jambo hili na mimi naamini tutakuwa na wengi watakaozikwa pale maana tunahitaji viongozi hawa wazikwe mahali pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kusema kwamba, yaliyosemwa hapa mengi ni mazuri yanahitaji sasa mtupe nafasi. Si vizuri kusema tukayazoe, maana ni kama mnaombea mtu afe mkazoe, lakini ni vizuri tuone huo Muswada katika miaka 10, 30 ijayo unafanya kazi na pengine kukiwa na haja ya kurekebisha huko mbele kwa kadri ya uzoefu tunaoupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwahakikishia kwamba, nia ya Muswada huu ni kujenga heshima kwa viongozi wetu wakiwa hai na wakiwa wamefariki. Hiyo ni nia

kabisa kabisa na pia Muswada huu hauondoi haki ya viongozi wa dini wa huyo kiongozi, watapata nafasi ya kutosha kumzika kidini.

Lakini tuwape nafasi Watanzania ya kuweza kuona mahali walipozikwa viongozi wao. Hivi sasa Watanzania mbalimbali wanakwenda pale alipozikwa Mwalimu Butiama.

Mimi rafiki yangu alitoka Masasi na mtoto wake na mkewe mpaka Butiama. Wengine wanakwenda Zanzibar kuona alipozikwa marehemu Karume. Sasa kwa miaka hiyo, tuwape nafasi Watanzania ya kwenda kuona mahali pamoja na hii ndio nia ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kujifunza wakati tunafanya kazi. Sasa Waziri ametoa hoja baada ya ninyi kuchangia, amejibu maswali na anachoomba katika hoja hii ni kwamba Muswada huu sasa usomwe kwa mara ya pili. Kwa hiyo, mimi nitaondoka hapa sasa nakwenda kubadilisha mavazi haya tunarudi tunakaa katika Kamati ya Bunge Zima ili kusudi tupitie Muswada ule kifungu kimoja hadi kingine.

Sasa wakati tunapitia kifungu kimoja mpaka kingine mtu anaweza kutoa mawazo yake ya kubadilisha maneno katika Muswada. Kama atafanya hivyo itabidi mimi nisimamishe mzungumze kidogo kama tunakubaliana, tunakubaliana kama tunakukatalia basi tunaendelea na Muswada. Hivyo hivyo katika nafasi hii Waziri angeweza kumaliza hivi akasema mimi sasa naurudisha Muswada huu kwenye Kamati ukaandaliwe tena lakini hakusema hivyo. Kwa hiyo, nitawahoji ninyi kusudi mkubali kwamba sasa Muswada huu usomwe mara ya pili.

Baada ya Kamati hii ya Bunge Zima kumalizika tena mimi narudi kuvaa nguo hii, narudi kukaa hapa. Sasa nikikaa hapa nitawahoji kama Muswada huu sasa usomwe mara ya tatu. Kwa hiyo, mkikubali Katibu atasoma kichwa cha Muswada huu na utakuwa umepita kwa upande wetu sisi unasubiri uandaliwe vizuri upelekwe kwa Rais akasaini halafu iwe sheria. Kwa hiyo, ni semina ndogo. (*Kicheko*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Pili*)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, katika Kamati ya Bunge Zima kama una hoja katika kifungu nitakachosema utazungumza dakika tano, kengele itagongwa halafu Waziri yecheleza hoja zenu.

Jina la Muswada

(*Jina la Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 1

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 2

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 3

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko*)

Kifungu cha 4

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili kwa niaba ya Serikali niweze kupendelekeza marekebisho katika Ibara ya 4(2) katika mstari wa pili. Tunapendelekeza tuondoe maneno “*whose appointment was revoked*” yanayoonekana katika Ibara hiyo na badala yake tuingize maneno “*who was removed from office due to gross misconduct or misbehavior*”.

NAIBU SPIKA: Rudia kama inawezekana.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Tunapendelekeza isomeke kama ifuatavyo:-

“*A specified leader who was removed from office due to gross misconduct or misbehavior shall not be entitled for funeral arrangements under this Act*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapendelekeza marekebisho hayo kwa sababu ilivyokaa sasa hivi neno *revoked* kwa Kiswahili wanaweza kusema kutengua, Rais anaweza kwa mfano tu, Rais kwa sababu yejote ile anaweza akatengua uteuzi mathalani wa Waziri Mkuu kwa sababu zake anazoona kwamba anahitaji apate mtu mwagine wa kumteua. Sasa katika hali hiyo kiongozi huyo wa Kitaifa hawezি akakosa stahili inayotajwa na Muswada huu kwa sababu tu ya kutenguliwa. Inaweza ikawa hivyo hivyo kwa upande wa Jaji Mkuu. Kwa hiyo, tuliona kwamba suala hili tuliangalie kwa umakini

zaidi na ndio maana Serikali inakuja na haya mapendekezo ya kufanya marekebisho hayo.

Baada ya kutoa ufanuzi huu, napenda nikushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio msimamo wa Serikali na mimi ni sehemu ya Serikali na asingesema hivyo kabla hatujashauriana, huo ndio msimamo wa Serikali.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nani atakayeama kwamba yule aliyeondolewa ameondolewa *through gross misbehavior* maana yake sasa ni *highly subjective*.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunajadili mabadiliko aliyotoa Waziri wa Sheria, kwa hiyo, Waziri wa Afrika Mashariki.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya uteuzi katika maeneo niliyoyataja inafahamika. Vigezo ni vipi mamlaka hiyo inatumia yenyewe ndio inafahamu. Huwezi ukaweka *objective standard* kwa utendaji wa kiongozi ambaye mamlaka ya uteuzi ni Rais.

Kwa upande wa Rais, Makamu wa Rais na kwa sehemu ndogo kwa upande wa Spika na Naibu Spika kuna utaratibu wa kuwaondoa viongozi hawa humu Bungeni. Kwa Rais na Makamu wa Rais kuna utaratibu wa *impeachment*. Kwa upande wa Naibu Spika na Spika kwa mujibu wa kanuni zetu utaratibu huo umewekwa. Sasa katika hali hiyo yawezekana Wabunge kwa sababu zao tu, nikichukua mfano tu Naibu Spika wameona kwamba hakucheka nao vizuri wamechoka wanassema basi tunakuondoa sasa haiwezekani kwa Spika ambaye ndiye ametajwa mmoja wa viongozi hawa wakaona kwamba sasa apoteze stahili yake ya kuzikwa kwa utaratibu huu kama na yeye alikuwa ameridhia iwe hivyo. Ndio tunajaribu kuboresha hiyo ili iweze kufanyika kwa staha zaidi.

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na mabadiliko*)

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 10

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi kwamba hiyo *collected version* naikosa lakini nadhani ujumbe unaweza ukapokelewa chini ya kifungu hiki.

Kama unaniruhusu ni kwamba tumekuwa kimya juu ya wale ambao tayari tumewazika nje ya Dodoma, Je, tunaweza tukaleta miili yao hapa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jackson Makwetta kama ukisoma kanuni ya 72(1) kinasema katika *stage* hii huwezi kuleta hoja ambayo itabidi ijadiliwe na ingetakiwa iletwe kwa maandiko utabadilisha tu, sasa isomeke hivi. Hili la kwako ingetakiwa iletwe hoja kabisa. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

Muswada wa Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa wa Mwaka 2006
(The National Funeral Bill, 2006)

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu baada ya Waheshimiwa Wabunge kukaa kama Kamati ya Bunge Zima na kuitia kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake Wabunge wamekubali Muswada wa kushughulikia mazishi ya Viongozi wa Kitaifa kwa mwaka 2006 (*National Leaders Funeral Act 2006*). Naomba sasa upitishwe kuwa sheria pamoja na mabadiliko yote yaliyofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

*(Saa 01:02 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano
Tarehe 15 Februari, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*